

Uwe Halisi Kwa Mungu

na Larry Chkoreff

Toleo 1.6
Chapa ya Kwanza - 2000
Chapa ya Pili 2007
Chapa ya Tatu 2008

Hati miliki © 1999 na Larry Chkoreff
Kimechapishwa na kutolewa na International School of the Bible,
Marietta, Georgia,
U.S.A.

Kitabu hiki ni mali ya mwandishi. Kinaweza kuzalishwa tena bure, ila kwa kugawa bure, bila gharama na kwa ruhusa ya mwandishi au mzalishaji. Hakiruhusiwi kubadilishwa bila idhini iliyotolewa kwa maandishi na mwandishi au mchapishaji na mtoaji. Hakiruhusiwi kubadilishwa au kuhakikiwa kwa njia yoyote ile. Kitabu hiki hakiruhusiwi kutumika bila ruhusa ya mwandishi kwa ajili ya kuuzwa tena au kurekebisha.

Isipokuwa kwamba, nukuu za Maandiko zinatoka katika Biblia ya NKJV. Hatimiliki 1979, 1980, 1982 na mtoaji, Thomas Nelson. Kimetumika kwa ruhusa.

Kwa maelezo zaidi kuhusu kuzalisha tena kitabu hiki wasiliana na
ISOB katika:

Barua pepe - bereal@isob-bible.org
Mtandao wa ISOB ni www.isob-bible.org.

Mwandishi, Larry Chkoreff, pamoja na mkewe Carol, ni waanzilishi wa International School Of The Bible (ISOB) huko Marietta, Georgia U.S.A. ISOB hutoa zana na mafunzo ya muhimu kwa ajili ya kukuza wanafunzi, na kusaidia katika kuanzisha makanisa.

ISOB imeanzisha sehemu za mafunzo ya wanafunzi katika maeneo mengi Africa na nchi za Asia.

Ni tumaini letu kwamba kitabu hiki kitawasaidia wale wanaotafuta kupata ushirika wao na Mungu, Muumbaji, wakijitunza mbele Zake kwa ukweli na uhalisi, na kwamba itawasaidia waamini kutembea na Mungu wakiwa na furaha na uhuru.

Kuna mamilioni ya watu duniani wanaokuja kumjua Yesu kila wiki. Idadi ya ukuaji inaongezeka. Hawa watu wanahitaji mafundisho rahisi, yaliyo mafupi yaliyo pandwa katika msingi wa kuukuza ushirika wao na Mungu. Tumaini letu ni kwamba kitabu hiki kitawasaidia wengi wao kufupisha njia ya uanafunzi na kufanyika viongozi katika Ufalme wa Mungu. Ni maombi yetu kwamba unaposoma kitabu hiki utakutana na uwepo mzito wa Mungu, na utapata shauku kuu ya kuendelea kuandamia uwepo Wake.

Kitabu hiki kimewekwa wakfu kwa Yesu Kristo, aliye mwanzo na mwisho wa imani yangu.

Vitabu vingine vya ISOB:

Mtiririko wa Seamina ya Kukua au Kufa - Uanafunzi - onyesho la agano la damu, Kuzaa matunda, na ushirika wa karibu sana na Mungu.

Kozi Nzima ya Kukua au Kufa - Hii inabeba mambo yote ya uanafunzi

Vitabu vingine vilivyotolewa na ISOB:

Mtiririko wa semina ya Kukua au Kufa - Uwanafunzi-Ikielezea agano la damu, kuzaa matunda, na ushirika wa karibu na Mungu.

Kozi kamili ya Kukua au Kufa - Asili ya masomo ya uanafunzi huu yanajumuisha zaidi ya masomo 100. Kozi hii inapatikana kwa kuitoa kwenye tovuti bure.

www.isob-bible.org, au kutoka kwenye CD-ROM katika komputa yako.

Kutoka Takataka Hadi Vito vya Thamani - Jinsi ya kubadilisha huzuni zako kuwa baraka

Safari Za Ayubu - Kutoka Dini Hadi Utukufu

Biashara ya Zaburi Ya Kwanza - Muongozo wa Kikristo Wa Biashara Ndogo ndogo

Damu Ya Agano La Milele

Barua pepe ni bereal@isob-bible.org

Yaliyomo

Utangulizi - Uwe Halisi	5
Sura Ya 1 - Habari, Jina Langu Ni Yesu.....	12
Sura Ya 2 - Habari Mbaya, Habari Njema.....	17
Sura Ya 3 - Ni Kitu Gani Kilichonitokea?	25
Sura Ya 4 - Ni Mungu Gani Huyu Uliyekutana Naye?	32
Sura Ya 5 - Mimi Ni Nani	40
Sura Ya 6 - Mauti Imetanguliwa.....	52
Sura Ya 7- Yesu Kama Bwana?.....	56
Sura Ya 8- Kuendelea Na Maombi.....	69
Sura Ya 9- Kuendelea Ndani Ya Neno.....	76
Sura Ya 10- Kuendelea Na Kuwa Unabadilishwa.....	88
Sura Ya 11- Ubatizo Wa Maji.....	97
Sura Ya 12- Njia Mpya Ya Maisha: Tabia Mpya.....	101
Sura Ya 13- Roho Mtakatifu.....	114
Sura Ya 14- Tunahitaji Kuwekwa Huru.....	122
Sura Ya 15- Kusonga Mbele Na Kanisa.....	136

Sura Ya 16- Vita Vya Kiroho.....	149
Sura Ya 17 - Mateso Na Dhiki.....	158
Sura Ya 18- Yesu Anarudi.....	172

Utangulizi Uwe Halisi

Asili ya mpango wa kwanza wa Mungu wa maisha yako ulikuwa kuwa katika uhusiano na Yeye uliyo hai. Kusudi la kitabu hiki ni kukusaidia upate uhusiano huo na uenende katika huo. Siyo kuongeza matabaka ya mambo tunayoyapitia katika maisha, hasa mambo ya kidini na matendo ya kidini tunayoyatenda. Ni maombi yangu kwamba kitabu hiki kitakutia moyo uwe muwazi kwa Mungu, Muumbaji wako, na kupitia uwazi huo kupata pendo la ajabu na neema ya Mungu ambayo itakufinyanga urudi kwenye mpango wa kwanza wa maisha yako.

Wagalatia 1:15,16 Inasema, “Lakini Mungu, aliyenitenga tangu tumboni mwa mama yangu, Akaniita kwa neema yake, Alipoona vyema kumdhihirisha mwanawe ndani yangu, ili [_____ *Kusudi la Paulo katika maisha liliwekwa kwenye nafasi hii iliyo wazi*].” Hii ni nukuu ya kwanza ya Paulo aliyeandika barua katika karne ya kwanza kwa kanisa la Galatia. Alikuwa ni mtenda kazi hodari, na muuwaji, akiwauwa Wakristo katika karne ya kwanza akidhani maisha yake yanatimiza kusudi la Mungu kwake mwenyewe na kwa Mungu. Tazama misemo hiyo mikuu, “*Lakini Mungu,*” na “*Kwa neema yake.*” Hiki ni kitu ambacho Mungu amekifanya! Alimfunulia Paulo kusudi lake katika maisha. Wote tunataka kujua kwanini tuko hapa na tunataka kujua makusudi yetu.

Kila mmoja wetu anadesh _____ kwa ajili ya makusudi yetu katika maisha, na ni tofauti kwa kila mwanadamu. Hauwezi kujaza hiyo desh; Ni Mungu pekee ndiye anayeweza. Paulo hakuweza nafasi iliyowazi mpaka alipokutana na uwepo wa Mungu uliyo wa ajabu na baada yakutembea na Mungu kwa miaka mingi. Lakini Paulo hatimaye alijaza desh hiyo. Mungu anataka akufunulie kusudi lako.

Kila mmoja wetu huanza kama vile jinsi tulivyo.



Kisha tunaanzisha tabia mbalimbali za jinsi tunavyotaka kuwa.

“Mambo tunayoyataka” Ndiyo tuyafanyayo. Mara nyingi maamuzi haya hufanyika bila kufikiria. Mienendo yote hii hujenga matabaka kama ya kitunguu katika maisha yetu. Ni kusudi la Mungu kuturudisha kwenye uhalisi wetu, “Wewe” halisi. Ambaye ni “wewe” apendwaye sana na Mungu na ni “wewe” pekee ambaye Mungu anaweza kutenda kazi pamoja nawe kukufanya kamili na kutimilishwa katika maisha.

Tunaogopa ugunduzi wa jinsi tulivyo halisi. Kwa miaka mingi tumejenga matabaka ya kujidanganya kibinafsi juu yetu wenyewe kama vile maganda ya kitunguu. Tunanjia nyingi za kujificha nyuma ya mienendo yetu ambayo watu wengine au sisi wenyewe tumeijenga. Mienendo hii inatudanganya wenyewe na tumepotelea kabisa katika mienendo hiyo kiasi kwamba tumeshindwa kujikwamua. Kabla hatujagundua kwamba tumejificha katika matabaka mengi ambapo tunajidanganya kabisa na tunafanana na ayasemayo Yereimia, “Moyo huwa mdanganyifu kuliko vitu vyote; unaugonjwa wa kufisha; nani awezaye kuujua?” (Yereimia 17:9).

Hata hivyo, ni Mungu tu mwenye uwezo wa kumenya maganda.

Naweza nikakumbuka Mungu akisema nami miezi michache tu baada ya kukutana na Yesu kwenye miaka ya 1979. Haikuwa ni sauti ya kusikika, bali ilikuja kwa njia ya kanda ya redio ambayo ilirekodiwa katika ibada iliyofanyika umbali wa maili 2,400. Hakikuwa ni kitu ambacho kiko juu na kikuu au cha kidini kabisa, Kilikuwa ni cha kawaida sana. Hata hivyo, niliposikia nilijua katika “ufahamu” wangu (ndani sana) kwamba ni Mungu alikuwa akinena moja kwa moja na mimi. Ilikwenda hivi:

“Naona mpango wa kwanza wa maisha yako. Ni kama karatasi iliyokunjwa inayo kunjuka. Jinsi inavyo kunjuka maandishi ya maisha yako yanaandikwa juu yake. Hata hivyo pembe za karatasi hii ya kukunja zimeungua na majivu yake yamesambazwa kiasi kwamba hakuna mtu, hata wewe, anayeza tena kusoma karatasi hii. Hakuna mwanadamu anayeweza kuyakusanya majivu yote, na kuyaweka pamoja katika sehemu sahihi na kuiumba upya hiyo karatasi.

Hata hivyo, sijaisahau. Mimi ni Mungu Mwenyenzi, na ninauwezo

wa kuyakusanya majivu yote, na kuyafufua yarudi katika hali ya karatasi na kuyarudisha palepale yalipokuwa ili kwamba wewe na wengine waweze kukuona jinsi ulivyo, ili kwamba maisha yako yarudie hali yake ya kwanza. Hili litafanyika polepole na kuendelea, Na kitakuwa kitendo cha neema yangu tu. Unahitaji kutembea karibu Yangu tu na Unipe moyo wako, ambayo pia inamaanisha kuwa mkweli wa kina Kwangu wakati wote.”

Ninaweza nikashuhudia kile ambacho Mungu aliniambia katika mwaka 1980 kimekuwa ndiyo mazoea yangu na bado ni mazoea yangu. Mungu hawezi kusema uongo!

Kuridhika kuliko halisi katika maisha ni kufahamu kwamba wewe halisi unakubalika. Nikujua kwamba huwezi kujua jinsi ya kuwa halisi kabisa katika tukio moja kubwa, Lakini jinsi unavyoendelea na maisha Mungu atasababisha matabaka kubanduliwa kidogokidogo kadri unavyoendelea kuyavumilia na kukubaliana nayo. Unagundua kwamba Mungu anakukubali jinsi ulivyo, Hata hivyo anataka kubandua maganda kukupata wewe halisi. Utagundua kwamba Mungu ni mpole katika hatua hizi zote. Utagundua kwamba hata upole unaweza kuumiza.

Unaweza kuwa na vitu vilivyojificha katika maisha yako ambavyo hutaki mtu yoyote, hasa Mungu, Avifunue na kuviweka wazi. Unajua kwamba itauma sana. Lakini Mungu atakuambia, “Endelea na uniruhusu nikukuguse maumivu hayo mara moja tu. Ninaweza kuongeza maumivu mwilini mwako kwa jinsi ninavyo kugusa, lakini baada ya hapo, uponyaji unakuja. Je Inastahili?” Ni kama daktari wa upasuaji anapouliza, AJe inastahili kuvumilia maumivu ya kisu changu kama inamaanisha ni kuukata ugonjwa?”

Ni Mungu pekee awezaye kuleta nuru katika “nyakati zako za giza.”

“Basi Yesu akawaambia tena, akasema, ‘Mimi ni nuru ya ulimwengu, yeye anifuataye hatakwenda gizani, kamwe bali atakuwa na nuru ya uzima” (Yohana 8:12).

Ndiyo maana kitabu hiki kina kichwa cha habari “Uwe Halisi Kwa Mungu” Hakika ni shauku yangu kwamba umfahamu Yesu kama

bado hujamfahamu. Katika kitabu hiki utakutana na mafundisho ambayo Mungu anatamani uyafahamu. Utakutana na vidokezo vilivyoelekezwa kwenye utii ambavyo ni lazima uwenavyo kama unataka kukomaa katika Kristo. Hata hivyo uhusiano wako na Mungu na utiifu Kwake lazima ujengwe juu ya kuwa halisi kwako mwenyewe na Kwake. Kama uta igiza igiza mbele za Mungu utakuwa na wakati mgumu sana na kukosa fursa pekee ya kuwa huru na kamili.

Tunaweza kushirikiana na Mungu.

Jambo pekee ambalo Mungu anaweza akashughulika nalo ni ukweli wako. Moja ya majina Yake ni kweli. “Yesu akamwambia,” ‘mimi ndimi njia, na kweli, na uzima ...’” (Yohana 14:6a). Yesu alipokuwa kwenye majaribu katika maisha yake, alikuwa na majadiliano na mtawala wa Rumi, Pilato, ambapo waliongea kuhusu ufafanuzi wa kweli. “Basi Pilato akamwambia, ‘Wewe umfalme basi? Yesu akajibu, ‘Wewe wasema, kwakuwa mimi ni mfalme. Mimi nimezaliwa kwa ajili ya haya na kwa ajili ya haya mimi nilikuja ulimwenguni, ili nishuhudie kweli. Kila aliye na hiyo kweli unisikia sauti yangu’”(Yohana 18:37).


Kunakanuni katika sayari ya dunia ambayo mara zote hufanya kazi: Inaitwa kupanda na kuvuna (Wagalatia 6:7-8). Mara zote mtu huvuna chchote kile alichopanda. Kanuni hii inatumika kwenye kweli pia. Ukipanda kweli utavuna kweli. Ukipanda ulaghai na uongo, utavuna giza na kweli haita angaza maishani mwako. “Kila aliye na hiyo kweli hunisikia sauti yangu” (Yohana 18:37b).

Mfalme Daudi alisema hivi katika Zaburi 32:2-3 baada ya kujaribu kuficha dhambi zake mbaya sana kwa Mungu. Daudi hakuweza kuwa hai ndani yake mwenyewe, bali aligundua kwamba Mungu anaheshimu kweli na kwamba kweli itamfanya mtu awe huru.

“Heri BWANA asiye mhesabia upotovu, Ambaye rohoni mwake hamna hila. Niliponyamaza mifupa yangu ilichakaa kwa kuuguwa kwangu mchana kutwa”. (Zaburi 32:2-3). Nakushauri uisome Zaburi yote ya 32.

Mara zote huwa kunagharama kwakuwa mkweli. Mithali 23:23 inasema, “Inunue kweli, wala usiiuze; naam, hekima na mafundisho na ufahamu..” Gharama moja unayohitaji kujiandaa kuilipa ni unyenyekevu.

Naamini kwamba uovu ulitokea kwenye dunia yetu na unaendelea kuwepo kwaajili ya uongo wa mwanadamu. Michoro iliyoko hapo chini inaelezea jambo hili. Kwa kiwango kile ambacho hauwi mkweli, ni kiwango cha uovu au giza ambacho kinakuwepo katika maisha yako. Jinsi pengo linavyokuwa kubwa, ndivyo uwezekano wa uovu unavyoongezeka.



Kanuni hii hutenda kazi kwa watu wote.

Unaweza kuwa Myahudi na ukawa umelelewa katika nyumba inayomuhofu Mungu na katika desturi iliyokufundisha “kutokubadilika” na kutowasiliza “Wakristo hao.” Naelewa umekuwa ukitii ushauri huo. Wakristo wengi wamekuwa na moyo mgumu dhidi ya imani yako na desturi yako.

Unawezakuwa Muislam, Muhindu, Mbudha, Mnew age, au asiyejua kama kuna Mungu. Unaweza ukawa unaabudu viumbe katika

ulimwengu wa roho au sanamu. Unaweza ukawa mpagani au mtu aliyejitosheleza na hakuona haja ya kuwa na Mungu. Unaweza ukawa unasoma kitabu hiki ukiwa kama mwamini mpya na unashauku ya kukua. Inawezekana umewahi kuwa na imani kubwa wakati fulani, lakini sasa unamashaka juu ya Mungu. Naheshimu pale ulipo.

Kama wewe ni wa kiroho Mungu hataki uwe wa kidunia.

Kama wewe ni wa kidunia au kisayansi, Hakuuambii uamini roho ambazo hazistahili kuaminiwa. Hakuuambii ubadilishe desturi zako au uwe kama Wakristo wengine uliowahi kukutana nao. Hakuuambii ujiunge na kanisa lolote au dini yoyote. Hakuuambii uwe wa “kidini.”

Anachotaka wewe ufanye ni uwe mkweli katika mahitaji yako ya maisha. Wote tumesha wahi “Kuwa katika hali ya uhitaji.” Vipengele vikuu vitatu ni upendo, usalama na kuwa muhimu. Tunahitaji upendo usio na mipaka. Tunahitaji kupendwana mtu ajue mambo yote yanayotuhusu na bado anatumkubali.

Tunahitaji usalama kwaajili ya vitu mbalimbali na mahitaji ya kihisia na hatima ya milele. Tunahitaji kuwa muhimu, au tunahitaji kujua kwamba tunajaliwa na tunathamani fulani. Mungu ana shauku kuu ya kukidhi mahitaji hayo, kama jinsi tutakavyoona kwenye sura zijazo.

Tayari *unamgeukia* mtu au vitu kwaajili ya mahitaji haya. Inawezekana umekuwa ukitegemea nguvu ya nafsi yako mwenyewe, ambayo inajumuisha akili, elimu, na vipaji. Siyapuuzii haya lakini inabidi yawekwe katika mtazamo sahihi. Haya yanaweza yakaonekana kufanya kazi kwa kiwango fulani. Inawezekana umekuwa ukitegemea dini ya kiroho ambayo inakuunganisha na viumbe vya kiroho vilivyo halisi. Naelewa kwamba hii ni halisi na inaweza kuonekana inafanya kazi kwa kiwango fulani. Hataivyo mwishoni, hawa “miungu wengine”¹ siyo wakutegemea. Ni walazimishaji sana. Mara zote wanakuweka katika hofu na wanalazimisha kuwaabudu. Wanaahidi njia zilizo rahisi za kukupatia mahitaji yako. Hata hivyo nikama kutumia kadi ya mikopo; Hatimaye bili itakuja na itakuhitaji kuilipa.

Mungu, muumbaji, ni wakutegemewa. Jina Lake ni Kweli. Neno Lake ni Kweli. Anapojidhihirisha kwako itakuwa sawasawa na Neno Lake kiasi kwamba hutakuwa na wasiwasi kwamba umekutana na Mungu au

“mingu mwingine”

Jambo moja nililigundua kumhusu Mungu ni kwamba Yeye sio mbishi. Mara zote hujidhihirisha tu na ubishi wote hunyamaza. Anayo shauku yenye kina kukufikishia kweli kuliko jinsi unavyoweza kuipokea. Alikuumba ili uwe na uhusiano wa kibinafsi ulio wa karibu na Yeye. Hakukuumba ili utegemee dini au maroho. Hajaiacha hatma yako ya milele katika mikono ya watu wengine ambao wanajaribu kukushawishi kwamba wanayo kweli.

Kwenu wote watafutaji, Mungu anaweza kudhihirisha jina Lake kwako. Hauhitaji kutegemea mabishano ya watu.

Kwenu wote mnao songa mbele kuelekea kukomaa, Yeye ni mwalimu. Anataka kukuongoza kwenye kweli yote na kukufanya ufanane naye kibinafsi.

Sasa, nakutia moyo ufanyie mazoezi ukweli mbele za Mungu. Hakuna njia iliyo sahihi ya kuomba. Ongea naye tu kama vile ambavyo ungeongea kama angekuwa ni rafiki yako wa karibu aliyekaa pembeni yako. Mwambiye mambo unayo yaamini na usiyo yaamini. Mwambie jinsi unavyojisikia, Mpe mashaka yako yote, hofu na uchungu. Mwambie mahitaji yako na jinsi ulivyojaribu kuyakidhi.

“Nanyi mtanitifuta na kuniona, mtakaponitifuta kwa moyo wenu wote” (Yeremia 29:13).

Uwe halisi tu kwa Mungu!


Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti yake.

“Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda.”

1"Miungu wengine itaelezewa kwenye sura zijazo

Sura Ya 1 “Habari, Jina langu ni Yesu”



Hitaji moja la mwanadamu lililo kubwa kuliko yote ni kujijua yeye ni nani na kwanini yuko hapa.

Mwaka 1970, miaka tisa kabla Mungu hajaja kwenye maisha yangu, nilikuwa na wakati wa mpito uliyo wa kuvutia na Mungu. Nilikuwa na miaka thelathini na nilifanya biashara iliyokua na faida sana. Ilikuwa ni ndoto ambayo niliotta tangu nilipokuwa mdogo. Asubuhi moja nilikuwa nje nikikata majani kwa kutumia mashine yenye kelele sana. Nilikuwa nauliza swali, “Kwanini niko hapa, Na mimi ni nani?” Nadhani nilikuwa nikiongea na Mungu ingawa sikuwa na uhusiano Naye.

Nikaitazama nyumba yangu iliyo nje kidogo ya mji nikasema, “Ninaenda kazini kila siku asubuhi ili niweze kulipa deni kwa ajili ya nyumba hii. Ninafanya hivyo ili niweze kurudi katika nyumba ile kila jioni ili nile na kulala. Ninafanya hivyo ili niweze kuamka kila asubuhi na kwenda kutafuta pesa zaidi ili kulipa deni zaidi la nyumba.” Nikaanza kulia, “Je maisha ndiyo yako hivi? Je kuwa na mafanikio huwa unajisikia hivi? Nilionekana kuwa na mwili uliyo jengeka vizuri. Una maelfu ya maili ya mishipa ya damu. Moyo unaodunda kunifanya niwe hai, na ubongo ambao hakuna mwanadamu anayeweza ku-uunda. Ninaonekana kuwa nimeumbwa na Mungu. Je Mungu ameniumba ili niishi kama panya kwenye kisanduku kilichowekwa kwenye gurudumu linalozunguka lisilokwenda popote?” Nikaanza kuomboleza bila kujizuia na kumlilia Mungu.

Mungu, katika hekima yake ya milele, alisubiri miaka tisa kabla ya kujibu swali langu.

Hataivyo alinjibu kwa njia kubwa na yenye nguvu sana.

Kusema ukweli, kukutanana na Mungu hakukuondoa matatizo yangu mara moja na kujibu maswali yangu yote. Kiurahisi niliendelea kuwasiliana na Mungu, kuishi na Mungu ambaye aliweza kujibu maswali yangu yote polepole. Bado anaendelea kuyajibu.

Ilikuwa ni tarehe 26 Mwezi wa nane 1979, saa 11:30 jioni. Nilikuwa na miaka 39 na nilikuwa nimeishi maisha yangu kwa ajili yangu mwenyewe, kivyangu. Kwa mtazamo wa haraka maisha yangu hayakuonekana mabaya, lakini kiundani ni Mungu tu ndiye aliyeiona haja yangu. Nilitaka kujua kwamba nitakwenda wapi baada ya kufa na nitaishi wapi milele. Vilevile nilisikia maoni mbalimbali. Wengine husema unalala usingizi tu. Wengine husema kwamba unakwenda katika sehemu “bora zaidi.” Wengine husema kwamba maisha yako yanakomea hapa tu hakuna kuendelea. Wengine huzungumza juu ya Mbingu na Jehanam..

Fikiria kuhusu hilo. Hili ni swali muhimu kuliko yote ambalo unaweza kujiuliza katika maisha yako hapa duniani. Ni heri usisikilize maneno ya mtu yeyote. Ni bora uwe na uhakika. Umilele sio muda mrefu tu ni milele. Ndani yangu nilikuwa na uhakika na kitu nilichokijua kwamba ni bora nisipoteze hatima yangu ya milele kwa maoni ya watu. Hata watu waliosema kwamba wanalijua jibu hawakukubaliana mmoja na mwingine.

Kwa kiasi fulani niliamini kuhusu Mbinguni na Jehanam, Lakini nilidhani kuwa Mungu hutoa kipimo kulingana na matendo. Kwa mfano, kama kulikuwa na watu wabaya kuliko mimi, kama wauwaji, nk., Basi ningejikuta nimeangukia sehemu fulani na angalau ningepata alama ya “C” na kufanikiwa kuingia Mbinguni. Hatimaye nikawa halisi mbele za Mungu na kumuuliza swali, “Je unakwenda wapi baada ya kufa?”

Kijana wangu wa kiume alikuwa akinisaidia kusoma Biblia kwa mara ya kwanza. Nilianza saa 6:30 mchana na saa 11:30 niliacha na kusema, “Yesu yu hai, Yeye ni Mungu na Aliandika Biblia. Si hivyo tu Yesu ni hitimisho la ushindi juu ya uovu wote. Mungu anataka kuwa baba yangu na kutawala maisha yangu.”

Nilisikia Mungu akisema nami. Alisema, “Nikasikia sauti kubwa kutoka katika kile kiti cha enzi ikisema, ‘Tazama, maskani ya Mungu ni

pamoja na wanadamu naye atafanya maskani yake pamoja nao, nao watakuwa watu wake naye Mungu mwenyewe atakuwa pamoja nao. Naye atafuta kila chozi katika macho yao. Wala mauti haita kuwapo tena wala maombolezo, wala kilio, wala maumivu hayatakuwapo tena; kwa kuwa mambo ya kwanza yamekwishakupita.”(Ufunuo 21:3,4).

Ghafla, nikawa kama Yohana 7:37-39 inavyosema, “Hata siku ya mwisho, siku ile kubwa ya sikukuu, Yesu akasimama, akapaza sauti yake akisema, ‘mtu akiona kiu, na aje kwangu anywe, aniaminie mimi, kama vile maandiko yalivyonena mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake.’ Na neno hilo alilisema katika habari ya Roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maana Roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa.”

Yesu alifanyika halisi kwangu. Nikamwona kwa macho yangu ya rohani katika njia ambayo ilimfanya awe halisi kama mtu mwingine yeyote. Na alisema, “*Habari yako, Jina langu ni Yesu.. Nakupenda.*” Nilisikia “mito ya maji ya uzima” ikibubujika kutoka ndani yangu. Nikamwambia, “Nimeyaharibu maisha yangu. Asante kwa kufanyika baba yangu na kuahidi kunitunza. Nitaifanya chochote kile utakacho sema.” Ninaweza kukumbuka hisia za kuwa na baba halisi ambaye anaweeza kunitunza, mtu ambaye ningemgeukia nikiwa na haja zozote. Nilikuwa nikiwategemea “miungu wengine.”

Mambo haya niliyopitia yalisababisha shauku moyoni mwangu ambayo imekuwa nguvu inayosukuma maisha yangu. Tunapokutana na Mungu ana kwa ana, mafundisho, dini, madhehebu, desturi za kifamilia yote, maqambo haya yote hutupwa dirishani. Shauku hii imenisababisha nimwandamie Mungu kwa moyo wangu wote. Na nilipomwandama nilimjua zaidi na kuujua utu Wake.

Mtume Paulo alipitia mambo fulani katika safari yake kuelekea Dameski. Alikuwa ni farisayo wa mafarisayo. Alijua sheria na desturi za kidini kuliko mtu mwingine yeyote katika wakati wake. Hataivyo, hakuwa amemjua Mungu hadi alipopitia mambo haya. “Hata alipokuwa akisafiri, ikawa anakaribia Dameski; ghafula ikamwangaza kotekote nuru kutoka mbinguni. Akaanguka chini, akasikia sauti ikimwambia, Sauli, Sauli, mbona waniudhi?” (Matendo 9:3,4)

Gundua nikitu gani cha kwanza Paulo alichokisema wakati nguvu za Mungu zilipomwangusha chini. “Akasema, U nani wewe, Bwana?” Naye akasema, ‘Mimi ndimi Yesu unayeniudhi wewe.’”

Akasema, “U nani wewe, Bwana?” Paulo hakujua huyu kiumbe ni nani, lakini alijua ya kwamba ni bora amwite Bwana kwa sababu ya nguvu alizo zisikia katika uwepo wake. Kisha Paulo alitaka kujua Bwana huyu alikuwa nani. Paulo alijua kwamba alikutana na kiumbe mwenye nguvu kuliko wote ulimwenguni, Hakujua tu kwamba alikuwa nani. Hakika hakuwa Mungu yule yule aliyeelezewa na desturi ya dini yake,

Mungu anataka akutane na wewe. Ninakuomba uwe mkweli na muwazi na umkaribishe afanye hivyo. Ninakuhakikishia hautakuwa kama ulivyokuwa!

Nilipoacha kufikiri kwanini ilinichukua muda kupata mahitaji yangu kwa Yesu, Nina weza nikajibu hivi: Tunahitaji kuelewa haja kuu kwa Mungu kabla hatujaweza Kumwona kuwa Yeye ni nani. Ukweli ni kwamba, tuna haja kwa ajili ya Mungu na kuelewa kwamba Yesu ni Mungu mwenyewe. Tatizo ni kwamba tumegundua mbinu za kuzika haja hizi. Tumegundua jinsi ya kuwalaghai watu, jinsi ya kuwaendesha watu, jinsi ya kufanya mambo katika maisha kiasi kwamba tunakidhi mahitaji yetu. Tunapogundua kwamba haya hayafanyi kazi, tunajaribu dini, au tunageukia vichocheo mbali mbali, ambayo yote huishia kutufanya watumwa. Wakati mwingine tunajisikia kana kwamba yanafanya kazi. Kama tukiwa wakweli, tutakubali kuwa kuna kitu fulani ndani yetu ambacho hakiridhishwi na kitu chochote ila Muumbaji.

Imesemwa na wengi kuwa tunahitaji kuanguka kifudufudi na kushindwa katika maisha kabla ya kumpata Yesu. Siamini kwamba ni kweli (ingawaje watu wengi wamepitia hayo). Ninaamini kinachohitajika ni mtu kuwa mkweli kabisa mwenyewe. Watu wa jamii na maadili mbali mbali wanaweza kumpata Mungu wa kweli anayeishi, Muumbaji wa ulimwengu, Yesu Kristo. Wanachotakiwa kufanya ni kuwa wa kweli mbele zao wenyewe na mbele za Mungu. Mungu atafanya yaliyobaki. Ni kazi yake kujidhihirisha mwenyewe kwa watu.

Dini (za aina zote) zinatambia kwamba tunatakiwa kuteseka ili kufanya mambo fulani au kuwa katika namna fulani ili kuipata kweli au Mungu. “Miungu mingine” hutuweka katika mateso ili kututawala, kutulaghai na kuwaridhisha. Lakini Biblia inatambia kuwa ni Mungu mwenyewe anayetuvuta kwake na Hujidhihirisha kwetu kwa njia isiyo ya kawaida. Inatambia kwamba Mungu anajua tunachohitaji na anajua jinsi ya kutusaidia.

Anatujua kiundani sana. Anajua inahitaji nini ili tuweze kuona kweli. Hatuhitaji kuchukua maneno ya mtu mwingine kwa ajili ya kweli. Hilo litatisha kuweka hatima yangu ya milele katika mikono ya maoni ya mwanadamu mwengine! Mungu atakukumbatia kwa fadhili zake popote ulipo katika maisha, Uwe tajiri au maskini, kijana au mzee mwenye maadili au asiye na maadili.

Mungu ana uwezo wa kulidhihirisha jina lake kwako.

Kuwa mkweli na sikiliza maneno haya,

“Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda.”

Sura Ya 2 Habari Mbaya, Habari Njema



Kabla mtu hajawa tayari kwa ajili ya habari njema (injili maana yake ni habari njema) anahitaji kukabili habari mbaya kwanza. Daktari anaweza akakuandikia dawa nzuri sana ziponyazo, lakini kama hatutakabiliana na habari mbaya kwanza, kamwe hatutapona

Habari mbaya kwanza.

Mwanzo 1:26 inatuambia kwamba Mungu alimuumba mwanadamu (Adam) kwa mfano wake na sura yake. Mungu aliuumba mwili wa Adam kwa udongo. Alimpa Adam uwezo ambao wanyama wengine hawakuwa nao; ambayo ni kuwa na utatu. Alimfanya mwanadamu kuwa kiumbe mwenye roho yenye nafsi na mwili. Mungu alivuvia Roho yake ndani ya Adam. Alimpa Adam mpangilio wa jinsi ya kuishi, lakini Adam alitaka kujitegemea mbali na Mungu na Neno la Mungu (mti wa uzima). Alipojitegemea, Roho wa Mungu akatoka nadani ya Adam. .Huu ulikuwa ni mwanzo wa utengano kati ya Mungu na mwanadam.

Umezaliwa kwa mfano wa Adam, mtu aliyetenganishwa na Mungu. Adam ni baba yako wa kwanza. Unao uwezo wa kuwa ndani ya sura ya Mungu lakini haukuzaliwa hivyo.

Sasa habari njema.

(Kwanza kabisa, matukio haya yanayofuata ambayo ni ya

kihistoria yalitabiriwa kwa ukamilifu kabisa miaka ma mia na hata maelfu kabla ya kutimia).

Mungu hakukata tamaa kwa Adam na Hajakata tamaa kwako. Adam aligundua kuwa kunakitu ambacho hakikuwa sawa baada ya kujitegemea na akaanza kuishi maisha yake bila Mungu. Alijaribu kufunika aibu yake kwa majani ya mtini. Tunajaribu kufanya mambo mbalimbali ya kidini ili tuweze kuuvumilia uhuru wetu , lakini hakuna kinachofanya kazi.

Mungu alimtaadharisha Adam kwamba kama hata mtii atakufa vifo viwili, kifo cha kiroho na kifo cha kimwili. Adam alistahili kifo lakini alipokea rehema! Kwa jinsi gani? Kwa nini? Mwanzo 3:31 inatambia kuwa Mungu alimuuwa mnyama, alimwaga damu, na kumfunika Adam na Eva kwa ngozi. Mungu alizihamishia dhambi za Adam kwenda kwa kiumbe kisicho kuwa na dhambi. Tendo hili la kumwaga damu lilikuwa ni kivuli cha yale Mungu atakayoyafanya hapo mbele. Kutoa dhabihu ya mnyama lilikuwa ni tendo ambalo lilitabiri kuhusu Mesia ambaye atamwaga damu yake kwa ajili ya Adam. Hukumu ya kifo ya Adam ilibadilishwa. Adam yuko hai leo Mbinguni pamoja na Mungu. **Laana** iliyosababishwa na dhambi iliamishwa kwa mnyama.

Sio yale tunayoyatenda ndiyo yanayohesaibiwa bali ni jinsi tulivyo

Sio lile *tunalolifanya* ndilo linaloendelea kututenga na Mungu, bali ni *jinsi tulivyo*. Tukiwa kama uzao wa Adam tumetengwa na Mungu. Hatujatengwa katika maisha haya ya dunia tu, bali kama Bibla inavyotambia tumetengwa milele na hatima yetu ni kuishi bila uwepo na upendo wa Mungu milele. Hii inaitwa Jehanam. Tunahitaji Mungu atutendee yale aliyomtendea Adam na Hawa. Dhambi zetu zinahitaji kuhamishwa kupitia umwagikaji wa damu.

Mungu hataki hataki tuwe wa kidini, Lakini anataka tujue kuwa ametoa agano la damu kwa ajili yetu ili kwamba tuunganishwe naye. Hii ndiyo Injili; Hizi ni Habari Njema!

Mungu alipanga, kabla ya wakati kuwepo, kuwe na njia ya mwanadamu kuunganishwa na Yeye tena.

Agano la damu ndio kitu pekee kinachoweza kubadilisha asili ya mtu ya kiroho. Aganao la damu litatupa kuzaliwa upya na kutupa utambulisho mpya wa kiroho. Agano la damu litamruhusu Mungu kuunganisha Roho Yake na Roho yetu na kurudi kwenye mpango alio kuwa nao kwa Adam; kuwa katika sura ya Mungu.

Hii hapa Habari Njema. Mungu alikuumba ili uwe na ushirika na Yeye ili kwamba akubariki kwa utele Wake. Sasa Mungu, Muumba, anataka awe na agano la damu na wewe! Anataka achukue kila kitu ambacho ni kibaya katika maisha yako na akupe mema Yake yote na utele Wake.

Agano la damu ni nini?

Katika agano la damu kila upande unachukua utambulisho wa mwingine. ile kilichohitajika katika asili ya mwanadamu ni mtu aliye unganishwa na Mungu kabisa ili kwamba asili ya mwanadamu iweze kupata unganiko hilo. Tulihitaji mtu fulani ambaye roho yake iliunganika na Roho ya Mungu, mtu ambaye Roho ya Mungu ilikuwa inaishi ndani yake. Hata hivyo, mtu aliye unganishwa na Mungu itambidi aichukue asili ya mwanadamu, ya kuto kuunganishwa, na kupata mateso kwa ajili ya hukumu ya kutokuunganishwa.

Mpango wa Mungu ni Huu Hapa.

Kwanza tunahitaji kujua Yesu ni nani. Biblia inatuambia katika Yohana 1: 1-2 kwamba Yesu ni Mungu mwenyewe, kwamba Yeye ni Neno la Mungu, na kwamba Yeye ni Mwana wa Mungu ambaye aliviumba vyote kwa maneno Yake. Biblia inatuambia kuwa Mungu ana sura zingine; sura ya Baba na sura ya Roho

“Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyo mwanzo alikuwako kwa Mungu. Vyote vilifanyika kwa Huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika chochote kilicho fanyika” (Yohana 1: 1-3).

“Alikuwako ulimwenguni hata kwa yeye ulimwengu ulipata

kuwako, wala ulimwengu haukumtambua. Alikuwa kwake, wala walio wake hawakumpokea. Bali wote waliompokea aliwapa uwezo wa kufanyika watoto wa Mungu, ndiyo wale waliaminio jina lake; waliozaliwa, si kwa damu, wala si kwa mapenzi ya mwili, wala si kwa mapenzi ya mtu, bali kwa mapenzi ya Mungu. Naye Neno alifanyika mwili akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama mwana pekee atokaye kwa baba; amejaa neema na kweli”(Yohana 1: 10-14).

Neno la Mungu lililonenwa na malaika kwa Mariamu (Luka 1:26-38) lilisababisha unganiko la ki-Mungu na mwanadamu la Yesu kama mtoto katika tumbo la bikira wa ki Yahudi. Mungu alimuumba Adamu kwa Neno lake na pumzi yake (Mwanzo 1:28 & 2:7). Alisababisha Yesu kuingia ulimwenguni kwa njia ile ile. Mariamu alipata mimba kwa kupitia Neno la Mungu. Katika asili ya kuzaliwa huko, Yesu hakurithi asili ya Adamu (kutengwa na Mungu), lakini alikuwa mwanadamu. Muujiza wa namna gani! Yesu alikuwa ni mwanadamu wa kwanza kuzaliwa tangu Adamu bila kuwa katika uzao wa Adamu. Biblia inamwita Yesu Adamu wa pili. Yesu alikuwa uzao wa Adamu kwa sababu Mariamu alikuwa mama yake. Lakini hakuwa uzao wa Adamu kwa sababu Mungu alikuwa Baba Yake.

Huyu hapa mtu mkamilifu wakufanya naye agano. Tungeweza kuchukua asili yake kama angependa kuchukua asili yetu. Tatizo pekee ni: Je angekuwa tayari kuchukua asili yetu, Ile ya kutengwa na Mungu milele siyo duniani tu ila Jehanamu pia?

Habari nyingine nzuri hizi hapa. Mungu alitupenda sana kiasi kwamba Yuko tayari kulipa deni kwa ajili yetu. Yuko tayari kumtoa Mwanawe pekee atengwe Naye, Baba. Yesu kamwe hakufanya jambo lolote lililo nje na Baba Yake kama Adamu alivyofanya, japokuwa Shetani alimjaribu sana kufanya hivyo. Ilipofika wakati wa Yesu kufanya agano la damu na sisi, alikuwa ni mwanadamu sahihi aliyeweza kubadili asili na sisi. Watu walimsulubisha Yesu, kwa mateso ya kikatili yaliyowekwa kwa ajili ya waalifu wabaya. Yesu alimwaga damu Yake kama sehemu ya agano Lake.

Kile Yesu alichokisema kabla hajafa Msalabani kimeandikwa

katika Mathayo 27:46: “Na kama saa tisa, Yesu akapaza sauti yake kwa nguvu akasema, ‘Eloi, Eloi, lama sabakthani?... Yaani Mungu wangu, Mungu wangu, mbona umeniacha?’” Huu ni uthibitisho ambao Yesu aliuchukua kwa ajili ya asili yetu. Yesu alitengwa mbali na Mungu.

Yesu alienda Kuzimu. “Yeye mwenyewe akitangulia akayaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu” (Matendo 2:31). Yesu alishinda mauti Kuzimu na kaburi.

Yesu hakubaki amekufa; Alifufuliwa! “Hayupo hapa; kwani amefufuka kama alivyosema. Njooi, mpatazame mahali alipolazwa. Nanyi nendeni upesi, mkawaambie wanafunzi wake, Amefufuka katika wafu. Tazama awatangulia kwenda Galilaya; ndipo mtakapomuona, haya nimekwisha waambia.” (Mathayo 28:6,7)

“Hiyo ndiyo mara ya tatu ya Yesu kuonekana na wanafunzi wake baada ya kufufuka.” (Yohana 21:14).

Yesu hakufufuka tu; alipaa kwenda mbinguni kama mwanadamu. “Akisha kusema hayo, walipokuwa wakitazama, akainuliwa, wingu likampokea kutoka machoni pao. Walipokuwa wakikaza macho mbinguni, Yeye alipokuwa akienda zake, tazama, watu wawili wakisimama karibu nao, wenye nguo nyeupe, wakasema, Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyohiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni” (Matendo 1:9-11).

Yesu alituma Roho mtakatifu arudi duniani ili tuunganishwe tena na Mungu si katika maisha haya tu bali ya milele pia. “Kukaja ghafla toka mbinguni uvumi kama uvumi wa upepo wa nguvu ukiendakasi, ukaijaza nyumba yote waliokuwa wameketi. Kukawatokea ndimi zilizogawanyika kama ndimi za moto uliowakalia kila mmoja wao. Wote wakajazwa Roho Mtakatifu, wakaanza kusema kwa lugha nyingine, kama Roho alivyowajalia kutamka” (Matendo 2:2-4).

Hatimaye, Mungu alirudi ndani ya mwanadamu ili kuishi ndani yake kama alivyofanya kwa Adam. Hata hivyo, wakati huu Roho wa Mungu alikuwa na ubora mpya; ule wa kufufuka kutoka kwa wafu. Shetani hakuwa na utawala tena juu ya mwanadamu, lakini sasa mwanadamu

anamtawala yeye.

Kwa utimilifu wa mpango huu, asili ya mwanadamu imefanyika kuwa jambo kuu zaidi kuliko Adam wa kwanza. Tunayo maisha ya kufufuka kwa Yesu yanayo kaa ndani yetu. Tumeunganishwa na Mbingu nasi tu washindi juu ya mambo yote ya Shetani wakati tunaishi duniani. Mungu hajatuahidi maisha ya starehe, bali ametuahidi uwezo wa kushinda katika hali yoyote ile. Ametuahidi furaha, amani, upendo, imani na malengo katika maisha. Ametuahidi kwamba hatatuacha kamwe. Ametuahidi uhusiano wa karibu, wa kiundani na kibinafsi na Yeye. Ameyafanya maisha ya hapa duniani yawe yanastahili kuishi!

Hatulazimiki kuyaelewa haya yote ki akili. Mtu wa kidini sana aliyeshi nyakati za Yesu aliyelitwa Nikodemu hakuweza kuyaelewa mambo yote kwa akili yake. Yesu alikuwa na jibu kwa ajili yake na kwa ajili yako na mimi. Yesu alinena na Nikodemo kuhusu habari ya Agano la Damu.

“Basi palikuwa na mtu mmoja wa mafarisayo, jina lake Nikodemo, Mkuu wa wayahudi. Huyu alimjia usiku, akamwambia, ‘Rabi, twajua yakuwa umwalimu, umetoka kwa Mungu; kwa maana hakuna mtu awezaye kuzifanya ishara hizi uzifanyazo wewe, isipokuwa Mungu yu pamoja naye’. Yesu akajibu, akamwambia, ‘amin, amin, nakwambia, mtu asipozaliwa mara ya pili, hawezi kuuona ufalme wa Mungu.’ Nikodemo akamwambia, ‘awezaje mtu kuzaliwa akiwa mzee? Aweza kuingia tumboni mwa mamaye mara ya pili akazaliwa?’ Yesu akajibu, ‘amin, amin, nakwambia, mtu asipozaliwa kwa maji na kwa Roho, hawezi kuingia ufalme wa Mungu. Kilichozaliwa kwa mwili ni mwili; na kilichozaliwa kwa Roho ni Roho. Usistaajabu kwa kuwa nilikwambia, hamna budi kuzaliwa mara ya pili. Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho.’ Nikodemo akajibu, akamwambia, ‘yawezaje kuwa mambo haya?’ Yesu akajibu akamwambia, ‘Je! Wewe u mwalimu wa Israeli, na mambo haya uyafahamu? Amin, amin, nakwambia kwamba, lile tulijualo twalinena, na lile tuliloliona twalishuhudia; wala ushuhuda wetu hamuukubali. Ikiwa nimewaambia mambo ya duniani, wala hamsadiki, mtasadiki wapi niwaambiapo mambo ya mbinguni? Wala hakuna mtu

aliyepaa mbinguni, ila yeye aliyeshuka kutoka mbinguni, yaani, Mwana wa Adam. Na kama vile Musa alivyomwinua yule nyoka jangwani, vivyo hivyo Mwana wa Adamu hana budi kuinuliwa; ili kila aaminiye awe na uzima wa milele. Kwa maana jinsi hii Mungu aliuoenda ulimwengu, hata akamtoa mwanawe pekee ili kila mtu amwaminiye asipotee bali awe na uzima wa mielele. Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye” (Yohana 3:1-17).

“Miungu mingine” yote haikupendi.

Wanatabia ya ubinafsi, ya kujitafutia mambo yao wenyewe dhidi yako. Lakini Mungu, Muumbaji, analo pendo kamili juu yako. Anakupenda kwa hisia kali, kwa upendo usio na masharti, usio wa kibinafsi. Anataka yaliyo bora zaidi kwa ajili yako. Alimuweka Mwanawe Yesu Msalabani badala yako. Unaweza kumwamini!

Unatakiwa kufanya nini ili upokee muujiza huu mkuu wa Agano la damu?

Kwanza, uwe wa asili. Lazima uwe halisi! Usiwe bandia. Kuwa mkweli kwa Mungu kuhusu mashaka yako, hofu na mahitaji yako. Yesu ni Kweli. Roho Mtakatifu ni Roho wa Kweli. Mungu anatengeneza njia salama ya wewe kuamini. Lazima uuamini ukweli kwamba Amemuweka Mwanawe Yesu Msalabani badala yako.

Mambo mawili ya kuhitimisha yanapatikana katika Warumi 10:9-11 inayosema, “Kwa sababu ukimkiri Yesu kwa kinywa chako ya kuwa ni Bwana, na kuamini moyoni mwako ya kuwa Mungu alimfufua katika wafu, utaokoka. Kwa maana kwa moyo mtu uamini hata kupata haki, na kwa kinywa hukiri hata kupata wokovu. Kwa maana andiko la nena, 'kila amwaminiye hatatahayarika.’”

Lazima ujue moyoni mwako kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu. Ikiwa unalijua hili kama hadithi ya Biblia tu halitafanya kazi. Ukijjarisha imani ili ifanye kazi tu haitafanya kazi. Ni lazima ujue kwamba Yeye yu hai kwa sababu Amejidhihirisha Mwenyewe kwako.

Mara unapojua kwamba Yesu alifufuka kutoka kwa wafu na

sasa yuko hai, Ni lazima Umfanye Bwana. “Bwana” ni neno la zamani lenye maana “Mkuu” au “bwana mkubwa”. Huwezi kununua kuzaliwa upya kwako lakini baada tu ya kupokea, Lazima ugundue kwamba wewe ni mali ya Mungu na huwezi kamwe kujitegemea mwenyewe kama Adam alivyotaribu kufanya. Kumfanya Yesu kuwa Bwana inamaanisha kwamba lazima kugeuka kutoka kwenye “miungu mingine” kumwelekea Yeye, Katika Neno Lake, kwa mahitaji yako, kwa jinsi unavyotembea kwa utii mbele Zake. Tutalielezea hili kwa undani zaida katika sura zinazofuata.

Kama huna uhakika kuhusu mambo haya, hii ndiyo namna ya kuomba.

“Ee, Mungu, mimi nakutafuta. Ninataka kujua ukweli kuwa Wewe ni nani na kuhusu mambo ya kiroho. Nataka ujidhihirishe mwenyewe kwangu. Nataka Uniambaie jina lako. Nataka jambo hili likwe la kibinafsi sana, sio jambo lililotoka kwenye kitabu au kutoka kwa mwanadamu”. Sasa, mimina moyo wako kwa Mungu na umwambie ukweli kabisa unavyojisikia. Jumuisha mashaka yako, hofu, nk.

Kama unataka kuomba ili kupokea agano la Damu, unaweza kufanya sasa hivi.

“Ee, Mungu, Ninaamini kuwa ulimtuma Yesu ili kuchukua asili yangu ya zamani na ninataka kupokea asili Yake. Nataka kuzaliwa tena katika familia yako ili kwamba niweze kuunganishwa na wewe. Naamini kuwa Yesu alimwaga damu Yake kwa ajili yangu kama sehemu ya agano lake. Naamini kwamba Alipokufa Alichukua asili yangu ya zamani pamoja na deni langu. Ninaamini kwamba alifufuka kutoka wafu ili anipe maisha yake. Nilikubali agano hili kwa Kumfanya Yesu kuwa boshi wangu, Bwana wangu” (Hii ndiyo njia tunayomwaga damu yetu, kwa kuyaweka maisha yetu chini na Kumruhusu Yeye atawale. Hatuhitajiki kuikata miili yetu kabisa.)


Uwe Halisi Kwa Mungu, na Atakuwa halisi kwako.

Utamsikia Akisema,

“Habari, Jina Langu ni Yesu. Nakupenda.”

Sura ya 3 Ni Kitu Gani Kilichonitokea?

Baada ya kukutana na Yesu katika mwezi wa Nane mwaka 1979,



Nilijisikia kama nahitaji kujua ni kitu gani kilichonitokea. "kujisikia" sio msembo sahihi wa kuutumia hapa, Lakini nilijua kwamba nilijisikia tofauti. Nilijua kwamba kuna kitu kilichonitokea. Nilijua kwamba nilikutana na Muumbaji, Yesu. Nilijua kwamba Biblia ilikua sahihi 100% na Mungu ndiye aliye ongoza uandishi wake. Nilichokijua ndicho hicho tu. Yesu anapojidhihirisha kwako kupitia Neno Lake na kwa nguvu ya Roho Mtakatifu juu yako, matokeo ni maarifa yapitayo akili zote. Kukutana na Mungu kama nilivyokutana Naye hakuwezi kuelezeka ni lazima ikutokee mwenyewe.

Sikuwa "mtu wa kanisa," hivyo sikuwa na mapokeo ya "kuyafuta," sikuwa na haja ya kushinda mipaka ya kimadhehebu na kwakweli sikuwa na ubaguzi wowote. Nilikuwa wazi kabisa na nilikuwa sponji ya kiroho.

Nilikuwa na raha ya kuweza kukaa nyumbani juma lote la kwanza baada ya kukutana na Mungu ili niweze kusoma Agano Jipya. Nilipata nakala (Toleo la kijana) ambalo nilipewa miaka iliyopita. Nililisoma kwa masaa manne hadi matano kila siku. Nilijaza daftari langu kwa maswali kuhusu mambo niliyoyasoma. Kulikuwa na mengi sana ambayo sikuyaelewa.

Nakumbuka nilienda katika kanisa la karibu baada ya wiki mbili za kusoma Biblia na kumwambia mchungaji, "*Mungu ameniokoa!*" nilipokuwa nikiongea nilikuwa natetemeka na kulia sana bila kujizuia. Sikuwa na uhakika ni kitu gani alichofikiria. Hata mimi mwenyewe nilishtuka kwa sababu sikujua nini maana ya "kuokoka". Nilijua alishtuka na alikuwa na majibu machache mno. Nilichukua daftari langu kwenda kwa mtumishi huyu kila Jumanne na kukaa ofisini kwake ni kim-

bana kwa maswali yangu aliweza kujibu baadhi yake, lakini si yote. Alikuwa ni mtu mzuri na mshukuru Mungu kwa ajili yake!

Ninaandika sura hii kukusaidia uelewe kitu gani kilichokutokea kama Yesu amekuwa Bwana kwako.

Kwanza, nataka niweke msingi kwamba maisha yetu na Mungu si dini bali ni mahusiano. Mahusiano yanaweza yakaelezewa vizuri kati ya sehemu mbili zinazohusiana. Hivyo basi, nataka kusema kwamba wakati hakuna njia za mkato za kukuza uhusiano wako na Yesu, natumaini kwamba nilichogundua kitakusaidia kuongeza mwendo huo na kuusababisha uchanue na uzae matunda haraka iwezekanavyo.

Yesu anafafanua uhusiano wake kwetu kama hali ya kuwa na ukaribu wa kina ambao viumbe wawili wanaweza kuwa nao: "Mimi ni mzabibu; ninyi ni matawi, akaaye ndani yangu nami ndani yake, huyo uzaa sana; maana pasipo mimi ninyi hamuwezi kufanya neno lolote" (Yohana 15:5). Hakuna chochote kilichokaribu zaidi kupita mzabibu na matawi yake. Uhai wa mzabibu huhifadhi tawi. Hutegemeana mmoja kwa mwingine. Ni hali ya umoja. Soma Yohana 15 yote ili uweze kupata ufunuo juu ya hili.

Mwezi wangu wa kwanza katika kumjua Bwana, Nilimsikia mwinjilisti mmoja akisema "Yesu ni rafiki yangu mkubwa. Ni halisi zaidi kwangu kupita rafiki yangu wa karibu hapa duniani." Usemi huu ulinifanya niwe na njaa. Nilimwambia Mungu kama mtu huyu anaweza kuwa na haya hata mimi pia naweza. Nilimwomba kwa ajili ya hilo. Tumeahidiwa hili katika 2Wakorintho 13:14 ambayo inasema "Neema ya Bwana Yesu Kristo na pendo la Mungu, na ushirika wa Roho Mtakatifu ukae nanyi nyote. Amina." Hili ni jambo ambalo limenitokea tangu mwaka 1979. Mungu asifiwe kwa hilo!

Kama umekutana na Mungu na umemfanya Yesu kuwa Bwana, umepitia muujiza mkubwa ambao unaweza kumtokea mtu.

Umepitia kifo na kuzaliwa tena! Unaweza kusema, "Haionekani kama nimekufa na kuzaliwa tena." Hiyo ni kwa sababu kulikuwa na tendo lisiloonekana lililotokea; hataivyo, lilikuwa halisi zaidi kuliko lingetokea kimwili.

Yesu alimwambia Nikodemo, "Upepo huvuma upendako, na sauti yake waisikia, lakini hujui unakotoka wala unakokwenda; kadhalika na hali yake kila mtu aliyezaliwa kwa Roho" (Yohana 3:8). Hatuwezi kuuona upepo kwa macho yetu ila tunaweza kuutambua kwa milango mingine ya fahamu. Tunaweza kuona matokeo yake. Sasa unauhai mpya ndani yako na utaweza kutambua matokeo yake.

Kifo na kuzaliwa tena. "Hamfahamu ya kuwa sisi sote tuliobatizwa katika Kristo Yesu tulibatizwa katika mauti yake? Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wakfu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima. Kwa maana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwa mfano wa kufufuka kwake; mkijua neno hili, ya kuwa utu wetu wa kale ulisulibishwa pamoja naye, ili mwili wa dhambi ubatilike, tusitumikie dhambi tena; kwa kuwa yeye aliyekufa amehesabiwa haki mbali na dhambi. Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu"(Warumi 6:3-10).

Kanuni hii yaweza kulinganishwa na vizazi katika hali ya asili. Ulikuwa ndani ya baba na mama yako hata kabla hujazaliwa. Kama baba yako angekufa [kabla ya wakati], usingezaliwa kamwe. Kwa tukio hilo, ulikufa pamoja naye. Hata hivyo, ingekuwa baba yako angekufa na kufufuka kwa muujiza usio wa kawaida na kuingia katika utu upya, nawe pia ungeurithi utaratibu wote. Kwa hiyo, ulipozaliwa, ungechukuwa historia yote ya baba yako ya kufa na kuzaliwa tena.

Tito 3:5 inasema kwamba tunapitia kuzaliwa upya (fufua tena) kwa vitu viwili; Roho Mtakatifu na Neno la Kweli. Neno la Mungu ni mbegu. Soma Marko sura ya 4. Unapolisikia Neno la Mungu na kulipokea linachipuka ndani ya roho yako kama mbegu zichipukavyo kwenye udongo. "Kwa kuwa umezaliwa mara ya pili; si kwa mbegu iharibikayo bali ni kwa ile isiyoharibika; kwa neno la Mungu lenye uzima, lidumulo hata milele"(1Petro 1:23).

Msichana Mariam, mama yake Yesu, alipokea Neno la Mungu kutoka katika kinywa cha malaika, na akatunga mimba ya Yesu katika mwili. Tunalipokea Neno la Mungu na tunampokea Yesu katika roho zetu.

Tulipozaliwa tena au kufanywa upya tulimrithi Baba mpya. Tulibadilisha asili yetu.

Kamusi ya biblia ya W.E. Vine inalielezea neno la Kiyunani (moja kati ya tafsiri mbili) "baba" kama "Pater," kutoka katika mzizi unaomaanisha mrutubishaji, mlinzi, mwinuaji, mzazi aliye karibu sana, baba katika kizazi cha watu; mwanzilishi wa familia au kampuni ya watu waliowekwa pamoja kwa roho yake mwenyewe. Kufanywa upya imetoka katika maneno mawili: "palin" inayomaanisha tena, na "genesis" inayomaanisha kuzaliwa. Palingenis au kufanywa upya ni kumbadilisha Baba yako.

Tulibadilisha asili yetu. Tulimwitaji baba mpya katika kizazi cha watu. Tulimwitaji mwanzilishi wa familia au kampuni ya watu waliowekwa pamoja kwa roho yake mwenyewe Nilipoona maelezo hayo katika Kamusi ya Biblia ya W.E. Vine, ilinisisimua. Kama Mungu anakuwa Pater, basi katika kuingiza Roho Yake ndani ya miili yetu Roho yake inatuhisha. Hiyo inabadilisha asili yetu, urithi wetu, jinsi tunavyokuwa, asili yetu. Dunia ilifikiria na kuona kuwa ni ajabu katika miaka 1960, Huko Afrika Kusini, Kwamba mtu aliwekewa moyo mwingine. Je! wangepikiria nini kama wangeweza kufikiria juu ya KUWEKA UHAI UPYA?

Ujuzi huu ni zawadi ya jumla. Haujafanya kitu chochote kustahili hiki.

"Kwa maana mmeokolewa kwa neema, kwa njia ya imani; ambayo hiyo haikutokana na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu"(Waefeso 2:8,9) ikamate vizuri katika ufahamu wako. Hukufanya kitu kustahili zawadi hii ya ajabu ambayo Mungu amekukirimia. Hakuna mtu ambaye ni mwema vya kutosha kustahili uzima mpya. Hii ni zawadi tu. We si bora zaidi ya jirani au ndugu yako ambaye hajaokoka. Hukustahili zawadi hii. Neema ni

kupokea kitu ambacho hakikugharimu.

Kwa hiyo hii inatokeaje?

Mungu ameuweka Ulimwengu ili uzima uwe katika damu.

"Kwakuwa uhai wa mwili ukatika hiyo damu; nami nimewapa hiyo damu juu ya madhabahu ili kufanya upatanisho juu ya nafsi zenu; kwani hiyo damu ifanyayo upatanisho kwa sababu ya nafsi"(Mambo Ya Walawi 17:11). Agano la damu ni mabadilishano ya maisha kati ya watu wawili wanao husika. Yesu na wewe " kila mmoja alikunywa damu ya mwingine" na kubadilishana asili. Alifanya tendo la kunywa damu yako katika bustani ya Gethsemane Alipozibeba dhambi zako, na kumwaga damu yake kwa kupenda katika msalaba wa Golgotha

"Unakunywa" damu Yake unaposhiriki na kupokea Neno la Ahadi. Bahati nzuri kuzaliwa kwetu upya hakukuhitaji wewe kunywa damu kwa jinsi ya kimwili (Biblia imekataza hilo) "Roho ndiyo itiayo uzima, mwili haufai kitu; maneno hayo niliyowaambia ni roho tena ni uzima "(Yohana 6:63). Kwa hiyo ni Neno la Mungu ambalo linafanya kazi ya kuhamisha Agano la Damu.

Jambo hili ni zuri! Yesu alichukua asili yako na wewe ulichukua asili Yake. Hiyo ni sababu ya tukio la kuzaliwa na bikira lilitokea. Mtu hurithi damu kutoka kwa baba yake. Baba wa Yesu ni Mungu mwenyewe. Alipokea damu ya Mungu kama Adamu alivyopokea. Yesu ni Adamu wa mwisho.

"Hata imekuwa, mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; ya kale yamepita tazama! Yamekuwa mapya" (2Wakorintho 5:17). Neno lilitumika hapa la "kiumbe kipya" kwa ukweli linamaanisha aina ya kiumbe ambaye hajawahi kutokea kabisa. Hii sio kama muundo mpya wa gari la zamani, lakini badala yake ni kama muundo mpya wa gari ambao haujawahi kutokea kabisa.

Vipi kuhusu muda?

Hatukuwepo pale miaka 2000 iliyopita Yesu alipomwaga damu Yake.

Ukweli mmojawapo wa kuuweka katika ufahamu unapotafakari mambo ya Mungu ni Anaishi katika umilele. Milele sio muda mrefu, ni kupitiliza wakati. Mungu ana vipimo tofauti vya nyakati. Sisi

tuna kipimo kimoja tu. Mungu ana vipimo tofauti vya nafasi na sisi tunavyo vitatu tu. Mungu yupo katika wakati uliopita, uliopo na ujao zote katika wakati mmoja. Hivyo basi, haijalishi unaishi katika wakati gani, Roho wa Mungu wa milele atakuchukua kukurudisha mpaka siku ile Yesu alipoteswa hadi akafa juu ya Msalaba wa Kalivari.

Andiko moja linalofafanua hili ni katika Waebrania 9:14 isemayo "Basi si zaidi damu yake Kristo, ambaye kwamba kwa Roho wa **milele** alijitoa nafsi yake kwa Mungu kuwa sadaka isiyo na mawaa, itawasafisha dhamiri zenu na matendo machafu, mpate kumwabudu Mungu aliye hai!"

Kwahiyo unaweza ukakubaliana na andilo lisemalo " Nimesulubiwa pamoja na Kristo, lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Kama umekuwa ukiabudu mababu au maroho mengine, utakuwa umegundua msingi wa kweli. Ulimwengu wa roho ni halisi. Maroho hujishughulisha kuonekana kwamba zinatenda kazi katika maisha yako. Sasa changamoto yako ni kubadilisha familia yako kwa Agano la Damu ili kwamba urithi mambo ya Mungu, Muumbaji. Mungu anataka kukubariki! Kizuri ambacho "miungu wengine" wanachoweza kukufanyia ni kuleta laana katika maisha yako tu. "Huzuni zao zitaongezeka wambadilio Mungu kwa mwingine; sitazimimina sadaka zao za damu wala kuyataja majina yao mdomoni mwangu" (Zaburi 16:4).

Ni faida gani tunayoipata?

Faida bora kuliko zote na muhimu kupita zote ni kwamba sasa unao uzima wa milele. Utakaa na Mungu Mbinguni milele na hauta tunganishwa na Mungu, ambako huko huitwa jehanam. Adui wa mwanadamu aliye mkubwa kuliko wote ambaye ameshindwa katika maisha yako ni mauti! Kila mtu anaishi milele mahali fulani. Kama mwamini na kiumbe kipya utaishi Mbinguni milele.

"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminie mimi, ajapo kufa, atakuwa anaishi,'" (Yohana 11:25).

"Kwa kuwa mapenzi yake Baba yangu ni haya, ya kwamba kila

amtazamaye Mwana na kumwamini Yeye, awe na uzima wa milele; nami nitamfufua siku ya mwisho" (Yohana 6:40).

"Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mnamakao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi muwepo" (Yohana 14:1-3).

Ingawaje, Uzima wa milele ni zaidi ya kuishi milele. Yohana 17:3 inaelezea uzima wa milele kama ubora wa maisha unayoishi ungali unaishi duniani. "Na uzima wa milele ndiyo huu, wakujue wewe, Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliyemtuma" (Yohana 17:3). Neno "jua" ni neno muhimu sana. Linabeba wazo la ukaribu sana. Tunaweza kuwa na uhusiano wa karibu sana na Mungu sio baada ya kufa tu, bali zaidi sana wakati huu tungali tunaishi duniani.

Maombi.

"Yesu, Nataka kukwambia ni jinsi gani ninafurahia zawadi hii uliyonipatia. Asante, sana, kwa kunipatia maisha mapya, umenipatia uzima mwingine. Asante kwa kunipatia Roho Mtakatifu. Asante kwa kufanya uwezekano wa ushirika wa karibu kati yangu na Wewe kama mzababu na matawi yake. Asante kwa gharama ambayo ulipenda kuilipa ili mimi nipate zawadi hii. Asante kwa upendo Uliopita kiasi Ulioumwaga kwa ajili yangu, ukinijusha jinsi ninavyo stahili na jinsi nilivyo na thamani. Yesu, nataka kurudisha upendo kwa kuyatoa maisha yangu yote Kwako."

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, jina langu ni Yesu. Nakupenda."

Sura ya 4 Ni Mungu Gani Huyu Uliyekutana Naye?



Kama mtu angejaza vitabu vyote duniani bado kusingekuwa na nafasi ya kutosha ya kumwelezea jinsi Mungu alivyo. Hakuna mwanadamu yoyote anayeweza kumwelezea jinsi Mungu Alivyo. Wanadamu wamejaribu, lakini hicho ni kujivuna tu kwasababu Mungu ndiye aliyewaumba. Kiumbe hakiwezi kuelezea muumbaji wake.

Mungu hutufunulia mambo muhimu yanayo muhusu Yeye.

Tunahitaji kujua, ingawaje, Hajawahi kuacha kujifunua kwetu na hata achakamwe. Wakati wote kuna jambo jipya la kujifunza kumuhusu Yeye. Tunajifunza kumuhusu Yeye kupitia ushirika tulionao pamoja na Yeye, ana kwa ana.

Kuna baadhi ya mambo ninayoweza kuanza kuelezea ili kuanzishia. Baada ya kuyasoma haya, yapeleke kwenye maombi na muombe Mungu Ajifunue kwako binafsi.

Kitu cha kwanza tunachohitaji kujua kumuhusu Mungu ni hiki Yeye ni Muumbaji! Nilipo kutana na Yesu kwa mara ya kwanza mwaka 1979, Nilikuwa nikiwaambia watu kuwa nimekutana na Mungu Ambaye Ameumba ulimwengu! Nilikuwa na hakikisha kuwa nimeisema kwa jinsi hiyo. Inawezekana ikawepo "miungu wengine." Wanadamu wamefanya kazi nzuri ya kufanya miungu kwa mfano wake. Lakini kuna Muumbaji mmoja tu! Muumbaji ndiyo Huyu uliyekutana Naye.

Sio kwamba Yeye ni Muumbaji tu, bali katika Yeye, vitu vyote vinakuwako na vinashikiliwa pamoja.

Wakolosai 1:16-17 inasema, "Kwakuwa katika Yeye vitu vyote viliumbwa, vilivyo Mbinguni na vilivyo juu ya nchi, vinavyoonekana na visivyoonekana; ikiwa ni vitu vya enzi au usultani, au enzi, au mamlaka;

vitu vyote viliumbwa kwa njia Yake, na kwa ajili Yake. Naye Amekuwa kabla ya vitu vyote, na vitu vyote hushikana katika Yeye.

Waebrania 11:3 inasema, "Kwa imani twafahamu ya kuwa ulimwengu uliumbwa kwa Neno la Mungu, hata vitu vinavyoonekana havikufanywa kwa vitu vilivyo dhahiri."

Waebrania 1:2&3b (Tafsiri iliyo fafanuliwa zaidi) inasema, "Bali mwisho wa siku hizi Amesema na sisi kupitia Mwana, Aliyemweka kuwa mrithi na mmiliki halali wa vitu vyote, tena kwa Yeye na katika Yeye aliiumba dunia na utajiri wa nyakati, enzi ambazo Ameziumba, Amezitengeneza, Amezijenga, amezifanyia kazi na kuzipanga katika mpango kamili.[Mstr3b]... Akauchukua na kuuhifadhi kuulinda na kuuendesha ulimwengu wote kwa amri ya uweza wa Neno Lake."

Hizi ni sifa nyingine za Mungu. Kwa hakika hizi sio sifa zote au hazijakamilika, bali ni mahali pa kuanzia. Ninakushauri sana kwamba uangalie Maandiko katika Biblia yako na umwombe Mungu Ajidhihirishe mwenyewe kwako. Anapo nena nawe mashaka hutoroka!

1. Yeye Hakuumbwa na ni wa milele (Yohana 1:1-3 na Mwanzo 21:33)

2. Yeye ni mwenye nguvu zote. (Luka 1:37)

3. Yeye huyajua yote. (Zaburi 147:5)

4. Yeye yupo milele yote. (Yeremia 23:23-24)

5. Yeye ni kiumbe wa roho. (Yohana 4:24)

6. Yeye ni utatu, watatu katika mmoja. Mungu Baba, Mwana, Roho Mtakatifu (Mathayo 3:16-17, Yohana 1:1-14, 14:9-20)

Nakumbuka jinsi nilivyokuwa nasumbuka juu ya hili katika miezi ya kwanza baada ya kumjua Bwana. Ghafla, siku moja *nikajua*. Maswali yangu yakakoma. Kuna somo zuri katika ISOB ² mtiririko wa masomo kuhusu Utatu. Inaelezea somo kama, "Kwanini Mungu anataka kuwa na Utatu?"

² International School of the Bible Curriculum inapatikana bure katika www.isob-bible.org, au unaweza kutuma barua pepe kwenye info@isob-bible.org.

Utatu ni suala ambalo haliwezi kueleweka katika ufahamu wa mwanadamu wenyewe. Mungu lazima alidhihirishe hili kwako binafsi. Hatuna Mungu watatu waliogawanyika; lakini kila nafasi ya Mungu ina utendaji tofauti. Baba ndiyo chanzo cha mawazo na mipango, Yesu ni Neno linaloyanena, na Roho Mtakatifu ndiye anayetokeleza maagizo. Yesu ni Mwana wa Mungu pia. Yesu alifanyika mwanadamu akachukua dhambi zetu na asili ya dhambi zetu na kuzipeleka msalabani kwaajili yetu.

Ninaelewa kwanini wasioamini hupinga suala zima la Utatu Mtakatifu. Nimepata shutuma kutoka kwa wamomoni na wengine kwaajili ya kuamini ukweli huu. Hata hivyo, kama upotayari kabisa kujua kweli, mwombe Mungu, kisha rudi nyuma, Mtazame akinena na wewe.

7. Yeye hana kikomo. (Isaya 40:12-13)

8. Asili Yake ni upendo. (Waefeso 2:1-7, 1Yohana 4:9-10)

Mungu *hana* upendo, Yeye Ni pendo. Mungu anatupenda sisi na upendo usio na kipimo. Upendo wake hautegemei kwamba sisi ni wazuri au wabaya kiasi gani. Alitupenda ngali tu wafu dhambini, Mtu mfu hawezi kufanya lolote isipokuwa kupokea uzima! Wanadamu hupenda wakiwa na vigezo. Kwa mfano, "Kama wewe ni mzuri vyakutosha, au unayafanya ninayokuambia, basi hapo nitakupenda." Sio Mungu! Anapenda kwa kuwa Yeye Ni pendo. Huo unaitwa AGAPE, ukiwa na maana ya hakuna kipimo au sababu.

9. Tabia Yake ni tunda la Roho lililo elezwa katika wagalatia 5: 22-23 inayosema, "Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole kiasi; juu ya mambo kama hayo hanna sheria."

10. Yeye habadiliki kamwe. Matendo Yake huwa hayawi moto au baridi kama matendo ya wanadamu. (Waebrania 13:8)

Yakobo 1:17 inaelezea kivuli cha kugeukageuka kinachofuata jua liendako wakati wa mchana. Lakini Yakobo anamuelezea Yesu, kwamba Kwake hakuna kivuli kinachogeukageuka. Kwa maneno mengine, Yeye hung'aa wakati wote kama jua la mchana! Unaweza Kumtegemea.

11. *Yesu ni Neno. Yesu ni Mungu mwenyewe pia.* "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, Naye Neno alikuwako kwa Mungu, Naye Neno Alikuwa Mungu. Huyu Neno alikuwako kwa Mungu, Vyote vilifanyika

katika kwa huyo; wala pasipo Yeye haikufanyika chochote kilichofanyika. Ndani yake ndimo ulimokuwa uzima, nao uleuzima ulikuwa Nuru ya watu" (Yohana 1:1-4). "Naye Neno alifanyika mwili, akakaa kwetu; nasi tukauona utukufu wake, utukufu kama wa Mwana pekee atokaye kwa Baba; Amejaa neema na kweli" (Yohana 1:14).

Huu ndio mstari unaotenganisha kati ya Ukristo na mambo mengine yote: Yesu ni Mungu na ni mwanadamu. Yeye ni Mungu aliyedhihirika kama uumbaji Wake, mwanadam. Ikiwa bado hauko tayari kwa ajili ya hilo, kuwa mkweli kwa Mungu naye atajidhihirisha kwako.

12. Yesu alizaliwa na bikira. (Luka 1:26-38) Warumi 1:3-4 inasema kwamba: "Yaani, habari za Mwanawe, aliyezaliwa katika ukoo wa Daudi kwa jinsi ya mwili, na kudhihirishwa kwa uweza kuwa Mwana wa Mungu, kwa jinsi ya roho ya Utakatifu, kwa ufufuo wa wafu, Yesu Kristo Bwana wetu." Je fikiria kama ungeweza kumuuliza kijana Yesu, wazazi wako ni akina nani? Yesu angeweza kusema, "Aaa unaona upande wa mama yangu, nimetokea katika familia ya Daudi, lakini upande wa baba yangu, MIMI NDIMI."

13. Roho Mtakatifu ni Mungu. (Yohana 14:16-23, Yohana 16:7-15)

14. Bora zaidi ya yote, Mungu ni pendo! Anakujali zaidi ya unavyojijali, zaidi ya wazazi wako na familia yako wanavyokujali.

15. Mungu anaishi katika umilele na sio katika wakati. Milele siyo wakati mrefu, bali inapitiliza wakati. Mungu anajua kwanzia mwanzo hadi mwisho na kuanzia mwisho hadi mwanzo.

16. Mungu hashindwi na maadui zake, wala na maadui zetu. Wakati mwingine, tunajiuliza kama ni kweli Mungu ndiye anaye tawala tunapoitazama dunia hii na kuyatazama maisha yetu. Tunaweza kusema, "Kama Mungu ndiye anayetawala, basi kwanini kuna mateso mengi?" Au, "Kwa nini mambo mabaya yanawatokea watu wema?" "Mimi ni Mkristo sasa, kwanini maisha yangu hayawi bora?"

Zaburi 2:1- 4 inasema, "Mbona mataifa wanafanya ghasia, na makabila wanatafakari ubatili? Wafalme wa dunia wanajipanga, na wakuu wanafanya shauri pamoja, juu ya BWANA, na juu ya mpakwa mafuta wake, 'na tuvipasue vifungo vyao, na kuzitupia mbali nasi kamba zao.'

Yeye aketiye mbinguni anacheka, Bwana anawafanyia dhihaka."

Jambo moja ambalo ni gumu zaidi kwa watu wengi kuamini ni kwamba kweli Mungu anatawala dunia na maisha yetu. Mambo mabaya yanayotokea katika dunia hii hayatokei kwasababu Mungu anabonyeza kizibo kinachosema "mabaya." Mambo mabaya yanatokea kwasababu Mungu aliwapa wanadam uchaguzi wa hiari ambao hatakiuka. Hata hivyo, tazama Maandiko hapo juu katika Zaburi 2:1-4. Pia, tazama katika Warumi 8:28 ambayo inasema, "Nasi twajua ya kuwa katika mambo yote Mungu hufanya kazi pamoja na wale wampendao katika kuwapatia mema, yaani, wale walioitwa kwa kusudi lake." Kama Yesu ni Bwana wako, basi hata "mambo mabaya" yatatenda kazi kwa faida yako.

Hata watu waovu na mapepo ambao ni maadui wa Mungu wanatengeneza mipango kwa ajili yake. Zaburi 33:10 inasema, "BWANA huyabatilisha mashauri ya mataifa, huyatangua makusudi ya watu. Shauri la BWANA lasimama milele, makusudi ya moyo wake vizazi na vizazi."

Ikiwa bado unapata wakati mgumu na wazo hili, kumbuka tu kwamba tunaishi katika sayari ambayo iko vitani. Mungu alimpa Adam aitawale dunia na Adam akatoa mamlaka yake kwa adui wa Mungu Shetani. Yesu alikuja duniani na kuimarisha "himaya" au mahali pa salama dhidi ya adui kumkomboa mwanadam na dunia. Sasa Kanisa linaitwa kueneza ushindi huo duniani. Kwa kweli, Yesu alishinda msalabani, na sisi tunao ushindi kiroho, lakini ni juu yetu kueneza katika ulimwengu wetu unaotathiri. Mungu anayo misingi ya utawala katika historia iliyopita na wakati ujao. Hata hivyo sasa mwanadam anakipeo cha utawala kwasababu ya uchaguzi wa hiari ambao Mungu hata kiuka. Hiyo ndiyo sababu kuna mateso na maumivu duniani leo. Siku moja, dunia hii itafanywa upya na mateso kwa watoto wa Mungu yatakwisha. Ikiwa tutakwenda kuwa na Bwana kabla ya wakati huo, hapo ndipo mateso yetu yatakwisha. Wasiyoamini watakuwa hawana mwisho wa mateso!

17. Mungu ni Neno, na tunaweza kuliadini (Yeye). Kama kuna jambo moja ambalo Neno la Mungu linadiriki kufanya ambapo hakuna kitabu kingine duniani kinaweza kufanya, ni kutabiri wakati ujao kwa usahihi. Nimejifunza Biblia kwa bidii tangu 1979 na kujua kwamba ni kamilifu. Si dai kwamba ninaielwa yote, lakini ni kamilifu. Nimejifunza

unabii wa ki-Biblia kwa nguvu. Ni dhahiri kwamba Mungu aliivuvia Biblia na ni kamilifu. Unabii wa Biblia unathibitisha ukamilifu wake kwa kutoa vithibitisho ambavyo havina malumbano. Sababu pekee ambayo watu hawaamini hivyo vithibitisho ni kwasababu itawalazimu wamwite Yesu Bwana wao, na wengi sana hawako tayari kufanya hivyo.

Sura ya 9 ya kitabu hiki tutaingia kwa undani zaidi kuhusu unabii wa Kibiblia, ambao unatoa uhakika kamili bila shaka yoyote kuwa Mungu ndiye aliyechanzo cha kila neno katika Biblia na hilo ni sahihi kabisa.

18. Mungu anaweza kujulikana kibinafsi. Dini nyingi na hata madhebu ya Kikristo hawaamini kuwa Mungu anaweza kunena na kusikiwa na mwanadamu. Hawaamini kuwa Mungu anaweza kuwa rafiki yao wa karibu. Mungu anataka kuwa na ushirika na sisi. Moyo wake humuuma kwa kutaka kuwa na mazungumzo na sisi. Yesu anaelezea uzima wa milele ni kumjua Mungu. Neno "kujua" linamaanisha ushirika wa karibu. "Na uzima wa milele ndio huu, wakujue wewe Mungu wa pekee wa kweli, na Yesu Kristo uliye mtuma." (Yohana 17:3).

Yesu ni nani sasa?

Itakuwa ni vigumu kulijibu swali hili kikamilifu. Kitabu cha Waebrania, Waefeso, Ufunuo na vingine vinatupa majibu na kutuwezesha kuchungulia Mbinguni.

Katika Ufunuo sura ya 1 Yohana anamuona Yesu jinsi alivyo sasa! Yuko tofauti na wakati alivyomuona mara ya mwisho. Yeye ni Kristo aliye paa na kufunuliwa! Amefunuliwa kama mwaminifu, shahidi anaye aminika, Mzaliwa wa kwanza wa waliokufa, Mwana wa Wafalme wa dunia, Ajaye mapema, Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, na Mwenyezi Mwenye Uwezo wa Yote!

Kumbuka kuwa Yesu alikuwa ni Mungu aliyejidhihirisha katika mwili wa mwanadamu. Alikuwa ni Mungu wa yote, na wakati huo huo mwanadam! Alipouwawa, kwa kweli alikufa. Hata ivyo, kwa kuwa hakuwa na dhambi, Kuzimu haikuwa na madai juu yake. Hivyo basi Mungu Baba alimfufua. Alipofufuka kutoka wafu alikuwa amezaliwa tena kama kiumbe kipya, wakati huo huo akiwa mwanadam (mwanadam wa aina tofauti) na bado ni Mungu, Muumba. Sasa Yesu yuko Mbinguni

akiutawala ulimwengu. Bado Yeye ni Mungu, na wakati huo huo mwanadam!

Yeye ni zaidi ya mtawala. Yeye ni mtetezi wetu, au kwa kuliweka kwa namna nyingine, wakili wetu ambaye yuko pale kuhakikisha tunapokea urithi wetu. Kuna majina mengi ambayo amepewa kutokana na kazi Zake kama mwombezi, mtetezi, kuhani mkuu, nk.; hata hivyo, jambo rahisi la kukumbuka ni kwamba anataka sisi tupokee urithi wetu hapa Duniani, na Mbinguni, na atahakikisha kwamba hilo linatokea.

Anatembea nasi katika mioto na majaribu ya maisha. Anaturaji na kututia moyo. Yote haya yanafanywa kwa kupitia Roho Mtakatifu ambaye Alimwagiza achukue nafasi Yake.

Tunapokabiliana na matokeo ya dhambi, (siyo dhambi zetu tu, bali laana pia ambazo zimepitishwa na mababu zetu tukirudi nyuma yote hadi kwa Adam), Yesu yuko pale kuibeba adhabu yao halisi kwa ajili yetu, kama hati za kukunjua za maisha yetu zinapo kunjuka, mara zote Haondo hali za mambo mabaya, ila mara zote ataondoa mambo yanayodhuru katika hali mbaya. Siyo tu alichukua laana zetu miaka 2,000 iliyopita, bali yupo katika kazi ya kuwaondoa wale waliobaki ambao bado wanajaribu kutudhuru.

Yeye ni Mfalme ajaye upesi. Kama kuna jambo moja ambalo Yesu aliahidi tena na tena lilikua ni kwamba siku moja Yeye atarudi duniani. Hakutuambia muda na tarehe, bali amefanya kurudi kwake kwa mara ya pili kuwa ni jambo la uhakika.

"Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti" (1Wathesalonike 4:15).

"Yesu akamwambia, 'wewe umesema; lakini nawaambieni, tangu sasa mtamwona Mwana wa Adamu ameketi mkono wa kuume wa nguvu, akija juu ya mawingu ya mbinguni.'" (Mathayo 26:64).

"Wakasema, 'enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo, mlivyomwona akienda zake mbinguni.'" (Matendo 1:11).

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti yake.

"Habari, Jina langu ni yesu. Nakupenda."

Sura Ya 5 Mimi Ni Nani?



Wanadamu huenda mbali sana kwa ajili ya kujaribu kujitambua.

Tunavaa aina fulani ya nguo, tunaendesha magari ya aina fulani, tunachana nywele zetu katika namna fulani, tunakuwa na marafiki wa aina fulani, kuna mambo tunayopenda kufanya, na orodha inaendelea. Baadhi wanajaribu kutengeneza fedha nyingi, na wengine hutoa viapo vya umaskini. Wengine hujiunga na dini mbali mbali au kurithi mila za kifamilia. Tunakwenda kwa "miungu mingine" kutaka kujitambua.

Watu huruhusu watu wengine na matukio mbalimbali kuwaelezea utambulisho wao binafsi. Kama ukijifunza saikolojia ya mtumwa utagundua kuwa wanapata uthibitisho wao kwa jinsi wanavyo fanya mambo na jinsi wengine wanavyotoa uamuzi wa utendaji wao.

Wanasayansi wamegundua mambo ya kushangaza kuhusu tabia.

Mawimbi ya ubongo wetu yanaweza kufundishwa kufanya mambo kwa jinsi fulani. Haijalishi kama mazingira yanabadilika, Bado tutatenda katika namna ile ile. Huwa tunatengeneza mazoea kwa kufanya mambo kwamakisio kama siku ishirini na moja. Mazoea baadaye huumba tabia. Hivyo tunajikuta tunakuwa kama mtu tusiyotaka kuwa kwa kushindwa kufanya yale yatupasayo. Hatujui ni kwa jinsi gani tumekuwa hivyo.

Mtoto wa tembo hufundishwa kwa kufungwa kamba mguuni na kamba hiyo ikafungwa kwenye kisiki, Kama mtoto haiwezi kulegea hivyo humfanya atembe katika mduara. Mtoto huyo anapokua, ingewezekana

kiurahisi kung'oa kisiki kile, lakini hafanyi hivyo. Mtoto huyo hujihisi lile fundo la kamba hivyo ubongo wake humwambia bado amefungwa.

Hii ni katika uchunguzi, samaki waliwekwa katika kisanduku cha kufugia samaki pamoja na mawindo wayapendayo, baadhi yao ni samaki wadogo zaidi. Hata hivyo, samaki wadogo waliwekwa kwenye mifuko ya plastiki kiasi kwamba samaki wakubwa hawakuweza kuwapata. Hatimaye, samaki wakubwa wakakata tamaa. Hapo mambo yakabadilika. Samaki wadogo wakatolewa kwenye mifuko ile ili kuwa mawindo, mara nyingine wakaanza kuogelea katikati ya samaki wakubwa. Samaki hawa wakubwa walikua na njaa kali sana lakini walishawishika kuwa hawawezi kuwala samaki wadogo.

Wanadamu wako vivyo hivyo. Mawimbi ya ubongo wetu huambia kuwa sisi ni watumwa, wakushindwa, na chini ya nguvu za shetani na matatizo mbalimbali. Tunajisikia kuwa maisha yanatuchoma kama moto, tumepigwa na dhambi, na tunaishi na ufahamu unao endeshwa na dhambi. Kama tumekuwa tukiwatumikia "miungu wengine" wangetuacha katika hofu na kutokuwa na uhakika.

Hafla, Yesu ametupatia uzaliwa mpya; tumezaliwa upya na tumekuwa viumbe vipya ndani ya Kristo. Tunakutana na Mungu na tunaona, "Sasa tunalo kusudi, sasa tunajua kuwa sisi ni nani." Lakini suburi kidogo. Kikawaida siyo rahisi namna hiyo. Tumeumba mawimbi akilini mwetu na mazoea ambayo sio rahisi kuyabadilisha. Ni kweli kwamba tunayo asili mpya, bali katika ubongo wetu bado tunazo "kompyuta" ambazo zinahitaji kuwekewa programu mpya.

Katika Yohana 8:34, Yesu aliwaambia Wayahudi walio wakidini kwamba wao ni watumwa wa dhambi. Je aliwaona wakitenda dhambi? Inawezekana kuwa hakufanya hivyo. Hata hivyo, Yesu alijua kwa matendo yao tu kwamba walikuwa hawajiamini na hawajajithibitisha wenyewe zaidi ya watu wengine wanavyowafikiria. Huu ni utumwa halisi kwasababu huwezi kuwapendeza watu kamwe. Kusema kweli, watu unaojaribu kuwapendeza au kuwafurahisha mara nyingi hao ndio watakao kutawala na kukurubuni kwa hitaji lako la kutaka kukubalika.

Tumefundishwa sana jinsi ya kushindwa, kiasi kwamba Shetani anauwezo wa kutushinda. Ndipo Mungu huja na kutuambia anataka tuwe

huru! Anataka tujijue sisi ni nani! Anataka tujijue kweli! Yohana 8:31-32 inasema, "Basi Yesu akawaambia wale wayahudi alio mwamini, 'Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru.'"

Kujitambua wewe halisi.

Watu hutumia masaa mengi na maelfu ya dola kwa jitihada za kufuatilia vizazi vyao na mitiririko ya ukoo wao. Hakuna tatizo lolote juu ya hilo na inaweza kuwa ya msaada na yenye thamani. Hataivyo, kizazi kilicho bora zaidi unachohitaji kukifuatilia ni kile ambacho ni matokeo yako ya kuzaliwa mara ya pili na siyo kuzaliwa kwako kwa asili. Usijitafute wewe halisi katika sehemu ambazo siyo sahihi!

Ninawaona Wakristo walio wengi bado wanataabika kupata uthibitisho wao kwa kutumia njia zisizo sahihi. Niliteseka na hili kwa miaka. Mara zote nimekuwa mtu mwenye tabia ya utendaji, nikimaanisha kwamba nilipata uthibitisho wangu kutokana na jinsi nilivyotenda na jinsi watu wengine walivyofikiria kuhusu jinsi nilivyotenda.

Hatimaye, siku moja mwanzoni mwa mwaka 1990, Mungu alinena na mimi. Kwanza aliniuliza kama nimechoka. Hakika nilikuwa nimechoka. Kisha akanionyesha kitu ambacho kiliyabadilisha maisha yangu. Alinikumbusha katika Yohana 13 Alikwisha kuwaosha wanafunzi wake miguu, na kuosha miguu kwa kipindi hicho ilikuwa ni sawa na kusafisha choo kwa siku hizi.

Kwa mathalani, Aliniambia kwamba kama raisi wa Marekani angekuja nyumbani kwangu na kusafisha choo, Kituo cha habari cha CNN kinge hakikisha kinaonyesha habari hizo, siyo kwa sababu kusafisha choo ni jambo zuri sana au kwasababu mimi ni mtu maarufu, bali ni kwasababu raisi ndiye aliyekuwa anafanya hivyo.

Yesu aliniambia kwamba alifanya kitendo cha kuosha miguu kuwa ni kitendo cha kuheshimika tangu Alipokifanya. Sasa lilikuwa ni jambo jema la kufanya. Alileta heshima katika kitendo hicho kiurahisi tu kwasababu Yeye ni Mungu.

Kisha akanipa mfano kwamba Mungu, kwa kupitia Roho Mtakatifu alikuwa akiishi ndani yangu akiwa ameunganika na roho yangu. Kila

mahali nilipoenda nilileta heshima mahali hapo (kama Yesu alivyoleta heshima katika kuosha miguu) kwa sababu Mungu alikuwa anakuja katika sehemu hiyo ndani yangu. Alinikumbusha kuwa mawazo ya wengine juu yangu yasingenipa uthibitisho wangu au heshima.

Mungu alinipatia uthibitisho na nilipata fursa ya kuleta heshima popote pale nilipoenda. Aligeuza fikira zangu juu chini. Nilijuwa kuwa mimi ni chombo kinachombeba Mungu na sikuhitaji tena chanzo chochote kutoka nje kiniambie mimi ni nani. Huu ni uhuru!

Waamini wengi hawatambui ushindi maishani mwao kwa sababu mara zote wanajaribu kufanikisha baadhi ya malengo yao kwa Mungu. Njia ya ushindi ni kuugundua ushindi na kazi iliyomalizika pale Msalabani. Sisi *tayari* tunao ushindi, *tayari* tunayo haki, *tayari* sisi ni washindaji, lakini bado hatujaligundua hilo,

Tatizo ni kwamba watu hawajui jinsi Mungu alivyowafanya wawe kupitia kuzaliwa upya. Hawana uthibitisho wao wa kweli. Zaidi ya hilo hawawezi kufikiria kwamba Mungu amewafanya wenye haki kwa kupitia neema na imani na kwamba hawakuhusika na lolote. Ukristo siyo utendaji tu. Ni jinsi Mungu alivyokufanya wewe kuwa ndani ya Kristo, kwa imani, kwa neema; ilikuwa ni zawadi ya bure.

Jibu la kuelewa uthibitisho wetu ni kwamba fahamu zetu zinahitaji kufanywa upya. Tunapokutana na Mungu, tunapokea roho mpya. Mara moja tunafanywa wenye haki pamoja na Mungu. Miili yetu inapokufa mara moja tunakwenda kuwa na Bwana Mbinguni. Lakini kwa wakati huu tunazo nafsi ambazo bado hazijakamilishwa. Nafsi zetu zimefanywa kutokana na hiari yetu (utashi), ufahamu na hisia. Nafsi zetu huchukua muda wa maisha yetu yote kubadilika!

"Basi, ndugu zangu, nawasihi, kwa huruma zake Mungu, itoeni miili yenu iwe dhabihu iliyo hai, takatifu, ya kumpendeza Mungu, ndiyo ibada yenu yenye maana. Wala msiiifuatishe namna ya dunia hii bali mgeuzwe kwa kufanywa upya nia zenu, mapate kujua hakika mapenzi ya Mungu yaliyo mema, ya kumpendeza, na ukamilifu" (Warumi 12:1,2).

Vuta pumzi sasa hivi na ujione wewe u nani halisi katika macho ya Kweli. Neno la Mungu ni kweli pekee inayoelezea ukoo wako ili

kukujulisha kuwa wewe ni nani.

Neno la Mungu ni kitu pekee ambacho kinaweza kugeuza akili zetu kuelekea kwenye kweli! Jifunze na uzitafakari kweli hizi, kiri Maandiko, kaza nia kuziamini bila kujali hisia zako zinakuambia nini, hadi zifanye upya nia yako.

Ingawaje, hautaweza kamwe kugeuzwa nia yako kwa kweli ya Neno la Mungu mpaka pale utakapomtolea Mungu ukweli kuhusu wewe mwenyewe. Ni lazima ufungue "vyumba" ndani ya nafsi yako. Unafanya hili kwa urahisi kabisa kwa kuongea na Mungu kama rafiki yako wa karibu sana.. Mwambie kuhusu hisia zako, dhambi, fadhaa, kutokusamehe, hali zote za kushushwa moyo. Usifiche kitu! Hawezi kukuonyesha jinsi ulivyo katika Yeye, mpaka umwonyeshe jinsi ulivyo bila Yeye. Kushindwa kufanya hili kutakuweka kifungoni!

Tunapaswa kupata uthibitisho wetu wa kweli kutoka kwa Mungu kwa kupitia Neno la Lake. Ninakushauri ujifunze kisa katika Hesabu Sura ya 13 na 14 kuhusu Wana wa Israeli na wapelelezi kumi na mbili waliokwenda katika nchi ya ahadi (Imeelezewa pia katika kitabu hiki katika sura ya 14). Mungu aliwaahidi nchi ya ahadi. Ni wapelelezi wawili kati ya kumi na mbili, Yoshua na Kalebu ndio waliokuwa na imani ya kutosha katika Neno la Mungu kujiona wenyewe kama washindi dhidi ya maadui zao. Wale wengine kumi walisema, "Kisha huko tuliwaona Wanefili, (wana wa Anaki, waliotoka kwa hao Wafilisti) tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; na hao ndivyo walivyotuona sisi." (Hesabu 13:33).

Shetani hupanda mbegu ili kuzalisha mtazamo potofu ndani yetu.

Katika Mathayo 13:1-23 Yesu aliwaambia wanafunzi wake mfano kuhusu Neno la Mungu likiwa limepandwa ndani ya mioyo yao kama mbegu. Aliwaelezea jinsi linavyofanya kazi na jinsi Shetani anavyojaribu kulizuia lisifanye kazi. Kisha akaelezea kwamba Shetani hatajaribu kuiba Neno ndani ya mioyo yao tu lakini yeye (Shetani) pia ni mpanda mbegu.

"Akawatolea mfano mwingine, akisema, 'ufalme wa Mbinguni umefanana na mtu aliyepanda mbegu katika konde lake; lakini watu walipolala, akaja adui yake akapanda magugu katikati ya ngano, akaenda

zake" (Mathayo 13:24,25).

Zifuatazo ni kweli katika Neno ambazo unatakiwa kuzitafakari. Kweli hizi ni mbegu njema, ambazo zitazaa matunda mema katika maisha yako.

Ulipotea bila matumaini. Hiyo inamaanisha kwamba ilimbidi mtu mwingine akutafute. Waefeso 2:12 (a & b) inasema, "Kwamba zamani zile mlikuwa hamna Kristo... mlikuwa hamna tumaini, hamna Mungu duniani."

Ulikufa katika dhambi zako. Hakuna jinsi nyingine kwa mtu aliyekufa, isipokuwa kupokea uzima. Waefeso 2:1 inasema "Nanyi mlikuwa wafu kwa sababu ya makosa ya dhambi zenu."

Kumwagika kwa Damu ya Yesu Msalabani kulifanya zaidi ya kusamehe na kuondoa dhambi. Gundua katika maandiko kwamba tuna msamaha na ukombozi "KATIKA YEYE" Wakolosai 1:14 "Ambaye katika Yeye tunaukombozi, yaani msamaha wa Dhambi" Waefeso 1:7 "Katika Yeye huyo, kwa damu yake, tunao ukombozi wetu, masamaha ya dhambi, sawasawa na wingi wa neema Yake."

Asili yetu "msamaha" mara nyingi hueleweka vibaya. Wengi hujiona kuwa bado ni watu wale lakini Yesu ameondoa, "amewaombea msamaha" au amesamehe dhambi zao.

Sivyo! Ulisulubiwa na Kristo. Jambo la kwanza Mungu alilolifanya kwa ajili yako lilikuwa "kukuweka wewe" katika Kristo ili upitie kifo cha pamoja na yeye. Asili yako ya kwanza ya Ki-Adamu, "wewe wa kwanza," haikuwa na tumaini la kusafishwa. Ilikubidi ufe. Mshahara wa dhambi ni mauti. Habari njema ni kwamba ulikufa. Tayari ulikuwa "ndani ya Kristo" Aliposulubiwa; ulihitaji kuligundua kuliadini na kulikubali.

Tayari ulikuwa "ndani ya Kristo" wakati matukio haya yalipotokea.

Ulisulubiwa pamoja na Kristo. "Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu hai ndani yangu, na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya mwana wa Mungu,

ambaye alinipenda, akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu." (Wagalatia 2:20).

Ulikufa pamoja na Kristo

“Kwamaana kama mlivyounganika naye katika mfano wa mauti yake, kadhalika mtaunganika kwamfano wa kufufuka kwake”(Warumi 6:5)

Ulizikwa pamoja na Kristo. "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake" (Warumi 6:4). "Mkzikwa pamoja naye katika ubatizo" (Wakolosai 2:12). Kama unapata wakati mgumu kwa ajili ya uthibitisho, nakushauri ukariri Warumi 6. Kwa kufanya hivyo kulileta matokeo mazuri sana katika maisha yangu.

Ulifanywa hai pamoja na Kristo. "na ninyi mlipokuwa mmekufa kwa sababu ya makosa yenu na kutokutahiriwa kwa mwili wenu, aliwafanya hai pamoja naye, akisha kusamehe makosa yenu yote" (Wakolosai 2:13). "Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhisha pamoja na Kristo" (Waefeso 2:5).

Ulifufuka pamoja na Kristo. Umeketishwa pamoja na Kristo. "Hata wakati ule tulipokuwa wafu kwa sababu ya makosa yetu; alituhisha pamoja na Kristo; yaani tumeokolewa kwa neema. Akatufufua pamoja naye, akatuketisha pamoja naye katika ulimwengu wa roho katika Kristo Yesu." (Waefeso 2:5,6).

Huu ni msimamo wetu wa halali pamoja na Mungu leo na msingi wa haki zetu halali. Ulimwengu wa roho unaona kuwa, sehemu yako ni katika Kristo Mbinguni. Uko katika kiti cha mamlaka. Shetani na akili zako watakuambia kuwa haujaketishwa pamoja na Kristo Mbinguni, lakini huo ni uongo! Unahitaji kujua kwamba Mungu alikuketisha pamoja Naye ulipokuwa ungali mwenye dhambi!

Sasa wewe ni kiumbe kipya. " Hata imekuwa mtu akiwa ndani ya Kristo amekuwa kiumbe kipya; yakale yamepita na tazama,! Yamekuwa mapya" (2Wakorintho 5:17).

Unaweza kuuliza, Hili litawezekanaje? Swali zuri. Mungu ametuweka ndani ya Kristo. "Bali kwa Yeye ninyi mmepata kuwa katika Kristo Yesu, aliyefanywa kwetu hekima itokayo kwa Mungu, na haki, na utakatifu, na ukombozi" (1Wakorintho 1:30). Kuwa katika Kristo ni sawa na jinsi ulivyokuwa ndani ya baba yako na mama kama mbegu za kiumbe na yai. Umerithi historia katika mtiririko wa ukoo wako. Hebu fikiria

kuwa wewe ni kiweka alama ndani ya kitabu. Kitabu kikisogea, kiweka alama husogea nacho. Kitabu kikiwekwa juu ya kabati, kiweka alama huenda juu ya kabati. Kitabu kikichomwa kiweka alama nacho huchomwa. Kama kwa muujiza fulani kitabu kimerudishwa upya tena, hata kiweka alama nacho huwa hivyo hivyo.

Historia yako, na jinsi ndani ya Kristo ni matokeo ya Agano la Damu la Mungu kupitia kifo cha Yesu juu ya Msalaba na kufufuka kwake.

Wewe ni mwenye haki. Haki maana yake ni kuwa na msimamo sahihi na Mungu. Mtoto wa kiume (au wa kike) anakuwa na haki na baba yake kwa kuzaliwa. Yuko kwenye familia na anazo haki ambazo majirani hawako nazo. Sisi tuna haki kupitia kuzaliwa upya kwetu, sio kwa ajili ya kitu chochote tulichokifanya. "Yeye asiyejua dhambi alimfanya kuwa dhambi kwaajili yetu, ili sisi tupate kuwa haki ya Mungu katika Yeye" (2 Wakorintho 5:21). Tuna haki kwasababu Mungu ametuwekea uzima ndani yetu, sio kwa jinsi tunavyo tenda au tunavyoishi.

Utawala wa kishetani juu yako umevunjwa. Shetani alikuwa anauwezo wa kukutawala katika utu wako wa zamani, lakini utu wako mpya ni Roho wa Kristo ambaye alishamshinda shetani. Warumi 6: 8-10 inasema, "Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini yakuwa tutaishi pamoja naye; tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, *wala mauti haimtawali tena*, maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake amwishia Mungu" Kama roho ya dunia imekufanya uishi katika hofu, Mungu atakuweka huru *sasa hivi!*

Kwa sababu ya kuwa wewe ni nani ndani ya Kristo, "mambo mabaya" hayana nguvu juu yako tena. Badala yake, unazo nguvu juu yake na kuyabadilisha kuwa baraka. Wakolosai 1:20 inasema, "Na kwa Yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake."

Kwanini sijisikii kama maandiko haya yanavyosema?

Nimefurahi sana umeuliza. Swali hili ni lamuhimu sana. Itachukua miaka kwa wewe kuona mtazamo wa dunia na "miungu wengine" juu yako. Umefundishwa kuwa na hali ya kuhukumiwa na dhamiri, dhambi,

hofu na kuwa na hali ya laana, na itakuchukua muda kuweza kugeuza nia yako kuelekea kweli. Kutoka kwenye mtazamo wa shetani anajaribu kuiba mbegu za Neno kutoka kwenye moyo wako. Akiugandamiza kwenye matatizo yako vya kutosha na kuweka hukumu, unaweza ukaacha kuamini.

Kutoka kwenye mtazamo wa Mungu, anakujaribu. Anataka akuze tabia njema ndani yako. Sio aina ya majaribio ambayo waalimu huyatoa, faulu au feli, lakini kujaribu kama kulivyo hutumika katika kusafishia dhahabu. Neno jaribu maana yake ni weka katika moto na uunguze ili kutakasa. Mungu huvutiwa akiona uaminifu wako ukiwa kwenye majaribu; Anataka kujua kwamba utaendelea kuliadini Neno Lake hata kama mambo yako kinyume kabisa. Jinsi unavyoendelea kulitendea Neno kazi utapokea, na madhihirisho yataanza kuja.

Imani inathamani kuu mbele za Mungu. Imani kwa urahisi ni kuamini na kutegemea Neno la Mungu kwa kiwango ambacho utalikiri kwa kinywa chako na kulitenda litemwalo bila kujali ninini kinachoendelea katika maisha yako. "Basi Imani ni kuwa na hakika na mambo yatarajiwayo, ni bayana ya mambo yasiyoonekana" (Waebrania 11:1). "Lakini pasipo Imani haiwezekani kumpendeza; kwa maana yeye amwendeaye Mungu lazima aamini kuwa Yeye yuko, na kwamba huwapa thawabu wale wamtafutao" (Waebrania 1:6). "Maana twaenenda kwa Imani, si kwakuona" (2Wakorintho 5:7).

Imani katika Neno la Mungu ndiyo impendezayo Mungu. "Hata alipoingia Kapernaumu akida mmoja alimjia, akamsihi akisema, 'Bwana,' 'mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana.' Yesu akamwambia, 'nitakuja nimponye.' Yule akida akamjibu, akasema, 'Bwana, mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, 'Nenda,' huenda; na huyu, 'Njoo,' huja; na mtumwa wangu, 'fanya hivi,' hufanya.' Yesu aliposikia hayo alistaajabu, akawaambia wale waliomfuata, 'amin, nawaambieni, sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli'" (Mathayo 8:5-10).

Uthibitisho wa kwamba unaamini au la *haupo* katika hisia zako.

Kihakikisho ni kile kitokacho kinywani mwako kutokana na yale yaliyoujaza moyo wako. Laka 6:45 inasema, "Mtu mwema katika hazina njema ya moyo wake hutoa yaliyo mema, na mtu mwovu katika hazina yake mbovu hutoa yaliyo maovu; kwa kuwa mtu, kinywa chake *hunena* yale yaujazayo moyo wake." Kulinena Neno la Mungu kwa sauti mara kwa mara, sana sana maandiko yale yanayo fanana na jinsi ulivyo, kuna nguvu.

Njia pekee ya kushinda na kujiponya kutokana na dhambi, hofu, kujihukumu, mazoea mabaya, kujisikia kutokustahili, kujisikia kushindwa, nk., ni kukubaliana na kweli hizi. Tunapojua kwa kweli kwamba Mungu anatupenda na kwamba sisi ni mali Yake, na kwamba Ametufanya sisi kuwa kiumbe kipya na yakale yamepita, kwamba utu wetu mpya upo katika Kristo, na kwamba tumenunuliwa kutoka kwenye utumwa na tumepewa uchaguzi wa kweli kuchagua U-Bwana, mamlaka na utunzaji wa Mungu, sasa ndipo tunaanza kazi ya kuyashinda mambo yote mabaya katika maisha yetu.

Injili maana yake habari njema.

Habari njema ni kwamaba tulikuwa tumepotea bila matumaini na bila nguvu ya kuweza kujisaidia, Na Yesu Alikuwa na kutubadilisha tukawa kitu ambacho ni maalum sana. Hii ni Injili. Hili lina nguvu! "Kwa maana siionei haya Injili; kwamaana ni uweza wa Mungu uletao wokovu kwa kila aaminiye, kwa Myahudi kwanza na kwa Myunani pia" (Warumi 1:16).

Desturi za kidini zinazohubiri habari potofu ni mauti! "Naye ndiye alieye tutosheleza kuwa wahudumu wa Agano jipya; si maandiko bali wa roho; kwa maana andiko hua bali Roho huuisha" (2Wakorintho 3:6).

Nilipokuwa Mkristo mpya, Daktari Paulo Walker wa Kanisa la Mungu la Mountain Paran la Atlanta, Georgia, alikuwa akinijenga kila siku ya Jumapili asubuhi. Badala ya kuwahukumu watu na kwa udhaifu wao na dhambi zao, aliongelea Neema ya Mungu, pendo la Mungu, na alihubiri habari njema kwamba sisi tu nani katika Kristo. Mara zote angemaliza na neno la kutia moyo:

"Basi, tuseme nini juu ya hayo? Mungu Akiwa upande wetu nina aliye juu yetu?" (Warumi 8:31).

Sisi tu watu maalum kwasababu Mungu ametuumba sisi na kwasababu alitupa uzaliwa mpya ili kwamba aishi ndani yetu tena. Kwasababu ya uhalisi huu kwamba sisi ni vyombo vya Mungu kunatufanya tuwe maalum. "Lakini tuna hazina hii katika vyombo vya udongo, ili adhama kuu ya uwezo iwe ni ya Mungu, wala si kutoka kwetu" (2Wakorintho 4:7).

Usiwe kuku, wewe ni tai!

Siku moja, yai la tai lilianguka na kudondokea kwenye sehemu yenye mayai ya kuku. Lile yai la tai likatolewa kama yai la kuku, lakini alikuwa na tofauti jinsi alivyokuwa akikua. Hakuna aliyeweza kutambua kuwa yule hakuwa kuku, ila tai mwenyewe.

Dhoruba ilipokuja, yule tai alikimbilia kwenye nyumba ya kuku pamoja na kuku wengine, wakikimbilia sehemu ya usalama, lakini tai huangalia juu na kila upande, na aliwaona ndege hawa wa ajabu wakiwa bondeni. Hawakua na woga, wala hawakumbia. Walisimama na mbawa zao zikiwa zimewekwa kwenye mkao maalum (inawafanya wawe kama mbwawa zimeunganishwa kwenye kihunzi cha eroplani), wangekaza macho yao kuangalia dhoruba iliyokuwa inakuja hata kama iko umbali wa maili kadhaa. Wangesubiri na kusubiri na ghafla, puh! Dhoruba ingewapiga na badala ya kuwaumiza ilichokifanya ni kuwawezesha kupaa. Walienda moja kwa moja juu hewani, umbali wa futi 30,000 juu ya dhoruba kwenye hali ya hewa iliyo shwari. Sasa yule tai alijisemea moyoni mwake, "Aisee angalia wale jamaa, Natamani ningekua kama wao."

Siku moja liangali JUU, na alimwona tai akipaa juu na kupepea juu ya dhoruba. Ghafla akajua, "Mimi sio kuku, Mimi ni tai. Kwanini nikimbie?" Akapanda mlimani, akafungua mbawa zake, alipojiachia akaweza kupaa!

Rafiki yangu, wewe sio mwanadamu wa kawaida tu, wewe sio kuku. Umeumbwa ili upae katika mbingu pamoja na Kristo. Tazama juu!

Sasa kumbuka mfano wa mpanzi katika Marko 4 (soma). Shetani huja kuiba mbegu ya Neno la Mungu lililopandwa moyoni wako. Leo

mbegu ya wewe u nani imepandwa ndani yako. Kesho, simama imara kama mambo ya kukatisha tamaa yanapokuja kupitia shida mbalimbali. Neno li kweli! Matatizo huja na kuondoka.

Kusimama imara kunahitaji kuliadini Neno. Hauwezi kuliadini Neno la Mungu isipokuwa ulitafakari na kulisema mara kwa mara. "Potezea muda wako" kwenye Neno la Mungu na utashangazwa na matokeo yake.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

“Habari, jina langu ni Yesu. Nakupenda..”

Sura ya 6 Mauti imetanguliwa



Sasa, hizo ni habari njema zaidi
K uliko nilizowahi kuzisikia

Jambo ambalo lilinileta kwenye uchunguzi juu ya kweli ni mauti. Nilitaka kujua kuwa ninini kitakachonitokea mara baada ya kufa. Nilikuwa na hofu ya mauti, na hofu ya mambo yasiyojulikana.

Watu wananjia nyingi tofauti za kufunika hofu hizo. Ninasikia uongo wa kila aina kuwa watu wanategemea maisha yao baada ya kifo. Inaniumiza kuona watu wanadanganywa kiasi hicho. Nadharia zao nyingi zinasikika vizuri, lakini ni Neno la Mungu pekee linaloweza kutegemewa. Kama unategemea kitu kingine mbali na Neno la Mungu, basi inakubidi uwe na bidii kuchunguza kweli wewe mwenyewe kwani haujaahidiwa siku nyingine duniani!

Jambo lingine ambalo linanihuzunisha ni kwamba Wakristo wengi wanaogopa kifo. Hii inatakiwa kuwa hofu ya kwanza inayoondoka kama kweli umekutana na Yesu. Inawezekana kuwa haujawahi kupitia hali hii ya kuzaliwa upya, au labda hauja elekezwa kwenye Neno la Mungu.

Neno la Mungu linatoa msemo unaoshangaza sana kuhusu kifo. Linasema kuwa mauti imetanguliwa. Kutangua maana yake ni " Batili au kubatilika; kuharibu uhalali." Ni kama Mungu ameiweka mauti katika sehemu ya chini sana.

"Kwakusudi na neema ambayo sasa imedhihirishwa kwa kufunuliwa kwake Mwokozi wetu Kristo Yesu, *aliyebatili mauti*, na kuufunua uzima nakutokuharibika, kwa ile injili" (2Timotheo 1:10, tafsiri iliyochambuliwa zaidi).

Nilisafiri pamoja na familia yangu miaka kadhaa iliyopita na binamu wa mke wangu alikuwepo kwenye gari pamoja na sisi. Hakuwa

muumini. Nilisoma 2 timotheo 1:10, na niliipenda tafsiri iliyochambuliwa zaidi ambayo ilisema Yesu Alibatilisha mauti. Sikujua kuwa ndugu yangu alikuwa akifikiria jambo hilo hilo mpaka alipoanza kunishirikisha. Nikamweleza kwa urahisi kabisa yale niliyokua nikiyasoma asubuhi ile na jinsi Yesu alivyo nitoa kutoka kwenye hofu ya mauti. Miezi kadhaa baadaye niligundua kwamba alimpa Bwana maisha yake siku ile. Ndugu yangu anakwenda mbinguni kwasababu mauti imebatilishwa!

Tafsiri ya neno mauti iliyotumika katika agano jipya ni "kutenganisha" Mauti sio ukomo wa kuishi, ni utenganisho wa mwili huu wa kidunia (vazi letu la duniani) linalotengana na sisi, roho zetu na nafsi. Tutaishi mahali fulani milele. Mauti ya kiroho ni utenganisho wa roho zetu na Mungu. Mauti ya kiroho huanza hapa katika maisha ya kidunia na huendelea milele kama hatujazaliwa upya.

Ninaamini kuwa mauti kwa mwanadamu ni jambo la kutisha sana. Nimesikia shuhuda za kutosha kwa madaktari na wahudumu walio shuhudia hili. Na pia nimeshasikia hadithi za mambo yanayoendelea baada ya mauti. Hata hivyo, Ninaamini kuwa mwamini anapokufa, huwa hapitii hofu hizo na maumivu. Ninaamini kuwa mara kabla ya mauti kwa Mkristo, kwamba roho yake humtoka na kukutana na Yesu hewani, inafanana na "unyakuo" Waebrania 2:9 inasema kwamba Yesu alionja mauti kwaajili ya kila mmoja. Kuonja na neno zito. Hatuonji mauti kwasababu Yesu alishafanya hivyo kwaajili yetu.

"Ila twamwona yule aliyefanywa mdogo punde kuliko malaika, yaani Yesu, kwasababu ya maumivu ya mauti, amevikwa taji ya utukufu na heshima, ili kwa neema ya Mungu *aionje* mauti kwaajili ya kila mtu" (Waebrania 2:9).


Ninaamini kuwa tunapo tenganishwa kutoka kwenye mwili kupitia mauti, tunakuwa kwa wakati uleule katika uwepo wa Bwana. "Lakini tuna moyo mkuu; nasi tunaona niafadhali kutokuwako katika mwili na kukaa pamoja na Bwana" (2Wakorintho 5:8).

Ninaamini kuwa hili linasaidiwa kwa jinsi nyingine. Kama tumezaliwa upya, basi ni lazima kuwa tulisha kufa tayari. "Kwa maana kama mlivyonganika Naye katika mauti, kadhalika mtaunganika kwa

mfano wa kufufuko Kwake" (Warumi 6:5).

"Nimesulibiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo Yu hai ndani yangu; na uhai nilionao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, Ambaye alinipenda, Akajitoa nfsi Yake kwaajili yangu" (Wagalatia 2:20).

Ulipozaliwa mara ya pili uliwekwa
ndani ya Kristo



Haya ni baadhi ya Mandiko makuu ya kutafakari yanayoendana na uhuru kutokana na mauti.

"Kumcha BWANA ni chemchemi ya uzima, ili kuepukana na tanzi za mauti" (Mithali 14:27).

"Yesu akamwambia, 'Mimi ndimi huo ufufuo, na uzima. Yeye aniaminiye Mimi, ajapokufa atakuwa anaishi, naye kila aishiye na kuniamini hatakufa kabisa hata milele. Je! Unayasadiki hayo?'"(Yohana 11:25,26).

"Ambaye Yeye peke Yake hapatikani na mauti' amekaa katika nuru isiyoweza kuharibiwa;" (1Timotheo 6:16a Biblia iliyofafanuliwa)

"Ku wapi, Ewe mauti kushinda kwako? U wapi, Ewe mauti uchungu wako?" (1Wakorintho 15:55).

“Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa” (Waebrania 2:14-15 Toleo lililofafanuliwa).

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa isikilize sauti Yake.

“Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda.”

Sura ya 7 Yesu kama Bwana?



Hakuna mtu wakuniambia
nini cha kufanya

“Kwasababu, ukimkiri Yesu kwa kinywa chako yakuwa ni Bwana, na ukiaimini moyoni mwako yakuwa Mungu alimfufua, katika wafu, utaokoka”(Warumi 10:9). Hebu tambua kwamba haijasema kama ukiamini kwamba Yesu alikufa kwaajili ya dhambi zako utaokoka. Imesema kama ukiamini kwamba Alikufa na sasa Yuko hai, na katika "kuwa hai kwake" unamfanya kuwa Bwana wako.

"Kuokoka" ni Neno linalo maanisha kuhuishwa kabisa na kuokolewa kutokana na hatari. Hili halimaanishi tu uzaliwa upya, lakini linahusisha kazi endelevu ya Roho Mtakatifu akiponya na kuhuisha maeneo mbalimbali yaliyoharibiwa na kuhuisha maeneo ambayo bado yanakusababishia hatari.

Mwanadamu aliumbwa ili awe chini ya mamlaka ya mtu mwingine.

Ni uchaguzi wetu. Hatuwezi kuwa njia panda. Kama hatutaki kumfanya Yesu kuwa Bwana, mtu mwingine au kitu kisichofaa kitakuwa bwana wetu. Hatuna uchaguzi juu ya hili zaidi ya kumchagua mmoja au mwingine. Ninaweza kushuhudia kibinafsi juu ya hili na nimewaona watu wengi sana wakiangukia katika hatari hii.

Yesu aliwaambia wanfunzi wake kwamba swala hili la mamlaka lilikuwa likiwachanganya. Aliwaambia kwamba katika ulimwengu wa mataifa (watu wasio na Mungu) mamlaka maana yake ni "ubwana" juu yao kwanjia ya ukali sana. Yesu aliwaeleza kuwa mamlaka ni kutumikia wengine. "Yesu akawaita akawaambia, 'Mwajua kuwa wale wanaohesabiwa kuwa wakuu wa mataifa huwatawala kwa nguvu, na wakubwa wao huwatumikisha. Lakini haitakuwa hivyo kwenu; bali mtu anayetaka kuwa mkubwa kwenu, atakuwa mtumishi wenu, na mtu anayetaka kuwa wa kwanza wenu, atakuwa mtumwa wa wote'" (Marko 10:42-45).

Mamlaka ni suala kubwa sana kwa Mungu. Mungu aliumba kila kitu kwa mamlaka Yake. Ni njia yake ya kudhihirisha nguvu Zake.

Kwa nini Mungu ni mkuu sana katika mamlaka? Kuna kitu ninachokiita kanuni ya mamlaka. Kanuni ya mamlaka inaamuru kwamba mtumishi anapokea faida ya mali, na ulinzi na nguvu ya mwenye mamlaka. Mwenye mamlaka analazimika kumjali mtumishi wake. Kama mtu hatamnyenyekeka mwajiri wake, mwajiri wake hataweza kumlipa mshahara wake. Kama mtu hawezi kunyenyekeka mamlaka iliyowekwa na polisi, polisi hawataweza kumlinda.

Ndivyo ilivyo katika mahusiano yetu na Mungu. Mungu sio mbabe mwenye ubinafsi anayetamani wote walioko chini Yake wamsujudie ili kuwahakikishia kuwa Yeye ni nani. Mungu anaupendo wa ajabu kwa ajili yetu, Shauku iliyo kuu kutujali kabisa, lakini hawezi kufanya hivyo hadi tutakapoyanyenyekeza maisha yetu kwake. Kama mtu hawezi kujinyenyekeza mbele za Yesu, Yesu hawezi kumlinda.

Sheria bila mahusiano inaleta uasi! Tunapolelewa kwa upole bila nidhamu ya kutosha, tunakua katika hali ya uhuru sana na uasi. Kinyume chake, tunapolelewa kwa nidhamu kubwa bila upole tunakuwa waasi pia. Kuna uwiano unaohitajika.

Ninamfahamu mwanaume Muislam aliyemuoa mwanamke Mkristo. Alikua njiani kuamini kuwa Yesu alikuwa Masihi; Alikuwa akitafuta kujua kwa moyo wake wote. Hata hivyo, tatizo lake kubwa lilikuwa ni kutambua tabia ya Mungu. Alisema anaweza kutii kwa urahisi maagizo ya Mungu pale anapoyapokea, lakini hakuweza kuelewa kuhusu kuwa na

uhusiano wa karibu na wa kibinafsi na Mungu. Uzoefu wake katika maisha ni alikuwa na baba kama kielelezo tu ambaye alikuwa na masharti tu bila mahusiano.

Watu wengi wanauhusiano na Yesu na pia wanashindwa kuuendea ushindi katika maisha yao kwasababu hawalielewi neno "bwana" au wanaelewa vibaya tabia ya Yesu. Kwa hiyo watu wengi Wanamwona kama Bwana wa majukumu yaliyo magumu na wanasoma Biblia wakiwa na hali hiyo. Sijui jinsi ya kuelezea hili, lakini Yesu ni mtu wa ajabu!

Neno bwana siyo maarufu katika mawazo ya watu wa Magharibi. Huko Magharibi, tunapenda neno demokrasia. Kwa uelewa wa watu wa Mashariki linaweza kubeba maana ya mtoza ushuru aliye mkatili ambaye ni vigumu sana kumpendeza. Neno bwana kwa uhalisi limebeba maana ya "mtoa mkate". Kwa wanadamu wote wa dini na kabila zote, wazo hili la kujinyenyekeza chini ya mamlaka ni kinyume cha asli yao. Hali hiyo ilirithiwa kutoka kwa baba yetu, Adam. Hilo ndilo lilikuwa tatizo lake. Uasi dhidi ya mamlaka ndiyo dhambi ya kwanza.

Suala zima ni hili, unamchagua nani atakayekuwa mpaji wako. Mungu anataka awe mpaji wako. Anataka akupatie upendo unaouhitaji, ulinzi na umaana. Hicho ndicho mabwana hufanya. Hicho ndicho miungu hufanya. Huyu bwana anammiliki mtumwa na anawajibika kumtunza mtumwa huyo. Kuna matabaka tofauti ya mabawana, lakini baada ya kuelezea utaona kuwa hakika unao uchaguzi wa aina mbili tu.

Chaguzi hizo mbili ni:

1. Mungu, Muumbaji, Aliyejidhihirisha kama Yesu Kristo, Neno la Mungu.
2. "Miungu mingine."

Chaguzi hizi pia zinajulikana kama Ufalme wa Mungu (Yesu ni Mfalme)

Ufalme wa dunia (Shetani ni mwana wa mfalme).

Katika bustani ya Edeni, Adam na Eve walichagua "miungu wengine."

Walifuatisha ushauri wa kiumbe cha roho kinachoishi, shetani, ambaye alikuwa akijidhihirisha mwenyewe kupitia baadhi ya mambo ambayo Mungu aliyaumba; Nyoka. Ushauri ulikwa ni wao kutumia nguvu zao

wenyewe(Akili zao wenyewe na vipaji ambavyo vinamtegemea Roho wa Mungu) ili ziwe miungu yao wenyewe. Wakaufuata ushahi huo. Kitu ambacho hawakukijua ni hiki, ingawaje, ni yule kiumbe anayeishi alikuwa adui wa Muumbaji wao, na sasa ananafasi ya kuwatawala katika maisha yao. Unaweza ukachukua sasa kanuni ile ambayo ilifanya kazi kwa Adam na Eva na ukaelezea "miungu mingine" yote kwa kutumia masharti hayo.

Na "miungu wengie" wanaweza kuelezewa katika matabaka mawili:

1. uhai wa viumbe, wa kiroho. Watu wengi wanajua kwa uhakika kabisa kwamba wana mawasiliano na roho zinazo ishi. Hali hii inaitwa kuabudu mizimu. Karibu kabila zote za kale na dini za familia zilijengwa juu ya hali hii ya kuabudu mizimu. Wengi wao waliabudu mizimu ya babu zao. Watu hawa waliokua wakiabu waliamini kuwa roho hizi au mizimu hii ilikuwepo kwaaji ya kuwaletea faida. Waliomba miti, maziwa, na hata baadhi ya watu ambao wamekufa. Waliabudu baadhi ya vitu vilivyoundwa na Mungu, badala ya kumwabudu Muumbaji. Uhindu, uchawi, New age na dini nyingine nyingi ambazo zimejengwa juu ya mizimu. Watu hawa huendelea bila kukoma kujaribu kuridhisha na/au kuvirubuni viumbe hawa kupitia kuabudu, mapokeo, kafara, na kujaribu upatanisho. Na wanawasiliana nao kupitia njia mbalimbali pamoja na kutafakari (MEDITATION), kuimbia mapepo, uasherati wa kipepo, kuchonga sanamu, madawa ya kulevya, pombe, wanyama, kucheza, yoga, kutoa watu kafara, na njia nyingine nyingi. Na mara zote hufanya makongamano ya kutoa heshima kwa mizimu. Mardi Gras huko Marekani ni mfano mzuri wa hili. Marafiki zangu kutoka Afrika ya Magharibi na kutoka Haiti wamenambia hadithi nyingi za kuvutia. Nimewahi kuhudhuria moja ya matukio haya mimi binafsi na nikahisi nguvu za kipepo.

Nataka kusema kuwa viumbe hawa wa kiroho ni halisi na kwa ukweli hutenda kazi na kutawala katika maisha ya mtu. Biblia inawaita kuwa ni mapepo wachafu na inafundisha kuwa wako chini ya uongozi wa shetani, aliyekuwa malaika mkuu Lusifa, ambaye alimwasi Mungu. Shetani ni mwanzilishi wa mambo yote yaliyo maovu. Huja ili aue, aibe

na aharibu(Yohana 10:10). Hatima yake ya milele na hatima ya wote wanao mfuta ni katika lile Ziwa liwakalo Moto.

Mtume Paulo alisema katika 1Korintho 10:19-20 (Tafsiri iliyo chambuliwa zaidi), "Basi niseme nini? Ya kwamba kile kilichotolewa sadaka kwa sanamu si kitu? Au yakwamba sanamu si kitu? Sivyo, lakini vitu vile wavitoavyo sadaka wavitoa kwa mashetani, - kwa nguvu za mapepo wachafu - wala si kwa Mungu kabisa; Nami sipendi ninyi mshirikiane na mashetani katika sherehe zao."

Kumbukumbu 32:17 inasema, "Walitoa sadaka kwa pepo wala si kwa Mungu, Kwa miungu wasio wajua, kwa miungu mipya iliyotokea siku za karibu, Ambayo baba zenu hawakuiofopa." Hawa "miungu wengine" kwa kweli wananguvu fulani. Lakini wanafanya kinyume ya yale Mungu ayafanyayo. Hawa sio wa kutegemea, wanaweka hali ya kotokuwa na uhakika pamoja na hofu, na watakuongoza katika maangamizi ya milele. Ni viumbe vilivyoubwa ambavyo havikuumbwa ili vitoe au vitunze mtu. Isaya 14:14 inamsema lusifa(shetani), "Nitapaa kupita vimo vya mawingu, Nitafanana na yeye Aliye juu." Shetani na mapepo yake yote ni roho zilizo chini ya mamlaka. Yesu na waamini wana mamlaka juu yao.

2. mambo yaki- ulimwengu. Watu wengi hawaamini katika roho wa dunia na wanategemea nguvu za nafsi zao wenyewe na mambo kama hayo kwaajili ya haja zao. Tatizo ni hili hatima ya kila kitu ni kiroho, hata mambo hayo ambayo yanaonekana juu ya dunia kuwa ni mambo ya kawaida ya kiulimwengu.

Mungu alimuumba mwanadamu awe na nafsi yenye nguvu sana, uendelevu wa utashi, akili na hisia. Tangu kuanguka kwa Adamu, mwanadamu amekuwa akitumi kijishemu tu cha uwezo wa nguvu ya nafsi yake. Naamini hii ni Neema ya Mungu. Biblia inauita "mwili" na "utu wa kale" Mwanadamu anaweza kufanya mambo yenye nguvu sana bila Mungu katika maisha yake(nguvu ya nafsi). Mwanadamu anaumba dini zenye nguvu sana na kazi mbalimbali za kisayansi. Anategemea nguvu zake kutoka kwenye utajiri, siasa, biashara, udanganyifu wa ibada, na njia nyingine nyingi.

Tatizo la nguvu ya nafsi ni kuwa ndani yake Mungu aliumba nafsi ili iwe mtumishi wa roho(Kuunganishwa na Roho wa Mungu) na bila

Mungu nafsi hutenda kazi bila nguvu na mpango ambao Mungu aliufanya. Pia, roho chafu za kipepo hujiunganisha na nguvu ya nafsi na kwa uhalisi kabisa huipa nguvu ya ziada ya kutawala.

Waburudishaji wengi maarufu na wafanya biashara hukiri waziwazi (Nimesikia shuhuda zao) hupata nguvu zao kutoka kwa roho wa dunia. Ezekieli 28:4-5 inamsema shetani, " Kwa hekima yako na kwafahamu zako umejitia utajiri, nawe umepata dhahabu na fedha katika hazina zako; kwa hekima yako nyingi, na kwa biashara yako umeongeza utajiri wako, na moyo wako umeinuka kwa sababu ya utajiri wako." Shetani ame utia nguvu "utendaji wa dunia" na "miungu wengine" kwa nguvu za muda mfupi tu za utajiri. Yeye amebobea.

Nafsi ya mwanadam na roho wa dunia haviwezi kumfanya mtu awe kama Mungu alivyomuumba awe. Sana sana zinaweza kutimiza tu baadhi ya mahitaji ya mtu, lakini hata utimizwaji huu hudumu, kwa muda mfupi na hauna uthamani utakao dumu. Na hitimisha lake ni utengano wa kimilele na Mungu. Utaishi na mungu wako milele. Lazima *uchague* kuwa mungu wako ni nani.

"Miungu wengine "uahidi kutimiza mahitaji kwa wepesi. Yesu Anaahidi kutimiza mahitaji kwa kupitia Neno Lake. Neno Lake hutenda kazi katika kanuni ya kupanda na kuvuna, na kulitii Neno Lake. Hili linajumlisha muda, uvumilivu na kuteseka kimyakimya. Sio jambo la kutatuliwa mara tu. Hata hivyo, Mungu Ameahidi mambo ambayo "miungu wengine" hawawezi kuahidi: uhusiano wa karibu, uhusiano wa kibinafsi na ushirika wa karibu pamoja Naye katika uwepo Wake, na uzima wa milele. Ukweli ni kwamba wanadanganya na kuahidi uzima wa milele na kuwapatia maisha mapya, nk.. Lakini hayo yote ni uongo. Hata Yesu alijaribiwa kutumia "njia nyepesi" kwa ajili ya mahitaji Yake. "Kisha Shetani akampandisha [Yesu], akamwonyesha milki zote za ulimwengu kwa dakika moja. Ibilisi akamwambia, 'nitakupa wewe enzi hii yote na fahari yake, kwa kuwa imo mikononi mwangu, nami humpa yeyote kama nipendavyo'" (Luka 4:5,6).

Mara zote utateseka pale utakapombadilisha "bwana" wako, au kumbadilisha yule atakayekuwa mpaji wako. Hili haliji kiurahisi! Katika Marko sura ya 4 Yesu anaelezea kwamba upatikanaji wa mahitaji katika

Ufalme wa Mungu utaongezeka kwa kadri matunda ya mbegu za Neno Lake linavyokua limepandwa katika moyo wako. Vilevile alisema kwamba Shetani atajaribu kuziiba mbegu za Ufalme na kupanda mbegu zake mwenyewe. Waamini wengi huangushwa na mgandamizo huu na kurudi kwa "miungu wengine". Kutakuwa na vita pale utakapoamua kuwa Yesu akutane na mahitaji yako yote kwa kupitia Neno Lake. Lakini inastahili, kwa ajili ya sasa na milele!

Pata somo toka kwa Kijana Tajiri.

"Hata alipokua akitoka kwenda njiani, mtu moja akaja mbio, akampigia magoti, akamwuliza, 'Mwalimu mwema, nifanye nini ili niweze kuurithi uzima wa milele?'" (Marko 10:17). Kijana huyu alikuwa ni kiongozi wa kisiasa, alikuwa ni tajiri, na alichunguza sheria za kiyahudi katika maandiko (ndivyo alivyofikiri). Mstari wa 21 unasema kwamba Yesu alimpenda sana akamwambia kwamba auze vyote alivyonavyo, na kuwapa fedha zake maskini na kisha amfate Yeye. Yule mtu alihuzunika kwasababu alikuwa na mali nyingi na hakutaka kufanya kama Yesu alivyomwagiza. Kumbuka kwamba Yesu alimpenda sana mtu huyu na alijua alichokihitaji. Yesu alikua anajaribu kumfanya ageuke kutoka kwa "miungu wengine."

Kisha wanafunzi wakatoa dukuduku zao kwa Yesu kwa mafundisho Yake na hawakuelewa kwamba yule mtu tajiri angeokolewaje. Petro akamkumbusha Yesu kwamba yeye na wengine waliacha vyote ili kumfuata Yesu. Yesu akasema, "Amin nawaambieni hakuna mtu aliyeacha nyumba, au ndugu waume, au ndugu wake, au mama, au baba, au watoto, au mashamba, kwa ajili Yangu na kwa ajili ya injili, ila atapewa mara mia sasa wakati huu, nyumba na ndugu waume, na ndugu wake, na mama, na watoto, na mashamba, pamoja na udhia; na katika ulimwengu ujao uzima wa milele." (Marko 10:29-31). Gundua kwamba Yesu alitoa onyo "pamoja na udhia."

Huu ndio uhakikisho wako kutoka kwenye Neno la Mungu kwamba Yesu atakutana na mahitaji yako utakapogeuka kutoka nguvu za nafsi yako na "miungu wako wengine." Gundua kwamba Yesu alionyesha kwamba iliwabidi watu waache mila na desturi na miungu, mali zao, na

kitu kingine chochote chenye sifa ya sanam au "miungu wengine." Pia gundua thibitisho. Tunapotoa "dhabihu" kwa kile tunachokiamini tutapokea mara mia sasa kwa wakati huu, lakini pamoja na udhia, na pia katika ulimwengu ujao, uzima wa milele.

Usiogope kuwaacha "miungu wako wengine." Yesu atakupa marejesho mara mia, lakini itakuwa pamoja na udhia. Lakini kuna faida!

Hatimaye utakuwa na tabia ya mpaji wako.

Utafanana na yule anayekutumizia haja zako. Utakuwa na tabia za yule unayemtii. Uliumbwa uwe mtumwa wa mtu fulani. Unafanyika mtumwa kwa yule unayemtii. "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yuke mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uletao mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uletao haki?" (Warumi 6:16). "Sanamu za mataifa ni fedha na dhahabu, kazi ya mikono ya wanadamu. Zina vinywa lakini hazisemi, Zina macho lakini hazioni, zina masikio lakini haisikii, wala hamna pumzi vinywani mwake. Wazifanyao watafanana nazo, na kila mmoja anayezitumainia." (zaburi 135:15-18). Warumi 8:29 inasema kwamba mmechaguliwa tangu asili ili mfananishwe na mfano wa Yesu, Mwana wa Mungu.

Maneno ni mbegu. Neno la Mungu sio tu litakupatia mahitaji yako, bali litabadilisha tabia yako kwa Yake. Ikiwa utaendelea kutumia maneno na picha za "miungu wengine," utafanania kama wao. Hii ndio njia ya kupand ana kuvuna.

Matokeo ya mwisho ni kwamba unalo kusudi katika maisha; kusudi ambalo Mungu ametengeneza kwa ajii yako. Kusudi hili ni "kumtukuzi" Mungu. Kwa maneno mengine, ni kumwonyesha Mungu kwa wengine. Ndiyo, Mungu anataka awe mpaji wako, lakini haiishii hapo. Mungu hatubariki tu ili kwamba tubarikiwe. Hicho ndicho kilichowafanya waamini Agano la Kale waingie katika matatizo. Waliangukia katika uchafu na uasherati walipoishi kwa kuzitegemea baraka zao wenyewe. Mungu hutubariki ili tuwabariki wengine. Anataka ajidhihirishe mwenyewe kwa waliopotea katika

ulimwengu huu. Anawapenda, anakutaka wewe uwaendee. Anataka atumie kipawa alichokiumba kwa ajili yako ili uwashawishi watu waliopo katika mazingira yako. Mungu anataka akubadilishe ili uwe mtoaji. Mungu aliahidi kumbariki Abraham, Muebrania wa kwanza. Vilevile alimwambia kwamba asizichukulie baraka kama jambo rahisi tu badala yake kama wajibu fulani (Mwanzo 12:1-3).

Hataki wewe upoteze muda wako kuwa na wasiwasi kuhusu upatikanaji wa mahitaji yako kama wafanyavyo wasioamini. Anataka akuweke huru ili umpe utukufu. "Bali utafuteni kwanza ufalme wake na haki Yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33).

Nilipokutana na Yesu nilikuwa kama niko katika mafunzo ya kijeshi!

Kwanza, aliuumba uhusiano wetu, kisha akaidhihirisha tabia Yake kwangu kisha akanijulisha ni jinsi gani nilivyokuwa wathamani Kwake. Aliingia kazini ili kubadilisha tabia yangu ili kwamba nifurahie mamlaka iliyo katika Neno Lake. Aliniweka chini ya nidhamu ya Roho Mtakatifu. Pia Aliniweka chini ya nidhamu ya mamlaka zilizoteuliwa. Miaka hii katika maisha yangu ilikuwa ni majaribu mazito. Lakini kupitia hayo niligundua mambo muhimu kuhusu mimi binafsi na kuhusu tabia ya Mungu.

Yesu ni mfano wetu. Japokuwa Alikuwa ni Mungu katika mwili, Aliikana nguvu ya nafsi Yake na kumwamini Baba Yake wa Mbinguni. "Basi Yesu akajibu akamwambia, 'Amin, amin, nawaambia, mwana hawezi kutenda neno mwenyewe ila lile ambalo anamwona Baba analitenda; kwa maana yote ayatendayo yeye ndiyo ayatendayo mwana vilevile'" (Yohana 5:19). Yesu alipokuwa duniani alitegemea kabisa kusikia kutoka kwa Baba Yake. Alijinyenyekeza kabisa kama mwanadamu kwa Baba Mungu. Ikiwa ilimpasa Yesu kufanya hivyo na sisi pia.



Nachagua “miungu wengine,” “dunia.” Hili linakwenda kuwa jambo la kufurahisha na rahisi! U pagani, upotoshaji roho wa ulimwengu. Roho za mababu. Nguvu ya nafsi. U tajiri. U binafsi. Siasa. Sayansi. Elimu.

Unapokwenda kwa “miungu wengine” unakuwa mtumwa wao, na unafanana nao. Utaiishi pamoja nao milele. Wanakwenda kwenye Ziwa la Moto.

Namchagua Yesu, Mungu, Muumbaji, kukutana na mahitaji yangu ndani ya Neno Lake. Inaweza kuchukua muda zaidi, nami naweza kupitia baadhi ya mateso, bali Anastahili na ni mwaminifu

Unapomwendea Yesu, ambaye ni Neno la Mungu, Anakupatia mahitaji yako, unafanana Naye, na unaiishi pamoja Naye milele. Yeye yuko Mbinguni

Njia ya kweli ya kumfanya Yesu awe Bwana ni kuliweka Neno la Mungu lichukue nafasi ya kwanza katika maisha yako. Yesu ni Neno kama ilivyoelezwa katika Yohana 1:1-2. "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu, Naye Neno alikuwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwa kwa Mungu" (Yohana 1:1,2).

Ni muhimu kuwa mtendaji wa Neno. "Lakini iweni watendaji wa Neno, wala si wasikiaji tu, hali mkijidanganya nafsi zenu" (Yakobo 1 :22). Imani sio tu kuamini kwa akili ya mtu; imani ya kweli ni kuliamini Neno la Mungu moja kwa moja kiasi kwamba mtu anaweza akalitii na kulitendea kazi kiuhalisi.

Yesu alifurahia sana pale Akida alipolichukua Neno Lake na kulitendea kazi. "Hata alipoingia Kapernaumu, akida mmoja alimjia, akamsihi, akisema, Bwana, mtumishi wangu amelala nyumbani, mgonjwa wa kupooza, anaumwa sana. Yesu akamwambia, nitakuja, nimponye. Yule akida akamjibu, akasema, Bwana, mimi sistahili Wewe uingie chini ya dari yangu; lakini sema neno tu, na mtumishi wangu atapona. Kwa maana mimi nami ni mtu niliyewekwa chini ya mamlaka, mwenye askari chini yangu; nikimwambia huyu, nenda, huenda; na huyu njoo, huja; na mtumwa wangu, fanya hivi, hufanya. Yesu aliposikia hayo, alistahajabu, akawaambia wale waliomfuata, amin, nawaambieni, sijaona imani kubwa namna hii, kwa yeyote katika Israeli. Nami nawaambieni, ya kwamba wengi watakuja kutoka mashariki na magharibi, nao wataketi pamoja na Ibrahim, na Isaka, na Yakobo katika ufalme wa Mbinguni; bali wana wa ufalme watatupwa katika giza la nje, ndiko kutakuwako kilio na kusaga meno. Naye Yesu akamwambia yule akida, nenda zako; na iwe kwako kama ulivyoamini. Mtumishi wake akapona saa ile ile" (Mathayo 8:5-13).

Gundua kaitka kisa hiki kwamba yule akida alijali afya ya mtumishi wake. Alijua maana halisi ya mamlaka!

Kipimo chetu cha kumpenda Mungu ni kutokana na kuwa ni kiasi gani tunalitii Neno Lake. "Yesu akajibu, akawaambia, 'Mtu akinipenda, atalishika Neno Langu; na Baba yangu atampenda; nasi tutakuja kwake, na kufanya makao kwake. Mtu asiyenipenda, yeye hayashiki maneno Yangu; nalo neno mnalolisikia siyo Langu ila ni Lake Baba aliyenipeleka'" (Yohana 14:23-24).

Njia nyingine ya kujinyenyekeza chini ya Ubwana wa Yesu ni kwa kupitia mamlaka zilizoteuliwa. Wakristo wengi wanalielewa vibaya swala hili. Mamlaka iliyoteuliwa ni mtu aliyetumwa kwa jina la mwingine. Kwa mfano, kama nitamtuma mmoja wa wafanyakazi wangu kwenda kwa mfanyakazi mwingine akiwa na idhini yangu ili kutekeleza jambo, hivyo yule aliyetumwa ndiye mamlaka yangu niliyoyatuma. Kutomtii yule aliyetumwa ni sawa na kutomtii yule mwenye mamlaka. Biblia imeliweka wazi kwamba tunayo mamlaka yaliyoteuliwa katika maisha yetu yote. Baadhi ya hayo ni mazuri na baadhi si mazuri sana, au ni maovu. Serikali za nchi zetu na miji yetu na mapolisi wake ni mamlaka iliyoteuliwa na Mungu. Ukijifunza kitabu cha Matendo ya Mitume utaona jinsi waamini wa karne ya kwanza walivyopitia mazingira magumu sana. Yesu, alipokuwa anahukumiwa maisha Yake, alijinyenyekeza chini ya mamlaka iliyoteuliwa ya Warumi na hata ya dini ya Kiyahudi. Hakujinyenyekeza kwa mtu mwenyewe, bali kwa ofisi walizoziwakilisha.

Tunazo mamlaka zilizoteuliwa katika familia zetu, katika maisha yetu ya kiroho na ya kikanisa, katika maisha yetu ya shuleni, na katika maisha yetu ya kiufundi. Mwombe Mungu akusaidie utembe katika maisha yenye uwiano pamoja na mamlaka yako uliyoyateuwa

Je Unampenda kiasi gani?

Upendo ni tendo. Utii kwa maneno unayoyasikia ni kuuelezea upendo wako. Ikiwa ungemkamata mtoto wako akiiba pesa kutoka kwa jirani ungechukua hatua kali sana ili asijekuwa mwizi katika utuuzima. Huyu mtoto anaweza kukwambia, "Lakini mama, nakupenda." "ndiyo," utasema, "lakini kama unanipenda, basi fanya kile ninachosema."

Kujinyenyesha kwa Yesu mara zote ni kitendo cha kujitolea.

Katika Agano la Kale na desturi za Kiebrania, kuwa na watumwa ilikuwa ni jadi ya kawaida. Hataivyo Mungu aliamuru kwamba watumwa watendewe kwa haki. Aliwapatia watumwa uhuru baada ya muda fulani. Cha nyongeza ni kwamba, aliruhusu mtumwa kubaki na familia iliyomtawala, kama mtumwa wa kujitolea, kama angependa.

"Lakini huyo mtumwa akisema waziwazi, 'mimi nampenda bwana wangu, na mke wangu na watoto wangu; sitaki mimi kutoka niwe huru,'

ndipo hapo huyo bwana wake atamleta mbele ya Mungu na kumleta mlangoni, au penye mwimo wa mlango; na bwana wake atalitoboa sikio lake kwa uma; ndipo atamtumikia siku zote" (Kutoka 21:5,6).

Uzoefu wangu pamoja na Bwana Yesu tangu 1979 umekuwa ni moja ya mwenendo wa kutoka katika njia zangu ili kutafuta jinsi ya kumpendeza Yeye. Ameheshimu sana tabia yangu kupita kitu kingine chochote ninachoweza kufikiri. Kuna usalama kuyaweka maisha yako yote katika mikono Yake. Kunafaida kutafuta Neno Lake na kumtii Yeye. Ni busara kuachana na shauka zako ili kuzitafuta shauku Zake. Yeye ni Mungu! Anayaweza mambo yote. Sisi ni viumbe vilivyoubwa tu; tunamipaka. Anataka kufanya mambo makubwa katika maisha yetu, lakini Yeye huwekewa vikwazo kwa jinsi gani au kwa upungufu kiasi gani tunavyonyenyekea chini ya Ubwana Wake.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa isikilize sauti Yake.

"Habari, Jina Langu ni Yesu. Nakupenda."

Sura ya 8 Kuendelea Na Maombi



Mungu, unasikiliza kweli?

Nilipokutana na Yesu kwa mara ya kwanza, Nilimuuliza aliwezaje kusikiza maombi yangu na ya watu mamilioni wengine kwa wakati mmoja. Nilijua kwamba nimetengeneza muunganiko pamoja na Mungu kupitia Yesu na Roho Mtakatifu, lakini sikuwa na uhakika ni jinsi gani mawasiliano yangu na Yeye yangefanya kazi. Sikuwahi kufundishwa desturi zozote za kidini, (asante Mungu) na hivyo basi sikulazimika “kubadilisha” kanuni zozote zisizo za kimaandiko za maombi.

Nakumbuka siku moja, mwanzoni mwa mwenendo wangu na Bwana, kumsikia Roho Mtakatifu akinena na mimi. Alisema, "Kama utatoa zaka ya muda wako na kunipa 10% yake, nitazibariki 90% kupita jinsi unavyoweza kufikiri." Nilifanya hivyo tu. Nilidhamiria kumpa Mungu muda usiopungua masaa 2.4 kwa siku kwa ajili ya maombi na ushirika katika Neno Lake. Aliheshimu ahadi yake. Alizidisha muda wangu zaidi ya mtu yoyote ambavyo angeweza kufanya.

Siku ya kwanza ilikuwa ya ajabu ajabu. Nilikaa katika gari yangu nikamwambia Bwana, "sawa, nitajifanya kana kwamba umekaa hapa na mimi, nami nitaongea na kioo cha gari na kuamini kwamba unanisikia." Naye alinisikia, na muda wangu wa maombi ukageuka kuwa ni kipindi cha kuvutia sana kiasi ambacho ninakitamani sana kuliko kitu kingine chochote.

Nikamwambia Bwana kwamba nilipendelea zaidi kusoma Neno Lake kuliko kuongea Naye. Alinijibu na kusema, "Soma Neno Langu katika maombi. Maombi si kitu kingine bali ni mazungumzo kati ya

wawili kati Yangu na wewe. Usomapo Neno Langu, Mimi ndiye ninenaye. Kuna muda wako wa kuongea.

Mara nyingi sana naingia katika Neno la Mungu au kwenye kitabu kingine chochote cha kujisomea Biblia kabla sijaongea na Mungu. Ili kwamba niweze kusogea karibu kuyaomba mapenzi yake kwa ajili ya maisha yangu na wengine. Mungu anataka sisi tuombe, lakini na hisi kwamba anataka kutupatia maombi anayoyataka ili sisi tuyaombe. maombi ya msingi ninayomwomba Mungu ni ukiri wa dhambi na udhaifu wangu, na kusifu na kuabudu.

Huu ni mfano wa kile ninachomaanisha. Mungu anataka kumuongeza Israeli, Lakini anamwambia Israeli kuomba mapenzi Yake. "BWANA Mungu asema hivi, tena kwa ajili ya jambo hili nitaulizwa na nyumba ya Israeli, ili niwatendee; nami nitawaongeza kwa watu kama kundi la kondoo" (Ezekieli 36:37).

Kuna muhtasari wa masomo katika ISOB ambayo yanahusu maombi nayo ni mazuri sana. Lililo la msingi linaitwa "Mto Unao Tiririka"

Moja ya kanuni katika masomo hayo yahusiana na jinsi ya kuuendea uwepo wa Mungu katika muda wako wa maombi. Mungu ametuachia ramani au njia za kufuata ambazo anaziheshimu. Simshushi Mungu na kumweka katika kanuni, lakini baadhi ya hatua hizi zitakusaidia utengeneze muunganiko.

1. Gundua thamani ya msalaba wa Yesu na msamaha wa dhambi. Kwanza, chukua muda kukiri dhambi zako kwa Mungu. "Tukiziungama dhambi zetu Yeye ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu na kutusafisha na udhalimu wote" (Yohana 1:9). Unapofanya dhambi, mkimbilie Mungu, usimkimbie Yeye.

Mimina moyo wako Kwake. Hili ni jambo la muhimu sana unaloweza kufanya ili kuongeza uhusiano wako na Yesu. Nimegundua kwamba ananiheshimu mimi pamoja na uwepo wake mara ninapo mimina moyo wangu, yaliyo mema, yaliyo mabaya na yasiyopendeza. Chukua muda kuyatoa mambo yaliyomo moyoni mwako. Ninapofanya hivi

nasema, "Mungu, hivi ndivyo ninavyojisikia. Ninajua nimekosea, lakini hapa ndipo nilipo." Mara zote huiheshimu tabia hii.

Weka kumbukumbu. Chukua muda kutulia na kuwa na tabia ya kuweka kumbukumbu. Andika chini mawazo yako, matatizo yako, maumivu yako, hofu zako na umwandikie Mungu. Katika mawazo yako ona kwamba Yeye amekaa na wewe chumbani kwako. Nikweli amekaa! Kisha chukua muda kumsikiliza Yeye, na andika chini yaliyomo katika moyo wako wa ndani, Anasema na wewe. Unaweza ukafanya makosa mwanzoni, lakini ni sawa. Kama watoto tunaanguka lakini hatukati tamaa. Hili ni la muhimu sana katika kuongeza ushirika wetu wa ndani na Mungu.

2. Ingia katika Neno. Wakati mwingine kusoma Zaburi kadhaa na Mithali kadhaa husaidia. Muda wa faragha na Mungu, vitabu na kanda vinaweza kusaidia sana. Roho Mtakatifu hutenda kazi katika Neno la Mungu. Inakubidi uliweke Neno la Mungu liwe kitu cha kwanza katika maisha yako

3. Chukua muda kutoa shukurani, bila kujali matatizo gani unayokutana nayo. Hili ni jambo la muhimu sana. Mungu hauheshimu moyo usio na shukurani. Mshukuru kwa kukupa nguvu za ufufuo kubadilisha hata mambo mabaya yaliyoko katika maisha yako ili yawe baraka.

4. Chukua muda wa kubadilisha mapenzi yako kwa Yake. Mara nyingi tunakuwa na mambo fulani katika fahamu zetu tunayotaka Mungu ayafanye. Mungu siyo mtumishi wetu. Anataka mapenzi yetu yawe sambamba na mapenzi yake.

Naweza kukumbuka mwanzoni katika mwenendo wangu na Mungu wakati ambao mambo yalikuwa hayaniendei vizuri katika biashara. Nilikuwa na nung'unika na kumlalamikia Yeye. Naye alisema, "Larry, ni vipi kama tukikubaliana kitu! Vipi kama nikakupa kila kitu ulichoniomba na sitazidisha kitu au kupunguza kitu?" Nililifikiria kwa dakika chache na nikajibu, "Hapana Bwana, mimi sijui nataka nini." Akasema, "Hiyo ni sawa. Lakini kumbuka Waefeso 3:20, isemayo, "Basi atukuzwe Yeye awezaye kufanya mambo ya ajabu mno kuliko yote tuyaombayo na tuyawazayo, kwa kadri ya nguvu itendayo kazi ndani yetu," Nikajibu, "Ndiyo Bwana, mapenzi yako yatimizwe."

5. Basi chukua muda kufanya jambo hilo kwa akili zako na hisia zako. Uzibadilishe kwa zake. Ziamuru hisia zako zimsifu Yeye. “Maana, ni nani aliyefahamu nia ya Bwana amwelimishe?” Lakini sisi tunayo nia ya Kristo” (1Wakorintho 2:16).

Kama umechukua muda kuzifanya hatua hizi mara nyingi utajikuta uko katika uwepo wa Mungu. Kuusikia uwepo Wake ni zaidi ya hisia. Baada ya mazoezi kadhaa utajifunza kuutambua uwepo Wake, kumbuka Anaishi ndani yako.

Mara nyingi ninapokuwa katika uwepo Wake, ninagundua kwamba mahitaji yangu hupotea au hubadilika. Wakati mwingi ninahisi kwamba Mungu amenipa ahadi katika Neno Lake ili niweze kusimama kwa hilo.

Unaposikia kwamba Mungu amekupa ahadi katika Neno Lake, ndipo unaweza ukalichukua na kulisimamia kana kwamba kazi imekwisha. Inaweza kuchukua muda fulani ili iweze kujidhihirisha lakini inafaida kusubiri.

"Ombeni bila kukoma" (1Wathesalonike 5:17). Nilikuwa najiuliza tungewezaje kuomba bila kukoma, bila kupumzika. Sasa ninafanya hivyo. Siku nzima nakuwa na mawasiliano na Mungu katika roho Yangu. Wakati mwingine inakuwa ni kimya kimya. Mara nyingi naomba kwa lugha yangu ya maombi. Na wakati mwingine namshukuru tu kwa yote Aliyoyatenda. Kuna njia ya kuwa katika uwepo wa Mungu katika maisha yetu ili tuwe katika mawasiliano pamoja Naye kwa siku nzima.

Kama umewahi kujisikia kuwa hauna mawasiliano, fanya kitu. Inaweza kuwa ni hisia zako tu, ambazo si za kutegemea, hata hivyo, inaweza kuwa ni jambo ambalo linakuhitaji umtafute Mungu. Moja ya sheria bora za kufuata ni; kama unawasiwasi, kaza mwendo na ugundue ni kitu gani kinachoendelea. Mara nyingi tutahisi mgandamizo wa Shetani. Lakini wakati mwingine Mungu anaweka mzigo ndani yetu kumwomba mtu fulani na tunajisikia kuwa roho yake iko pamoja nasi. "Lakini chakula kigumu ni cha watu wazima, ambao akili zao, kwa kutumiwa, zimezoezwa kupambanua mema na mabaya" (Waebrania 5:14).

Zitakuwepo hatua za mabadiliko ya kukua katika ushirika wako na Bwana. Wazazi wa mtoto mchanga huitikia kwa haraka sana mara

mtoto anapolia. Lakini mtoto anapokomaa wazazi husubiri dakika kadhaa kabla ya kumwendea mtoto. Baadaye, mtoto anapoendelea kukomaa wazazi hujizuia kumtimizia anachokihitaji kama hatua ya nidhamu katika hali ya uvumilivu na jitihada za kuzuia ubinafsi. Hii inaitwa mabadiliko katika kukua. Bwana hukuza pia. Anaweza kukupatia "tikitimaji" zima kama zawadi ulipokuwa mwanafunzi mpya, lakini baadaye anaweza kukupatia "mbegu ya tikitimaji." Unavyoendelea kutembea pamoja na Yeye, Ataruhusu mashambulizi juu ya mbegu hiyo ili uweze kukua katika imani.

Nataka nikutahadharishe kuhusu wakati huu wamabadiliko ya kukua. Waamini wengi "Huusikia" uwepo wa Mungu walipomfahamu kwa mara ya kwanza, na baadaye mambo magumu huja na wanarudi nyuma kwa sababu hawakuweza kuona na kuhisi kuwa Mungu anatenda kazi. Kama utasonga mbele katika Neno na maombi, kama utamtafuta Mungu kwa ajili yake na sio tu kwa kujiridhisha mwenyewe, hautamwona nyakati za ukame tu (kipindi cha mabadiliko ya kukua), lakini ushirika wako na Yeye utaongezeka joto na ukaribu.

Asubuhi ndio muda ulio bora zaidi wa kuomba. Mimi ni mtu wa kufanya maombi asubuhi, kwa hiyo naweza nikasema hili kwa urahisi zaidi ya wengine. Tafadhali usihukumwiwe au kukosolewa na ninavyopendelea mimi. Unaweza kuchelewa kulala kila siku na kuwa na maisha mazuri sana ya maombi ambayo yanampendeza Bwana sana. Ninajua Mungu amewaita waombezi ambao huchelewa kulala au huamka mapema sana usiku na kuomba kwa masaa. Ninaona kwamba ni muhimu kujiweka sawa na Mungu katika Neno Lake asubuhi kabla hujafanya chochote.

Sitaki kabisa kumweka Mungu katika boksi au katika utaratibu fulani. Hataivyo, kutokana na yale ninayoyasoma katika maandiko, kuna jambo fulani muhimu sana kuhusiana na asubuhi. Nimegundua kwamba mapepo yanatenda kazi sana usiku, sanasana kati ya saa 4 usiku na saa 10 alfajiri. Inaonekana kwamba hali ya ulimwengu wa kiroho uko wazi wakati wa asubuhi. Naamini kwamba ndiyo sababu ya waombezi wengi hupendelea kuomba katika saa hizi za "giza". Mke wangu na mimi tuligundua hili wakati wa safari yetu ya kimisheni ya Haiti. Vitendo vyao

vya kichawi vilipamba moto kati ya saa 4 na saa 10 alfajiri. Ninajua kwamba mapepo hutenda kazi wakati wote hata mchana, lakini huonekana kuwa na nguvu sana wakati wa usiku. "Hautaogopa hofu ya usiku, wala mshale urukao mchana" (Zaburi 91:5).

Ninaomba siku nzima, lakini kama nikijaribu kufanya kitu chochote asubuhi bila kuwasiliana na Mungu kwanza, siku yangu haiendi vizuri. Inaonekana ama kuna baraka maalum kama tukianza na Mungu, Neno Lake, na maombi.

Zaburi 5:3 inasema "Bwana, asubuhi utaisikia sauti yangu, asubuhi nitakupangia dua yangu na kutazamia."

Zaburi 88:13 inasema hivi " Lakini mimi nimekulilia wewe, BWANA, na asubuhi maombi yangu yatakuwasilia."

Marko 1:35 inasema hivi "Hata alfajiri na mapema sana akaondoka akatoka akaenda zake mahali pasipokuwa na watu, akaomba huko."

Kutoka 34:4 inasema "Naye akachonga mbao mbili za mawe mfano wa zile za kwanza; na Musa akainuka na mapema asubuhi, naye akakwea katika mlima wa Sinai, kama BWANA alivyomwamuru, akazichukua hizo mbao mbili za mawe mikononi mwake.

Kutoka 9:13 Inasema "BWANA akamwambia Musa, 'ondoka asubuhi na mapema ukasimame mbele ya Farao, umwambie, BWANA Mungu wa Waebrania asema, 'wape watu wangu ruhusa waende ili wanitumikie.'"

Zaburi 55:17 inaonyesha kwamba wakati wowote ni wakati sahihi wa kuomba. Inasema, "Jioni, asubuhi, na adhuhuri nitalalama na kuugua, Naye ataisikia sauti yangu."

Kama hauna uhakika wa kuomba, omba Neno. (sura 16 inaelezea suala hili kabisa; yafuatayo ni utangulizi). Moja ya njia zenye nguvu sana kwa ajili ya kujiombea mwenyewe na wengine ni kuomba Neno. Liweke Neno la Mungu kinywani mwako na ulitamke kwa nguvu.

Yesu huchukua ukiri wetu na kuufanya kuwa na nguvu. Waebrania 3:1 inasema, "Kwa hiyo, ndugu watakatifu, wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume wa Kuhani Mkuu, wa maungamo yetu, Kristo Yesu." Tunapolinena Neno la Mungu Yesu hulichukua na kulipeleka kwa Baba na kumwomba Yeye alitende. Kisha tunaweza kuingia katika pumziko na kuachilia Neno lifanye kazi.

Waebrania4:1 inasema "Basi, ikiwa ikalipwa ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana amekosa."

Waebrania 4:12 inasema "Maana Neno la Mungu li hai, tena linanguvu, tena linakali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo."

Malaika huanza kufanya kazi mara wasikiapo Neno la Mungu.
(Zaburi 103:20) ***Maepo hutoroka*** (Zaburi 149:5-9)

Maombi lazima yakuzwe kati yako na Mungu kama kitu fulani ambacho ni binafsi na halisi. Mwombe Akufundishe na Atafanya hivyo.

Jambo kubwa sana katika maombi ni kuwa halisi kwa Mungu!

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda."

Sura 9

Kuendelea Ndani ya Neno.



Nitashinda bila hata kusoma
Neno kila siku; hatahiwyo,
nashughuli nyingi sana

Neno la Mungu limekuwa jambo kubwa sana maishani mwangu tangu nilipokutana na Yesu. Mwaka 1979 wakati nilipokutana Naye kwa mara ya kwanza nilikuwa katika hali kadhaa za kukatisha tamaa. Muda pekee nilipopata pumziko na amani maishani mwangu ulikuwa pale nilipokuwa nasoma Neno. Nilikuwa kama mlevi sugu ambaye alihitaji kupata Neno wakati wote. Sikuweza kutosheka na Neno. Lilinea na roho yangu, lilinifahamu, likanipa tumaini nyakati zisizo na tumaini, na jema kuliko yote halikuwa "kakitu" bali "Yeye". "Hapo mwanzo kulikuwa na Neno, naye Neno alikuwa kwa Mungu. Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu." (Yohana 1:1,2).

Kama nilivyogusia, nilikutana na Bwana nikiwa ninasoma kitabu cha Ufunuo na nikijifunza unabii wa Biblia. Baada ya siku hiyo ya wokovu, nilisoma Ufunuo kwa pupa karibia miaka miwili. Nilishangazwa na jinsi Neno la Mungu lilivyokuwa kamilifu namna hiyo. Niligundua kuwa Agano la Kale liliendana kwa ukamilifu kabisa na Agano Jipya. Niliona mamia ya nabii zikitimizwa hadi tarehe ile, kama ilivyotabiriwa mamia, hata maelfu ya miaka iliyopita. Ilinishangaza namna Mungu alivyoiuvua Biblia na akatuachia sisi. Ni hazina ya namna gani nilikuwa nimepata!

Moja kati ya mambo mengi ya kushangaza sana nililogundua lilikuwa kwamba, si tu niliweza kuisoma Biblia bali pia Biblia iliweza kunisoma mimi. Iliniambia mambo yaliyo nihusu mimi ambayo ni Mungu pekee angeweza kuyajua. Na endapo ningelilia majibu, Roho Mtakatifu

angefungua hadithi katika Agano la Kale inayoendana kabisa na hali yangu. Naamini kuna andiko katika Biblia kwa kila wakati kwa maisha yetu. Tunayopaswa kufanya tu ni kuomba, kutafuta na kubisha hodi.

Kama wewe ni mwamini mpya, lazima ujifunze kulipa Neno la Mungu nafasi ya kwanza maishani mwako! Hakuna njia nyingine ya kuwa na uhusiano wa ndani na Mungu na kupata ushindi wake katika kila hali.

"Kila andiko lenye pumzi ya Mungu lafaa kwa mafundisho, na kwa kuwaonya watu makosa yao na kuwaongoza na kuwadibisha katika haki" (2Timotheo 3:16). Biblia imeletwa kwa wanadamu kwa pumzi ya Mungu, ambayo ni Roho Mtakatifu. Ni Roho Mtakatifu ambaye huyachukua maneno ya maandiko na kuyafanya hai kwa ajili yako katika maisha yako.

Kuna maana mbili za "neno" katika maandiko: moja ni Logos; na nyingine ni rhema. Logos humaanisha Neno la Mungu kwa ujumla. Rhema humaanisha Neno la Mungu linalokuja kwako moja kwa moja kutoka kwenye mdomo wa Yesu. Ni Neno binafsi kwa ajili yako. Roho Mtakatifu hulichukua Logos na kulifanya rhema!

Baadhi ya watu huweza kukariri Biblia na wanabaki ving'ang'anizi "... si wa andiko, bali wa Roho; kwa maana andiko huua bali Roho huhuisha" (2Wakorintho 3:6b).

Biblia inahusu nini kwa ujumla?

Nilipokutana na Bwana mara ya kwanza, niliendelea kuwauliza watumishi wanipe muhtasari mfupi wa yale Biblia inahusu kwa ujumla. Kamwe sikupata kutoka kwao. Na kwa hakika sina nafasi ya kufanya hivyo hapa. Hata hivyo natamani kukupatia mwongozo wa msingi ambapo unaweza kujengea kadri unavyoendelea kujisomea mwenyewe.

Biblia inamhusu Mungu akiumba kila kitu kwa Neno lake pasipo kutokana na kitu. Inatuambia kuhusu Yeye akiumba mwanadamu. Kisha inatuambia habari kumhusu mwanadamu. Inaeleza jinsi alivyoasi mamlaka ya Mungu na kujiweka chini ya mamlaka ya Shetani. Inatuambia vile mpango wa ajabu wa Mungu wa ukombozi ulivyotekelezwa ili mwanadamu aweze kurejeshwa katika uhusiano halali na Mungu.

Agano la Kale linaingia ndani zaidi likieleza kitendo cha Mungu cha kujumbia familia katika kabila ya Israeli akianzia kwa Ibrahimu. Sehemu kubwa ya Agano la Kale linaweka mtazamo katika habari ya Waisraeli. Hilo ni muhimu maana Yesu alikuwa wa uzao wa Ibrahimu, Isaka na Yakobo, ambaye baadaye jina lake lilibadilishwa kuwa Israeli. Yesu alikuwa ni mpango wa Mungu, kumkomboa mwanadamu kumrudisha kwa Mungu, na Israeli ilichangia sehemu kubwa sana katika hilo. Waisraeli waliyatunza maandiko kwa uangalifu sana na Yesu alikuja kama Muisraeli. Yesu alisema "Ninyi Wasamaria mnaabudu msichokijua; sisi tunaabudu tukijuacho; kwa kuwa wokovu watoka kwa Wayahudi" (Yohana 4:22).

Agano la Kale sio tu ni historia ya Waisraeli, lakini pia hutupatia vivuli na matukio, kupitia hadithi zake ambao twaweza kuyatumia katika maisha yetu leo. "Basi mambo hayo yalikuwa mifano kwetu, kusudi sisi tusiwe watu wa kutamani mabaya, kama wale nao walivyotamani" (1Wakorintho 10:6).

"Basi mambo hayo yaliwapata kwa jinsi ya mifano, yakaandikwa ili kutuonya sisi, tuliofikiwa na miisho ya zamani" (1Wakorintho 10:11).

Mfano angalia katika 1Wafalme 17:8-16. Soma habari kuhusu mwanamke aliyekitoa chakula chake kidogo wakati wa njaa, na jinsi Mungu kwa namna ya kushangaza alitoa chakula kwa ajili yake na Eliya. Unaweza kulitumia hili kwa maisha yako binafsi kama vile nami nimefanya. Mungu aweza kutumia njia za kiungu ili kukutimizia mahitaji yako.

Injili zote nne kwa sehemu ni mchanganuo wa kihistoria wa kuzaliwa pamoja na maisha ya Yesu na ya baadhi ya mambo ambayo Bwana wetu Yesu Kristo aliyafanya wakati alipokuwa akitembea juu ya dunia hii. Yanafunua kwetu tabia za Mungu. Watu wa dini, kipindi hicho, na wa wakati wetu pia, walifikiri kuwa Mungu ana moyo usio na huruma, mtu mzee ambaye ni vigumu kumpendeza. Yesu alimfunua Mungu kama Mungu wa rehema na neema. Mungu amefunuliwa kama rafiki wa maskini, wagonjwa, wenye dhambi na wasio na msaada. Alitufundisha masomo mengi kuhusu Ufalme wa Mungu katika Injili.

Injili inaeleza vile Yesu alivyokufa kwa ajili ya dhambi zetu, alifufuliwa kutoka kwa wafu siku ya tatu, na jinsi alivyowatuma wanafunzi wake ulimwenguni kuhubiri Habari Njema.

Nyaraka zina ujumbe mbali mbali. Paulo aliyeandika theluthi mbili ya Agano Jipya, alikuwa amepokea kutoka kwa Bwana ufunuo maalum kuhusu kile kilichotokea msalabani wakati Yesu alipokufa, na wakati alipoketi mkono wa kuume wa Baba Yake. Alikuwa na ufunuo wa kushindwa kwa Shetani na Mungu alivyotufanya sisi kuwa ndani Yake. Paulo alikuwa na ufunuo wa Bibi Harusi wa Kristo, yaani kanisa. Petro, Yakobo, na Paulo wanatupa ushauri mzuri wa kivitendo juu ya kuishi maisha ya kiKristo.

Paulo aliandika ujumbe maalum sana kwa Wagalatia. Anakazia kabisa kuwa si tu kwamba tumeokolewa kwa neema, neema peke yake, bali kuwa twaweza kuishi kwa neema na kwa matendo ama sheria. Asili yetu ya zamani, mwili huendelea kujaribu kututawala kwa njia zozote ziwezekanazo. Njia mbili zitumiwavyo na mwili ni sheria na kujihesabia haki. Tuisisahau kuwa kila kitu huanza na kumalizikia na neema ya Mungu.

Nyaraka huzungumza juu ya ujio wa pili wa Yesu. Hili ni somo ambalo limeeleweka vibaya kwa waamini na wasio waamini kwa karne nyingi. Tatalijadili zaidi somo hili katika sura zijazo.

Waraka kwa waebrania unasisitiza Damu ya Agano na hulinganisha Agano la Kale na Agano Jipya. Unamfunua Yesu kwa namna ya ajabu.

Kitabu cha Matendo kipo katika daraja lake la kipekee. Kwa juu, ni historia ya miaka kadhaa ya kwanza ya kanisa baada ya kupaa kwa Yesu. Kinaonesha Roho Mtakatifu akimwagwa juu ya wanadamu wote, akianzia siku ya Pentekoste. Kinaonesha Mungu akiwajumuisha Mataifa katika wokovu. Kinaonesha mwanzo wa kanisa la mwanzo, na safari za kimisheni zilizofanywa na waumini wa karne ya kwanza katika kupanda makanisa. Kinaonesha huduma ya Roho Mtakatifu akitenda kazi kupitia watu wa kawaida kana kwamba Yesu mwenyewe alikuwa akitenda kazi (katika Jina la Yesu). Kitabu cha Matendo hakina mwisho. Kiufundi bado kinaendelea.

Kitabu cha Ufunuo huenda ndicho kitabu kilichoeleweka vibaya kuliko vitabu vyote katika Biblia. Wakati nikiamini kuna mambo mengi yanahitajiwa kujifunza kuhusu siku za mwisho katika Ufunuo, naamini wengi hukiwekea mipaka kitabu hiku kuwa ni cha habari za siku zijazo, na hivyo hawakitumii katika maisha yao ya siku za leo. Tutakijadili kwa undani siku zijazo.

Naweza kuliadini Neno la Mungu?

Kwa dhahiri hakuna kitu duniani kinachoweza kuaminika isipokuwa Neno la Mungu. Watu huja na kwenda, watumishi huja na kwenda, taasisi, shule, watoto, wazazi huja na kwenda, kila kitu hubadilika "Mbingu na nchi zitapita, bali maneno yangu hayatapita" (Mathayo 24:35). "Ee, BWANA, neno lako lasimama imara mbinguni hata milele" (Zaburi 119:89). "Nitasujudu nikikabili hekalu lako takatifu, nitalishukuru jina lako, kwa ajili ya fadhili zako na uaminifu wako, kwa maana umeikuza ahadi yako, kuliko jina lako lote" (Zaburi 138:2).

Twahitajika tuweze kuliadini Neno la Mungu bila kujali nini kinatujia! Ikiwa liko jambo moja ambalo Neno la Mungu hudiriki kulifanya ambalo hakuna kitabu kingine duniani kinalifanya, ni lile la kutabiri kwa usahihi kabisa juu ya siku zijazo. Hili huthibitisha zaidi ya mabishano kuwa ni Mungu pekee aliyeweza kuiandika Biblia.

Wawezaje kujua kuwa maandiko yaliyopo juu yanayoshuhudia Neno ni ya kweli?

Unabii huthibitisha zaidi ya mabishano kuwa ni Mungu peke yake ndiye angeweza kuiandika Biblia. Kuna mistari 8,352 ambayo moja kwa moja ama si moja kwa moja huhusika na unabii katika maandiko. Mstari mmoja kati ya sita hueleza matukio yajayo. Changamoto aliyoweka Mungu kwa ulimwengu ni kuwa tumthibitisho. "Maana Mimi ni BWANA; mimi nitanena, na neno lile nitakalolinena litatimizwa" (Ezekieli 12:25a)

Wabudha, Wakonfyushenisti, na wafuasi wa Muhamadi wanayo maandiko yao matakatifu, lakini ndani yake kipengele cha unabii hakimo kwa kiwango cha kushtusha. Kuharibiwa kwa Tiro, uvamizi wa Yerusalemu, kuanguka kwa Babeli na Rumi, yote haya yalitabiriwa na

kutimizwa kila kipengele kwa usahihi kabisa. Kuingia kwa Yesu Yerusalemu kulitabiriwa na Danieli mamia ya miaka kabla ya kutokea -HADI SIKU ILE. Kuundwa kwa Israeli kama taifa jipya mwaka 1948 ilishatabiriwa hadi siku na mwezi katika Agano la Kale.

Nabii kuhusu Yesu

Kuna nabii zaidi ya 300 ambazo Yesu alitimiza katika kuzaliwa kwake, maisha, kifo, na ufufuo, ila chukulia kumi na saba tu zinazojulikana sana, kama mfano.

Kwa hisabati za "probability"uwezekano wa nabii hizo kumi na saba kutukia unaleta jawabu la:

Nafasi 1 katika 480,000,000,000,000,000,000,000,000,000.
(480 bilioni x 1bilioni x 1trilioni)

Isaya 42:9 unasema, "Tazama mambo ya kwanza yamekuwa, nami nahubiri mambo mapya; kabla hayajatokea nawapasheni habari zake"

Napendekeza sana usome masomo mengi katika mtaala wa ISOB, kama vile somo la 110 hadi 114 kuhusu Neno la Mungu.³

Najitiisha kwamba haiwezekani kabisa kuwa Biblia isiwe Neno la Mungu lililovuviwa! Mashaka hayanabudi kukujia, hasa kama mwamini mpya. Tunza kweli hizi katika nia yako na kuziangukia nyakati unapojaribiwa, na Mungu atakuona. Neno la Mungu ni kweli na ni kamilifu. Waweza kulitumaini!

Wakristo wengi hawalipi uthamani wa kutosha Neno la Mungu.

Wanahisi kuwa ni la elimu ya juu sana na si jepesi kueleweka. Pia wengine huhisi kuwa linakasoro, ama angalau hadithi zisizo na maana.

Isaya alikwishatabiri kuwa watu wasinge mthamini Yesu wakati alipokuja. Watu wengi mno bado hawampi uthamani Yesu, ambaye ndiye Neno la Mungu.

³ International school of Bible curriculum inapatikana bure katika www.isob-bible.org ama tuma barua pepe kwenda info@isob-bible.org

"Maana alikuwa mbele zake kama mche mwororo, na kama mzizi katika nchi kavu; Yeye hana umbo wala uzuri na tumwonapo hana uzuri hata tumtamani. Alidharauliwa na kukataliwa na watu, mtu wa huzuni nyingi ajuaye sikitiko. Na kama mtu ambaye watu humficha nyuso zao alidharauliwa wala hatukumhesabu kuwa kitu" (Isaya 53:2,3).

Namna Neno linavyofanya kazi.

Neno la Mungu ni mbegu. Mbegu haitoi kelele, wala ukuaji wake hauonekani wazi wazi. Neno la Mungu lina uzima, kama pia zilivyo mbegu. Ndani yake lina kabila na roho ya mzungumzaji.

Hii ni siri ya ufalme wa Mungu!

Nashauri sana utafakari Marko sura 4, mfano wa mpanzi na ile mbegu, ambayo ni Neno la Mungu. Ni moja ya mafundisho muhimu sana ya Yesu.

Yesu alisema siri ya ufalme imekumbatiwa ndani ya mfano huu: "Akawaambia, Ninyi mmejaliwa kujua **siri** ya ufalme wa Mungu: bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano" (Marko 4:11).

Ufalme wa Mungu waweza onekana kama uko mbali sana na wewe, lakini Yesu alisema uko karibu nanyi sasa. Alisema kuwa mkigeuka (mkitubu) mtaona ufalme wa Mungu uko karibu nanyi.

Yesu alikuwa anatuambia kubadilika, **ku**-tubu kutokana na jitihada zetu ili kutimiza mahitaji yetu, na tuwe wazaaji matunda kwa Neno la Mungu.

"Tokea wakati huo Yesu alianza kusema, 'Tubuni, kwa maana ufalme wa mbinguni umekaribia'" (Mathayo 4:17). Hiyo ni kugeuka na kubadili mwelekeo. Ukifanya hivyo utaona ufalme wa Mungu uko karibu kiasi kwamba unaweza kuushika.

Waweza kujiuliza, Alimaanisha nini? Kugeuka kutoka kwenye nini? Ufalme wa Mungu ni nini? Naamini tunapaswa kugeuka kutoka kwenye namna ya maisha ya ulimwengu, kwenda katika namna ya maisha ya Ufalme. Naamini hili linatendakazi katika maisha yetu ya milele. Pia naamini Yesu hakuwa tu anawaambia watu hawa "Acheni kutenda dhambi

na mtubu kutokana na njia zenu za tamaa”.Hapana. Yesu alikuwa akitupa mpango wa jinsi ya kuishi.

Marko sura 4 inatuambia kuhusu Neno. Neno hupandwa mioyoni mwetu na Ibilisi huja na kuliiba. Jinsi gani? Hufanya hivyo kwa kutumia hali mbali mbali za moyo wetu.

a. Moyo mgumu, pembeni mwa njia ama barabarani, Marko 4:15. Mara moja Shetani huunyakua ujumbe uliopandwa ndani yao. Watu wengine si makini na hawajali.

b. Mwamba, Marko 4:16. Wanalipokea na kulikubali mwanzoni. Lakini hawana mizizi. Wakati dhiki na udhia vikiwajia kwa sababu ya Neno, wanachukizwa, wanajikwaa, wanakerwa, na kusononeshwa; kisha wanajikwaa na kuanguka. Neno linapotea. Wengine hawawezi kustahimili mgandamizo. Hawawezi kuona kitu chochote kikiendelea kuongezeka, hivyo wanakata tamaa na kuacha.

c. Miiba, Marko 4:18. Neno hupandwa kama mbegu na hukua, hata hivyo masumbufu, wasiwasi, mashaka, anasa, tama na fahari ya macho hulizonga. Madanganyifu ya utajiri, tamaa na hamu ya mambo mengine huingilia kati na kulizonga Neno. Wengine huingia katika mgandamizo ya kuwapendeza watu na hamu zao za kuwa maarufu na wenye mali.

Sababu mojawapo ya sisi kutokuwaamini wengine na kutoliamini Neno la Mungu ni kwa sababu ya hali ya moyo wetu. Sababu inayotufanya tufikiri wengine wanatudanganya hata wakiwa wakweli kabisa ni kwa sababu ya asili yetu. Sababu inayotupa wakati mgumu sana kumwaamini Mungu ni kwa sababu hatuwezi kujiamini hata sisi wenyewe.

d. Udongo mzuri huzaa matunda, Marko 4:20. Kukua hakutegemei hali nzuri ya hewa, bali udongo mzuri. Luka 8, mfano uleule, unasema udongo mzuri ni moyo ulio na uaminifu, wema, haki, utu na uthamani. Huzaa mara thelathini, sitini, mia zaidi ya ile iliyopandwa. Neno “mia” kulingana na Strong's Concordance, humaanisha kiasi kisichoeleweka cha kile cha kwanza.

Mungu ametupa Neno lake ili kutupatia mahitaji yetu yote. Mahitaji yetu matatu ya msingi ni upendo, usalama na umuhimu. Kama tutalipokea Neno moyoni mwetu na kumpinga Ibilisi anapojaribu kuliiba,

Mungu atasababisha matunda yakue katika maisha yetu ambayo yatatupatia mahitaji yetu yote. Hii sio theolojia isiyo na maana. Naweza binafsi kushuhudia kuwa Neno la Mungu kweli kweli hutenda kazi namna hiyo. Ibilisi analijua hilo, Mungu analijua hilo, sasa twahitaji kulijua hilo pia!

Nakupa changamoto kuisoma mfululizo Zaburi 119 kama ushuhuda wa kile Neno la Mungu litakachofanya.

Baadhi ya mifano ambayo Zaburi 119 inasema kulihusu Neno:

Mungu alikuamuru ulitunze moyoni mwako; Neno huongoza njia zako; hutaabishwa; Mungu hatakuacha; njia yako itasafika kwa Neno; Neno litakuwa kwako ni zaidi ya utajiri wote; utayaona maajabu ndani ya Neno; Mungu alikupatia Neno ili usijisikie kama mgeni duniani; Mungu huwakemea wenye kiburi na washupavu watangao na kuliacha Neno; Neno hukushauri na kukufurahisha.

Neno hukuhuisha na kukusisimua (mst 25); unapolitafakari Neno unafahamu maajabu ya Mungu; Neno litakutia nguvu wakati maisha yako yanapoonekana kuyeyuka na kukosa tumaini, Neno litakuondoa katika njia ya uongo; yakupasa uchague njia ya kweli na kuliweka Neno mbele yako; Mungu atakupa moyo uliotayari kwenda njia ya Neno; Neno litakuhifadhi dhidi ya sanamu; Neno ni kwa wale tu wanaomcha Mungu na kumwabudu Mungu; Neno litaondoa aibu yako; Neno litahuisha maisha yako; Neno litakupatia wokovu wa Mungu, litakulinda na kukuponya; litawapa jibu wale wakudhihakio na kukudharau (mst.42).

Neno litakupa uhuru (mst.45); litakulinda usiaibishwe; Neno huleta tumaini na kusudi la Mungu katika maisha yako; Neno litakufariji na kukubembebeza katika mateso yako; Neno litakuponya na kukutoa hatarini, litakupatia mahitaji yako, litakufariji na kusema nawe, litakuwa nawe hatarini, litakuweka mbali na hatari; adui wanapo kushambulia Neno linakulinda; Neema na upendeleo wa Mungu huja kupitia Neno; Hukufundisha maamuzi mazuri, hekima na maarifa; Litakulinda waovu watakaponena uongo juu yako (mst.69).

Neno ni bora kuliko dhahabu na fedha; uliumbwa ili ulisikie Neno; Neno hukupa tumaini, lakini wakati mwingine yapaswa unyamaze na kulingoja; Neno limefichwa na kuachwa na kwa ajili ya wale wanaotafuta;

Rehema za Mungu huja kwa Neno; Litaufanya moyo wako usiwe na lawama, wa kweli, na uliokamili; Japokuwa utateseka mara nyingine hapo ndipo utajua kuligeukia Neno; Neno ni aminifu na kweli; Milele Neno lasimama Mbinguni (mst.89). Kama usingekuwepo ndani ya Neno ungeangamia; Lilikulinda pale adui alipokujia; Kila kitu kinamipaka yake isipokuwa Neno (mst. 96).

Hukufanya mwenye hekima kuliko adui zako. Hukupatia mafunuo zaidi ya ndani kuliko hata waalimu wako; Waweza kulitunza Neno wakati tu unapobaki mwaminifu; Neno ni tamu; Neno ni taa ya miguu yako na mwanga wa njia yako; Neno hukuponya na kukupatia uzima; Neno hukupa furaha; Neno ni mahali pa kujificha; Yakupasa uwe na marafiki washirika wazuri ili uweze kulitunza Neno; Neno ni bora kuliko chochote kinachotungwa na mwanadamu (mst.129); Huwapatia wajinga maarifa na ufahamu; Neno huyazuia mabaya yasikufikie; Neno ni safi na unalipenda; Hata uwapo taabuni Neno hukuletea mambo ya kupendeza; Neno hukufungamanisha na umilele [husafirisha uzima wa Mungu hadi kwako]; Ulitumaini Neno la Mungu kama mtoto mdogo.

Neno humleta Mungu karibu nawe, karibu zaidi kuliko adui zako; Inaonesha kwamba wakati mwandishi alipokuwa taabuni Neno lilimaanisha zaidi kwake. Waovu hawawezi kutatua mambo vizuri kwa sababu wako mbali na Neno; Neno lote la Mungu ladumu milele; Unalifurahia Neno kama mtu aliyevumbua hazina; Neno hukusababisha wewe umsifu Yeye; Neno humfanya Mungu akusikie na kukuokoa; Huufanya mkono wa Mungu kuwa tayari kukusaidia; Hata wakati umekwenda mbali kama kondoo aliyepotea, Neno hubakia ndani yako likurudishe kwa Mungu; Kwa kuwa Neno la Mungu ni kitu thabiti, basi wahitaji kuyapima maneno mengine yote yaliyo kinyume na Mungu ama sifa zake dhidi ya sifa za Mungu.

Neno litafanya nini?

Shetani aliposikia Neno katika bustani ya Edeni alishindwa. Farao alipolisikia Neno aliwaruhusu Waisraeli waende. Musa alipolisikia Neno bahari ya Shamu iligawanyika. Kuta za Yeriko zilipolisikia Neno zilianguka. Gideoni alipolisikia Neno jeshi lake dogo liliwaua maadui. Samweli alipolisikia Neno hakuwa na uhakika alikuwa ni nani. Eliya

alipolisikia Neno, aliwafufua wafu, alisimamisha mvua, na akaianzisha tena. Naamini alipolitii Neno ukoma wake ulitakaswa. Goliathi alipolisikia Neno aliangushwa kwa jiwe na kijana. Yehoshafati alipolisikia Neno maadui zake waliangamizana wenyewe vitani. Nehemia alipolisikia neno, Hekalu na ukuta vilijengwa kwa wakati. Esta alipolisikia Neno aliliokoa taifa zima. Ayubu alipolisikia Neno, hata mateso yake yalimstahili: Alimwona Mungu na baraka zake zilirejeshwa tena. Daudi alipolisikia Neno alifarijiwa, akasalimishwa na kusamehewa kutokana na jinai mbaya kwa mtu kudiriki kufanya. Sulemani alipolisikia Neno lilikuwa la thamani kuliko fedha na dhahabu. Mwanamwali katika wimbo wa Sulemani alipolisikia Neno aliangukia katika penzi na mpenzi wake wa milele. Isaya alipolisikia Neno midomo yake ilitakaswa na akatabiri habari za mwokozi ambaye angekufa kwa dhambi zetu. Yeremia alipolisikia Neno Waisraeli walipaswa kuwa watumwa kwa ajili ya dhambi zao; Lakini baadaye mabwana zao waliangushwa. Shadraka, Meshaki, na Abednego walipoliona Neno, alikuwa nao ndani ya tanuru kali la maisha. Danieli alipoliona Neno, Liliyafunga makanwa ya simba. Ezekieli na manabii wengine walipolisikia Neno, walimwona Mfalme ajaye ambaye agewaokoa kutoka kwa adui zao.

Yule mtu kipofu alipoligusa Neno, aliona. Neno lilipomgusa mkoma, alitakasika. Mapepo yalipoliona Neno yalikimbia. Akida alipolisikia Neno, mtumishi wake alipona. Mwanamke mzinzi alipoliona Neno, alisamehewa. Kahaba alipoligusa Neno, alitakaswa na kupendwa mno. Yohana alipoliona Neno alimwona MwanaKondoo aondoaye dhambi zetu. Yohana alipoliona Neno mara ya kwanza aliliona Neno likifanyika mwili. Watu wa dini walipomwona Neno walibishana Naye nakusema ana pepo. Makutano walipomwona Neno walimchukulia kuwa hana thamani, wakayafanyia biashara maisha yake badala ya mwizi, na kumwua kwa hukumu ya mvunja sheria. Ingawa alinena huu ulimwengu ukatokea, hawakumtambua. Walimwona kama "mmwaga damu" msalabani.

Yohana alipoliona Neno katika kitabu cha Ufunuo alimwona mshindi aliyeshinda mauti, kuzimu, na kaburi; Yule aliyefufuliwa kutoka kwa wafu, na kuvikwa vazi liliyofika miguuni Mwake na vazi la dhahabu katika kifua chake. Kichwa chake na nywele zake zilikuwa nyeupe kama

theluji (nyeupe kama ndani ya moto), na macho yake yaling'aa kama miali ya moto. Miguu yake iliwaka kama shaba iliyosuguliwa kama iliyosafishwa katika tanuru, na sauti yake ilikuwa kama sauti ya maji mengi. Yohana alimwona mtawala na mhukumu ulimwengu!

Shetani alionapo Neno lililofunuliwa, huona kuwa Yeye, Neno ndiye Mfalme wa wafalme na Bwana wa mabwana. Macho yake yang'aa kama mwali wa moto na juu ya kichwa chake yapo mataji mengi ya kifalme. Katika kila moja ya "vita vyetu vya mwisho" katika maisha haya, Shetani humwona na upanga mdomoni mwake juu ya farasi mweupe, amevikwa kanzu iliyochovywa katika damu. "Naye ana jina limeandikwa katika vazi lake na paja lake, MFALME WA WAFALME NA BWANA WA MABWANA" (Ufunuo 19:16).

Unahitaji kuendelea katika Neno kwa mafunzo ya Biblia yenye utangamano. Kunayo mengi sana unaweza ama waweza kujitengezea moja kwa ajili yako. ISOB inatoa kozi bure kwa njia ya mtandao ama kwa CD-ROM kwa kutumia katika kompyuta yako.⁵

Uwe halisi kwa Mungu

Sasa sikiliza sauti Yake.

“Habari, jina langu ni Yesu. Nakupenda.”

⁵International School of the Bible curriculum hupatikana bure kwenye www.isob.org, au tuma email: info@isob-bible.org

Sura 10. Kuendelea Na Kuwa Unabadilishwa.

Kubadilishwa? Kwani hivi
nilivyo nakosa gari?



Mambo mengine hubadilika papo hapo, mengine huchukua muda.

Naweza kukumbuka moja ya mambo ya kwanza aliyonifunulia Mungu nilipokutana naye mara ya kwanza lilikuwa ni vile pazia la Hekalu lililopasuka toka juu mpaka chini Yesu alipokufa msalabani (marko 15:38). Roho Mtakatifu aliitumia hiyo kunifunulia aliyotenda Yesu alipokuwa Msalabani, kuwa yalinifungulia mlango kuingia katika uwepo wa Mungu. Sikuwa na la kufanya ili kujipatia ama kustahili hili, lilikuwa kwa ujumla ni kitu Alichokifanya. Katika toleo la King James neno lililotumiwa badala ya “pasuka” ni “chana”. Nilizoea kwenda namwambia kila mmoja "pazia lilichanwa pazia lilichanwa!" Waliniangalia kama niliyekuwa katika kuendeshwa na madawa ya kulevya ama kitu kama hicho. Lakini nilijua nilichokuwa nafanya.

Nilikuwa namiliki duka wakati nilipokutana na Yesu mara ya kwanza.

Mamia ya watu waliniona nilibadilika kwa usiku mmoja! Nakumbuka mtu aliniuliza “kwa kuwa wewe sasa ni Mkristo, utaacha kufanya hili ama lile?” Nilisema “Naweza kufanya chochote nitakacho”. Na waliniangalia kwa mshangao. Kwa kupambanua swali ndani ya fahamu zao nilisema “Swala ni hili, nitakacho kimebadilika. Mambo pekee nitakayo ni yale yanayompendeza Mungu”. Sasa wakati matakwa yangu si yale yaliyo sawa, Roho Mtakatifu hunifanya kuwa kituko.

Nilikuwa "nakunywa kidogo" nilipokutana na Yesu.

Najua hili ni somo tata kwa baadhi ya mila, lakini wakati nikikwambia hivi si uchaguzi ama maoni yangu, ni vile Bwana alivyonishughulikia;

ni ushuhuda. Siku nisiyoisahau miezi kadhaa baada ya kukutana na Yesu, nilinyoosha mkono kuchukua bia ndani ya friji, na nilisikia sauti ya Roho Mtakatifu ikisema, "Hilo litanihuzunisha". Nilimwuliza kwa nini? Akasema "Kwa sababu linachukua nafasi ya kile ninachopaswa kukufanyia". Sijajuta kutokunywa pombe tangu hapo. Kwangu mimi, pombe ni moja ya "miungu mingine". Waulize waganga wa kienyeji wa Afrika na Haiti kuhusu pombe.

Mungu alibadilisha ninayotaka na nisiyotaka haraka sana.

Hata hivyo sikuwa na wazo jinsi gani hasa nilikuwa nimepotea na nilikuwa nikikabiliana na changamoto gani. Sikuwa na wazo ni kwa kiasi gani maisha yangu yalikuwa yamepotoka kutoka kwenye mpango halisi aliokuwa nao Mungu kwa ajili yangu. Nilifikiri hakika Mungu alikuwa amepata zawadi aliponipata mimi! Taratibu alibadilia nia yangu, akiniruhusu nitambue kuwa nilikuwa wa thamani sana kwake; Lakini kwamba nilihitaji kubadilika.

Kwa uaminifu naweza kukuambia baada ya kutembea na Mungu tangu 1979, kadri ninavyomsogelea ndivyo ninavyoona jinsi nilivyokuwa nimeenda mbali na mpango wake halisi kwa ajili ya maisha yangu. Unahitaji kulikabili somo hili kwa unyenyekevu mkubwa na kusudi ili kukiangusha kiburi chako nakujihesabia haki.

Kusudi la milele la Mungu kwa ajili ya maisha yako, limeelezwa katika Warumi 8:29, ambayo inasema, "Maana wale alio wajua tangu asili, aliwachagua tangu asili, wafananishwe na mfano wa Mwana wake ili yeye awe mzaliwa wa kwanza miongoni mwa ndugu wengi."

Ilichukua chini ya dakika moja kupokea uzima wa milele wa Mungu ndani ya roho yako na kumfanya Yesu Bwana, lakini itachukua maisha yako yote kubadilishwa kuwa katika mfano Wake. Kweli, unao uzima wa Mungu ukiishi ndani ya roho yako, na umesulibiwa pamoja na Kristo (Wagalatia 2:20). Kwa kweli, ulipokea haki kamili ulipopokea uzima wa Mungu maishani mwako. Usimwache yeyote akuondolee ukweli huo. Kuchukuliana juu ya ukweli huu itapooza kutembea kwako na

Mungu. Hata hivyo, kuna ukweli mwingine kwa ajili yako unaotakiwa kuutambua.

Nilipitia huzuni nyingi nikimtafuta Mungu kujua namna jambo hili linavyotenda kazi. Niliendelea kumwuliza “Iwapo yote ni kwa neema, basi, kwa nini ninapaswa nifanye kazi? Ni neema kweli, ama inachanganywa na kazi zangu na utendaji pia?”

Nimekuwa nikisisitiza Neema ya Mungu na Rehema ya Mungu.

Nimekuwa nikisisitiza kuwa hatukuwa na la kufanya ili kupata upendeleo wa Mungu ama njia yetu kuelekea Mbinguni. Hili ni kweli, na tafadhali usimwache yeyote aliondoe kwako. Soma kitabu cha Wagalatia na ugundue ujumbe Paulo aliokuwa anautoa kwa kanisa la Galatia.

Wazo rahisi la neema ni hili: Kuwa Mungu alihamia kwako na akachukua nafasi yako. Unapotenda dhambi/ama kufanya makosa, ama huwezi kutimiza mahitaji yako yoyote yawayo, ama utubu/umgeukie Yeye, na uzima wake ndani yako utaishia maisha yako. Hiyo ni neema. Anavyoishi maisha Yake ndani yako, utahisi kiwango cha utakatifu na uzima tele ukiishi ndani na kupitia wewe.

Hata hivyo kuna upande wa pili wa sarafu tunaohitaji tuuone. Kwa kuwa sasa wewe ni mwamini wa Bwana, unapaswa uwe na shauku na hamu kuishi maisha yanayomstahili Bwana. “Kwa hiyo nawasihi mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mliloitiwa” (Waefeso 4:1). Hapa Paulo mtume anawahimiza waamini wa Efeso kuishi maisha yamstahiliyo Bwana. Hili linamaanisha kuwa walikuwa na uchaguzi wa kuishi maisha yamstahiliyo Bwana.

Kabla sijalifikisha hili mbali sana, nahitaji kuweka msingi. Mungu alimwumba mtu kwa mfano wake. Moja ya vitu hivyo ni uhuru wa kuchagua ama mamlaka huru ya kujitegemea kimaamuzi. Mtu ndicho kiumbe pekee kilicho na uhuru wa utashi. Kweli, malaika walimwasi Mungu pamoja na Shetani; lakini hilo halifanani na uhuru wa utashi wa mwanadamu. Naamini kuwa huenda Mungu aliwapa malaika chaguo moja

huru la kufuata uasi wa Shetani ama kubakia Naye. Malaika walioanguka hawawezi kamwe kuchagua ukombozi kama anavyoweza mwanadamu.

Mbwa wanaweza kuchagua kwenda kushoto ama kulia, lakini lazima mara zote watende kama mbwa. Wameshawekewa programu kimbele. Hata hivyo mwamini anaweza kuchagua kutenda kama asiye mwamini hata ingawa ameshapokea roho aliyopandiwa yenye asili ya Mungu Mwenyewe. Ni kweli, uzima wa Mungu unakaa ndani ya mwamini, ila uhuru wa utashi wa mwamini bado uko hai na unaweza kuchagua kutenda alivyotenda zamani kabla hajawa mwamini.

Sipendekezi kuwa mtu atende kama mwamini ama amwigize Mungu. Hiki ni kichekesho, hakuna anayeweza kumwigiza Mungu lazima yawe ndani ya mtu huyu naye achague kuruhusu uzima wa Mungu kudhihirishwa kupitia nguvu na uweza kwa Roho Mtakatifu.

Sura hii inajadili wajibu wako kama mwamini. Kwa vyovyote sishauri namna yoyote ya sheria ama “mpango wa utendaji” ili kupata kibali kwa Mungu. Neema ya Mungu haijawahi kamwe kuwa “rahisi”. Mungu alilipa gharama ya juu kabisa kukuokoa kutoka kwa Shetani na ulimwengu.

Kama unahisi kuwa waweza kuishi maisha yako kama mwamini namna ile ile ulivyoishi zamani, yawezekana kwamba kamwe hujamfanya Yesu kuwa Bwana kwa uhalisi, na yawezekana kamwe hujazaliwa mara ya pili. Hakuna anayeweza akakuhukumu, hata hivyo chukua hili kama onyo lenye rehema. Usidanganyike, huwezi kuwa Mkristo mwenye afya isipokuwa unashauku kufanana na sura ya Yesu. Elewa, sikusema, hukuwa na afya kama hukuwa mkamilifu. Nilisema uwe na shauku ya kubadilishwa kuwa katika mfano Wake. Hakikisha hauendi kwa “miungu mingine” kutafuta mahitaji yako. Hilo ndilo chanzo mara nyingi cha msimamo usio na afya. Uwe mkweli kwa Mungu katika hili. Ni swala la uzima wa milele na kifo cha milele.

Waweza kuchukua somo kutoka kwa Paulo Mtume aliyekuwa na shauku ya kufanana na chapa ya Yesu, hata hivyo aliendelea kuwa na mapungufu. Paulo alisema katika Warumi 7: 15-25 “ Maana sijui nifanyalo; kwa sababu lile nilipendalo, silitendi; bali lile nilichukialo ndilo ninalolitenda. Lakini kama nikilitenda lile nisilolipeda, naikiri ile sheria ya

kuwa ni njema. Basi sasa si mimi nafsi yangu ninayetenda hilo, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Kwa maana najua ya kuwa ndani yangu, yaani, ndani ya mwili wangu, halikai neno jema; kwa kuwa kutaka nataka, bali kutenda lililo jema sipati. Kwa maana lile jema nilipendalo, silitendi; bali lile baya nisilolipenda ndilo nilitendalo. Basi kama lile nisilolipenda ndilo nilitendalo, si mimi nafsi yangu nilitendaye, bali ni ile dhambi ikaayo ndani yangu. Basi nimeona sheria hii, ya kuwa kwangu mimi nitakaye kutenda lililo jema, lipo lililo baya. Kwa maana naifurahia sheria ya Mungu kwa utu wa ndani; lakini katika viungo vyangu naona sheria iliyo mbali, inapiga vita na ile sheria ya akili zangu, na kunifanya mateka ya ile sheria ya dhambi iliyo katika viungo vyangu. Ole wangu maskini mimi! ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti? Namshukuru Mungu, kwa Yesu Kristo Bwana wetu. Basi, kama ni hivyo, mimi mwenyewe kwa akili zangu naitumikia sheria ya Mungu, bali kwa mwili wangu sheria ya dhambi".

Wewe sio wawili wanaokaa ndani ya mwili mmoja! Wakristo wengine kwa kweli huamini hivyo. Hapana, wewe ni kiumbe kipya na utu wako wa zamani umefishwa. Paulo hakusema alikuwa na asili mbili. Alisema kulikuwa na “sheria ya dhambi” ikitenda kazi katika viungo vya mwili wake, iliyopigana vita na sheria ya akili zake.

Naamini kuwa utu wako wa zamani ni kama mti uliokwisha katwa, lakini bado una matawi ambayo hayajafa bado. Bado ungali na mikanda ya kumbukumbu za zamani ndani ya ubongo wako ambayo ingali inataka kucheza. Kushindana kwako kwingi hasa kutakuwa dhidi ya akili yako. Hata hivyo, waweza kushughulikia ngome za kiroho ama ngome za kipepo. Tutazijadili hizi katika sura zijazo.

Hivyo tunampendezaje Mungu, na wajibu wetu ni nini? Fuata mfano wa Paulo wa jinsi alivyopambana na hali ya kutokuamua kulikoelezwa katika Warumi 7. “Sasa, basi, hakuna hukumu ua adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu. Kwa sababu sheria ya Roho wa uzima ule ulio katika Kristo Yesu imeniacha huru, mbali na sheria ya dhambi na mauti. Maana yale yasiyowezekana kwa sheria, kwa vile ilivyokuwa dhaifu kwa sababu ya mwili, Mungu, kwa kumtuma Mwanawe mwenyewe katika mfano wa mwili ulio wa dhambi, na kwa sababu ya dhambi, aliihukumu

dhambi katika mwili; ili maagizo ya torati yatimizwe ndani yetu sisi, tusioenenda kwa kufuata mambo ya mwilii, bali mambo ya roho. 5 Kwa maana wale waufuatao mwili huyafukiri mambo ya mwili; bali wale waifuatao roho huyafikiri mambo ya roho". (Warumi 8:1-5).

Kwanza, twahitaji kujua kuwa tumekwisha wekwa huru. Paulo alitumia kielelezo katika Warumi 7 cha mateso ya Mrumi wakati aliposema, "Ni nani atakayeniokoa na mwili huu wa mauti" (Warumi 7:24). Palikuwa na desturi ya kirumi ya kuifungamanisha maiti na mwili wa muuaji wake. Kisha muuaji angejaribu kuishi maisha yake kwa namna hii. Hata hivyo, haingekuwa muda mrefu sana kwa mauti kuenea katika mwili wake (muuaji) na kumwua yeye pia. Lakini gundua Paulo anasema "Ashukuriwe Mungu [aliniweka huru]... kwa njia ya Yesu Kristo Bwana wetu!" (Warumi 7:25).

Kwa maneno mengine PAULO alifahamu kuwa mwili wake mfu ulikuwa kisheria umeshaachiwa, na kile alichokuwa anashugulika nacho ni yale mabaki tu ndani ya ufahamu na viungo vyake. Ukilitunza hili katika ufahamu, utaishi katika ushindi.

Kinachofuatia, wahitaji kuyaangalia maneno ya Paulo katika Warumi 8:1-5 yaliyoelezwa hapo juu. Ambayo ni kuishi "kwa kufuata mambo ya Roho, na dunia mambo ya Roho".

Kisha lazima ujifunze kutembea katika Roho, ama kuishi kwa kufuata mambo ya Roho. Hilo linamaanisha nini?

Wagalatia 5:16 inasema "Basi nasema, Enendeni kwa Roho, wala hamtazitimiza kamwe tamaa za mwili".

Warumi 8:1 inasema, "Sasa, basi, hakuna hukumu ua adhabu juu yao walio katika Kristo Yesu, wasioenenda kwa kuyafuata mambo ya mwili bali kwa kuifuata Roho".

Kuenenda katika Roho ni njia rahisi, ila ya tofauti ya kuishi. Ndiyo njia rahisi kabisa niujuayo ya kuwa mwenye haki kila siku. Utaratibu unakweda namna hii.

1. Unaendelea kujiangalia katika Neno la Mungu (kioo) na kumwuliza Mungu kukuonesha jinsi ya kuishi. Mwulize, na utafute viwango vya maisha kwa ajili yako. Kwa mfano, Anasema, kutosema uongo, kuwatendea rafiki zako kwa upendo, kujitiisha kwa wazazi na

waalimu wako, kuwatendea kaka na dada zako kwa fadhili, kutolewa, kutokuwa mbinafsi, kutokuwa na hasira, kusamehe mara zote pasipo kujali ni jambo gani, n.k.

2.Ukusodie kuishi namna Mungu atakavyo wewe uishi, ukijua kuwa waweza kuishi maisha yamstahiliyo Bwana peke yake kupitia uzima wa Yesu kuishi ndani yako.

3.Ukishindwa na uwe kwa ujumla mwaminifu kwako mwenyewe, kwa Mungu na kwa wengine wanaokuzunguka. Tubu (geuka) haraka. Ahadi ni kwamba ukitubu(ukigeuka) ufalme wa Mungu “umekaribia”, ama unafikika.

4.Kiri dhambi zako kwa Mungu. 1Yohana 1:9 inasema, “Tukiziungama dhambi zetu yeye, ni mwaminifu na wa haki hata atuondolee dhambi zetu”.

5.Kiri yale Neno la Mungu lisemayo kuhusiana na hali yako. Wagalatia 2:20 inasema, “Nimesulubiwa pamoja na Kristo; lakini ni hai; wala si mimi tena, bali Kristo yu ndani yangu; na uhai nilio nao sasa katika mwili, ninao katika imani ya Mwana wa Mungu, ambaye alinipenda akajitoa nafsi yake kwa ajili yangu”.

6.Unapoendelea kuishi namna hii zile tabia na njia za zamani za dhambi zitaanza kupotea. Neema ya Mungu itachukua nafasi nakukupatia tabia za Mungu badala ya tabia zako za zamani.

7.Neema “huchukua nafasi” kwaajili ya dhambi zako. Haukuwa mwenye haki kwa matendo uliyokuwa ukiyafanya. Kwa hiyo haki yako ingalipo; ni kwamba tu inauchafu juu yake. Wakati unaenenda kwa Roho, Mungu hukupatia neema kwa ajili ya makosa yako. Huichukua adhabu ya dhambi ambayo mara zote ungeichukua, na hukupatia baraka ambayo hukuistahili.

"Kuenenda katika Roho" kwaweza pia kuelezwa kama vile Yesu alivyokuita “kujitwika msalaba wako kila siku”. “Akawaambia mtu yeyote akitaka kunifuata na ajikane mwenyewe, ajitwike msalaba wake kila siku anifuata”. (Luka 9:23). Kumbuka kuwa uhusiano wako na Mungu unamsingi katika agano la damu. Miaka elfu mbili iliyopita Alijitwika msalaba makusudi Akamwage damu kwa ajili ya agano. Sasa, ili kufanya

agano lifanye kazi na kulifanya liwe kitu halisi maishani mwako, lazima ujitwike msalaba wako, ambacho ni kitendo cha “kumwaga damu”.

Gundua kuwa Yesu alisema “jikane mwenyewe”. Maneno hayo mawili yakichukuliwa kwa pamoja kwa urahisi yana maanisha useme hapana kwa “utu wa kale”. Lazima useme hapana kwa matakwa yako mwenyewe, elimu na hisia na uzibadilishane na kusudi la Mungu, na nia ya Mungu na hisia za Roho Mtakatifu zinazoishi ndani yako. Nakuhakikishia kuwa hili halikufanyi wewe uwe mashine au roboti, bali linachanganya tabia za Mungu na utu wako wa kipekee na kukufanya uwe mtu uliyetimia.

Kanuni mojawapo ninazozitunza ndani ya nia yangu ni kutokuishi kwa kanuni. Wakolosai 2:20-23 inasema, “Basi ikiwa mlikufa pamoja na Kristo mkayaacha yale mafundisho ya awali ya ulimwengu, kwa nini kujitia chini ya amri, kama wenye kuishi duniani, Msishike, msionje, msiguse; (mambo hayo yote huharibika wakati wa kutumiwa): hali mkifuata maagizo na mafundisho ya wanadamu? Mambo hayo yanaonekana kana kwamba yana hekima, katika namna ya ibada mliyojitungia wenyewe, na katika kunyenyekea, na katika kuutawala mwili kwa ukali; lakini hayafai kitu kwa kuzizuia tamaa za mwili”.

Kama umewahi kujaribu kuachana na tabia fulani, kama vile kula kupita kawaida, utaelewa andiko hili. Kadri unavyoifikiria tabia hiyo mbaya ama hata dhambi ndivyo inavyozidi kuwa na nguvu. *Badala* yake lazima tufikirie ama tutazamishe mawazo yetu kwenye vitu vingine ama watu wengine.

Hili limeelezwa katika Wakolosai 3:1-5. ambayo inasema “Basi mkiwa mmefufuliwa pamoja na Kristo, yatafuteni yaliyo juu, Kristo aliko, ameketi mkono wa kuume wa Mungu. Yafikirini yaliyo juu, siyo yaliyo katika nchi. Kwa maana mlikufa, na uhai wenu umefichwa pamoja na Kristo katika Mungu Kristo atakapofunuliwa, aliye uhai wetu, ndipo na ninyi mtafunuliwa pamoja naye katika utukufu. Basi, vifisheni viungo vheni vilivho katika nchi, uasherati, uchafu, tamaa mbaya, mawazo mabaya, na kutamani, ndiyo ibada ya sanamu”.

Mara zote utaelekea kuwa kama chochote ambacho utakikazia macho yako!

Je, unashauku na hamu ya kuishi maisha yanayo mstahili Bwana? Kama sivyo, uwe halisi kwa Mungu. Mwambie kuhusu hilo naye atakupatia. Kama una shauku hiyo, kumbuka, ishi maisha bila hukumu na “enenda kwa Roho”.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura ya 11. Ubatizo Wa Maji

Haya mambo ya kubatizwa yanatisha!



"Batiza" maana yake imeelezwa katika Strongs Concordance kama ifuatavyo:

"Baptizo. Usilichanganye na neno Bapto. Mfano ulio wazi kabisa ambao unaonesha maana ya baptizo ni aya kutoka kwa Myunani Nicander aliyekuwa mtunga mashairi na tabibu aliyeishi miaka 200 K.K. Ni maelezo ya namna ya kuandaa pickle na yanasaidia kwa kuwa yanatumia maneno yote mawili. Nicander anasema kuwa ili kutengeneza pickle, mboga za majani lazima kwanza 'zichovywe' (bapto) ndani ya maji yanayochemka na kisha 'zibatizwe' (baptizo) ndani ya maji ya limao. Maneno yote yanahusu kuzamisha mboga za majani ndani ya kimiminika. Lakini la kwanza si la kudumu. La pili, ambalo ni kubatiza mboga linatokeza badiliko la kudumu.

Linapotumiwa katika Agano Jipya, neno hili mara nyingi zaidi hurejea muunganiko na kuhusiana kwetu na Kristo kuliko ubatizo wetu wa maji. Mfano, Marko 16:16. 'Aminiye na kubatizwa ataokoka'. Kristo anasema kukubali tu kwa akili hakutoshi. Lazima kuwepo muunganiko naye, badiliko la kweli, kama vile mboga za majani kuwa pickle.

Jarida la Mafunzo ya Biblia. James Montgomery Boice, Mei 1989."

Ubatizo ni kitendo cha kuonekana, cha nje kinachowakilisha kile kinachotendeka ndani yako, ambacho ni, kifo, kuzikwa na ufufuo.

Mathayo 28:19 inasema , "Basi, enendeni mkawafanye mataifa yote

kuwa wanafunzi, mkiwabatiza kwa jina la Baba, na Mwana, na Roho Mtakatifu". Kwa halisi hii inamaanisha kuzamisha ndani ya jina la Mungu na sifa za Mungu Mwenyewe. Ubatizo ni kitendo kinachoendelea maisha yote katika kubadilika na kuwa katika chapa ya Yesu, ambacho kinajumuisha kutumbukizwa ndani ya Maji.

Kama ungewekwa ndani ya bwawa la maji na ukafa kwa kukosa hewa na kisha ukazaliwa tena na uzima wa Mungu ndani yako, huo ndio ungekuwa mfano mzuri wa kile kilichotokea kwako katika ulimwengu wa roho. Ndiyo sababu Yesu anatutaka tubatizwe. Inaonesha ulimwengu, mapepo, mwili wetu wa nyama, mwili, na akili kilichotendeka kwetu kwa uhalisi katika ulimwengu wa roho. Kitendo halisi cha kwenda ndani ya maji na kutoka kwa kweli hakitendi jambo lolote kwako, isipokuwa kukupa nafasi ya kumtii Mungu.

Ubatizo haukupi wokovu.

Ni tendo la utii ambalo linakuongoza kwenye wokovu wa juu zaidi. Wokovu haumaanishi tu uzoefu wa mwanzo wa kuzaliwa mara ya pili. Wokovu ama kuokolewa, inatokana na neno la Kiyunani ambalo linamaanisha kuondoa kitu kwenye hatari na kukifanya kiwe kikamilifu. Baada ya uzoefu wetu wa kwanza wa wokovu, tunahitaji kusogea mbele katika "kufanywa wakamilifu" ama wokovu. Ubatizo ni moja ya vitendo vya utii ambacho kinafungua njia ili kukuza uhusiano wako na Mungu. Ni wa muhimu sana, lakini si kupita vyote katika kwenda kwetu Mbinguni.

Pia ubatizo ni tukio la hatua kwa hatua na si la mara moja.

Neno "jina" humaanisha tabia za mtu fulani. Ubatizo katika Jina la Yesu, jina la Baba na jina la Roho Mtakatifu, kwa uhalisi humaanisha kuzamishwa ndani ya tabia ili uwe kama wao. "Aminiye na kubatizwa (kuzamishwa ndani ya tabia za Baba, Yesu na Roho Mtakatifu) ataokoka (atafanywa kamili, atatolewa katika hatari na kufananishwa na chapa kamili ya Yesu), bali asiyeamini atahukumiwa" (Marko 16:16).

Paulo aliongelea kuhusu kubatizwa kwetu na Kristo wakati tulipokuwa tunazaliwa mara ya pili. Warumi 6:4 inasema, "Basi tulizikwa pamoja naye kwa njia ya ubatizo katika mauti yake, kusudi kama Kristo alivyofufuka katika wafu kwa njia ya utukufu wa Baba, vivyo hivyo na sisi tuenende katika upya wa uzima".

Wakolosai 2:12 inasema, "Mkazikwa pamoja naye katika ubatizo; na katika huo mkafufuliwa pamoja naye".

Yesu alibatizwa. Hakuwa na dhambi, bali hii ilikuwa ni ishara kuwa anakwenda kubainisha na kufyonza dhambi zetu.

Mathayo 3:13-17 inasema, "Wakati huo Yesu akaja kutoka Galilaya mpaka Yordani kwa Yohana ili abatizwe. Lakini Yohana alitaka kumzuia, akisema, 'Mimi nahitaji kubatizwa na wewe, nawe waja kwangu? Yesu akajibu akamwambia, Kubali hivi sasa; kwa kuwa ndivyo itupasavyo kuitimiza haki yote'. Basi akamkubali. Naye Yesu alipokwisha kubatizwa mara akapanda kutoka majini; na tazama, mbingu zikamfunukia, akamwona Roho wa Mungu akishuka kama hua, akija juu yake; na tazama, sauti kutoka mbinguni ikisema, 'Huyu ni Mwanangu, mpendwa wangu, ninayependezwa naye.'"

Yesu alisema kuhusu mateso yake kuwa ni ubatizo wake mwingine. Mathayo 20:22 inasema, "Yesu akajibu akasema, 'Hamjui mnaloliomba. Je! mwaweza kunywea kikombe nitakachonywea mimi?' Wakamwambia, 'Twaweza.'"

Wengine wanabishana kuhusu kunyunyiziwa ama kuzamishwa. Naweza kukwambia kuwa katika nchi za Kiislamu watu wanapompokea Yesu kama Bwana, wale wanaobatizwa kwa kuzamishwa majini ndio wale wanao uawa na kuteswa. Huwezi kubadilishwa na kuwa katika mfano wa mtu mwingine kwa "kunyunyiziwa" na tabia zake; lazima uzamishwe ndani ya tabia na mifano yake.

Huhitaji kubatizwa na mtu maalum wa kiroho ama dini. Rafiki alinibatiza mimi katika bwawa la kuogelea la nyuma ya uwanda. Nami nimewabatiza baadhi ya watoto wangu mtoni.

Yohana alisema juu ya ubatizo katika Roho Mtakatifu kama aina ingine ya ubatizo.

Luka 3:16 inasema, "Yohana alijibu akawaambi wote, Kweli mimi nawabatiza kwa maji; lakini yujua mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahihili kulengeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto". Ubatizo huu umezungumziwa katika sura ingine.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura ya 12. Njia Mpya ya Maisha: Tabia Mpya.



Kabla sijaenda katika wazo hili la maisha na tabia mpya, nataka kusimika kitu fulani kuhusu kile ninachohisi sana. Kinahusika na mila mbali mbali. Ninaandika kitabu hiki nikiwa ni mtu ninayetokea U.S.A. Najua watu wengi kutoka mila tofauti tofauti watakisoma kitabu hiki. Kumekuwa na nyakati nyingi katika historia ambapo wamishenari wa Magharibi wameweka mila zao pamoja na Injili; kwa mfano katika Afrika. Uharibifu mkubwa umefanywa kutoka katika malengo mazuri.

Rafiki yangu mzuri kutoka Afrika Kusini anauliza swali, "Tunachomeka mila katika injili ama Injili katika mila?" Mmarekani aweza kumkosoa mama katika nchi za ulimwengu wa tatu kutokana na kumnyonyesha mtoto awapo ndani ya kanisa? Je, Mwafrika amkosoe Mmarekani kwenda katika kumbi za sinema na kulipia gharama kwa ajili ya viburudisho (ambalo halingesikika katika mila nyingi)?

Kanisa la mwanzo lilikumbana na mgogoro huu pia kuhusiana na Wayahudi na wa Mataifa. Viongozi walifanya mkutano wa kihistoria uliojulikana kama "Baraza la Yerusalemu" katika Matendo sura ya 15. Wakaja na makundi mawili tu ambayo yalipita tofauti zao za kimila na hayo yalikuwa; (1) wajiepushe na vitu vilivyotolewa sadaka kwa sanamu, damu, vitu vilivyosongolewa, na (2) uasherati.

Rafikia yangu kutoka Afrika Kusini na mimi tulilijadili swala hili na tukakubaliana namna hii: si kazi ya mmishenari ama mwalimu anayemrudi Mkristo kujaribu kubadilisha mila yake. Hiyo ni kazi ya Roho Mtakatifu. Tunaamini Roho Mtakatifu hatabadili mila ya mtu isipokuwa katika maeneo yale yanayoharibu uhusiano wa mwamini na Yesu. Mfano, kucheza wakati wa ibada kanisani hakuwezi kuathiri uhusiano wa mtu na

Yesu. Hata hivyo kutokusamehe kutaathiri uhusiano. Kuishi maisha yasiyo na msingi katika kumpenda Mungu na kuwapenda wengine kutaathiri uhusiano, ambapo, kunyonyesha kanisani hakutaathiri.

Roho Mtakatifu hataki wakristo wote wafanane. Lengo, lake pekee ni kumfanya kila mwamini awe karibu na Yesu iwezekanavyo. Roho Mtakatifu atamshawishi tu mtu kuacha tabia inayo muumiza. Endapo mwamini mwenza akifanya marudio hayo pengine haitakuwa kwa moyo wa upendo ambao Mungu peke yake anao. Roho Mtakatifu hufanya marudio yanayohitajika kwa faida na upendo kwa mtu huyo.

Mtu hana uhalali kumrudi mwingine kabla kwanza ya kuwa na uhusiano wa karibu na wakuaminika na mtu huyo; na kisha marudio yafanyike kwa maelekezo na kwa upendo.

Ukamilifu.

Mojawapo ya tabia za Mungu zilizoelweka vibaya ni ukamilifu Wake. "Ukamilifu", ni neno linalomaanisha namba kamili. Namba kamili haina sehemu, ni nzima na iliyotimia. Ukamilifu hubeba maana ya kuwa bila uchafu, unyoofu, uaminifu, kamili, shabihiana, iliyomalizwa, iliyotimia, na inayoheshimika. Mtu mkamilifu hana uchafu; hajachanganywa na kiasi cha kweli na kiasi cha uongo. Hajachanganywa na kiasi cha uaminifu na kiasi cha upotovu.

Mungu ni mkamilifu na anatamani kuzifanya tabia hizo ndani yetu kadri tunavyozidi kukua ndani yake. Wakati mwingine watu huanza kutembea na Bwana baada ya kuishi pasipo ukamilifu na hivyo wanachukulia kuwa Mungu ni kama wao tu. Hata hivyo, Mungu anataka kutubadilisha kuwa katika mfano Wake; kuwa watu wakamilifu.

Jambo la kwanza Mungu aliloanza kulitenda maishani mwangu, baada ya kuwa Bwana wa maisha yangu lilikuwa kuniondolea upotovu na kukosa ukamilifu. "Heri wenye moyo safi [wasiochanganywa, wakamilifu], maana watamwona Mungu". (Mathayo 5:8). Kama kweli unataka kumwona Mungu tafuta moyo safi!

Nilikuwa nimemfahamu Bwana kwa miezi kama sita tu wakati alipoanza kunifunulia mambo tangu yaliyopita ambayo yalihatiji malipizi. Kwa tabia nilikuwa silipi kiasi kamili cha kodi zangu za serikali kabla

sijawa Mkristo (uite huu ni udanganyifu tu). Bwana alinielekeza nilipe kiasi chote nilichodanganya serikali.

Kiasi nilichokadiria kilikuwa zaidi ya kile ambacho ningeweza kulipa, lakini hata hivyo nikamwambia mhasibu wangu afanye marekebisho ya lazima. Akanishauri nisifanye hivyo, kwani ilikuwa ni maoni yake kuwa nisingekamatwa. Nilimwambia kuwa tayari Mungu ameshanikamata. Hakujua cha kufikiri kuhusu hilo! Aliendelea na akanipatia ripoti ya kiasi cha nyuma. Tangu hapo nimebadili wahasibu!

Kama ilivyojitokeza, huo ulikuwa mwaka ambao sheria mpya zilitolewa, kutozwa kodi kubwa kwa ajira za wanafunzi. Nilikuwa namiliki biashara ya rejareja na nilikuwa nimeajiri dazani za wanafunzi. Kodi hiyo ilikwangua kiasi chote nilichomiliki.

Kwa kuongezea, Bwana alinipa ahadi katika Mathayo 17:27 ambayo inasema, "Lakini tusije tukawakwaza, enenda baharini ukatupe ndoana, ukatwae samaki yule azukaye kwanza; na ukifumbua mdomo wake utaona shekeli; ichukue hiyo ukawape kwa ajili yangu na kwa ajili yako". Kila mwaka tangia hapo (1980), nimepokea muujiza wa aina fulani wakati wa kulipa kodi yangu ulipofika! Huwa naita hiyo "kupata samaki mwenye shekeli mdomoni mwake" kwa ajili yangu. Mhasibu wangu mpya hupenda kutazamia "samaki" kila mwaka!

Biblia imesheheni ahadi kwa watu wakamilifu!

"Aendaye kwa unyofu huenda salama; bali apotoshaye njia zake atajulikana" (Mithali 10:9).

"Na wewe ukienda mbele zangu kama alivyokwenda Daudi baba yako, kwa ukamilifu wa moyo, na kwa adili, kufanya hayo yote niliyokuamuru, na kuzishika sheria zangu na hukumu zangu, ndipo nitakapokifanya imara kiti cha ufalme wako juu ya Israeli milele..." (1Wafalme 9:4-5a).

Hii hapa ni ahadi kwa ajili ya watoto wako. "Mwenye haki aendaye katika unyofu wake, watoto wake wabarikiwa baada yake" (Mithali 20:7).

Yesu ni mkamilifu. " Hata walipofika walimwambia, Mwalimu, twajua ya kuwa wewe u mtu wa kweli, wala hujali cheo cha mtu; kwa maana hutazami sura za watu; lakini katika kweli waifundisha njia ya

Mungu" (Marko 12:14). Walijua Yesu alikuwa mtu mkamilifu mtu mkamilifu kwa kuwa waligundua kuwa watu hawakumyumbisha. Huwezi kumpedeza Mungu na wanadamu. Hakika utaama mmoja wapo.

"katika mambo yote ukijionesha wewe mwenyewe kuwa kielelezo cha matendo mema, na katika mafundisho yako ukionyesha usahihi na ustahivu" (Tito 2:7).

Huenda ikaonekana kuwa ni vigumu kuwa mtu mkamilifu, hasa wakati wa miezi na miaka michache ya kwanza ya ukristo wako, lakini hii ndiyo njia pekee ya kuwawezesha kuendelea wewe na Mungu. Ukweli unaweza kukuweka huru, lakini kwanza unaweza kukuweka katika hali mbaya. Hata hivyo mara zote huwa ni wa thamani!

Pesa ni mojawapo ya kipimo muhimu cha kujitoa kwetu kwa Mungu.

" Hakuna mtumishi awezaye kutumikia mabwana wawili; kwa maana, ama atamchukia huyu na kumpenda huyu, ama atashikamana na huyu na kumdharau huyu. Hamwezi kumtumikia Mungu na mali" (Luka 16:13). Lile neno "mali" laweza kumaanisha fedha. Kwa usahihi zaidi linajumuisha wazo lote la utajiri ama fahari ya kidunia. Yesu alitumia muda mwingi kuongelea kuhusu Mbingu na Jehanamu.

Alimwambia kijana mtawala tajiri katika Mathayo 19, kuwa dini yake, madaraka, ushawishi na ujana visingempatia uzima wa milele. Yesu alimwambia kutoa vyote alivyokuwa navyo awape maskini na aje amfuate. Yule mtawala hakuweza kufanya vile Yesu alivyomwambia. Mungu hatuambii siku zote kutoa pesa zetu zote, bali hututaka kuvisalimisha vyovyote tulivyo navyo ambavyo vingeweza kuchukua nafasi ya Mungu. Mtu huyu alikuwa akitumainia "miungu mingine".

Yesu kamwe hakuniambia kuzitoa pesa zangu, ila kwa hakika nilifanya. Nikiangalia nyuma naweza kuona kuwa alikuwa ni Mungu aliyenishawishi. Niliingia kwenye msisimko wa utoaji nilipokuja mara ya kwanza kwa Mungu. Iliwachanganya baadhi ya watu, lakini Mungu alisema nami wakati senti ya mwisho ilipomalizika. Akasema "Sasa umepanda kiharibikacho, utavuna kisichoharibika" (1Wakorintho 15). Naweza kukwambia kwamba tangu 1979, Mungu amekuwa mwaminifu

kwa lile aliloniambia! Kulikuwa na nyakati ambazo haikuonekana kama angekuwa mwaminifu, lakini mara zote alikuwa.

Mungu hutaka ufanikiwe . Ingawa anaangalia sana tabia na ukamilifu wako kuliko anavyoangalia faraja yako kifedha. Neno "mafanikio" hubeba mzizi wa maana ya ukamilifu. Huwezi kuwa na mafanikio ya kimungu pasipo kuwa na ukamilifu. "Mpenzi naomba ufanikiwe katika mambo yote na kuwa na afya, kama vile roho yako ifanikiwavyo" (3Yohana 1:2). Nimeshajifunza kuwa mafanikio ya roho ndiyo huja kwanza na ndilo jambo muhimu zaidi. Mafanikio yote ya vitu vya kuonekana ambavyo Mungu ameviweka kwa ajili ya maisha yako vitakuwa ni mmiminiko unaotokana na maisha ya roho yako.

Mafanikio ya vitu vinavyoonekana yaweza kumaanisha vitu tofauti tofauti kwa kila mila, ingawa kwa Mungu naamini ina maana rahisi sana: kuwa na vyanzo vya kutosha ili kutendea kazi wito wako, na kuwa na ziada ya kuwapa maskini na kutoa kwa ajili ya Injili. Pia tumeitwa ili kuibariki Israeli!

Kuna mengi ya kusema kuhusu fedha, hata kitabu chote hiki kisingetosha. Hata hivyo nitagusia baadhi ya mambo ya muhimu.

Kutoa zaka

"Leteni zaka kamili gharani ili kiwemo chakula katika nyumba yangu, mkanjaribu kwa njia hiyo, asema BWANA wa majeshi; mjue kama sitawafungulia madirisha ya mbinguni na kuwamwagieni baraka, hata isiwepo nafasi ya kutosha ama la" (Malaki 3:10).

"Zaka" humaanisha moja ya kumi. Yapaswa urudishe moja ya kumi ya faida yako, ghalani. Neno 'ghala' humaanisha jengo la kutunzia silaha, ambapo tunatoa silaha zetu. Hili linarejea kwenye Neno la Mungu. Hasa, kulingana na Agano la Kale, unapaswa kutoa zaka kwa "kuhani wako". Kuhani wako wa Agano jipya ni Yesu. Unapaswa kutoa 10% yako kwa Yesu (kwa maombi) na umruhusu akuambie ni wapi pa kuipeleka. Sehemu salama ni katika kusanyiko lako la mahali pamoja, mahali ambapo huwa unapokea upako. Mambo makuu ni toa zaka, toa sadaka, na usikilize kutoka kwa Yesu.

Mbona unapaswa utoe zaka? Ni kwa vile Mungu anahitaji fedha zako? Ni kwa vile kanisa lako linahitaji fedha zako? Hapana! Hapana! Hapana!

Kanuni ya utoaji huenda namna hii: Chini ya Agano la kale, kama mtu angetoa 10% ya kwanza ya maongeo yake kwa Mungu, 90% iliyobaki ingebarikiwa. Mungu anajua fedha ni kitu cha mfumo wa kidunia na kimelaaniwa. Na pia anajua unahitaji uitumie wakati unapoishi katika sayari, Dunia. Hivyo, alitoa njia kwa fedha ili iwe baraka kwako wala si laana. Ukitoa zaka 10% ya kwanza ndipo 90% itabarikiwa na itaendelea kuizidi hata ile 100% ya kwanza.

Kama hujaajiriwa ama huna uwezo kifedha wa kutoa basi toa kitu kingine chochote. Toa zaka yako. Toa zaka ya muda wako ambao unautumia kazini. Toa angalau saa nne kwa wiki (10% ya saa arobaini) kanisani kwako na hata zaidi kwa maskini. Ama leta 10% ya chakula chako kanisani na/ama kwa maskini. Iwapo unasifa ya kuwa wewe ni mmojawapo wa "maskini", unahitaji kutafuta kitu fulani kutoa zaka na kutoa sadaka. Kama huwezi kuanzia pale ulipo, Mungu hawezi kukupa ongezeko. Unahitaji kutoa, vinginevyo, unaziwekea mipaka baraka za Mungu.

Kutoa zaka sio kutoa sadaka. 10% ya kwanza ni ya Mungu. Huwezi kumpa Mungu kile ambacho tayari ni chake. Hii ni kama kurudisha kitu ulichoazima. Tunapaswa kutoa zaidi ya zaka zetu. Tunapaswa kuwapa maskini, kutoa kwa ajili ya huduma,n.k. Kutoa (sio kutoa fedha peke yake) uwe ndio mfumo wa maisha yetu ndani ya Kristo Yesu.

Mungu ni mtoaji na hatuwezi kuishi katika sifa zake pasipo kuwa watoaji. Upendo huelezwa katika utoaji. Waweza kutaka kurejea somo la 321, la ISOB, "Utoaji zaka na Uchumi"⁶. Ungesoma pia Mambo ya Walawi 27 na pia maandiko mengine kuhusiana na zaka.

⁶International School of the Bible curriculum hupatikana bure kwenye www.isob.org, au tuma email: info@isob-bible.org

Huwezi "kumzidi utoaji" Mungu.

"Heri amkumbukaye mnyonge; BWANA atamwoko a siku ya taabu. BWANA atamlinda na kumhifadhi hai, Naye atafanikiwa katika nchi; Wala asimtie katika hali wamtakiao adui zake. BWANA atamtegemeza alipo mgonjwa kitandani katika ugonjwa wake umemtandikia" (Zaburi 41: 1-3).

"Wapeni watu vitu, nanyi mtapewa; kipimo cha kujaa na kushindiliwa, na kusukwa-sukwa hata kumwagika, ndicho watu watakachowapa vifuani mwenu. Kwa kuwa kipimo kile kile mpimacho ndicho mtakachopimiwa" (Luka 6:38).

Kufanyakazi kwa bidii dhidi ya uvivu.

Mungu kamwe hatariki uvivu. Wakristo wanaojihisi sasa "wanaishi kwa imani" na hivyo hawafanyakazi, tena wamenisumbua sana mimi. Wanahisi kama Mungu angeleta watu wawasaidie. Naweza kukwambia si Mungu anayewapa wazo hili!

Biblia inaonekana kuwa kama inaeleza uongo ambao huenda una ukweli juu ya pointi hii, lakini hakika sivyo. Inatambia kuwa iwapo hatutoi mahitaji ya familia zetu, basi sisi ni wabaya kuliko wasioamini (1Timotheo 5:8).

"Kwa kuwa hata wakati ule tulipokuwapo kwenu tuliwaagiza neno hili, kwamba ikiwa mtu hataki kufanya kazi, basi, asile chakula" (2Wathesalonike 3:10).

"Mwibaji asiibe tena; bali afadhali afanye juhudi, akitenda kazi iliyo nzuri kwa mikono yake mwenyewe, apate kuwa na kitu cha kumgawia mhitaji" (Waefeso 4:28).

Naipenda kanuni hii katika Waefeso 4:28. Lazima tufanyakazi ili tuweza kutoa. Tunapotoa tunafanyakazi katika Ufalme wa Mungu na haswa atatoa mahitaji yetu.

"Bali utafuteni kwanza ufalme wake, na haki yake; na hayo yote mtazidishiwa" (Mathayo 6:33). Yesu alifanya kazi ya useremara hadi kufikia umri wa miaka thelathini. Alikuwa katika huduma duniani kwa muda wa miaka mitatu tu.

Mungu ni wa vitendo na sio mtiaji moyo tu. Kamwe hatakuwa mshirika wa tamaa zetu za kimwili za uvivu na kuwaachia wengine watusaidie mahitaji yetu.

Endapo umo katika hitaji maalum na huwezi kujitunza mwenyewe, ndipo Mungu atatoa mahitaji yako. Kama wewe ni mlemavu, kama wewe ni mjane, kama huwezi kupata ajira, Mungu hatarajii wewe ufanye yale usiyoweza. Lakini anakutaka umtumaini Yeye na usiangalie msaada kutoka kwa watu wengine. Litumaini Neno la Mungu, na wala si vya kupewa. Kuna tofauti!

Mara zote Mungu hushughulika kwa hatua kama ilivyo katika mfano wa talanta katika Mathayo 25. Aliweka kwenye kila mkono wa watumishi wake watatu; talanta tano, mbili, na moja kila mmoja. Akawaambia kila mmoja wao azitumie zile alizompa. Aliporudi, aliwapa thawabu, wale waliozitia na wakawa na zaidi, na akawaambia kwenda kufanya hivyo tena. Nadhani wakati aliporudi tena, thawabu iliendelea kuongezeka ukubwa. Hata hivyo, mtumishi yule mmoja aliyeificha talanta na hakuitumia alitwa mvivu. Sio tu hakupewa thawabu, hata alipoteza ile talanta aliyokuwa nayo.

Mungu huheshimu uchapa kazi

Mungu anaheshimu kule kuwa mwaminifu kwa kile tulicho nacho leo mkononi. Mungu huheshimu uvumilivu ambao una maanisha kustahimili kwa kipindi kirefu. Uaminifu na ustahilivu hujenga tabia ambazo Mungu huzitua.

Kama huna uhakika wa kile Mungu anachotarajia kutoka kwako ama hata asichotarajia, nenda ukamwulize. Ataufunua mpango wake kwa maisha yako. Uwe halisi kwa Mungu.

Hadi hapa nimeshashughulikia njia mpya za ukamilifu wa mtu, jinsi ya kushughulika na fedha, na kushughulika na kazi.

Sasa nakwenda kuzungumza juu ya mahusiano binafsi.

Hili laweza kuwa kuwa moja ya vikwazo vikubwa katika mwendo wako wa ukristo. Naweza kuonesha kuwa iwapo maisha yako binafsi ya faragha na Yesu yanaenda vizuri, basi maisha yako ya nje katika

mahusiano pia yataenda vizuri. Hata hivyo ukijitahidi sana kwa yale maisha ya nje huku mahusiano na maisha ya faragha na Mungu hayana mwingiliano na Yeye, maisha yako ya nje yatashindwa.

Usiwarubuni watu.

Usiruhusu wewe mwenyewe urubuniwe. Huu ni moja ya ugonjwa mkubwa sana duniani leo. Mungu harubuniwi, wala kamwe habariki kurubuni. Shetani ndiye hutumia mbinu hii nawe usitake kutumiwa naye!

Jinsi ya kushughulika na marafiki zako wa zamani. "Msiipende dunia, wala mambo yaliyomo katika dunia. Mtu akiipenda dunia, kumpenda Baba hakumo ndani yake" (1Yohana 2:15). Pengine kwa muda mrefu umekuwa na kundi la marafiki ambao walikushawishi mabaya. Kuna nafasi nzuri sana kwamba huenda Mungu atakutaka kupangilia tena urafiki wako. Kunayo pia nafasi nzuri sana kwamba kama kweli utakuwa imara kwa Mungu, wengi wa marafiki zako wa zamani watakuacha na hawatataka kufanya jambo lolote na wewe.

Yesu alisema kuwa Anataka tuwe ulimwenguni lakini si wa ulimwengu. Anataka tuwashawishi watu waliopotea wa ulimwengu, lakini hataki wao watushawishi sisi.

Yesu alisema, "Mimi siombi kwamba uwatoe katika ulimwengu; bali uwalinde na yule mwovu. Wao si wa ulimwengu, kama mimi nisivyo wa ulimwengu" (Yohana 17:15,16).

Uwe mkweli kwa rafiki zako. Waombe msamaha kwa kutokuwa rafiki wa kweli kipindi kilichopita. Wajulishe kilichotokea kwako. Usitandaze 'mtego wa kidini' juu yao; uwe mkweli tu ushuhuda wako. Nyenyekea na uwe na roho iliyoshuka na iliyo na upole.

Ikiwezekana wape kitu cha kusoma, kinachowaambia kuhusiana na Injili. Waombe rafiki zako. Endelea kuwaandikia, ila usiwahubiri. Waambie tu kile Mungu anachotenda katika maisha yako.

Kama una rafiki ambaye ulikuwa na uhusiano naye wa kimapenzi, uvunje mara moja. Kama mlikuwa na ahadi, kwa haraka liweke hilo "madhabahuni" pa Mungu na umruhusu aliondoe ama aliweke kama aonavyo vema.

Vipi kuhusu familia yako?

Familia yaweza kuwa ni swala lenye utata mwingi kuliko marafiki. Yesu ni mwezeshaji wa familia, hata hivyo, anaelewa kuwa kwa mazingira fulani uhusiano wa familia unaweza kuingilia mwenendo wako na Mungu.

"huku mkilitangua neno la Mungu kwa mapokeo yenu mliyopokeana; tena mwafanya mambo mengi yaliyo sawasawa na hayo." (Marko7:13).

"apendaye baba au mama kuliko mimi, hanistahili; wala apendaye mwana au binti kuliko mimi, hanistahili." (Mathayo 10:37).

"Kwa maana ye yote atakayeyafanya mapenzi ya Baba yangu aliye mbinguni, huyu ndiye ndugu yangu, na umbu langu, na mama yangu" (Mathayo 12:50).

Hili ni somo makini sana na unahitaji kusikiliza mwenyewe kutoka kwa Mungu kuhusiana na swala hili. Unaweza kuzama upande wowote wa meli na hilo likawa baya.

Twahitaji kuwaheshimu na kuwastahi wazazi na familia zetu.

Hata hivyo, twahitaji kuwa macho na hatari ya kujitiisha chini ya ushawishi wao wenye nguvu usio wa ki Mungu. Twapaswa kujua kuwa laana husafirishwa kwa njia ya familia. Kama tukijifungamanisha kwa karibu sana na mwanafamilia ambaye hajajiuza kwa Mungu kikamilifu, tunaweza kuwa katika hatari ya kushawishiwa katika njia mbaya. Tafadhali rejea majadiliano juu ya roho za mababu waliokufa katika sura ya 7.

Ipende familia yako. Wafahamishe unasimamia wapi kwa Mungu, ila usiwahubiri na kuwa kikwazo. Watakuwa na heshima nyingi kwa pendo na msamaha kuliko wanavyoweza kuwa kwa ukali wako na msimamo wako wa kuhukumu.

Vipi kuhusu mahusiano ya mapenzi?

Hili laweza kuwa kikwazo kikubwa katika mwendo wako na Bwana. Mungu hakumleta Hawa kwa Adamu hadi akisha kuwa na uhusiano imara na Mungu. Kwa nini? Kwa sababu kila mmoja wetu ana mahitaji mengi yanayo hitaji kutimizwa. Huwa tunaelemea kuwaangalia watu wengine kukutana na mahitaji hayo. Tunapofanya hivyo,

tunawawekea mahitaji yasiyo wezekana. Aina hizo za uhusiano mara nyingi zitageuka kuwa ubinafsi na mwishowe ni balaa. Kwanza, unahitaji kutimiziwa mahitaji yako na Mungu. Kisha mruhusu kukubariki na penzi hilo kamilifu kwa wakati Wake.

Usiende "ukiwinda" mapenzi; itaishia balaa. Mtumaini Mungu na uridhike kubaki peke yako hadi Mungu atakapoona kuwa umekuwa tayari kwa swala la mapenzi. Jitunze katika usafi kimapenzi. Kama uliwahi kufanya makosa huko nyuma, Mungu amekusamehe na amekufanya weupe kama theluji!

Hii hapa ni kanuni ya kuishi. Mapenzi hayakutengenezwa kuwa kati ya watu wawili hadi wajibu kamili uambatane nayo. Huwezi kuwa na jambo moja pasipo kuwa na lile lingine; haitafanya kazi!

Ndoa. Hili ni somo ambalo laweza kuchukua maktaba nzima ya vitabu! Ni la muhimu mno mno. Kwa hiyo tutaangalia kikamilifu baadhi ya mambo muhimu hapa. Nashauri sana kusoma vitabu vingine vya ndoa ukijumulisha: Agano la Ndoa; kilichoandikwa na Derek Prince, Whiteker House, New Kensington, PA; 1978. Derek Prince pia ana kitabu cha kuisisimua kinachoitwa Mungu ni mtengezaji wa Wanaofanana.

Uhusiano wetu na Mungu ni kupitia agano la damu Mahusiano yetu na wenzi wetu ni kupitia katika agano la damu *pamoja na Yesu Kristo*. Tuwapo ndani ya agano pamoja na kaka na dada zetu katika Kristo kwa njia ya kuzaliwa mara ya pili, tuna uhusiano maalum na mtu mmoja wetu, mwenzi wetu. Ni siri ya kiroho. "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari Kristo na kanisa." (Waefeso 5: 31-32). Andiko hili lasema hao wawili watakuwa mmoja, kama vile katika agano la damu. Naamini kuwa hasa huwa tunabadilika kiroho tunapokuwa tumeoana katika Bwana. Watu wawili kwa hisia hawawi na ndoa kamili isipokuwa wamekuwa mmoja. ISOB ina mfululizo wa mikanda ya video inayoenda sambamba na kitabu cha Derek Prince.

Ndoa ni maalum sana kwa Mungu. Anampango mkamilifu, "ramani" kwa ajili ya uhusiano huu. Kutokana na mazingira mbalimbali katika maisha, si kila mtu amewahi kuwa na nafasi ya kuutambua mpango

huu kamili. Hata hivyo, aweza kuwabadilisha watu na kutenda miujiza kutoka katika makosa, kama alivyofanya kwangu. Amenipatia, katika maisha yangu ndani Yake, mke ambaye nilikuwa na ndoto naye kabla sijakutana Naye.

Kama kuna maswala ambayo nina yaeleza hapa ambayo hayakukufurahisha katika ndoa, usijihisi duni ama kuhukumiwa. Jitahidi tu kwa kiwango chako na mazingira yako na umtumaini Mungu kuichukua ndoa yako katika njia ya kupitia kuelekea mpango kamili., utafute uso wa Mungu katika mazingira yako Yawayo yote, mtumaini, naye atayafanya maisha yako kuwa kamili. Uchukue mpango wa Mungu na uchora ndani ya watoto wako kama maono kwa maisha yao. Usijisikie kuhukumiwa kama umepitia kushindwa katika ndoa, hata talaka. Talaka zingine ni kimaandiko, zingine siyo. Kwa hali yoyote, Mungu anakutaka uendelee na ufurahie utele wake kwa maisha yako yajayo.

Mpango wa Mungu kwa ndoa ni kwa wote mume na mke kuwa watumishi wa kila mmoja wao. Wapendane pasipo pendo la masharti, wakiwatanguliza wenzao, pasipo ubinafsi. Inagharimu wote wawili kuwa na uhusiano halisi. Mwenzi mmoja peke yake hawezi kufanikisha hili. Mweke mwenzi wako katika mikono ya Mungu na usijaribu kumfanyia ujanja ama kumbadilisha.

Mapenzi na furaha ya tendo la ndoa viwe kigezo muhimu na cha kuendelea katika ndoa, ama ni matokeo ya uhusiano mzuri wa ndoa, usiotokana na mmoja peke yake.

Uhusiano wa karibu sana. Wengi huchanganya mwingiliano na uhusiano wa ngono. Mwingiliano ni zaidi ya hapo. Mara nyingi watu hukuza uhusiano wa karibu wakati wa uchumba wao, baada ya ndoa wanawachukulia kama watumwa. Uhusiano wa karibu unanza kwa maneno, kuonana kwa macho, na muda wanaotumia kuwa pamoja. Kujitenga ni moja ya kipengele muhimu kwa mwingiliano. Sehemu zote mbili zinahitaji kujua kwamba hakuna watu wengine wanaohusishwa. Yapaswa wajue kuwa ule upande mwingine umejitoe kikamilifu kwao. Wengine hukiita "jicho moja". Uhusiano wa ndoa unafananishwa na mwingiliano wa uhusiano na Bwana. Mwingiliano huhitaji kupata muda

wa kuzungumza na kusikiliza. Kuna hamu ya kutumia muda na mwenzi wako.

Uaminifu. Panaweza kutokuwa na uhusiano ama mwingiliano pasipo uaminifu wa ndani. Sijali huenda labda ina maumivu kiasi gani; uaminifu ndio njia pekee ya kuyakaribia mambo ya Mungu bora zaidi ya Mungu kwa ajili ya ndoa.

Wajibu wa mume ni kupenda kama vile Kristo anavyopenda. Yeye anapaswa aanzisha pendo lisilo na masharti. Ampatie mkewe usalama wa kihisia anaouhitaji. Wajibu wa mke ajitoe kwa mumewe ni kuheshimu, kustahi na kumtia moyo mumewe akimwonyesha kuridhika naye. Kumnyenyekea inamaanisha mke ajitoe kwa mumewe kwa kumkinga, kumlinda, kumwongoza, na kumpenda. Mume anahitaji aheshimu hekima ya mkewe kwenye wajibu wa uongozi. Kukosoana kwa wenzi husababisha kifo cha uhusiano.

Mmoja wa wachungaji wangu wapenzi alisema kutokea kwenye mimbari, "kama ukimpa mke ulinzi wa kihisia, atanyenyekea kila mahali".

Ndoa yaweza kuwa ndio kipawa kizuri kuliko vyote ambavyo Mungu hutoa. Naweza kusema kwa uaminifu, kuwa mke wangu, Carol, na mimi wote tumepokea kipawa hiki.

Hatimaye.

"Kwa hiyo, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyostahili wito wenu mlioitiwa" (Waefeso). Umekwisha pokea kipawa cha thamani kuliko vyote, ambacho ni uzima wa milele. Sasa ni juu yako kushirikiana na Mungu kuishi maisha yanayompendeza. Mwombe Mungu akuonyeshe maeneo ama tabia katika maisha yako ambazo anataka zibadilike. Anataka kukubariki kwa kukubadilisha.

Uwe mwaminifu kwa Mungu.


Kama huna msukumo wa shauku katika maisha yako ya kuishi maisha yanayostahili Mungu, mwombe Mungu akubadilishe. Ikiri kwake kama dhambi naye atabadilisha matakwa na yasiyo matakwa yako.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura 13. Roho Mtakatifu



"... maana ufalme wa Mungu si kula wala kunywa, bali ni haki na amani na furaha katika Roho Mtakatifu" (Warumi 14:17).

Sura yetu ya mwisho inayohusu laana za vizazi inaonesha vile historia ya nyuma ya familia yaweza kusababisha laana katika maisha yetu. Laana hizo zina udhihirisho mwingi, ikijumuisha tabia mbaya, kama ulafi na ulevi. Zaidi kupita yote laana hizo zote husababisha kutokuwa na haki na ukosefu wa amani. Lakini gundua kile Warumi 14:17 inachosema kwamba Roho Mtakatifu atakifanya ndani yako, kinyume na tabia yako ya zamani.

Kama tulitenda kama mababu zetu waliokufa kabla hatujazaliwa mara ya pili, kwa nini tusitende kama Baba yetu mpya mara moja baada ya kuzaliwa mara ya pili? Jibu ni kuwa, utu wetu wa kale umeshikamanishwa ndani ya nafsi zetu, na huenda hatujaruhusu asili mpya, Roho Mtakatifu avamie na kubadilisha nafsi zetu!

Katika Luka 3:16 Yohana Mbatizaji alisema, "Yohana alijibu akawaambi wote, Kweli mimi nawabatiza kwa maji; lakini yuaja mtu mwenye nguvu kuliko mimi, ambaye mimi sistahihili kulengeza gidamu ya viatu vyake; yeye atawabatiza kwa Roho Mtakatifu na kwa moto"

Uzoefu wangu.

Yesu alipoingia maishani mwangu, nilimwona katika kitabu cha Ufunuo kama Kristo aliyeshuka, mshindi na mkombozi. Hadi hapo nikawa mtu aliyejaa Roho Mtakatifu kikamilifu. Mito ya maji yaliyo hai ikaanza kububujika ndani ya roho yangu. "Amiaminiye mimi, kama vile maandiko

yalivyonena, mito ya maji yaliyo hai itatoka ndani yake'. Na neno hilo alilisema katika habari ya roho, ambaye wale wamwaminio watampokea baadaye; kwa maaana roho alikuwa hajaja, kwa sababu Yesu alikuwa hajatukuzwa" (Yohana 7:48,39).

Kazi moja kuu aliyoifanya Roho Mtakatifu katika maisha yangu tangu mwanzo, ilikuwa kumfanya Yesu kuwa halisi kwangu. Nilijua Yesu alikuwa hai. Niliweza kuwa na "mawasiliano halisi ya wakati" Naye kwa njia ya Roho Mtakatifu. Watu walijaribu kunipa maoni yao kuhusu Ukristo, lakini Roho Mtakatifu mara zote alikuwa mwalimu wangu.

Siwezi kueleza kila kitu kuhusu Roho Mtakatifu wa Mungu.

Sizielewi kikamilifu njia mbali mbali ambazo Roho Mtakatifu anajidhihirisha kwa watu mbali mbali. Siwezi kueleza kikamilifu kwa nini baadhi ya watu hupokea Roho Mtakatifu kwa ukamili kuliko wengine. Kuna mambo machache rahisi ambayo naweza kushirikiana nawe.

Ili kuwa mwana wa Mungu, unahitaji Roho wake aunganike na roho yako. Hilo ndilo lilitokea wakati unazaliwa mara ya pili. Uliunganishwa na Mungu, kwa kiwango kile alivyokuwa Adamu kabla hajamwasi Mungu. "Au hamjui ya kuwa mwili wenu ni hekalu la Roho Mtakatifu aliye ndani yenu, mliyepewa na Mungu? Wala si mali yenu wenyewe" (1Wakorintho 6:19).

Ulifanyika chombo cha Roho Mtakatifu ulipomfanya Yesu kuwa Bwana.

Yesu alisema kuwa Roho Mtakatifu angekuja Yeye (Yesu) akishapaa Mbinguni, ili kuchukua nafasi Yake (Yesu) duniani.

Akijua vile tungejisikia yatima kama tusingehisi uwepo wake; Yesu alisema yafuatayo, "Sitawaacha ninyi yatima,[wasio na baba]; naja kwenu". (Yohana 14:18).

Aliwaambia wanafunzi wake, baada ya ufufuo lakini kabla ya kupaa, kwamba watazamishwa ndani ya Roho Mtakatifu. "ya kwamba Yohana alibatiza kwa maji, bali ninyi mtabatizwa katika Roho Mtakatifu baada ya siku hizi chache" (Matendo 1:5). "Lakini mtapokea nguvu, akiisha kuwajilia juu yenu roho Mtakatifu; nanyi mtakuwa mashahidi

wangu katika Yerusalemu, na katika Uyahudi wote, na Samaria, na hata mwisho wa nchi" (Matendo 1:8).

Aliwaambia wasiwe na hofu akishaondoka. Alieleza kuwa Roho Mtakatifu angechukua nafasi Yake na kumfanya Yeye (Yesu Mungu,) halisi kwao. Soma kile Yesu alichowaambia katika Yohana 14:16-26.

Yesu aliwaambia kuwa Roho Mtakatifu angemdhihirisha Yeye kwao. "Lakinii ajapo huyo Msaidizi, nitakayewapelekea kutoka kwa Baba, huyo Roho wa kweli atokaye kwa Baba, yeye atanishuhudia." (Yohana 15:26). "Lakini mimi nawaambia iliyo kweli; yawafaa ninyi mimi miondoke; kwa maana mimi nisipoondoka, huyo Msaidizi hatakuja kwenu; bali mimi nikienda zangu, nitampeleka kwenu" (Yohana 16:7).

Yesu aliwaambia watu wake kuwa angerudi mapema. Alifanya hivyo! Alirudi katika umbo la Roho Mtakatifu. Roho mtakatifu si watu tofauti; ni wale wale, lakini katika umbo tofauti. Roho Mtakatifu hasa anaweza kukaa ndani ya wanadamu wengi ambapo Yesu alikuwa amezuiliwa ndani ya mwili mmoja tu.

Hilo linasikika kirahisi, lakini Ibilisi anawashawishi wanaume na wanawake kuyafanya mambo yawe magumu. Mfumo mzima wa madhehebu umejengwa juu ya kile watu wanachoamini ama wasichoamini kuhusu Roho Mtakatifu. Mara nyingi kile watu wanachoamini ni aina ya desturi ambazo wala hazina msingi wa Biblia.


Huku kujazwa kunatokeaje?

Yohana 15 inasema kuwa tumeunganishwa na chanzo chetu kama tawi lilivyo kwa mzabibu. Sisi si vyombo vinavyojitegemea kama ilivyo glasi ya maji ambayo lazima ijazwe kutoka kwenye chanzo cha nje.

Ni swala tu la kubaki umeungana na mzabibu. Utomvu katika mzabibu unawakilisha Roho Mtakatifu, Yesu ni mzabibu, nasi tu matawi. Yesu anasema utii wetu kwa Neno lake ndicho kitatufanya tuendeleo kukaa. Ubatizo wa Roho Mtakatifu ni kugharikishwa na Mungu tunapokuwa tumeunganishwa Naye, kama tawi kwa mzabibu. "utomvu" Wake hutiririka kuja ndani yetu na tunabakia umeungwa endapo tutakaa.

Ninakubali kuwa tunagharikishwa ama kujazwa na Roho

Mtakatifu wakati vikwazo mbali mbali, kuhusiana na tawi na mzabibu, vinapokuwa vimeondolewa.



Je, kuna viwango vya kujazwa? Ninakubali kuwa kuna viwango. Unapokuwa umejaa Roho Mtakatifu, maeneo yote ya maisha yako yataanza kubadilika. Tunda la Roho litaanza kudhihirika katika maisha yako. " Lakini tunda la Roho ni upendo, furaha, amani, uvumilivu, utu wema, fadhili, uaminifu, upole, kiasi; juu ya mambo kama hayo hakuna sheria" (Wagalatia 5:22,23). Utakuwa na njaa ya Neno la Mungu. Yesu atakuwa halisi kwako. Ukristo utakuwa zaidi ya ufahamu wa kiakili; utakuwa hai na halisi. Utajua kuwa uko katika uhusiano na Mungu.

Kila mkristo yafaa ajazwe Roho Mtakatifu pindi anapozaliwa mara ya pili. Mara zingine inatokea hivyo (kama ilivyotokea kwangu), lakini si mara zote. Agano Jipya linaonyesha uzoefu tofauti tofauti. Pale Efeso, Paulo alikutana na kundi lililokuwa limeamini, lakini walikuwa hawajawahi hata kusikia kuwa kuna Roho Mtakatifu. "Na Paulo, alipokwisha kuweka mikono yake juu yao, Roho Mtakatifu akaja juu yao; wakaanza kunena kwa lugha, na kutabiri" (Matendo 19:6).

Tukio lingine lilitukia wakati Petro alipokuwa akihubiri Injili kwa wa Mataifa. "Petro alipokuwa akisema maneno hayo Roho Mtakatifu akawashukia wote waliolisikia lile neno. Na wale waliotahiriwa, walioamini, wakashagaa, watu wote waliokuja pamoja na Petro, kwa sababu Mataifa nao wamemwagiwa kipawa cha Roho Mtakatifu. Kwa maana waliwasikia wakisema kwaa lugha, na kumwaadhimisha Mungu..." (Matendo 10: 44-46).

Mjue Mungu kupitia mahusiano ya ndani!

Paulo aliombea baraka kwa kanisa la Efeso. Aliwataka wajue uhalisi wa Mungu katika maisha yao ya leo. "...na kuujia upendo wake Kristo upitao ufahamu wote ...mpate kutimilika kwa utimilifu wote wa Mungu." (Waefeso 3:19).

Naamini kuwa vikwazo vingi vinaweza kutuzuia kuufikia ukamilifu wa Roho Mtakatifu.

Vikwazo vikuu ni:

Kiburi. (Yakobo 4:6)

Desturi za kidini. (Marko 7:13)

Hofu. (Luka 11:11-13)

Mashaka. (Luka 11:9-10)

Kutojiweza. (Luka 11:13)

Vikwazo vingine vikubwa ni:

Kutosalimisha kikamilifu mapenzi yako kwa Mungu.

Kukataa kuacha dhambi zingine katika maisha yako.

Kutoishi kwa utii kwa neno la Mungu. (Yohana 14:21-23).

Kutogundua ngome za kiroho na kipepo katika maisha yako.

Kuwaendea "miungu mingine" kupata mahitaji yako.

Mwombe Mungu akuoneshe linalohusiana na maisha yako.

Roho Mtakatifu hutamani afanye mambo makuu mawili ya msingi katika maisha yako.

1.kumfanya Yesu halisi kwako. Hii ni ili uweze kuwa na mwingiliano Naye na, ili Yesu aweze kukufanya kuwa kamili. Anataka

akuweke huru mbali na viungo na magereza yaliyopita. Anataka akufanye mtakatifu kama Mungu.

2. kumfanya Yesu halisi kwa ulimwengu kupitia wewe. Kwa maneno mengine, kumtukiza na kumfunua Mungu. Mwili pekee wa Yesu duniani ni kanisa. Kanisa ni mwili wake. Tunamwakilisha ulimwenguni kwa namna ileile Yeye alivyomwakilisha Baba ulimwenguni alipokuwepo hapa. Wewe ni sehemu ya huo mwili wake, kanisa.

Vipi kuhusu karama za Roho?

Tafadhali soma 1Wakorintho 12, Warumi 12, na Wefeso 4. Aina mojawapo ya karama ni sehemu ya utu wetu, na sehemu zingine zimepewa kazi katika matukio maalum kama yanavyokusudiwa na Mungu. Binafsi mimi nimekuwa na vipawa vingi vikatendakazi katika maisha yangu muda hata muda, lakini si vyote. Nimeshuhudia vipawa kama neno la unabii. Na neno la hekima ambalo ni Roho Mtakatifu tu Ndiye angeweza kulinena. Mke wangu na mimi tulishirikiana na Roho Mtakatifu katika kutoa pepo, na tumeona matokeo ya watu kuponywa na kuwekwa huru.

Kukosoana si tendo takatifu.

Sijisikii kuwa ni halali kwa watu waliopokea vipawa kuwafanya wale wasiopokea vipawa kuwakosoa wale wasiopokea wajisikie kwamba kuna kitu fulani kibaya kwao. Wala si halali kwa wale wasiopokea vipawa kuwakosoa wale walionavyo; hiyo ni kumkosoa Mungu!

Kunena kwa lugha ni karama ya thamani na yenye nguvu.

Mungu huitumia si tu katika huduma kwa watu, kwa watu wa nje, lakini kwa umuhimu sana, huitumia kudhibiti akili zetu kwa faida Yake. Yakobo 3:4-5 inasema kuwa ulimi ni kama usukani unaoilekeza meli yote. Iwapo unataka kumpa Yesu usukani wa maisha yako, mpe ulimi wako. Utahuisha ufahamu wako, utaomba kadri ya mapenzi makamilifu ya Mungu, na kumpinga shetani. Kuomba kwa lugha katika faragha kwa vipindi virefu ina nguvu sana. Imetokeza miujiza katika maisha yangu. Kuna mafundisho ya ndani zaidi juu ya Roho mtakatifu katika mtaala wa ISOB, SOMO la 117 na 118⁷.

⁷ International School of the Bible curriculum hupatikana bure kwenye www.isob.org, au tuma email: info@isob-bible.org

Wakati mmoja, mwanzoni mwa kutembea kwangu na Mungu, nilimchukua rafiki Myahudi kwenda naye kanisani (aliniomba, sikumshurutisha).

Wakati wa ibada, mtu aliyekuwa nyuma yetu alisukumwa na Roho Mtakatifu kunena kwa lugha. Rafiki yangu aligeuka na kumshangaa wakati ananena. Baadaye rafiki yangu Myahudi alimpokea Yesu kuwa Bwana wake. Akamwona kama Masihi wa Kiyahudi.

Njiani tukirudi nyumbani aliniuliza kuhusu "lugha hii ya kuchekesha" ambayo mtu huyo alikuwa anaiongea. Nilieleza 1Wakorintho 12 kwake. Kisha aliniambia kuwa ameelewa kile kilichosemwa katika Waebrania na kile alichojifunza katika shule za Kiebrania akiwa kijana mdogo. Hiki hapa ndicho alichosikia rafiki yangu Myahudi asubuhi hiyo:

"Na itakuwa katika siku za mwisho, ...Na mataifa mengi watakwenda na kusema, 'Njoni, twende juu mlimani kwa BWANA, nyumbani kwa Mungu wa Yakobo, naye atatufundisha njia zake.' nasi tutakwenda katika mapito yake maana katika Sayuni itatokea sheria, na neno la BWANA katika Yerusalem ...nao watafua panga zao ziwe majembe, na mikuki yao iwe miundu" (Isaya 2: 2-5).

Hata hivyo, usemi mkamilifu katika lugha yako mama ni muhimu zaidi kwa Mungu. Maneno yako yana nguvu sana, zaidi sana kuliko unavyodhani. Kile unachosema hakitasababisha tu mambo yatokee duniani, bali maneno yako yatafungamanisha mawazo yako na akili yako pamoja milele. Maneno yasiyofaa yatakuweka wewe na wengine gizani. Maneno yanayofaa na yanayotawaliwa na Mungu yatakuweka wewe na wengine huru. Maneno yasiyofaa yataweka "Jehnamu" ndani ya moyo wako.

Mwombe Mungu akuoneshe maeneo katika maisha yako. yanayozuia ukamili wa Roho Mtakatifu usidhihirishwe ndani na nje yako. Uwepo wa Mungu kupitia Roho Mtakatifu unaweza kufanya marekebisho yoyote unayohitaji.

Maombi.

"Bwana Yesu, Neno la Mungu linasema kwamba wewe unahamu ya kunijaza na Roho wako ili kwamba Wewe na mimi tuweze kuingiliana

zaidi. Nina njaa yako na ya uwepo wako katika maisha yangu. Yesu, naliamini Neno lako. Nakiri kuwa ninataka kila kitu ulichonacho kwa ajili yangu. Njoo, Yesu, nibatize kwa Roho wako Mtakatifu na moto. Niko wazi na tayari kwa moto maishani mwangu. Ninazitupa na kuzitubia dhambi zote maishani mwangu. Namsamehe kila mmoja aliyenikosea. Najitoa mwenyewe kwako kuwa sadaka iliyo hai. Una mamlaka yote juu ya maisha yangu. Chukua njia yako. Navitoa kwako viungo vyangu vyote, kinywa changu, mikono yangu, miguu yangu, masikio na macho.

Vichukue vyote!

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Kwa taarifa zaidi kuhusu somo hili, soma sura ya 11 ya kitabu Grow or Die. Marejeo yako katika ukurasa wa pili wa kitabu hiki.

Sura ya 14. Tunahitaji kuwekwa Huru.



Mimi mtumwa? Hapana! Naenda kanisani mara tatu kwa wiki, Ninayo Biblia kubwa, ratoa kwa maskini, na nimekarani mistari 95 ya Biblia!

Tangu 1979 Yesu ameendelea kuniweka huru kutokana na "magereza" ambayo niliwekwa na dhambi. Nyingi ya "dhambi" hizi zilikuwa zilikuwa ni mambo niliyowekewa na wengine. Baadhi yake yalikuwa ni matendo yangu mwenyewe. Baadhi yake yalikuwa ni mapokeo niliyoyapokea kutoka vizazi vilivyopita. Naamini kwamba yote haya matatu ndiyo vyanzo vya vifungo na magereza katika maisha yangu yetu.

Watu wengi sana wanakiburi kiasi cha kutokubali kuwa wanahitaji msaada wa kuwekwa huru kutokana na utumwa. "Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru. Wakamjibu, Sisi tu uzao wake Ibrahimu, wala hatujawa watumwa wa mtu wakati wo wote; nawe wasemaje, Mtawekwa huru? 34 Yesu akawajibu, Amin, amin, nawaambia, Kila atendaye dhambi ni mtumwa wa dhambi. Wala mtumwa hakai nyumbani sikuzote; mwana hukaa sikuzote. Basi Mwana akiwaweka huru, mtakuwa huru kweli kweli" (Yohana 8:31-36).

Gundua kuwa, Yesu aliwaambia hili "Wayahudi waliomwamini". Hawakutaka kusikia kuwa walikuwa watumwa na kwamba walihitaji kuwekwa huru. Wakristo wengi leo wako hivyo.

Neno la utume wa Yesu alilolisema siku ile alipoanza huduma yake lilisisitiza kuwaweka watu huru. Alisema, "Roho wa Bwana yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafungwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata

kuona tena, Kuwaacha huru walioteswa, Na kutangaza mwaka wa Bwana uliokubaliwa" (Luka 4:18,19).

Paulo anatuambia katika Warumi Sura ya 6 kuwa "tayari" tumekwisha wekwa huru mbali na utumwa wa dhambi. "Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitoa nafsi zenu kuwa watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uleta mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uleta haki. Lakini Mungu na ashukuriwe kwa maana mlikuwa watumwa wa dhambi, lakini mliitii kwa mioyo yenu ile namna ya elimu ambayo mliwekwa chini yake; na mlipokwisha kuwekwa huru mbali na dhambi, mkawa watumwa wa haki" (Warumi 6:16-18).

Ni kweli tume wekwa (wakati uliopita) huru. Pia ni kweli kuwa tunahitaji (wakati ujao) kuwekwa huru. Kisheria sisi si watumwa tena wa dhambi na Shetani mara tulipomfanya Yesu kuwa Bwana. Hata hivyo, kuna mwendelezo wa kutambua ukweli huu. Pasipo kukoma, tunaufanyia kazi ukweli huo maishani mwetu.

"Basi, wapendwa wangu, kama vile mlivyotii sikuzote, si wakati mimi nilipokuwapo tu, bali sasa zaidi sana mimi nisipokuwapo, utimizeni wokovu wenu wenyewe kwa kuogopa na kutetemeka, [si kwa nguvu zenu]. Kwa maana ndiye Mungu atendaye kazi ndani yenu [akiwajaza na kuumba ndani yenu uwezo na hamu ya], kutaka kwenu na kutenda kwenu, kwa kuitimiza kusudi lake jema" (Wafilipi 2:12,13 - mistari iliyoongezwa inatoka katika "Biblia iliyotafsiriwa zaidi").

Mfano mzuri wa kuuona ukweli huu ni hadithi ya Waisraeli kutoka utumwani Misri na kupitia jangwani wakielekea nchi waliyoahidiwa na Mungu. Hadithi hii imeandikwa katika vitabu vya Kutoka na Hesabu.

Waisraeli walikuwa watumwa wa Wamisri kwa zaidi ya miaka 400.

Misri ni aina ya "ulimwengu" ambao sisi tulikuwa watumwa kabla hatujaokolewa na Yesu. Sidhani tunaweza kufikiri ni kwa ndani kiasi gani hizi fikra za kitumwa zilikuwa zimegandamanishwa ndani ya nafsi za Waisraeli hawa. Kizazi baada ya kizazi watu hawa hawakuwa na utambulisho, waume hawakufahamu wakati gani wake zao

wangechukuliwa, na akina mama hawa kufahamu wakati gani watoto wao wangechukuliwa. Hawakuwa na haki ya chochote.

Mungu alituma mkombozi, Musa, kumkabili Mkuu wa utumwa, Farao. Yesu alikuja na kumkabili kiongozi wetu wa utumwa Shetani.

Watu wa Israeli waliongozwa kuvukia Bahari ya Shamu kwa miujiza kutoka katika mikono ya Farao. Aliyekuwa kiongozi wao wa utumwa hakuwa na utawala juu yao tena. Vilevile, tulibatizwa katika Kristo na tumetolewa mikononi mwa Shetani.

Hata hivyo Mungu hakuwapeleka Waisraeli moja kwa moja kwenye

Nchi ya Ahadi. Aliwapitisha jangwani. Majangwa ya maisha yako yanakuja. Hayo ni sehemu ya mpango wa Mungu wa ukombozi kutoka utumwani, na unahitaji kufahamu jinsi ya kuitikia kwa imani. Waisraeli hawakuitikia kwa imani.

Tunaona katika Waebrania sura ya 3 na 4 kuwa Mungu anawaambia waamini wa Agano Jipya wajihadhari na njia za watoto wa Mungu wa Agano la Kale.

Mungu alitoa mahitaji ya Waisraeli huko jangwani kwa njia ya kushangaza. Mara kadhaa alitoa maji yakatiririka mwambani. Alitoa mkate mpya kila asubuhi (Kutoka 16:15). Nguo na viatu vyao havikuchakaa. Mungu aligeuza maji machungu katika bwawa la Mara yakawa maji matamu ajabu ya ziwa (Kutoka 15). Lakini bado waliendelea kunung'unika dhidi ya Mungu na Musa kwa kuwa Hawakuzoea kuishi kwa imani ndani ya Mungu asiyeonekana. Waliendelea kutaka kuishi kwa akili zao. Na hata wakiutamani utumwa.

Waisraeli hawa wanatuonyesha kwamba kuwa mtumwa kwa muda mrefu kunaweza kutupatia fikra za kitumwa ambazo si rahisi kuzishinda. Mungu anajua jinsi ya kututembeza kupitia utaratibu unaoshinda, lakini nyakati nyingi sana hatupendi njia za Mungu.

Ni zipi dalili za fikra za kitumwa?

Jikague mwenyewe.

Aina mojawapo ya utumwa uliojificha ni kuwa mtumwa wako mwenyewe, kwa jina jingine unaitwa ubinafsi. Tunapoendelea

kujitolea kwa matakwa yetu ya kibinafsi, tunakuwa watumwa wa asili yetu ya kale iliyokwisha anguka, ambayo ni mwili.

Kukosa utambulisho ni sifa ya msingi ya utumwa. Watumwa hupata utambulisho kutoka kwa mtu mwingine. Ndio maana unawaona watu katika mila za kimarekani wakikimbia huko na huko wakijaribu kupata magari aina fulani, kuwa na aina fulani ya marafiki, kuvaa kwa aina fulani, kuwa sehehu ya klabu za nyota wa sinema, n.k. Katika baadhi ya mila inaweza kujumuisha kuwa wa kabila fulani. Wanajaribu kueleza wao ni nani, kwa jinsi wanavyoonekana, vile wanavyoendesha na yule wanayejihusisha naye.

Jinsi gani twapaswa kupokea utambulisha wetu? Naamini kuwa Mungu alitumba tupokee utambulisho wetu kupitia kuwa na uhusiano na mtu mwingine. Tumetengenezwa ili tuwe kama yule tutayejiugamanisha naye ili tupokee utambulisho wetu kutoka kwake. Amechukua makazi ndani yetu. Kama hilo halikupi utambulisho, kustahili, na utu(heshima), basi hakuna litakalokupa!

Katika karne ya kwanza Warumi waliwakokota watu kutoka nyumbani kwao wakawafanya watumwa. Familia zilitenganishwa milele, kiasi cha kutokuwaona tena wazazi, watoto, kaka, dada, ama wenzi. Huenda wanawake na wanaume walibakwa na kupigwa. Walipoteza kabisa utambulisho wao.

Kutokana na fikra za mtumwa maisha yake sasa yalikuwa tofauti. Hakuwa na utambulisho wake mwenyewe; hakuwa mtu. Kitu pekee kilichobakia kwake kilikuwa nikile tu ambacho angefanya katika kazi yake. Kipimo pekee cha kuonesha yeye ni nani sasa kilikuwa ni jinsi alivyofanyakazi yake. Iwapo bwana wake angemwangalia vizuri kwa sababu amefanya kazi vizuri, angejisikia kujiheshimu. Hata kama mtumwa mwingine angefurahia kazi yake, ama labda mtu mwingine wa ngazi ya juu ya mamlaka angempongeza, kipimo chochote cha "vizuri sana" angejisikia vizuri.

Maisha yake sasa yalikuwa kanuni:
(jinsi ninavyotenda) + (jinsi wewe unavyojisikia kuhusu utendaji wangu)
= (uthamani wangu).

Mwanadamu aliumbwa na Mungu kupata uthamani wake kutoka

kwa Mungu katika upendo wa Mungu usio na masharti. Sasa hivi imetokea tofauti kabisa; Wanadamu wanahisi kama upendo wote unategemea kwa ujumla jinsi ya ufanisi, na mbaya zaidi, vile mabwana zao wanavyohisi kuhusu ufanisi wao.

Watumwa ni "wapendeza watu". (Waefeso 6:5).

Pasipo kukoma wanatafuta kukubaliwa na kusifiwa na watu wengine. Kazi yao haina maana nyingine. Kama wakubwa wao wa kazi, wazazi ama waalimu wamependezwa na kazi zao wajihisi vizuri kuhusu uthamani wao; la sivyo, wanajihisi wao "si lolote". Mara zote wanajaribu kupata marafiki watakaowapatia utambulisho wa uthamani.

Watumwa hutumikia kufanya kazi "huku wakiangalia". (Waefeso 6:5).

Wakiwa wanaangaliwa, wanachapa kazi, lakini mara tu wenye mamlaka wakiwapa migongo, wanalegea. Wanashikilia chuki dhidi ya mamlaka. Wanawapinga na kuwashusha chini mara zote.

Watumwa Hulalamika. Mara zote wanawalaumu wengine kwa matatizo yao. Ndani ya fikra zao, hali zao mbaya za kimaisha ni makosa ya mtu mwingine.

Baadhi ya watumwa huwa wazuri sana kwa mambo ya udanganyifu

Wanajifunza kuwapendeza ama "kuwapenda" wengine ili wao nao pia "wapendwe".

Watumwa hawapendi kutii mamlaka. Wamejifunza kuwa mamlaka ni mbaya; wanachukia mamlaka zinazowatawala.

Watumwa hawana mamlaka hivyo mara nyingi wanawafanyia wengine uongo ili wawatumikie mahitaji yao. Baadhi ya watumwa hutumia nguvu yao ya kikatili kama kufoka na kuguna ili kuwafanya wengine wawafanane.

Watumwa hawajiheshimu hivyo wanatumia watu wengine, dini, viburudisho, na zinaa, ambayo ni baadhi ya mambo waliyotumia Waisraeli jangwani, kupata kiasi cha hisia za uthamani.

Hebu turudi katika hadithi za Waisraeli.

Mungu alikuwa anawajaribu kuondosha fikra za kitumwa ndani

yao, kwa kutumia njia yao ya jangwani. Ni wawili tu walile kundi la mwanzo waliweza, Yoshua na Kalebu. Wengine tu walioweza kuingia Nchi ya Ahadi walikuwa ni watoto wa wale watumwa wa kwanza. Labda hawakuwa sana na "fikra ya zamani ya utumwa" waliyohitaji kusahau.

Kwa nini Yoshua na Kalebu waliweza kufika? Ukisoma maelezo katika Kutoka na hasa Hesabu, watu hawa wawili walitumia muda mwingi sana na Mungu. Walitumia muda mwingi nje ya Hema ya Kukutania ambapo uwepo wa Mungu ulikaa wakati wengine walifuata matakwa yao ya kidunia.

Ndivyo ilivyo kwako leo. Kama ukitumia muda wako mwingi kwa mambo ya viburudisho na kuwaza mambo ya ulimwengu kuliko unavyofanya kwa Mungu na Neno lake, wewe pia utabakia kama mtumwa.

Yoshua na Kalebu walikusudia kuamini alivyosema Mungu. Hawakuchukulia kuwa ukweli wa mwisho kabisa ni kile wanachokiona kwa macho yao. Ukweli wa mwisho kwao ulikuwa kile alichosema Mungu.

Katika Hesabu sura ya 13, Yoshua, kalebu, na wengine kumi walienda Nchi ya Ahadi ili kuipeleleza.

"Tuma watu, ili waende wakaipeleleze nchi ya Kanaani, niwapayo wana wa Israeli; katika kila kabila ya baba zao mtamtuma mtu mmoja, kila mtu na awe mkuu kati yao" (Hesabu 13:2)

Tambua Mungu alimwambia Musa kwamba aliwapa nchi hii wana wa Israeli. Hilo lilikuwa Neno la Mungu, ahadi Yake!

Wapelelezi kumi na wawili walienda. Kumi walileta taarifa mbaya. "Lakini watu wanaokaa katika nchi ile ni hodari, na miji yao ina maboma, nayo ni makubwa sana; na pamoja na hayo tuliwaona wana wa Anaki huko" (Hesabu 13:28).

"Kalebu akawatuliza watu mbele ya Musa, akasema, Na tupande mara, tukaitamalaki; maana twaweza kushinda bila shaka. 31 Bali wale watu waliopanda pamoja naye wakasema, Hatuwezi kupanda tupigane na watu hawa; kwa maana wana nguvu kuliko sisi" (Hesabu 13:30, 31).

"Kisha, huko tuliwaona Wanefili, wana wa Anako, waliotoka kwa hao Wanefili; tukajiona nafsi zetu kuwa kama mapanzi; nao ndivyo walivyotuona sisi" (Hesabu 13:33).

Kuonekana kama mapanzi mbele ya adui zao ilikuwa sehemu ya fikra zao za kitumwa. Wapelelezi kumi waliangalia maadui zao, wapelelezi wawili waliliangalia Neno la Mungu!

Kama tukijua kuwa ni mapenzi ya Mungu tuwe huru, basi twahitaji kujua nini tufanye ili kushirikiana naye ili kazi itimizwe. Kumbuka kuwa tuna uhuru wa utashi. Mungu hatatashinikiza kupata baraka zake. Lazima aone kuwa tuna utashi wa kupokea na kuacha yale mambo yanayotuzuia. Mungu hatatuweka huru na marafiki zetu bali tu na maadui zetu. Kama tunashikilia tabia zenye msingi wa utumwa wa zamani, kama kitu tunachokipenda na kukifurahia, Mungu hawezi kutusaidia kuwa huru.

Wakati mwingine Mungu huwaweka huru waamini wapya mara moja kutokana na hali za kipepo. Sifahamu kwa nini huwatendea wengine hivi na wengine huchukua njia ndefu. Inaonesha kama haina sababu kushughulika na mtu kuwekwa huru; kirahisi ni mpango wa Mungu kwa kila mmoja wetu.

Wakati mwingine ni muunganiko wa yote mawili. Yote ninayoweza kusema ni, ujiandae kumruhusu Mungu afanye njia yake maishani mwako.

Wakati mwingine tuna ngome za kipepo na wakati mwingine ngome ziko ndani ya "mwili" wetu ama hali za utu wetu wa kale. Wagalatia 3:13 inatuambia kuwa Yesu aliichukua laana yetu ili tuachwe huru. Hata hivyo tunahitaji maarifa na utashi wa kushirikiana na Mungu.

Ngome ni ukuta wa maarifa yaliyoaminiwa kuwa ni kweli. Jinsi ngome inavyonasa miguu yako katika maisha yako:

a.Dhambi zako. dhambi zote huwapa mapepo kukunasa, lakini kati ya mbaya zaidi ni dhambi ya uzinzi. Matendo ya ngono huwafungamanisha pamoja watu wawili kiroho kwa namna ya kipekee sana.

b.Dhambi za vizazi. Pepo hufuatilia familia kwa vizazi vingi, na wanapata haki ya kuwawekea magonjwa na laana(sheria ya urithi). Dini za kipepo zina msingi katika kuabudu roho za mababu ili kuendeleza laana na kuzitawala familia. Zinawashawishi watu, hata Wakristo, kuwa lazima wamlipe mganga ama roho ili walindwe na wabarikiwe. Wengine hata hununua vinywaji kama njia ya kupata kinga na baraka. Watu hawa

huamini kuwa kwa kuungana ama kugusana na roho za mababu zao waliokufa watabarikiwa na kukingwana mabaya. Kwa kweli kinachotokea ni kinyume chake. Wanakuwa wafungwa wa shetani, adui wa nafsi zao.

Maadhimisho mengi mfano Mardi Gras katika Amerika yamebuniwa kuendeleza laana kwenye majimbo. Wakati mwingine hata muungano wa familia waweza kutumiwa na pepo kuendeleza laana za kifamilia. Voodoo, majimbo mbali mbali na dini potofu zina maadhimisho. Laana za vizazi nimoja ya njia za laana zenye nguvu sana ambazo mapepo hujishikiza nazo. Roho za vizazi mara nyingi huwakamata vijana wa familia wakati wa ujana mbichi. Huu ndio wakati ambao uasi huonekana sana. Kama hazitafanikiwa zitajaribu tena baadaye katika maisha yao.

c. Dhambi ulimwenguni. Ulimwengu huu umejaa dhambi, ambazo zinahamasisha utendaji wa kipepo.

d. Mzigo, ama manyanyaso unayoweza kupata kuoka kwa mtu mwingine. Ujanja unaotumiwa na pepo mara nyingi sana ni kuwatumia vibaya kingono vijana wadogo na hivyo kuwaingia maisha yao yote yaliyobaki. Zito si dhambi uliyoifanya, bali ni manyanyaso dhidi yako kutokana na dhambi ya mtu mwingine.

e. Kupitia sanamu maishani mwako. Dini nyingi zinamsingi katika roho ya ulimwengu. Zinaamini kuwa vitu kama mawe, mito, miti, n.k. zina roho zinazoishi. Wazicha na kuziabudu roho hizi ili ziwape mahitaji ya maisha yao. Sanamu yaweza kuwa chochote utakachokifanya kuwa muhimu kuliko Mungu. Inaweza ikawa ni mti, tabia, destuli, ama hata dhehebu la dini ya Kikristo. Sanamu ni chochote ama yeyote maishani mwako unayemwendea kupata mahitaji yako badala ya Mungu. Unakiabudu chochote ama yeyote anayekupatia mahitaji yako. Ni kitendo cha uhuru wa utashi wako.

f. Uasi dhidi ya mamlaka. Kama mtu hajitiishi kwa Yesu kama Bwana, mtu huyo, kwa makosa, atakuwa chini ya utawala wa kiumbe kingine. Hawa alidanganywa na Shetani, naye akamdanganya Adamu. Adamu alipaswa kuchukua mamlaka dhidi ya Shetani lakini hakufanya hivyo. Hawa, kwa kweli, alichukua mamlaka asiyopewa na Adamu hakuyatumia mamlaka yake aliyopewa. Dhambi ya mwanzo inafafanua

vile mamlaka na dhambi zilivyofungamanishwa pamoja. Kwa dhahiri, wote wawili walipaswa kujitiisha chini ya mamlaka ya Neno la Mungu (mti wa uzima).

g.Wakristo wanaweza kuwa katika hatari (wengine hawakubaliani na hili). Kama tuna ushawishi wa pepo kabla hatujaja kwa Yesu, pangeweza kuwa na kipindi kabla hatujapokea ukombozi. Wengine kamwe hawapokei ukombozi kwa msingi kwamba hawataki kujitoa kikamilifu. Kwa dhahiri, Mkristo awezi kupagawa na pepo, lakini hakika wanaweza kushawishiwa. Haijalishi tukitumia Neno kupagawa, kushawishiwa, kuteswa ama vyovyote. Kinachojalisha ni kujua jinsi ya kuondokana na utendaji wa kipepo maishani mwetu!

Maandiko haya yanaonesha kuwa tungali katika hatari hata baada ya kuamini. "Basi Roho anena waziwazi ya kwamba nyakati za mwisho wengine watajitenga jna imani, wakisikiliza roho zidanganyazo, na mafundisho ya mashetani" (1Timotheo 4:1). "Wala si kama wajifanyao mabwana juu ya mitaa yao, bali kwa kujifanya vielelezo kwa lile kundi. 4 Na Mchungaji mkuu atakapodhihirishwa, mtaipokea taji ya utukufu, ile isiyokauka" (1Petro 5:8). "Lakini nachelea; kama yule nyoka alivyomdanganya Hawa kwa hila yake, asije akawaharibu fikira zenu, mkauacha unyofu na usafi kwa Kristo. Maana yeye ajaye akihubiri Yesu mwingine ambaye sisi hatukumhubiri, au mkipokea roho nyingine msiyoipokea, au injili nyingine msiyoikubali, mnatenda vema kuvumiliana naye!" (2Wakorintho 11:3,4).

Wengine husema kwamba damu ya Yesu huwakinga Wakristo. Ndiyo na hapana. Damu hutuinga tunapokuwa Wakristo watiifu. Hatuwezi kujidai tuna ulinzi wa Mungu Baba iwapo tunaisha katika uasi. "...kama vile Mungu Baba alivyotangulia kuwajua katika kutakaswa na Roho, hata mkapata kutii na kunyunyiziwa damu ya Yesu Kristo. Neema na amani na ziongezwe kwenu" (1Petro 1:2). Wakristo wanahitaji ukombozi. Binafsi nimeshiriki katika ukombozi wa kushangaza wa pepo, ambao ulisababisha Wakristo kuponywa na kuwekwa huru! Hii si kanuni bali ushuhuda wa ukweli wa mambo.

Maandiko yanatuonesha utaratibu anaotumia Mungu mara nyingi ili kutuweka huru. Kama ukiangalia Isaya sura ya 61 ambayo Yesu

alinukuu katika Luka 4:18-19, utaona utume wa huduma yake ukielezwa. "Roho wa BWANA yu juu yangu, Kwa maana amenitia mafuta kuwahubiri maskini habari njema. Amenituma kuwatangazia wafunwa kufunguliwa kwao, Na vipofu kupata kuona tena, Kuwaacha huru walioteswa, 19 Na kutangaza mwaka wa BWANA uliokubaliwa" (Luka 4:18-19).

Hapa ni jinsi Yesu alivyoanza utaratibu huo mara nyingi.

Huponya moyo wako uliovunjika. Anajua wakati unakuja kwake kuwa yawezekana kabisa umepigwa na ulimwengu na umevunjika moyo kwa hali fulani. Yaweza kuwa katika mahusiano, ujuzi, ama chochote. Kwa upole huponya hili kwa njia ya Roho Mtakatifu.

Hunena (hutangaza) Neno la kufunguliwa juu ya maisha yako.

Kwa kawaida Mungu hushughulika kwa njia ya Neno lake na ahadi.

Hukupatia macho ili umwone, uone aina ya hali uliyomo ama ulimokuwa. Mara zote unahitajika kufanya uamuzi. Hatakuweka huru na marafiki zako, ila na adui zako.

Kisha anakupatia uhuru mbali na kusetwa. Njia za Mungu za kutuweka huru zinashangaza. Anazo na anatumia njia nyingi mbalimbali. Naweza binafsi kushuhudia kuwa kweli huwa anafanya!

Isaya 61 inaendelea zaidi, akijumuisha kukupa furaha, kukufanya "mti wa haki" akiujenga upya utu na tabia yako, akikupatia mahitaji ya mwili, na akikuweka katika huduma Yake ili kuufikia ulimwengu uliopo wewe.

Wawezaje kushirikiana na Mungu?

Hivi ndivyo alivyosema Yesu juu ya kuwekwa huru. "Basi Yesu akawaambia wale Wayahudi waliomwamini, Ninyi mkikaa katika neno langu, mmekuwa wanafunzi wangu kweli kweli; 32 tena mtaifahamu kweli, nayo hiyo kweli itawaweka huru" (Yohana 8:3,32).

Kwanza lazima uendelee katika Neno Lake. Neno "endelea" ni neno lenye nguvu. Linamaanisha kutulia, kukaa, na kufanya Neno lake kuwa nyumbani kwetu. Haimaanishi kuangalia Neno Lake mara moja kwa wiki ama hata dakika tano kwa siku, inamaanisha kutegemeza maisha yako mwenyewe kwa Neno lake. "Naye akajibu akasema, Imeandikwa, Mtu

hataishi kwa mkate tu, ila kwa kila neno litokalo katika kinywa cha Mungu" (Mathayo 4:4).

Neno lililotumika katika andiko hili kama "neni" ni "rhema". Rhema humaanisha Neno lililozungumzwa kwako binafsi. Lazima uwekeze muda kwa Mungu ili kupokea rhema Yake.

Kinachofuatia, lazima umaanisha kuwa mfuasi wa Yesu. Hiyo inamaanisha kuunganishwa naye kiasi kwamba anakuwa mwalimu wako kwa kila jambo. Inamaanisha unakiacha kiburi na unamruhusu Mungu, ambaye anakufahamu kuliko unavyojipenda mwenyewe, afanye atakayo kwako. Pia anakupenda kuliko unavyojipenda mwenyewe. Unapopitia katika kuadibishwa na Bwana, kumbuka anafanya hivyo kwa kuwa anakupenda.

Matokeo ni kwamba, tutafahamu kweli, na hiyo kweli itatuweka huru. "Yesu akamwambia, Mimi ndimi njia, na kweli, na uzima; mtu haji kwa Baba, ila kwa njia ya mimi" (Yohana 14:6). Kumjua Yesu ni kuijua kweli. Kuwa na uhusiano binafsi, wa karibu, na kuingiliana Naye ndilo jambo pekee litakalokuweka huru kweli.

Mungu anaweza kutumia njia nyingi za kukupatia uhuru huu. Anaweza kuwafanya pepo wafukuzwe ndani yako, ama kutoka katika maisha yanayokuhusu. Ama anaweza kukupitisha njia ndefu ya kuwekwa huru kwa kumimina Neno lake katika maisha yako.

Uzoefu wangu mimi mwenyewe umekuwa hatua ya kuongezeka. Naendelea kumimina Neno katika chombo changu, na kila kitu kisicho cha Mungu kinatoka nje, wakiwemo pepo. Mathayo 8:16 ni mfano wa Yesu kutoa pepo kwa Neno lake. Linasema "Hata kulipokuwa jioni, wakamletea wengi wenye pepo; akawatoa kwa neno lake, akawaponya wote waliokuwa hawawezi".

Tunawajibika kwa kuwa watumwa wa vitu mbali mbalina watu mbali mbali (isipokuwa bila shaka, yale mambo ambayo yanahusiana na utoto wetu). Tunakuwa watumwa kwa yeyote ama chochote tunachojitoa kwacho. Tunaweza tu kutumia utashi wetu katika kujitoa. Tiba ni kuanza kujitoa kwa Yesu katika utii kwa Neno lake, na kwa kufanya hivyo utakuwa mtumwa wake. Katika hilo peke yake, utapata uhuru kamili.

"Hamjui ya kuwa kwake yeye ambaye mnajitua nafsi zenu kuwa

watumwa wake katika kumtii, mmekuwa watumwa wake yule mnayemtii, kwamba ni utumishi wa dhambi uleto mauti, au kwamba ni utumishi wa utii uleto haki" (Warumi 6:16).

Uwe mkweli. Kiri dhambi zako. Tenda kwa uaminifu na kweli kwa gharama yoyote. Unapodanganya unamfanya Shetani kuwa baba yako.

Tangaza kuvunja mgusano wowote na pepo uliokuwa nao; mziki, picha za ngono, TV, sinema, madawa ya kulevya, pombe, uchawi, karata za kuangalia bahati, mbao za kuagulia, kubashiri, n.k.

Tangaza kuvunja uhusiano wowote wa kifamilia ambao unaweza kupitisha laana zikakufikia. Unaweza kushirikiana na wana familia bila kupokea laana zao.

Kaa karibu na Yesu kwa njia ya maombi, Neno lake, marafiki wa kuchagua na makundi ya kanisa. Endelea kujaza ufahamu wako kwa mambo ya Mungu. Ufahamu ndio uwanja wa vita.

Uwe mwazi kwa njia yoyote Mungu anayotaka kukufungua nayo. Tamani kuwa huru na usimwekee Mungu mipaka. Anaweza kuwa na njia nyingi za kukuweka huru. Mpango wake ni kukuweka huru (Luka 4).

Samehe. Hili ni kubwa! Hii hapa ni kanuni ambayo mara nyingi huwa haiangaliwi. Yesu alifundisha kwa njia hii, "utusamehe deni zetu, kama sisi nasi tuwasamehevyo wadeni wetu" (Mathayo 6:12). Hili laweza kutafsiriwa, "utusamehe kwa kipimo kile tulichowasamehe wale waliotukosea sisi".

"Kwa maana mkiwasamehe watu makosa yao, na Baba yenu wa mbinguni atawasamehe ninyi. Bali msipowasamehe watu makosa yao, wala Baba yenu hatawasamehe ninyi makosa yenu" (Mathayo 6:14,15).

Sio kwamba Mungu hataki kukusamehe, hatalazimisha utashi wako. Kushikilia uchungu na hasira juu ya watu wengine kunatumiza sisi. Tunaifungamanisha dhambi hiyo nasi, na hilo litatungamiza sisi. Mshahara wa dhambi ni mauti. Tunachohitaji ni kipawa cha Mungu ambacho ni msamaha.

Watu wengi sana wanateswa maisha yao yote kwa kuwa hawataki kusamehe. Magonjwa, maradhi, umasikini na masaibu mengi yamepona wakati msamaha ulipokamilika.

Msamaha si hisia; ni kitendo cha utashi. Neno la mzizi kwa

msamaha hubeba maana ya kukata ama kuondoa.

Mtu anaponiumiza kweli kweli na hata akatumia njia za hilakujipatia faida kwangu, haiwezi kunifanya nihisi vizuri. Jambo la kwanza ninalolifanya ni kuyafichua na kuona haki inatendeka. Hata hivyo, najua hivyo sivyo Mungu atakavyo. Nakumbuka tena maana ya kusamehe; Kukata. Hivyo ninasema kwa kinywa changu, "Bwana, namsamehe fulani na fulani. Naichukua dhambi yake kwake na kuiweka Kwako". Unaona, bila Yesu, hatuwezi kusamehe kwa sababu yeye pekee ndiye anayeweza kuzichukua dhambi za mtu yeyote. Yeye ndiye njia pekee tunayoweza kusamehe.

Kama utafanya hivi kwa kila mmoja maishani mwako, Roho Mtakatifu atakujaza kwa nguvu sana, na utafungua mikono ya Mungu kutenda kazi badala yako. Utawekwa huru na vitu ambavyo wala hukufahamu kama vilikuwepo.

Maombi ya ukombozi.

"Bwana, Yesu Kristo, ninakiri kwamba wewe ni Bwana wangu".

1. Wewe binafsi imarisha imani yako ndani ya Kristo. "Bwana, Yesu Kristo, naamini kuwa Wewe ni Mwana wa Mungu na njia pekee kwenda kwa Mungu - kuwa ulikufa msalabani kwa ajili ya dhambi zangu na kufufuka tena kusudi nisamehewe na kupokea uzima wa milele".

2. Jinyenyekeze. "Ninakana kiburi chote na kujihesabia haki kidini na sifa zote zizotoka kwako. Sina dai lolote la rehema isipokuwa tu kwamba ulikufa badala yangu".

3. Kiri dhambi yoyote unayojua. "Nakiri dhambi zangu zote mbele yako na sifichi chochote". Sasa ziorodheshe.

4. Tubu dhambi zote. "Natubu dhambi zangu zote. Nageuka kuziacha na kukugeukia wewe, Bwana kupata rehema na msamaha".

5. Wasamehe watu wengine wote. "Kwa uamuzi wangu wa hiari, nawasamehe bure wote walioniumiza ama kunikosea. Naweka chini hasira, uchungu na chuki". Sasa ziorodheshe na uzikiri.

6. Achana na uchawi na dini zote za uongo. "Nakata muunganiko niliokuwa nao na uchawi ama na dini zote za uongo. Ninakana kazi zote za ibilisi, Shetani, na roho chafu zingine maishani mwangu. Ninakiri na

kukana vitendo vyangu vyote vya kichawi na dhambi kama machukizo mbele yako, Mtakatifu na Mungu wa Haki. Nakana ushawishi wowote wa kichawi kutoka kwa mababu zangu". Sasa ziorodheshe na uzikiri.

7. Jiandae kuachiliwa na kila laana juu ya maisha yako. "Bwana Yesu, nakushukuru kwa kuwa msalabani ulifanyika laana, ili nikombolewe na kila laana na nirithi baraka za Mungu. Nakana kila laana kutoka kwa mababu. Kwa msingi huo nakuomba kunifungua na kuniweka huru kupokea ukombozi ninaohitaji".

8. Chukua msimamo wako kwa Mungu. "Nachukua msimamo kwako, Bwana, dhidi ya mapepo wote wa Shetani. Najitiisha kwako, Bwana na ninampinga Ibilisi. Amina".

9. Fukuza. "Sasa nasema kwa pepo yeyote anayenitawala". Sema nao moja kwa moja. "Nawaamuru sasa muondoke kwangu. Kwa Jina la Yesu, nawafukuza! Naomba kuwa nguvu yoyote mbaya ama uwezo nilionao, ama ulionitesa ama kunipagaa, iharibike kabisa ama iondoke kwangu. Najiweka binafsi, mwili wangu, ufahamu wangu, utu wangu, hisia zangu, na ujumla wangu kwa Bwana Yesu Kristo kuwa Bwana na Mwokozi. Naomba haya kwa kwa Jina lenye nguvu la Yesu, nikiamini nimefunguliwa".

Ni muhimu kupata ushauri wa ki Mungu wakati na baada ya kufunguliwa.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura ya 15 Kuendelea mbele na Kanisa.

Waamini wengi wanawazo kuwa wanaweza kuwa na uhusiano na Yesu Kristo pasipo kuwa sehemu ya kanisa la mahali pamoja. Wakati ni kweli kuwa uhusiano wetu na Yesu ni jambo binafsi na halina masharti ya kuwa sehemu ya kanisa la mahali pamoja, ni kweli pia kuwa uhusiano wetu nayeye haukamiliki pasipo kanisa la mahali pamoja.

1Petro 2:5 inatuambia kuwa tunajengwa kuwa nyumba ya Roho. "Ninyi nanyi, kama mawe yaliyo hai, mmejengwa mwe nyumba ya Roho, ukuhani mtakatifu, mtoe dhabihu za roho, zinazokubaliwa na Mungu, kwa njia ya Yesu Kristo" (1Petro 2:5).

Neno "kanisa" limepindishwa maana yake wakati wa miaka 2000 iliyopita. Mara nyingi kabisa watu hueleza maana ya kanisa katika nuru ya kile destuli na mila zao zilichowafundisha.

Neno la Kiyunani kwa kanisa ni ekklesia. Ekklesia lina maana nyingi. Inamaanisha kundi la watu walioitwa pamoja. Hata hivyo, kuishia hapo hakulitendei haki neno. Kusoma historia na kanisa la karne ya kwanza linafunua zaidi. Makanisa mengi ya leo yameiga historia ya desturi za kipagani ambazo zilianzishwa karne ya tatu.

Wanadamu waliumbwa kuishi kwa umoja wa familia.

Hatukuumbwa turidhike na upweke; Mungu alitutengeneza hivyo. Hiyo ni sababu mojawapo, unaona watu wengi sana wanajazana kwenye baa kila usiku na wanakuwa na ushirika wa kunywa bia na pombe kali. Wako katika "familia". Familia hiyo inawakubali vile walivyo. Wanakuta kwamba kuna mtu pale mara nyingi anayewasikiliza maumivu yao na kuwapa rehema.

Hiki ndicho Ekklesia linapaswa kutoa. Huwa napenda kulieleza kwa njia hii. "Kuitwa kutoka familia yako ya kidunia ili uende pamoja na familia yako mpya ya kiroho". Kama vile familia zisivyo kamilifu, makanisa na familia za kanisa si kamilifu. Pamoja na hilo familia hizo ni mpango wa Mungu kwa maisha yetu.

Watu wametumia taasisi mbalimbali za makanisa.

Madhehebu yamekuwa yakufaa katika kuweka mamlaka na utaratibu wa umiliki wa ardhi kwa majengo ya makanisa. Baadhi ya madhehebu yamehamasisha kanuni za kianadamu zisizo za ki Mungu, ila Mungu hajayatupa. Sasa inaonekana kutembea kwa Mungu duniani ambapo kunavuka kuta za kidhehebu. Nimemsikia C. Peter akiita "udhehebu wa baadaye."

Kwenye kitabu chake The Gift of Apostle, Dk. David Cannistraci anatoa maoni yafuatayo kuhusu kile anachokiita kanisa la "kitume" ama la Agano Jipya.

Miaka ijayo, kanisa litakuwa gari atakalotumia Mungu kutimiza mapenzi yake. Agano Jipya linafunua kuwa kanisa ni chombo cha Mungu na mboni ya jicho lake. Anatuita sisi ukuhani wa kifalme (Ufunuo 1:6; 5:9,10), taifa takatifu (1Petro 5:3), mwili wa Kristo (1Wakorintho 12:27; Wakolosai 1:18), urithi wa Mungu (1Petro 5:3), hekalu la Mungu (Waefeso 2:20-22), bibi harusi wa Kristo (Waefeso 5:22,23) na hazina yake ya pekee (1Petro 2:5-9). Yesu analipenda kanisa, na alijitoa kikamilifu ili lipate kuwapo (Waefeso 5:25). Hakuna kitu kitawahi kuwa kikubwa ndani ya moyo na kusudi la Mungu kuliko kanisa lake.

Waandishi wengi wameona huduma (huduma za kuwafikia watu) zikiwa katika moyo wa uhai wa kanisa; hata hivyo, hakuna, aliyeandika picha halisi kuliko Emil Brunner: "Kanisa linaishi kwa huduma za misheni kama vile moto unavyoishi kwa kuwaka".⁸

Kitabu kinaendelea kueleza juu ya akiba zinazotengwa na kanisa la kitume: Baadhi yake ni hizi.

1. Uhusika wa msingi wa kanisa ni kuwafikia watu wote na kuwapelekea Kristo. Wana shauku kuona mila zote zina mkumbatia Yesu katika nguvu yake iokoayo, iponyayo na ikomboayo.

2. Ni makanisa ambayo yamejitoa kikamilifu kwa Ubwana wa Yesu.

⁸The Gift of Apostle, Dr. David Cannistraci, Regal Books, Ventura CA, 1996, ukrasa 175-176.

3. Ni makanisa yaliyo na washirika hai wa mwili wa Kristo. Hawazuiliwi na fikra yoyote ya mgawanyiko wa kikuhani. Watu wake wanahubiri, wanafundisha, wanatumika na wanatabiri kwa kadri ya karama zao za kiroho wakiwa kama viungo vya Kristo.

4. Makanisa haya yanaushirika wenye nguvu na Roho Mtakatifu. Yanaona nguvu za miujiza kwa sababu yamejikita ndani kabisa kimaombi, kufunga, karama za kiroho na imani.

Majengo ya makanisa yaliyo na mipango. Mara nyingi dhehebu ama kundi la waamini hujengajengo jipya la kanisa maeneo ya jirani na kisha huhamasisha kukua kwa kanisa. Mungu ametumia utaratibu huu, kwa njia kubwa sana, kuyagusa maeneo ya jirani kwa Injili. Kanisa linapokua linaanzisha vipindi vya watoto na makundi kadha wa kadha yanayohusiana. Hili linaitwa "kanisa lililo na mipango". Baadhi ya makanisa haya yaliyo na mipango yamekumbatia kanuni kutoka katika Neno la Mungu, hasa kitabu cha Matendo, na mengi yao yanafanya kazi muhimu, yenye nguvu na ya kushangaza.

Makanisa ya seli. Leo kuna mlipuko wa kisasa wa waamini kukutana katika vikundi vidogo nyumbani na makazini kama walivyofanya katika kitabu cha Matendo katika kanisa la karne ya kwanza.

Haya yanaitwa makanisa ya seli (hata hivyo, si makanisa yote ya nyumbani yaliyo makanisa ya seli). Haya yameenea katika (lakini hayajawekewa mipaka huko tu) maeneo ya China, ambako hakufanyiki ujenzi wa majengo ya kuabudia (kanisa), na serikali inazuia waamini kukutana pamoja.

Katika makanisa ya seli, waamini hukutana majumbani amasehemu za kazi katika makundi madogo madogo na kuhudumiana kila mmoja. Kila mwamini ana vipawa maalum na mwito ambao Mungu anautumia. Makundi haya madogo ya waamini hukutana muda hata muda katika kusanyiko kubwa na kufanya kundi kubwa. Mara nyingi kadri kusanyiko linavyokua, wananunua jengo kubwa la kukutania siku za jumapili. Kuna mamlaka na uongozi kupitia mitume, wachungaji, wazee, n.k.

Makanisa ya seli yaliyofanikiwa yamekua haraka sana kwa sababu

mbili muhimu. Kwanza, kila muumini alipewa nafasi ya kufanya huduma zaidi ya kukaa tu kwenye benchi. Pili, makundi husimamia kazi ya uinjilisti. Yakishakua zaidi ya watu kumi na tano, yanagawanyika tena kwa njia ileile seli ya mwilini mwa binadamu hugawanyika na kujizidisha. Washirika huwafikia watu katika maeneo yao ya ushawishi na wanawaleta kanisani. Mara nyingi wasioamini wanautayari kuhudhuria kusanyiko la nyumbani kuliko kwenda katika jengo la kanisa. Kupitia shule ya Kimataifa ya Biblia mke wangu na mimi binafsi tumehusika na upandaji wa makanisa ya nyumbani katika mataifa mbalimbali. Tumeshuhudia Mungu akifanya kazi isiyo ya kawaida.

Vifuatavyo ni vitabu vitatu mahili sana vya somo la makanisa ya seli:

Successful Home Cell Groups, David Yonggi Cho, BridgeLogos Publishers, North Brunswick, NJ, 1981.

The Cell Church, Larry Stockstill, Regal Books, Ventura, CA, 1998.

Where Do We Go From Here? Ralph W. Neighbor, Jr., TOUCH Outreach Ministries, Houston, TX, 1990.

Kwa njia yoyote siliinui kanisa la aina moja zaidi ya lingine.
Kanisa

la aina yoyote utakaloshiriki, jambo la muhimu ni kuwa upambanue sifa zifuatazo endapo viongozi wa kanisa wanavyo:

1. Tabia ya ukamilifu.
2. Ukamilifu katika fedha
3. Ukamilifu katika maandiko
4. Kama viongozi wanajaribu kuyatawala maisha ya waumini, kaa mbali. Kiongozi anatakiwa awepo kama mchungaji pasipo kuingilia uhuru wa utashi. Yapaswa ajaribu kuwaweka waumini wake chini ya utawala wa Roho Mtakatifu.
5. Shauku kwa waliopotea. Misheni na mikakati ya kuwafikia iwe ndio moyo wa huduma.
6. Aina ya uongozi unaohamasisha washirika wajihusishe na

huduma.

7. Viongozi wawe ni watu wanaotawaliwa na Roho Mtakatifu na sio kanuni za kanisa na dhehebu.

8. Viongozi wawe wamekomaa katika rehema, neema na upendo wa Mungu. Waachane na mambo ya sheria, bali wahamasishe kukua katika tabia za Kristo kwa neema.

Ninaupenda ujumbe wa maono ya kanisa langu, Mt Paran North Church of God in Marietta, Georgia, U.S.A.

"Kuwakumbatia watu wote katika kipindi chao cha uhitaji, kuwaongoza katika uwepo wa Kristo, kuwapenda kama watu wa Kristo, kuwakuza katika nafsi ya Kristo na kuwatuma nje kumtangaza Kristo"

Faida za kuwa katika ushirika.

Kuwa katika ushirika na waumini wengine yaweza kuwa na thawabu na maumivu pia. Nimewahi kukutana na hayo yote. Ndugu ama dada katika Kristo anapokuumiza, inauma sana. Hata hivyo, hizi ni nafasi za ajabu mno za kujifunza na kufundishwa na Mungu. Kama umekosea, Mungu atakusahihisha ukimruhusu. Kama haukuwa na kosa katika jambo hilo, kutakuwa na nafasi nzuri ya kujifunza uvumilivu na msamaha.

Mpango wa Shetani ni kuwakwaza watu ili waache kuhudhuria kanisani, ama zaidi waanze "kuchagua chagua makanisa". Hakuna ubaya kwenda kuchagua yaani kuhama kanisa na kwenda lingine, lakini fanya kwa uongozi wa Roho Mtakatifu na sio kwa sababu unamkimbia mtu aliyekuwaza. Kama ukikimbia kila wakati utakwazika, Shetani ataanza kukuongoza na si Roho Mtakatifu.

Ni vyema kubakia umepandwa katika kusanyiko la mahali pamoja; kufanya hivyo kutatokeza matunda na baraka. "Mwenye haki atastawi kama mtende, atakua kama mwerezi wa Lebanoni. **Walio pandwa** katika nyumba ya BWANA watastawi katika nyua za Mungu wetu. Watazaa matunda hadi wakati wa uzee, watajaa utomvu, watakuwa na ubichi. Watangaze kuwa BWANA ni mweye adili, Mwamba wangu, ndani yake hamna udhalimu" (Zaburi 92:12-15).

Jinsi ya kuwatendea waumini wengine

Ni muhimu mno kwa hali yako ya

Kiroho kuhusiana na watu wote kwa upendo. Naweza kukuhakikishia kuwa katika ushirika wako wa kanisa utapata nafasi ya kugombana na waumini wengine. Yaweza kuwa makosa yako ama yao; hilo halijalishi. Kinachojalisha ni kuwa adui asije akatumia aina hii ya ugomvi kukuumiza.

Yapaswa tukumbuke tumeingia katika agano la damu na Yesu, na tuko katika agano na waumini wengine, tukiwasengenya, tukiwasema vibaya, na kuwaumiza kwa njia yoyote, twaweza kuwa katika hatari. 1Wakorintho 11 hutuonya tunaposhiriki meza ya Bwana. Kushiriki meza ya Bwana ni kukumbuka agano la damu na Yesu, lakini pia inasababisha tukumbuke kuwa kwa njia yake tu tuko katika agano na waumini wengine. Maana alaye na kunya, hula na kunywa hukumu ya nafsi yake, kwa kutokuupambanua ule mwili." (1Wakorintho 11:29).

Hukumu yaweza kuja kwa njia mbambali. Yaweza kuja katika uhusiano na mwenzi, watoto wako, ama katika fedha zana yako, afya, biashara, n.k., usipoupambanua vyema mwili wa Bwana. Maana yake, usipomjali mtu mwingine kuwa ni sehemu ya mwili wa Kristo. Ukiupambanua mwili wa Bwana kwa kile unachokiona na si kwa kile Neno la Mungu linachosema, umo hatarini.

Ukuhani wa waumini

Kuna makanisa mengi yanayohamasisha aina moja ya daraja kumtumikia Mungu na wanawaita makasisi, na wanawaita watu waliobaki walei. Japo Neno la Mungu linaweka wazi kuwa wote walio wa Mungu wamtumikie.

Katika Kutoka sura ya 3, Mungu alimwambia Musa kuwaambia Waisraeli kuwa sababu ya wao kutolewa utumwani ni ili wamtumikie Yeye. Katika Kutoka 19:6 Mungu alisema, "... nanyi mtakuwa kwangu ufalme wa makuhani na taifa takatifu. Hayo ndiyo maneno utakayowaambia wana wa Israeli".

Hebu tusiangalie neno kuhani katika namna ya desturi ya kidini. kwa urahisi, kuhani ni mtu anayemwakilisha Mungu kwa mwanadamu, na mwanadamu kwa Mungu. Kuhani husimama kama daraja.. Hufanya

upatanisho kwa Mungu kwa ajili ya mwanadamu, na huleta Habari Njema za Mungu kwa mwanadamu. Makuhani walikula, waliishi, na kuchinja sadaka, yote hayo katika huduma ya Mungu. Kazi yao kuu ilikuwa kumtumikia Mungu. Endapo walikuwa na taaluma zingine kama waalimu, matabibu, n.k. hizo hazikuwa rasmi.

Hata hivyo, Waisraeli wote hawakukubali wito. Walawi peke yao waliitikia mwito kwa kuachana na sanamu na uhusiano mwingine usiostahili. Hata pamoja na hayo, ni wachache wao, wana wa Haruni waliruhusiwa kutumika Patakatifu pa Patakatifu ambapo uwepo wa Mungu ulikaa. Kwa sababu kadhaa fikra hiyo bado ipo hadi leo. Katika Agano Jipya, na kwa mwili wa Kristo duniani kote, waamini wote ni makuhani.

"Bali ninyi ni mzao mteule, ukuhani wa kifalme, taifa takatifu, watu wa milki ya Mungu, mpate kuzitangaza fadhili zake yeye aliyewaita mtoke gizani mkaingie katika nuru yake ya ajabu" (1Petro 2:9).

"...na kutufanya kuwa ufalme, na makuhani kwa Mungu, naye ni Baba yake; utukufu na ukuu una Yeye hata milele na milele Amina" (Ufunuo 1:6).

Yesu peke yake ndiye mpatanishi kati ya Mungu na mwanadamu (rejea 1Timotheo 2:5). Lakini kama sehemu ya mwili wa Kristo hakika tu mabalozi wa Mungu kuwaletea Habari Njema za neema ya Mungu (rejea 2Wakorintho 5:20).

Leo "huduma" haijaachwa kwa watu walio na shahada kutoka katika Seminari (ama popote), wala kwa watu wanaofanya kazi muda wote kanisani. Hayo ni mapokeo ya kanisa. Huduma ni kwa waumini wote. Waefeso sura ya 4 hueleza hili wazi. Paulo anatuambia kuwa kazi ya mtume, nabii, mchungaji, n.k. ni kuwaandaa watu wa Mungu ili kwamba (hao watu wa Mungu) wafanye kazi katika huduma. "Naye alitoa wengine kuwa mitume; na wengine kuwa manabii; na wengine kuwa wainjilisti; na wengine kuwa wachungaji na waalimu; kwa kusudi la kuwakamilisha watakatifu, hata kazi ya huduma itendeke, hata mwili wa Kristo ujengwe" (Waefeso 4:11,12).

Hakika, hili ni jepesi kuliongelea, kisha kulitendea kazi. Nimekuta kwamba kama ukimchukulia Mungu katika Neno lake ndani ya

somo hili, atakuweka ndani ya huduma alimokusimika. Kuna huduma inayokungoza uingie ndani yake. Wewe ni mtu aliyefuzu kabisa kwa huduma hii. Hata hivyo, usipoitika mwito, kazi ya Mungu haishuki, ataituma kazi hiyo kwa mwingine. Siku ya hukumu utatoa hesabu kwa kukataa mwito huu.

Kanisa la kwanza nililojiunga lilikuwa dogo sana. Nilikuwa na hamu sana ya kutumika. Sikuwa nimekomaa katika karama za kiroho, lakini nilifahamu namna ya kudeki na kusafisha. Hivyo nilideki kanisa na kusafisha vyoo. Niliipenda kila dakika niliyofanya hivyo, na nilihisi furaha ya Bwana nilipokuwa nafanya hivyo. Kidogo kidogo Bwana aliongeza kiwango cha huduma yangu. Sihitaji kutafuta cheo katika kumtumikia Mungu; sifurahishwi na watu wanaofanya hivyo. Najisikia vizuri kuwa mtumishi na kumwanganalia Mungu akishughulika na mahitaji yangu.

Mojawapo ya njia kuu tunayoweza kumtumikia Yesu ni kuwatumikia watu katika mwili wake. Mwelekeo wa asili wa watu ni kuwa wabinafsi na kudhania kuwa ulimwengu unawazunguka wao na matatizo yao. Makanisa mengi yamejaa watu wanaokimbia huku na huku wakitafuta baraka na watu watakaowabariki. Huu sio mpango wa Mungu. Mpango wake umeandikwa katika Mathayo sura ya 25: 14-30 katika mfano wa talanta. Hii ni sheria ya maongezeko. Tunatakiwa tukitumie tulichonacho mkononi kwa kuwatumikia wengine, na tukishafanya hivyo, Yesu hutupatia zaidi.

Kanisa linahitaji kuendelea kuwaka moto wa maono ya kuwafikia walio nje, na ukae ndani ya washirika wote. Pasipo hili, kupoteza hamu na kurudi nyuma ni matokeo ya kawaida. Baba yetu wa imani na Mwebrania wa kwanza alikuwa Ibrahimu. Mungu aliahidi kumbariki Ibrahimu, ahadi iliyokuwa ya ndani sana kwake kuielewa. Hata hivyo, Mungu aliweka wazi kuwa hakupaswa kubakia nayo baraka yeye peke yake, bali awabariki na wengine. "nami nitakufanya wewe kuwa taifa kubwa, na kukubariki, na kulikuza jina lako; nawe uwe baraka" (Mwanzo 12:2). Uzao wa Ibrahimu, Israeli, walikuwa na mwito uleule, ila hawakuinuka watende. Badala yake walizichukua baraka na kuziweka ndani yao tu, pasipo kuwashirikisha Mataifa habari njema. Uzao wa msingi kabisa wa Ibrahimu alikuwa ni

Yesu. Kwa njia ya Yesu sisi pia tu uzao wa Ibrahimu (rejea Wagalatia 3:16 & 29).

Nilipokutana na Bwana, nilikuwa namiliki duka dogo (hiyo ilikuwa hadi mwaka 1983). Kwa miezi miwili tu nilikuwa tayari nimesafisha kabati zote za duka na kuweka Biblia na vipeperushi vya Injili vya kugawa bure. Nilifanya shindano la Biblia. Nilifananya mafunzo ya Biblia katika mojawapo ya vyumba vya nyuma. Nilihisi kuwa nilikuwa nimepokea kitu cha thamani sana ambacho nilitaka kila mmoja akishiriki!

Siku moja mchungaji alinjia na kuniuliza kama niliogopa kushuka sana ki-biashara kwa sababu ya kuwa jasiri sana katika Yesu. Nilifikiria na kumwambia, "Sawa, iwapo nitapoteza biashara yangu, basi nitapata ajira. Na iwapo sitapata ajira, basi sitakuwa na chakula. Na kama sitakuwa na chakula nitakufa na hivyo kuwa na Yesu. Kwa vyovyote unavyoliangalia bado ninashinda!" Alikuna kichwa na kuondoka

Tafadhali soma Ezekieli sura ya 16, ambayo inaonesha Mungu akiwaambia Waisraeli kuhusu utele wa baraka kwake, na bado anamwambia, "Kama mimi niishivyo, asema Bwana MUNGU, Sodoma, umbu lako, yeye na binti zake, hawakutenda kama wewe ulivyotenda, wewe na binti zako. Tazama, uovu wa umbu lako Sodoma, ulikuwa huu; kiburi, na kushiba chakula, na kufanikiwa, hayo yalikuwa ndani yake na binti zake; tena hakuutia nguvu mkono wa maskini na mhitaji" (Ezekieli 16:48, 49).

Watu hawawezi kuishi bila kusudi.

Kama kusudi lako katika maisha si kusudi la Mungu kwako, utaishia pabaya labda hata kama Waisraeli. Hakuna kusudi katika maisha lenye maana sana litakalokuzuia kujiinua, isipokuwa kusudi la Mungu!

Mungu amemtengeneza kila mwamini kwa tofauti. Sisi wote si Wainjilisti ama Wachungaji. Lakini kila mmoja wetu ni kiungo muhimu sana cha mwili Wake. Kusema kweli, wachungaji na wainjilisti si walio juu sana katika "mnyororo wa chakula" wa kiroho. Hili limethibitishwa katika 1Wakorintho 12:20-24. Wewe na Huduma yako ni wa muhimu sana kwa ufalme wa Mungu na kanisa.

Mungu ameweka karama juu ya kila mmoja wetu, katika njia tuliyoizoea, na ametupatia utu wenye mazoea. Njia pekee ya kuelezea vipaji vyako ni kwa kuzaa matunda. Katika huduma. Tunda ni kitu pekee ambacho ni cha thamani halisi kwa Mungu. Yohana sura ya 15 inasema kuwa kama tukikaa ndani ya Kristo na kutii Neno Lake, matokeo yatakuwa ni tunda. Kupanga mipango "kimwili" hakutatoa matunda kwa Mungu. Matunda hutokana na maisha yaliyokabidhiwa kwa Mungu, na kwa kuruhusu hatua za ufuasi zifanye kazi maishani mwako. Matunda ni matokeo ya kulitumainia Neno la Mungu kukupatia mahitaji yako. Kadri Neno linavyokua ndani ya maisha yako, maisha na tabia za Mungu zitajengwa ndani yako, na Neno lake mara zote huwafikia waliopotea. Yesu ni mmishenari, na Bibi harusi wake yapaswa awe msaidizi wake! "Vitoto vyangu, ambao kwamba nawaonea utungu tena mpaka Kristo aumbike ndani yenu" (Wagalatia 4:19).

Faida zingine za maisha ya kanisa.

"Ingawa chuki hufunikiwa kwa hila; uovu wake utadhihirika mbele ya kusanyiko" (Mithali 26:26). Andiko hili linatujulisha kwamba kuna maeneo katika maisha yetu ambayo yaweza tu kufichuliwa katika kusanyiko. Kabla hatujawa huru kweli kweli, twahitaji maovu yetu yote yafichuliwe, bila kujali inauma namna gani.

"Kusanyiko la mataifa na likuzunguke, na juu yake uketi utawale" (Zaburi 7:7).

"Nitakushukuru katika kusanyiko kubwa; Nitakusifu kati ya watu wengi" (Zaburi 35:18).

"Sikusitiri haki yako moyoni mwangu, nimetangaza uaminifu wako na wokovu wako. Sikuficha fadhili zako wala kweli yako katika kusanyiko kubwa" (Zaburi 40:10).

"Haleluya. Mwimbieni BWANA wimbo mpya, sifa zake katika kusanyiko la watauwa" (Zaburi 149:1).

"Mungu huogopwa sana barazani pa watakatifu, ni wa kuhofiwa kuliko wote wanaomzunguka" (89:7).


"Na wamtukuze katika kusanyiko la watu, na wamhimidi katika baraza la wazee" (Zaburi 107:32).

"Haleluya. Nitamshukuru BWANA kwa moyo wangu wote barazani pa wanyoofu wa moyo na katika mkutano" (Zaburi 111:1).

Kanisa hutupatia nafasi ya kuelezea nguvu zisizo za kawaida za umoja.

Roho mtakatifu hutenda kwa nguvu sana kupitia umoja wa waamini kanisani. Yesu aliomba katika Yohana 17: 20-23 kwamba ulimwengu ujue upendo wa Mungu kwa njia ya Yesu Kristo wakati waamini watakapokuwa katika umoja kati ya mtu na mwingine. Waamini wanapokuwa na umoja, wanadhihirisha kipande kidogo cha mwili wa Kristo cha ki-Musa. Matokeo ni kuwa Roho Mtakatifu hazuiliwi kutenda kwa ubora sana. Roho Mtakatifu huondoa kitambaa kwenye macho ya wasioamini, huwaweka huru watumwa, na huwaponya waliovunjika moyo. Roho Mtakatifu humfanya Yesu kuwa halisi kwetu na kwa ulimwengu unaotuzunguka. Hutufanya tukamilike, roho,nafsi, na mwili, na hututuma kutangaza Habari Njema kwa wengine. Nahisi kuwa picha hii ilistahili maneno elfu.

Nguvu za umoja zisizo za kawaida



- | | | | | |
|--|--------------------------------------|-----------------------------------|--|--|
| Wakolosi 3:14 -
Wanammasomwa kwa Yesu | Wakolosi 3:5-11 -
Ujue "kuruhaka" | Kolosi 3:12-17 -
Ujue "kumpya" | Wakolosi 3:16 -
Nera Nera (Ziburi 91 inagumi) | Wakolosi 3:4
Mficheo ni kwamba
Mingwa ambaye |
|--|--------------------------------------|-----------------------------------|--|--|

- | | | | | |
|---------|--------------------------|---|---|---|
| Mfichao | Mfichao 4:13 -
matoto | Mfichao 4:24 - "Hio walipokita, wakampoa Mingu suti zokwa Wakolosi 3:14 wakisema: "Mh, uwendive Mingu ndive uliyefanyambingurandira bharirawili vyote vilivyomo" | Mfichao 4:28 -
Wakumbubupita Nera lakubiri kurwa Mingu | Mfichao 4:31 - Mficheo yaliku Nguvu za Rho Mkatifu. Hita walipokwisha kumwamba Mingu, malipale sulipokwisha pita hivyo, wote wakaja Rho Mkatifu, wakenarero h Mingu kwa upesi." |
|---------|--------------------------|---|---|---|

Hatimaye, tunahitaji kukumbuka kuwa kanisa, ama mwili wa Kristo, pia ni Bibi harusi wa Kristo. "Kwa sababu hiyo mtu atamwacha baba yake na mama yake, ataambatana na mkewe na hao wawili watakuwa mwili mmoja. Siri hiyo ni kubwa; ila mimi nanena habari ya Kristo na Kanisa" (Waefeso 5:31,32). "...Njoo huku nami nitakuonyesha yule Bibi-arusi mke wa mwana-Kondoo" (Ufunuo 21:9b).

Twapaswa kujua jinsi Yesu alivyo na shauku juu ya kusanyiko la Bibi-arusi wake na matarajio Yake ya kumwona katika utukufu wake wote. Tulitunze hili ndani ya ufahamu pale tunapochanganywa ama tutakapokuwa tumechanganywa na kanisa ama maisha ya kanisa.

Mara nyingi watu katika taifa ambalo huenda wamejitenganisha hurudia katika umoja wanapokabiliwa na vita. Hebu tuungane katika ukweli kwamba Yesu “ameshinda” duniani katika vita hivi na Shetani, na kuwa tumeitwa kuumalizia ushindi.

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura ya 16 Vita Vya Kiroho.



Vita? Nili dhani Yesu alikuja kuleta amani!

Hakuna ushindi pasipo mgogoro.

Lazima tutambue kuwa tunaishi ndani ya jimbo la adui. Lengo lake ni kuwafanya waliopotea wabakie wamepotea na waende Jehanamu. Lengo lake kwa Wakristo ni kuwafanya watamani ufalme wa ulimwengu na mfumo wake wa fedha, burudani, mamlaka, umaarufu, n.k; kwamba wabakie hawana hata ufahamu kuwa wangeishi kwa ufalme wa juu zaidi, Ufalme wa Mungu. Shetani anaweza kuwapooza Wakristo kwa kuwafanya wategemea ufalme wa ulimwengu na rasilimali zao.

Shetani alikuwa na uwezo wa kuwashawishi Adamu na Hawa kuwa wangeendesha maisha yao bila Neno la Mungu (Mwanzo sura 3). Shetani alimjaribu Yesu kwa swala hilo hilo katika Luka sura ya 4. Atatumia ujanja huohuo kwako. Kama Shetani atakufanya utende kwa kujitegemea mwenyewe pasipo kuliweka Neno la Mungu kwanza katika maisha yako, basi amefanikiwa.

“Basi nyoka alikuwa mwerevu kuliko wanyama wote wa mwitu aliowafanya BWANA Mungu. Akamwambia mwanamke, ‘Ati! hivi ndivyo alivyosema Mungu, Msile matunda ya miti yote ya bustani?’”(Mwanzo 3:1).

Kuwa na mashaka na Neno la Mungu ni silaha kuu ya Shetani. Huu ndio ulazima wa vita vya kiroho. Bila kutatanisha sana, vita vya kiroho kimsingi vinahusu kuliadini ama kuwa na mashaka na Neno la Mungu. Mungu anatumia tulumainie Neno lake kupita uthibitisho wote. Wakati

mwingine ni vigumu kuuamini ukweli ambao hatuwezi kuuona na kuuhihi kwa milango yetu mitano ya fahamu.

Kama unataka kutengeneza mwonekano wa umbile, kuna hatua za kusaidia unazoweza kuzichukua kama vile kula inavyotakiwa, kupata usingizi wa kutosha, kunywa vidonge vya kuongeza vitamini kila siku, n.k. Lakini katika uchambuzi wa mwisho, hakuna mbadala wa kufanya mazoezi ama kufanya kazi dhidi ya upinzani. Vile vile ni kweli katika maisha ya ukristo. Virutubisho halali kutoka katika Neno ni vya lazima, lakini pia "mazoezi." Katika nguvu za Mungu, kukumbana na kushinda majaribu na magumu, Mungu, ambaye ndiye kocha mkamilifu, anajua bayana, aina gani ya "zoezi" unalohitaji ili kugeuza eneo la udhaifu kuwa eneo la mfano wa Kristo.

"Ndugu zangu, hesabuni ya kuwa ni furaha tupu, mkiangukia katika majaribu mbalimbali; 3 mkifahamu ya kuwa kujaribiwa kwa imani yenu huleta saburi. 4 Saburi na iwe na kazi kamilifu, mpate kuwa wakamilifu na watimilifu bila kupungukiwa na neno" (Yakobo 1:2-4).

Shetani mara nyingi hatumii vitu "vibaya" kutujaribu, wakati mwingine hutumia vitu "vizuri" vya ulimwengu kutuvutia macho tuondoke katika Ufalme wa Mungu. Shetani hutumia mazingira na mawazo ili kutushawishi kuwa hatuja KETI pamoja na Kristo (nafasi yetu ndani ya Kristo), kuwa TUSIENENDE kama anavyo ENENDA (wajibu wetu), na kuwa tukate tamaa badala ya KUSIMAMA katika ahadi (vita vyetu vya kiroho). Sisi tu warithi wa Ufalme wa Mungu. Kwa nini tuishi kama watu wale wasio warithi?

Hivi ndivyo inavyofanya kazi:

Yesu alikuwa akiwafundisha wanafunzi wake katika Marko sura ya

4. Aliwaambia kuwa siri ya ufalme wa Mungu ilikuwa imebebwa ndani ya mfano huu. Akawaauliza katika mstari 13, "Akawaambia, Hamjui mfano huu? Basi mifano yote mtaitambuaje?" Yesu alitumia mfano huu wa kilimo unaoonekana, wa mbegu kupandwa ili kuelezea na kuifunua siri ya ulimwengu usioonekana. Marko 4:9-11 inasema, "Akasema, 'Aliye na masikio ya kusikilia, na asikie'. Naye alipokuwa peke yake, wale watu waliomzunguka, na wale Thenashara, walimwuliza habari za ile mifano.

Akawaambia, ‘Ninyi mmejaliwa kuijua siri ya ufalme wa Mungu, bali kwa wale walio nje yote hufanywa kwa mifano’”

Ufalme wote wa Mungu hufanya kazi kama mfano huu. Mungu hupanda mbegu ya Neno lake moyoni mwako (bila kujali hali ya moyo wako). Mbegu hizi huwakilisha kusudi lote la Mungu, kwa maisha yako. Kuzaliwa mara ya pili ni kusudi la kwanza. Linalofuata ni kujazwa na Roho Mtakatifu, kuponywa kimwili, kihisia, na kiakili, na kutimiziwa mahitaji yako. Neno litakuleta kwenye uhusiano wako halali katika maisha, na litatoa makusudi yote ya Mungu yanayofuata, kwa ajili yako. Mungu hutumia Neno lake ili kukupatia makusudi yake.

Marko 4:14-20 inasema, "Mpanzi huyo hulipanda neno. Hawa ndio walio kando ya njia, lipandwapo neno; nao, wakiisha kusikia, mara huja Shetani, akaliondoa lile neno lililopandwa moyoni mwao. Kadhalika na hawa ndio wapandwao penye miamba, ambao kwamba wakiisha kulisikia lile neno, mara hulipokea kwa furaha; ila hawana mizizi ndani yao, bali hudumu muda mchache; kisha ikitokea dhiki au udhia kwa ajili ya lile neno, mara hujikwaa. Na hawa ndio wale wapandwao penye miiba; ni watu walisikiao lile neno, na shughuli za dunia, na udanganyifu wa mali, na tamaa za mambo mengine zikiingia, hulisonga lile neno, Likawa halizai. Na hawa ndio waliopandwa penye udongo ulio mzuri; ni watu walisikiao lile neno na kulipokea, na kuzaa matunda, mmoja thelathini, mmoja sitini, na mmoja mia".

Tambua kuwa Shetani huja kuiba Neno. Hii ni silaha pekee halisi aliyonayo Shetani dhidi ya wanadamu; kuliiba Neno ama kutupofusha kutokana na Neno (2Wakorintho 4:4). Kama mtu yeyote angelipokea na kulitendea kazi Neno la Mungu, wangeokoka na kwenda Mbinguni. Kama mtu yeyote angelipokea na kulitendea kazi Neno la Mungu angefanywa kamili, roho, nafsi na Mwili, mahitaji yao yangetimizwa na maisha yao yangeenda katika utaratibu. Shetani hawezi kukuumiza kama ukiliamini na kulitendea kazi Neno la Mungu. Anaweza na atakujaribu, anaweza kukuwekea ishara juu yako ambazo zitaonesha kama Neno si kweli, lakini hawezi kukuumiza endapo umejitiisha kikamilifu kwa Ubwana wa Neno, ambaye ndiye Yesu Mwenyewe!

Mara Neno linapopandwa moyoni mwako, lazima "usimame", ama usubiri ukikabiriana na mazingira ya adui, hadi mche uliopandwa ukomae. "Kwa sababu hiyo twaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kushindana siku ya uovu, na mkiisha kuyatimiza yote, kusimama" (Waefeso 6:13).

Mara zote tutahitaji kuyashinda magonjwa na tunaweza kushinda na kupata ushindi! Njia tunayoitumia kushinda, yale matokeo ni kazi ya Mungu. Mara nyingi mambo hayaendi kama tunavyopanga. Hata hivyo, tunaweza kumtumaini Yeye katika mambo yote!

Hivyo basi kwa namna rahisi na ya kitoto ya kuangalia vita vya kiroho, hebu tuelekeze macho kwenye silaha pekee ya Shetani na pia mwikio wetu kwa vitendo vyake. Kusimama, au vita vya kiroho, havipo kwa ajili tu ya watakatifu wa Mungu ambao wametembea na Mungu kwa Miaka 20. Hapana, vipo kwa ajili ya kila mtoto wa Mungu. Mungu hutuwezesha sisi wote kupigana vita katika nguvu na uweza Wake. Hatuhitaji kuwa wataalam. Kumbuka Mungu huwapa neema wanyenyekevu. Yakobo 4:6 inasema, "Lakini hutujalia sisi neema iliyozi; kwa hiyo husema, Mungu huwapinga wajikuzao, bali huwapa neema wanyenyekevu".

Kwahiyo tunapiganaje vita hii?

1. Lazima kwanza tujue kitu fulani. Hekima.

Hekima nikujua na kuutegemea ukweli kwamba Msalaba wa Yesu ulifyonza mabaya yote na kila kitu lazima kibadilike kuwa baraka. Sheria ya uvutano ya dunia inasema kwamba chochote kinachokwenda juu LAZIMA kirudi chini. Sheria ya upatanisho (ambayo ndiyo sheria ya Msalaba - Wakolosai 1:20) inasema kwamba uovu wote umenyang'anywa silaha, na sasa lazima pawe na baraka, IKIWA utaamini.

Hekima ni kujua kwamba vitu vyote vimepatanishwa kwa njia ya Msalaba. Sio watu peke yake, bali ni vitu vyote. "na kwa yeye kuvipatanisha vitu vyote na nafsi yake, akiisha kufanya amani kwa damu ya msalaba wake; kwa yeye, ikiwa ni vitu vilivyo juu ya nchi, au viliyo mbinguni" (Wakolosai 1:20).

Kupatanisha ni Neno lenye nguvu. Strongs Concordance huliita "Kurejesha hali ya zamani ya amani". Linaelezwa kama "kukarabati, kurejesha katika kufanya kazi, kufanya amani kati ya maoni ama makundi

mawili yanayopingana". Vines Bible Dictionary hulifafanua kama "kubadilisha kutoka katika uadui na kuwa urafiki". Msalaba wa Yesu Kristo huchukua "adui" zetu wote, kama ni watu, mapepo, mazingira, magonjwa, umaskini, kila kitu, na kuyabadilisha kuwa rafiki. Hii ni Hekima! Kristo alisulubiwa!

2Wakorintho 5:18 inasema, "Lakini vyote pia vyatokana na Mungu, aliyetupatanisha sisi na nafsi yake kwa Kristo, naye alitupa huduma ya upatanisho...". Hivyo hii ni huduma yetu hapa duniani, kuwachukua maadui wote wa maisha, kuwazamisha ndani, ya damu na Msalaba wa Yesu Kristo, na kuwageuza wawe marafiki. Naweza kukwambia kwa Neno la Mungu na kwa uzoefu wangu kuwa hii ni kweli. Linafanyakazi kama utasimama.

Hekima ni kujua kuwa damu ya Yesu imemshinda Shetani. Ina maana gani kuwa na ushindi juu ya Shetani? Ina maana gani damu ya Yesu hutupatia nguvu? "Basi, kwa kuwa watoto wameshiriki damu na mwili, yeye naye vivyo hivyo alishiriki yayo hayo, ili kwa njia ya mauti amharibu yeye aliyekuwa na nguvu za mauti, yaani, Ibilisi, 15 awaache huru wale ambao kwamba maisha yao yote kwa hofu ya mauti walikuwa katika hali ya utumwa" (Waebrania 2:14,15).

"Lakini tukiwa tulikufa pamoja na Kristo, twaamini ya kuwa tutaishi pamoja naye; 9 tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena" (Warumi 6:8,9).

Mistari hii inasema kuwa Shetani "aliharibiwa". Hilo linamaanisha nini hasa? Anaonekana kufanya kazi ya kuzunguka zunguka akiharibu wengine.

Neno haribu linaelezwa katika Strong's Concordance kama:

1.) kufanya ikae tu, isiyo na kazi, isiyofanya kazi, kutotenda kazi
1a. kusababisha mtu ama kitu kutokuwa na uwezo wa kufanya kazi.

1b. kuondolea nguvu, ushawishi, uwezo.

Wakati Yesu na wewe na mimi tulipofufuliwa katika wafu, tulizaliwa mara ya pili kama kabila/jamii mpya ambayo haikuwa tena chini ya Shetani. Hana tena utawala juu yetu. Tunautawala juu yake. Shetani

alitumia nguvu yake kuu juu ya Yesu Msalabani na kisha Yesu alifufuliwa. Shetani hana nguvu zaidi ya kutumia. Ameishiwa na vifaa na silaha.

Bado anaweza kuwaharibu wasioamini, na anaweza kumdanganya mwamini, lakini kama tukiifahamu kweli, hataweza tena kutudhuru. Kwa umbali wote unaotuhusu ameshaharibiwa. Kama tukisimama katika kweli, Shetani anachoweza kufanya tu ni kutudanganya. Shetani hana nguvu juu ya viumbe vipya; ukijumuisha wewe na mimi!

"Naye ndiye kichwa cha mwili, yaani, cha kanisa; naye ni mwanzo, ni mzaliwa wa kwanza katika wafu, ili kwamba awe mtangulizi katika yote" (Wakolosai 1:18).

Hili ni andiko la maisha. Tunapaswa kutambua wapi tulipo ndani yake. Litatuwezesha kuyakabili mateso. Ndiyo, Yesu anarudi duniani siku moja, lakini pia "atarudi" kwako sasa kubadilisha tatizo lako kuwa baraka.

Mfano mzuri wa ushindi wa jinsi hii ni Danieli akiwa ndani ya tundu la simba katika Danieli sura ya 6. Danieli alikuwa akimfuata Mungu kikamilifu na aliteswa na maadui zake na maadui za Mungu. Badala ya kuokolewa *toka* katika tundu la simba, alishinda *ndani* ya pango la simba. Matokeo yalikuwa kwamba adui zake walishindwa kabisa.

"Mfalme akaamuru, nao wakawaleta wale watu waliomshtaki Danieli, wakawatupa katika tundu la samba, wao, na watoto wao, na wake zao; na wale simba wakawashinda wakaivunja mifupa yao vipande vipande, kabla hawajafika chini ya tundu. Ndipo mfalme Dario akawaambia watu wa kabila zote, na taifa zote, na lugha zote, waliokaa juu ya uso wa dunia; Amani na iongezeke kwenu. Mimi naweka amri, ya kwamba katika mamlaka yote ya ufalme wangu watu watetemeke na kuogopa mbele za Mungu wa Danieli; maana yeye ndiye Mungu aliye hai, adumuye milele, na ufalme usioharibika, na mamlaka yake itadumu hata mwisho. Yeye huponya na kuokoa, hutenda ishara na maajabu mbinguni na duniani, ndiye aliyemponya Danieli na nguvu za simba. Basi Danieli huyo akafanikiwa katika enzi ya Dario na katika enzi ya Koreshi, mwajemi", (Danieli 6:24-28).

Ninamashaka kama Danieli angefanikiwa na kwamba maadui zake wangeshindwa endapo hangepitia katika tundu la simba.

2. Pili, lazima tutende kitu. "Maana kama vile mwili pasipo roho

umekufa, vivyo hivyo na imani pasipo matendo imekufa" (Yakobo 2:26).

Kupigana vita, ama kusimama, kwa hitaji tutende kitu fulani, hatupaswi kutulia tu. Waebrania 6:12 inasema, "ili msiwe wavivu, bali mkawe wafuasi wa hao wazirithio ahadi kwa imani na uvumilivu".

a. Lazima tutunze "ubikra" wetu. Hii ni kwamba lazima tubakie wasafi mbele za Bwana. Lazima tutunze kumbukumbu fupi za dhambi zetu, na kuhakikisha zimetubiwa na kusafishwa mbele za Mungu na watu. Natumia Neno "ubikra" kwa kuwa ninataka ukumbuke kuwa Yesu hukufanya kana kwamba hujawahi kutenda dhambi kila wakati unaposamehewa!

Lazima tuishi maisha yanayomstahili Bwana na tukae katika uwepo Wake. "1 Kwa hiyo nawasihi, mimi niliye mfungwa katika Bwana, mwenende kama inavyoustahili wito wenu mlioniwa" (Waefeso 4:1). "Aketiye mahali pa siri pake Aliye juu atakaa katika uvuli wa Mwenyezi" (Zaburi 91:1). Hebu simama sasa na usome sehemu iliyobaki ya Zaburi 91.

Kama shetani atakufanya utende kwa kufuata tabia yako ya kale (kimwili) na kwa namna ya ulimwengu, anaweza kukututenga na uwepo ulio hai wa Mungu na anaweza kuiba ahadi za Mungu. Wagalatia 5:19-21 inasema, "Basi matendo ya mwili ni dhahiri, ndiyo haya, uasherati, uchafu, ufisadi, ibada ya sanamu, uchawi, uadui, ugomvi, wivu, hasira, fitina, faraka, uzushi, husuda, ulevi, ulafi, na mambo yanayofanana na hayo; katika hayo nawaambia mapema, kama nilivyokwisha kuwaambia, ya kwamba watu watendao mambo ya jinsi hiyo hawataurithi ufalme wa Mungu". (Mbegu ya Neno lizaalo matunda katika maisha yako.)

b. Biblia inatufundisha kuwa kuna kipindi cha kusubiri vitani na kwamba ututumie Neno la Mungu kama upanga. Waefeso 6:17b inasema, "... upanga wa Roho ambao ni Neno la Mungu."

Tunaambiwa katika Waebrania 3:1, "Kwa hiyo, ndugu watakatifu wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu. " Yesu huyapeleka maungamo yetu kwa Baba, akiwa kama kuhani wetu Mkuu, na Baba, huona kuwa yamekwisha, alimradi ni Neno la Mungu. Adui pia huyapeleka maungamo yetu, maungamo yasiyo sahihi, na hutimiza kile tunachosema.

Neno la Mungu linapoungamwa (kukiri) na kuombwa juu ya mtu ama hali, huwa lina nguvu! Yesu aliumba kila kitu kwa Neno lake. Yesu NDIYE Neno. Yesu alitupa mamlaka kulitumia Neno kana kwamba ni Yeye ndiye anenaye!

Yohana 1:1-3 inasema, "Hapo mwanzo kulikuwako Neno, naye Neno alikuwako kwa Mungu, naye Neno alikuwa Mungu. 2 Huyu mwanzo alikuwako kwa Mungu. 3 Vyote vilifanyika kwa huyo; wala pasipo yeye hakikufanyika cho chote kilichofanyika".

Wakati pasaka iliposimikwa kwa Waisraeli katika Kutoka 12, Waisraeli waliambiwa kuweka damu ya kondoo asiye na hatia juu ya milango yao na malaika wa mauti (pepo) ange "pita juu" na asiwadhuru. Yesu ni Mwana Kondoo wa Mungu, na tunaaweza kuiweka damu Yake juu ya milango yetu na ya wapendwa wetu tunaowaombea. Namna gani?

Ufunuo 12:11 inasema, "Nao wakamshinda kwa damu ya Mwana-Kondoo, na kwa neno la ushuhuda wao; ambao hawakupenda maisha yao hata kufa".

Maneno ya kinywa chetu yataitumia damu. Tambua katika Kutoka 12 kuwa muda wote damu ilipobaki tu ndani ya beseni, haikufanya lolote jema. Lakini walipochukua hisopo, wakaichovya katika damu na kuiweka katika milango yao, kisha Mungu na Ibilisi waliweza kuiona. Hisopo ilikuwa aina ya mmea ambao haukuwa na thamani sana. Maneno ya kinywa chetu hayaoneshi kuwa na thamani sana, lakini tunapoyachovya ndani ya Neno la Mungu (ambaye ndiye Yesu mwenyewe) na kuyatumia kama damu, Mungu huyaona na Ibilisi huyaona!

Yesu huchukua maungamo yetu na kuyafanya yenye nguvu. Waebrania 3:1 inasema, "Kwa hiyo, ndugu watakatifu wenye kuushiriki mwito wa mbinguni, mtafakarini sana Mtume na Kuhani Mkuu wa maungamo yetu, Yesu".

Tunapolinena Neno la Mungu Yesu hulipeleka kwa Baba na kumwomba alitekeleze. Yohana 16:23 inasema, "Tena siku ile hamtaniuliza neno lo lote. Amin, amin, nawaambia, Mkimwomba Baba neno lo lote atawapa kwa jina langu".

Kisha tunaweza kupumzika na kuliacha Neno litende kazi.

Waebrania 4:1 inasema, ", ikiwa ikaliko ahadi ya kuingia katika raha yake, na tuogope, mmoja wenu asije akaonekana ameikosa"

Waebrania 4:12 inasema, "Maana Neno la Mungu li hai, taena lina nguvu, tena lina ukali kuliko upanga uwao wote ukatao kuwili, tena lachoma hata kuzigawanya nafsi na roho, na viungo na mafuta yaliyomo ndani yake; tena li jepesi kuyatambua mawazo na makusudi ya moyo"

Malaika huingia kazini wanapolisikia Neno la Mungu. Zaburi 103:20 inasema, "Mhimidini BWANA, enyi malaika zake, ninyi mlio hodari, mtendao neno lake, mkiisiliza sauti ya neno lake"

Mapepo hukimbia! Zaburi 149:4-9. *"Watauwa na waushangilie utukufu, waimbe kwa sauti kuu vitandani mwao. Sifa kuu za Mungu na ziwe vinywani mwao, na upanga mkali kuwili mikononi mwao. Ili kufanya kisasi juu ya mataifa, na adhabu juu ya kabila za watu. Wawafunge wafalme wao kwa minyororo, na wakuu wao kwa pingu za chuma. Kuwafanyia hukumu iliyoandikwa; hiyo ndiyo heshima ya watauwa wake wote. Haleluya".*

Kumbuka kwamba haujaribu kushinda vita, Yesu Msalabani alikwisha shinda vita. Wewe umeitwa "kusimama". Hii inamaanisha kusimamishwa imara katika nafasi yako ya ushindi mbele ya mahakama ya sheria, ili kwamba uongo uliosemwa juu yako usishinde. Utakutana na msongo mwingi wa mawazo, lakini utashinda kama ukisimama.

Kusimama dhidi ya hila za ibilisi.

Waefeso 6:11 inasema, "Vaeni silaha zote za Mungu, mpate kuweza kuzipinga hila za Shetani".

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".

Sura ya 17
Mateso Na Dhiki.
Mlango wa kuingilia ulimwengu usioonekana.



Sasa hilo ndiyo jambo la kijinga
SIJAWAHI sikial!

Kabla sijakutana na Bwana, mara zote nilifuatilia raha na hali ya maisha ya furaha yasiyo na maumivu. Baada ya kukutana Naye, nilihisi kuwa angenisaidia kufuatilia hizo raha na maisha ya furaha. Hilo halijawa kweli. Ameniongoza katika uzima tele, lakini hilo limekuwa kupitia mgandamizo mwingi na majaribu na dhiki, ambapo katika yote hayo ninashukuru sana ninapoangalia yaliyopita.

Twapaswa kutambua kwamba tunaishi katika sayari ambayo imeangukia katika dhambi, au kwa kuliweka katika namna nyingine, mwadamu ameasi sheria zote za Mungu. Hilo likiunganishwa na vitendo viovu vya Shetani vya kuua, kuiba, na kuharibu, linatosha kabisa mateso kwa kila mmoja.

Maisha yana ukakasi, hayana haki, na yana tengeneza mateso kwa kila mtu kwa namna fulani. Watu hujaribu kuficha maumivu ya maisha kwa njia ya kutafuta fedha, ambayo inaweza kununua raha za muda mfupi. Pia wanafunika maumivu ya maisha kwa madawa ya kulevya, burudani, ufanisi, na vitu vingine vingi. Tunahitaji kujua na kutambua kuwa tunaishi vitani, na kuna mvutano kati ya Ufalme wa Mungu na ufalme wa ulimwengu. Vita vimekwisha shindwa katika umilele, lakini ni kazi yetu kuuleta ushindi katika mazingira yetu ya ushawishi. Mvutano huu utasababisha mateso; hata hivyo, hebu tuwe sahihi katika kueleza maana

ya mateso. Tunapaswa tumtafute Mungu ili kwamba tujue jinsi ya kuyapinga mambo yale ambayo Shetani anajaribu kutuwekea.

Mungu si mwanzilishi wa mateso ama wa mambo yasiyo ya haki katika maisha. Hata hivyo, Mungu anakusudia mambo magumu maishani yatulete kwenye hatima ya utajiri wetu wenyewe. Anataka kwamba tumgeukie Yeye. Tukifanya hivyo, Yeye hutenda miujiza na kugeuza matatizo yetu kuwa shangwe.

Waamini wengi mno wanashida katika kujifunza matarajio ya Mungu juu ya mateso, majaribu na dhiki.

Kuna kanuni kuu mbili zinazopingana. Moja inasema kuwa hatupaswi kupata mateso kwa kuwa ni waumini. Nyingine inasema kuwa sisi ni walewale watenda dhambi wa zamani hivyo Mungu hutufundisha kwa kutufanya tuteseke. Ile ya pili inapindisha tabia za Mungu kwa kiwango kikubwa sana! Mungu haweke maradhi na magonjwa juu yetu. Wala hana yoyote ya kutuwekea. Hadithi ya Ayubu inathibitisha hili. Mitazamo yote miwili iko mbali sana na ukweli. Mitazamo yote inachembechembe za ukweli, ila kanuni zake hazitafanya kazi wakati zikiwa kwenye "moto".

Naenda kushirikiana na wewe kile ambacho Mungu amenifundisha kuhusu hili.

Nilijifunza hili kupitia uzoefu na kupitia ufunuo katika maandiko. Ni vyema kama usipokubaliana nami. Najua kwamba sifahamu mambo yote yanayohusu mateso. Kamwe (bado) sijaitwa kupitia mateso ya kimwili ama sijawahi kukaa jela kwa sababu ya Injili.

Hakuna jinsi itakayonifanya nitumie nafasi yote katika kitabu hiki ili kutoa mafunzo timilifu kuhusu mateso. Wala sina sifa za kufanya hivyo, ila nimekuwa katika majaribu na mitihani mikali. Hivi ndivyo nimejua kupitia mazingira magumu, ambayo baadhi yake yalikuwa yanatishia uhai.

Je, tunatakiwa kuteseka? Aina gani ya mateso? Kwanza, nataka nitofautishe kati ya "mateso ya kipumbavu" na "mateso ya ukombozi".

"Mateso ya kipumbavu" ni pale tunapokuwa tunavuna matokeo ya uchaguzi mbaya, kitabia, kiroho, na kimwili. Tunahitaji kuja mbele za Mungu kupokea msamaha na kurudi katika njia Yake. Utamkuta Yeye

amefungua mikono ya rehema, akiwa tayari kugeuza makosa yako kuwa shangwe.

Kuna tofauti pia kati ya Mkristo aliyejitoa kikamilifu kwa Yesu na mtu wa kawaida (Mkristo ama asiye Mkristo) anayeishi maisha kwa ajili yake mwenyewe. "Mtu awaye yote asiyempenda Bwana na awe amelaaniwa. Maranatha" (1Wakorntho 16:22).

Mwandishi Gene Edwards amenukuliwa akisema,

*Wakati Mkristo anapoamua kuyatoa maisha yake yote, na kwa ukamilifu kwa Yesu Kristo pasipo kubakisha kitu, akiuacha ulimwengu, akiachana na usalama na kugeukia hali ya kupoa bali akaendelea ili kupata mambo ya Mungu ya ndani, yaani, mambo yaliyo karibu na yanayopendwa na Bwana; unaweza kuwa na uhakika kuwa muda mfupi baadaye atagusa kiasi fulani cha maumivu. Na akisha yapata, atakuwa ameanza safari yake isiyoepukika kuelekea barabara ya mateso. Safari hiyo ya hija itambeba kutoka utukufu hata utukufu, hata utukufu, hadi siku moja, kwa mkono wa Bwana Mwenyezi, atakapofanywa kitu fulani ingawa si kikamilifu, kinachofanana na Yeye. Kinachofanana na sura Yake, sana sana kupitia Mateso.*⁹

Mateso yetu mengi ni ya akili.

Tunajaribiwa na Shetani na kugeuzwa na miili yetu kuamini uongo. Mungu anatutaka tuliadini Neno lake bila kujali mambo mabaya yanaonekanaje. Mungu anatutaka tulikiri Neno lake dhidi ya hali zetu litumike kama chombo cha kubadilisha katika ulimwengu wa Ufalme wa Mungu. Kipindi cha muda huu tumewekwa katika *mgandamizo mkubwa*. Angalia Marko sura ya 4.

⁹. The Inward Journey, Gene Edwards, Christian Books, Goleta, CA, 1982, ukurasa 141

Vipi kuhusu waliouawa kwa sababu ya Injili?

Mungu amewaita baadhi kuuawa kimwili kwa kuteswa. Ufunuo 12:11 inasema kuwa tusiwapende maisha yetu hata kufa. Kanisa la mwanzo lilipiga hesabu kuwa kwa kila mtu mmoja aliyeuawa watu mia tatu waliokolewa. Sina uhakika, ila kwa kusoma maelezo ya Stefano katika Matendo 7 na maelezo ya hali zingine za kihistoria, inaonesha kama Mungu hutoa neema maalum wakati mtu anapoteswa kwa ajili ya Injili. Andiko linasema kuwa Yesu alionja mauti kwa ajili ya kila mtu.

Kuuawa kwa ajili ya Injili si jambo lililopita karne nyingi zilizopita; bado linaendelea duniani kote kwa idadi kubwa. Kwa wale kati yenu watakaoitwa katika huduma, nataka kuwaheshimu. Hakika sijafuzu kwa somo hili. Nataka kuamini kuwa kama Mungu aliniita ili niuawe kwa ajili ya Injili, itakuwa ni jambo nililopewa heshima kulipitia. Neema kwa jambo hilo haitangulii kuja.

Biblia inazungumza kuhusu kushiriki katika ushirika wa mateso yake kama ilivyoonyeshwa katika Wafilipi 3:10, Wakolosai 1:24 na 2Wakorintho 4:12.

"ili nimjue yeye na uweza wa kufufuka kwake, na ushirika wa mateso yake, nikifananishwa na kufa kwake" (Wafilipi 3:10).

"Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake" (Wakolosai 1:24). "Basi hapo mauti hufanya kazi ndani yetu, bali uzima ndani yenu" (2Wakorintho 4:12). Paulo alikuwa akiongelea aina ya mateso ya ukombozi. Kadri alivyokutana na mateso katika maisha yake alijua kuwa alikuwa akivunja ngome za kiroho akiwa mwombezi wa wengine.

Kiwango cha ushiriki wetu ni kidogo kuliko kile cha ushiriki wake. Yesu peke yake ndiye ana sifa za mateso ya ukombozi yanayookoa mwanadamu. Alibeba laana yetu kwa ujumla na kikamilifu pale Msalabani. Hatuwezi kuongezea hapo, wala kujadiliana ukweli huo. Hilo halimaanishi laana hizo hazitakuja juu yetu. Ina maana kuwa zinapokuja, tusimame katika ukweli wa Msalaba na tuzibadilishe laana hizo kuwa baraka. Na ni jinsi gani jambo hili linatokea katika maisha yetu, hiyo ni juu

ya Mungu. Yeye anampango kwa ajili ya maisha yetu. Kama utakaa karibu naye na iwapo hutajadiliani na ukweli wa Msalaba, atakupitisha nyakati ngumu kwa kusudi jema.

Paulo alijua kuwa Mungu angemtoa katika mateso yake. "Bali wewe umeyafuata mafundisho yangu, na mwenendo wangu, na makusudi yangu, na imani, na uvumilivu, na upendo, na saburi; tena na adha zangu na mateso, mambo yaliyoripata katika Antiokia, katika Ikonio, na katika Listra, kila namna ya adha niliyoistahimili; naye Bwana aliniokoa katika hayo yote" (2Timotheo 3:10,11).

Ni nini kusudi la mateso?

Ninatoa jibu lenye sehemu tatu kwa swali hili. Sehemu hizi tatu ni (1) maombezi kwa watu wengine (2) kuingia ufalme wa Mungu (3) kuthibitishwa na Mungu.

1. Mateso yetu mara nyingi sana hutenda kama maombezi na vita kwa ajili ya kanisa na waliopotea, na kwa kuwashinda maadui zetu wa kiroho. Hili linaitwa maombezi kwa watu wengine.

Maombezi kwa ajili ya wengine humaanisha kuchukua nafasi ya mwingine. Yesu alimshinda Shetani pale Msalabani, lakini sasa hivi ni juu yetu kuusimika ushindi huo na kuuhitimisha. "ili sasa, kwa njia ya kanisa, hekima ya Mungu iliyo ya namna nyingi ijulikane na falme na mamlaka katika ulimwengu wa roho"(Waefeso 3:10).

Mateso yetu yanashughulika na kuhitimisha ushindi dhidi ya Shetani. "Sasa nayafurahia mateso niliyo nayo kwa ajili yenu; tena nayatimiliza katika mwili wangu yale yaliyopungua ya mateso ya Kristo, kwa ajili ya mwili wake, yaani, kanisa lake" (Wakolosai 1:24).

Kushiriki kwetu mateso Yake si sawa na ushiriki Wake, lakini yetu si ya ukombozi. Bado kuna kitu kinapungua kwenye mateso Yake kuhusiana na wanaume na wanawake ambao bado wako katika vifungo. Yesu amefanya sehemu yake; Alikuwa ndiye pekee mwenye sifa za kuteseka kwa ajili ya wokovu wetu. Hata hivyo, bado kuna kitu kinachopungua katika mateso Yake kuhusiana na wanaume na wanawake ambao bado wako katika kifungo. Kuna sehemu ambayo bado

mwanadamu anapaswa kuifanya, na inahusisha zaidi ya kusema maombi tu.

Mateso yetu si jambo halisi; ni kivuli tu cha jambo halisi yanapolinganishwa na Yesu. Zaburi 23 inayaita bonde la uvuli wa mauti. Vivuli haviwezi kuumiza, lakini vinaweza kusababisha hofu. Zaburi 23 inaendelea kusema kuwa hatupaswi kuogopa maana yeye yuko nasi, na kuwa njia hii ni njia ya haki iliyochaguliwa na Mungu na sio Shetani. Zaidi inasema kuwa meza yetu imeandaliwa machoni pa watesi wetu, tumepakwa mafuta na kikombe chetu kinafurika kwa ajili ya baraka za wengine.

Kwa nini mateso yetu si jambo halisi? Angalia Ufunuo sura 4 na 5 Kwenye kiti cha enzi, Yohana alimwona MwanaKondoo ambaye alikuwa peke yake aliyestahili kukichukua kitabu, ambacho Zekaria anaieleza kuwa ni laana (Zekaria 5:3). Kisha kitabu kinafunguka na mlipuko unatokea (majanga katika kitabu cha Ufunuo). Huwa tunahisi uvuli wa laana zetu, ule mlipuko, na zinaoneka kama kitu halisi. Lakini MwanaKondoo anashikilia kitabu na ule mlipuko humpiga Yeye. Tunapomulika mwanga ndani ya kile *kivuli*, tunamwona MwanaKondoo akitiririka damu kwa ajili ya laana yetu akituambia, "Je, utakikubali kivuli cha hili kuwa ndiyo ufunguo wa kufungulia magereza ya wafungwa? Nakuahidi hakitakudhuru. Je, utafanya hivyo kwa ajili yangu?"

Yesu alifanyika maskini ili tuwe matajiri. Hebu waangalie watu maskini katika maeneo yako unayofahamika. Mtu anapaswa kukubali kivuli cha kuwa maskini kama ndiyo ufunguo wa mwisho wa kufungulia gereza lake.

Mateso hutupatia mamlaka kwa ajili ya huduma. "Heri mtu astahimiliye majaribu; kwa sababu akiisha kukubaliwa ataipokea taji ya uzima, Bwana aliyowaahidia wampendao" (Yakobo 1:12). "Taji" husimama kama mamlaka. "Uzima" ndicho tunachoeneza kwa ulimwengu uliopotea. Tunapata mamlaka kuwaleta waliopotea kwa Mungu.

Labda tungeyaita mafundisho haya "kuokolewa na kivuli".

Ninapokutana na aina hii ya mateso, kwa kweli ninaridhika na kuwa katika amani (muda mwingi) kwa sababu uwepo wake unauzito zaidi wakati huu kulikoni hapo awali. Kuna jambo fulani kuhusu kupitia haya

na kisha kuusikia moyo Wake wa upendo kuwaelekea watu unaonifariji na kunifanya nijue kutoogopa chochote kitakachotokea. Zaidi ya yote, tuna miaka michache tu iliyobaki ya kuwa maskini, ila wale watu ambao hawaokoki, kwakweli...

2. Hali zetu ngumu ni milango ya kuingilia Ufalme wa Mungu.

Tulipozaliwa mara ya pili kisheria tulihamishwa toka ufalme wa "ulimwengu" kwenda Ufalme wa Mungu. Hiyo yote ilifanyika kwa neema ya Mungu na haikuhusiana chochote na mateso yetu.

"Naye alituokoa katika nguvu za giza, akatuhamisha na kutuingiza katika ufalme wa Mwana wa pendo lake" (Wakolosai 1:13).

Hata hivyo, kama zilivyo kweli nyingi za kiroho, tunatambua faida za ukweli baada ya muda kupita. Ndiyo maana maandiko yanatuambia kuwa huwa tunaugundua zaidi Ufalme wa Mungu tunapopitia majaribu na dhiki. Tunakuwa na hayo yote kisheria wakati tunapozaliwa mara ya pili, ila tunazona faida baada ya kipindi cha muda fulani.

"...imetupasa kuingia katika ufalme wa Mungu kwa njia ya dhiki nyingi" (Matendo 12:22).

Tupo katika kizazi, ambapo falme mbili, ama ulimwengu wa aina mbili unaishi (Angalia mchoro katika ukurasa unaofuata). Mmoja ni ufalme unaoonekana unaoitwa "ulimwengu". Mwingine hauonekani kwa macho yetu nao ni Ufalme wa Mungu. Ufalme wa "ulimwengu" ulianzia nyuma katika kitabu cha Mwanzo kinachoeleza baada ya mwanadamu kuanguka katika utumwa wa Shetani. Ufalme wa Mungu ulianzia kwa Yesu.

Shetani ndiye mkuu wa mfumo wa ulimwengu huu. Yesu ni Mfalme wa Ufalme wa Mungu. Yesu alimshinda Shetani pale Msalabani. Ukisoma mwisho wa kitabu (Biblia), Ufalme wa Mungu unashinda. Hata hivyo, Mungu amefanya upendeleo kwetu tuulete ushindi wa Ufalme wa Mungu kwenye mazingira ya ushawishi wetu.


"...Yesu akaenda Galilaya, akihubiri Habari Njema ya Mungu, 15 akisema, Wakati umetimia, na ufalme wa Mungu umekaribia; tubuni, na kuiamini Injili" (Marko 1:14,15). "Nami nawaambia kweli, Wapo katika

hawa wanaosimama hapa, ambao hawataonja mauti kabisa, hata wauone kwanza ufalme wa Mungu" (Luka 9:27).

Tuna nafasi na upendeleo wa kutumika katika Ufalme wa Mungu sasa hivi hapa duniani kabla hatujafa. "na kulionja neno zuri la Mungu, na nguvu za zamani zijazo" (Waebrania 6:5).

Hatuna nafasi katika sura hii, ama hata katika kitabu chote hiki, kufundisha mafundisho yote yahasuyo Ufalme wa Mungu. Inatosha kusema, Ufalme wa Mungu si eneo la kijiografia. Si eneo fulani ambalo tunakwenda miili yetu inapokufa. Ufalme wa Mungu uko hapa hapa pamoja na ulimwengu ambao tunauona kwa macho yetu. Ni ulimwengu usioonekana ambamo Mungu anatawala, na humo ndimo waamini wanayo nafasi ya kumtii Mfalme na kuwa watawala.

Falme zote mbili zinaishi kwa pamoja wakati wa kizazi hiki.



Tunahitaji kujua kuwa mkandamizo ama ugumu wowote tunaopitia utakuwa mlango kwetu kuingia ndani zaidi katika Ufalme wa Mungu. Litaleta pia ushindi wa Ufalme katika mazingira ya ushawishi wetu.

"Heri walio maskini war oho; maana ufalme wa mbinguni ni wao" (Mathayo 5:3). Neno hili nililotumia kama "maskini" ni ptocheuo. Strongs

Concordance inalifafanua kama "ombaomba, asiye na namna, aliyechanganyikiwa, asiye na utajiri, anayetambua nafasi yake ya uduni, asiyejiweza". Wakati ufalme wa ulimwengu unapokupungukia, ndipo unakuwa na uwezo wa kuutafuta Ufalme wa Mungu. Hii inajumuisha maisha yajayo baada ya maisha ya sasa. Nilipojua kwa hakika kuwa sikuwa na mamlaka na kule nitakakoenda baada ya kufa, nilikuwa maskini, na Ufalme wa Mungu ukanjia kwa sababu ya uhitaji huo. Nilipojua kwa hakika kuwa nilikuwa maskini kwa ajili ya uponyaji wa mwanangu, Ufalme wa Mungu ulinjia.

Ufalme wa Mungu bado unaendelea kunijia kadri ninavyokumbana na namna mpya za "umaskini". Je, ninafurahi? Hapana! Nalishangilia? Ndiyo! Linaniingiza ndani zaidi kwenye uwepo wa Mungu kupitia ushirika wa mateso Yake, na linatenda kazi makini sana kwa ajili ya kanisa.

Kila wakati tunaposhinda hali mbaya, tunapata mamlaka zaidi ya kiroho. Tunafikiriaje lengo hili? Ni kwa kusafiri tu kuipitia njia ya mgandamizo kwenda katika kukuzwa, kutoka katika umaskini kwenda katika utajiri. Katika kitabu cha Danieli, watoto watatu wa Kiebrania walikuwa katika mgandamizo wa tanuru la moto. Badala ya kutafuta mlango nje ya tanuru, mtu wa nne aliutafuta akiwa ndani. Lakini matokeo yalikuwa ni kwamba ushawishi wa Mungu ulipanuka. Mungu aliruhusu majaribu kumkandamiza Ayubu, lakini majaribu yake yalimkandamiza kulielekea kusudi la Mungu. Kwa Yohana, kisiwa cha Patmo kilionekana kama mgandamizo ambao hakuna hata mmoja angeutaka; lakini bado lilikuwa ni gari kuelekea Ufunuo wa Yesu ni nani halisi.

Ufunuo 21:21 unatuambia kuwa "malango" ya Yerusalemu ya Mbinguni, ambao ni Ufalme wa Mungu, yametengenezwa kwa lulu. Mfumo wa kutengeneza lulu wa chaza kombe huanzia kwa hatua za maumivu. Kwanza, jeraha hutokea katika gamba na kipande cha mchanga huingia na kusababisha mwasho. Pili, mwili wa chaza kombe huitikia kwa kutoa maji maji ambayo huufunika mchanga na kuufanya sehemu yake ya juu iwe laini. Kisha matokeo yake huwa vito vya kupendeza. Ufunuo 21 inatuambia kuwa sehemu kubwa ya Ufalme imetengenezwa kwa vito vingine vya thamani ambavyo katika dunia ya asili yanafanyika kwa

kupitia mgandamizo mkubwa ndani ya ardhi.

Maisha ya Ukristo ni hatua za ukombozi kutoka ulimwengu mmoja kwenda mwingine, na kifo, kama vile ilivyokwisha semwa kweli, "ni njia pekee ya kutokea ulimwengu wowote tuliomo",¹⁰

Maisha ya Kikristo si kama ya ulimwengu.

Ulimwengu hujishughulisha na maendeleo na kuwa juu. Ufalme wa Mungu hufanya kazi kwa kanuni ya ufunuo. Bila kifo, ufufuo hauwezekani. Maisha ya Kikristo, kwa sababu hiyo, hushughulika na kifo kwanza, kisha ufufuo. Umaskini na mgandamizo si mwisho, ila haya ni mlango tu kuingia uzima tele! Tunapaswa kukumbuka kuwa tunajenga ufalme kwa ajili ya Mungu, ambao ni wa milele, na ambao viumbe vyake haviwezi kufikiwa na ulimwengu na Shetani. Ni kile tu kilichopitia kifo ndicho kinasifa. Hili limeonyeshwa katika Warumi 6:9-10 na maandiko mengine mengi.

"Tukijua ya kuwa Kristo akiisha kufufuka katika wafu hafi tena, wala mauti haimtawali tena. 10 Maana kwa kule kufa kwake, aliifia dhambi mara moja tu; lakini kwa kule kuishi kwake, amwishia Mungu" (Warumi 6:9,10).

Hadi hapa nimekupatia nadharia nyingi na maandiko. Sasa nataka kulifanya hili liwe kwa kitendo na liwe kwa kitu unachoweza kukitumia kwa maisha yako ya kila siku.

Maisha yetu na Mungu huonyesha kwenda kwa mzunguko ama ni hatua zinazoonekana kama zifuatazo:

a. Hitaji. Tunakutana na hali mbaya ya kukatisha tamaa na kugundua kuwa ziko nje ya uwezo wetu kuzitatua.

b. Ahadi. Tunamwendea Mungu kwa njia ya maandiko na Roho Mtakatifu na tunapokea ahadi Yake kama Neno la mbegu lililopandwa mioyoni mwetu. Marko 4:11 inasema kuwa hatua hii *ni siri* ya Ufalme wa Mungu.

¹⁰Mwandishi hajulikani: The Refiner's Fire, volume II, World Challenge, Lindale, TX., ukrasa 106.

c. Dhiki. Kama ilivyo katika Marko 4, Shetani huja na kuliiba Neno la ahadi ambalo lilipandwa ndani ya mioyo yetu. Tunahisi majaribu kutoka mwilini mwetu, kutoka kwenye masumbufu ya ulimwengu, na kutoka katika kila aina ya uongo ambao unatupwa juu yetu kupitia mazingira na "mabomu ya mawazo". Wakati huu, kusimama katika Neno huwa ni mgandamizo mkubwa. Wakati wa dhiki hii "ubinafsi" wetu wa zamani, asili ya kuzaliwa tuliyoirithi kwa Adamu, inakufa na asili mpya ya Kristo inachukua nafasi ndani yetu.

d. Tunafikia mwisho wa nguvu zetu. Tunajaribu kuendelea kuvumilia, lakini tunahisi kama hatuwezi kumudu. Tunahisi kama kukata tamaa. Haya ni mateso. Suluhisho letu ni kupumzika ndani ya Neno la Mungu. Mafundisho kamili ya jambo hili yamo katika mfululizo wetu, "Kukua au Kufa".¹¹

Mara nyingi sana, kuna hali ya kukatisha tama juu ya Mungu kwa sababu huwa Hatatui matatizo yetu kwa namna tulivyofikiri. Tunahisi tumetelekezwa. Kama tunapitia kusulubishwa kwetu wenyewe, basi tunahitaji kufahamu mambo mawili. La kwanza, hatuna mikono ya kutosha kujipigilia misumari wenyewe Msalabani, na la pili, kuhisi tumeachwa na Mungu ni sehemu ya utaratibu wa kupitia.

e. Mungu anakuchukua. Inaonesha kama vile tunapitia aina fulani ya "unyakuo", wakati Mungu anapotuchukua kutuketisha Naye katika ulimwengu waroho. Tunaona kiwango kipya cha uwepo Wake. Tunapokea ufunuo kuwa tumo katika barabara na Mungu, na kuwa kila kitu kitakuwa sawa. Hili hakika husaidia hisia zetu. Tunapokea amani Yake ipitayo ufahamu.

f. Kutengana na ulimwengu. Kuna mtengano usio wa hiari kutoka katika vitu na utajiri wa mfumo wa ulimwengu. Hatuangukii mwanadamu tena wala taasisi ya kutuokoa. Tunajua kuwa hatuwezi kujiokoa sisi wenyewe. Tunajua ni Mungu, tena Mungu pekee kwa wakati Wake na kwa njia yake atatuokoa. Tunakuwa hatuna msaada kama watoto wanaomsubiri baba yao awape mahitaji.

¹¹International School Of The Bible Publishers Grow or Die. ISBN# 0-9676731-0-0. Tuma barua pepe info@isob-bible.org kwa ajili ya maelezo..

g. Uelewa wa Ufalme. Kila wakati tunapitia mzunguko huu, tunaelewa zaidi kuhusu ulimwengu wa roho, ufalme wa Mungu, na nguvu za kishetani za mfumo wa ulimwengu.

h. Ukombozi. Mungu huingilia kati kwa wakati na njia Yake. Tunaona mkono wake ukitenda. Si kwa namna tuliyotarajia. Inatenda zaidi ya vile tulivyotazamia. Tunaona kuwa tumekwisha jitwika Msalaba wetu na sasa tuko tofauti.

3. Kujaribiwa.

Kwanza tuliongea vita vya kiroho na kisha tukaongelea kuhusu kuingia Ufalme wa Mungu; sasa tunakwenda kwenye kipengele cha tatu, ambacho ni kujaribiwa. "ili kwamba [kujaribiwa] kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo *hujaribiwa* kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo" (1Petro 1:7).

Neno "kujaribu" ni neno linalotumika katika kusafisha dhahabu na fedha. Kujaribu humaanisha kuweka dhahabu ndani ya moto ili kwamba uchafu na takataka ziungue na kutoka. Matokeo ni kwamba dhahabu ile inakuwa ya thamani zaidi na inakuwa safi. Tunapojaribiwa, njia zetu za zamani za kimwili na za kidunia zinaunguzwa na kutolewa na Mungu anakuwa amethibitisha kuwa tunafaa katika huduma Yake. Kama tulivyotaja mwanzoni, mara zote kuna vita, mateso fulani, na mvutano fulani wa kiroho unapoamua tu kumfanya Mungu kuwa ndiye mtoaji wa mahitaji yako. Ni kama "kumeguka" kutoka kwa mungu mwingine kwenda kwa Mungu aliye Hai. (Matendo 14:22). Yesu alisema katika Yohana 17:18 kuwa anatumia kwenda ulimwenguni vile vile kama Yeye naye alivyotumwa, kwa kupitia vita vya kiroho na magumu.

Kusafishwa huku kwaweza pia kuelezwa kama "kuuvunja mwili wetu", ambao ni asili yetu ya zamani na nguvu ya nafsi. Wakati mwingine utoshelevu wetu wenyewe waweza tu kufifishwa kupitia hatua ya kujaribiwa. "Amin, amin, nawaambia, Chembe ya ngano isipoanguka katika nchi, ikafa, hukaa hali iyo iyo pake yake; bali ikifa, hutoa mazao mengi" (Yohana 12:24). Gamba la nje la mbegu lazima livunjike ndipo mbegu itoe matunda. Gamba letu la nje ni ile roho yetu ya kujitosheleza, na nguvu ya nafsi yetu.

Hatimaye.

Waisraeli walipotoka Misri kupitia Bahari ya Shamu, moja ya vituo vyao vya kwanza jangwani kilikuwa ni kisima cha maji kinachoitwa Mara, ambayo inamaanisha "uchungu". Maji hayo hayakuwa yanafaa kwa kunywa, kwa kuwa yalijawa na madini mazito. Watu walikuwa na kiu sana na wakaanza kunung'unika nung'unika. Musa alimwuliza Mungu jambo la kufanya. Bwana alimwonyesha Musa mti fulani ili autupie ndani ya yale maji machungu. Alipofanya hivyo, maji yalifanywa matamu. Kutoka 15:25 inasema, "Naye akamlilia BWANA; BWANA akamwonyesha mti, naye akautia katika hayo maji, maji yakawa matamu. Basi akawawekea amri na hukumu huko, *akawaonja*" (Kutoka 15:25). Tambua hilo neno "akawaonja" au "kujaribiwa".

Ule mti ni alama ya Msalaba wa Yesu Kristo, ambao ukitupiwa ndani ya hali zetu chungu unazifanya kuwa tamu. Habari hii pia inatutia moyo kumtafuta Bwana kupata "mti" upi hasa wa kutupia ndani ya halizetu chungu. Musa angeweza kuchagua wowote kutoka msituni, na usingeleta matokeo kama yale ya ule alioambiwa na Bwana kuuchagua. Kwa maneno mengine, tunapopata uchungu maishani mwetu, tunahitaji kumsogelea Mungu ili kwamba tuweze kumsikia Yeye akituambia kwa usahihi hatua inayofuatia, tuichukua; daktari gani tumfuate, dawa gani tutumie, kazi gani tufanye, n.k.

Kutoka 15:26 inabeba sehemu ya kwanza ya ahadi yako ikiwa na "KWAMBA" kubwa. Inasema "akawaambia, Kwamba utaisikiza kwa bidii sauti ya BWANA, Mungu wako, na kuyafanya yaliyoelekea mbele zake, na kutega masikio usikie maagizo yake, na kuishika amri zake, mimi sitatia juu yako maradhi yo yote niliyowatia Wamisri; kwa kuwa Mimi ndimi BWANA nikuponyaye" (Kutoka 15:26).

Kutoka 15:27 inabeba ukombozi wako, na inasema, "Wakafikilia Elimu, palipokuwa na chemchemi kumi na mbili, na mitende sabini; wakapanga hapo, karibu na maji" (Kutoka 15:27).

Aina ya Ufalme wa Mungu ilioneshwa katika Elimu. Elimu ilikuwa na chemchemi kumi na mbili; kumi na mbili ikiwa ni alama ya Ufalme wa Mungu, na mitende sabini, hakika ni sehemu ya kivuli, faraja na baraka. Neno Elimu linamaanisha nguvu kwa kitu fulani kinachoonekana kupindishwa.

Palikuwa na mlango, mlango wazi uliowaongoza kuingia Elimu. Uliitwa mara, kisima cha maji machungu. Wakati mti, Msalaba, ulipotumiwa dhidi ya mazingira machungu, matokeo yalikuwa nguvu katika kazi ya Ufalme.

Habari hii inahitimisha kuwa kutakuwa na mateso kabla halijafikiwa lengo. Tunatiwa moyo tuning'inie juu yake na tuwe washindi. Inahitimisha kuwa mlango wa uchungu ulio wazi utatuongoza kwenye mambo ya Ufalme wa Mungu, huenda huduma, kama mhimili katika Hekalu la Mungu.

Paulo alisema, "Maana ndugu, hatupendi, msijue habari ya dhiki ile iliyotupata katika Asia, ya kwamba tulilemewa mno kuliko nguvu zetu, hata tukakata tamaa ya kuishi. Naam, sisi wenyewe tulikuwa na hukumu ya mauti katika nafsi zetu; ili tusijitumainie nafsi zetu, bali tumtumaini Mungu, awafufuaye wafu" (2Wakorintho 1:8,9).

Hata katika mateso yako:

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda."

Sura ya 18
Yesu Anarudi
Kuna hukumu.



Ohooo, huyo mwamuzi ni nani ?

Watu kwa asili wanawajibika zaidi kwa kile kinachokaguliwa kuliko kwa kile kinachotarajiwa.

Je, ukimtuma mtoto kwenda kufanya kazi fulani, ni busara kumwambia akupeleke kukuonyesha vile alivyoihitimisha? Ama unadhani ingekuwa busara kumwambia mtoto huyu mdogo aende kufanya kazi na kumwambia kuwa kamwe hutaenda kukagua jinsi alivyoifanya?

Mungu ni mwamuzi.

Atamwita kila mtu, kila tendo na kila neno kutoa hesabu, na atatoa thawabu ama hatatoa kulingana na ukweli uliopo.

"Hasha, usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; Mhukumu ulimwengu wote asitende haki?" (Mwanzo 18:25).

"Mwenye kuihukumu nchi, ujitukuze, uwape weye kiburi stahili zao" (Zaburi 94:2).

"...Mbele za BWANA; kwa maana anakuja, kwa maana anakuja aihukumu nchi. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa uadilifu wake" (Zaburi 96:13).

"Bali ninyi mmeufikilia mlima Sayuni, na mji wa Mungu aliye hai, Yerusalemu ya mbinguni, na majeshi ya malaika elfu nyingi, mkutano mkuu na kanisa la wazaliwa wa kwanza walioandikwa mbinguni, na *Mungu mwamuzi wa watu wote*, na roho za watu wenye haki

waliokamilika, na Yesu mjumbe wa agano jipya, na damu ya kunyunyizwa, inenayo mema kuliko ile ya Habili" (Waebrania 12:22-24).

Katika mstari huu wa Waebrania 12:22-24, Mungu ameonyeshwa kama mwamuzi.

Hata hivyo, iwapo hivyo ndivyo alivyo kwa ujumla, basi lazima tuogope sana. Neno linatuonyesha kuwa Mungu ambaye ndiye Hakimu ndiye pia Yesu ambaye ni Mpatanishi. Ndiye Yeye huyo anayeweza kusimama kati ya Mungu Mtakatifu mwenye haki na watu wenye dhambi waliopotea. Tambua pia katika aya hii ya Waebrania kuwa kuna ufunuo wa damu ya Yesu ikiwa ndiyo njia na bei iliyotumika kufanya upatanisho.

"Maana Mungu hakumtuma Mwana ulimwenguni ili auhukumu ulimwengu, bali ulimwengu uokolewe katika yeye" (Yohana 3:17).

"Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba" (2Petro 3:9).

Hukumu imehamishwa kutoka kwa Baba kwenda kwa Mwana.

"Tena Baba humhukumu mtu ye yote, bali amempa Mwana hukumu yote; 23 ili watu wote wamheshimu Mwana kama vile wanavyomheshimu Baba. Asiyemheshimu Mwana hamheshimu Baba aliyempeleka" (Yohana 5:22-23).

Somo la hukumu linaweza kuwa refu sana na hapa tutajaribu tu kuangalia zile ambazo wengi wanaziita hukumu mbili kuu. Kuhusiana na hukumu hizi tutajaribu tu kuziangalia juu juu na sio kwa ndani

Rejea imefanywa kwenye "kiti cha enzi (cha Kristo) cha utukufu". Hatutaelezea yote katika kitabu hiki. (Mathayo 25:31, Mathayo 19:28).

1. Hukumu ya waamini. Katika hukumu ya kwanza, kiti ambacho mwamuzi ataketi ni Kiti cha Hukumu cha Kristo. Wale watakao hukumiwa hapa ni wafuasi na watumishi wa Kristo mwenyewe. Tutaangalia yajayo na ya sasa ya hukumu hii.

2. Hukumu ya wasioamini. Kiti cha pili cha hukumu kinaitwa "Kiti cha Enzi Kikubwa, Cheupe". Waamini katika Kristo hawatahusika na hukumu hii kwa sababu majina yao yameandikwa kwenye "Kitabu cha Uzima cha Mwana-Kondoo".

Tunapendekeza usome kitabu The Spirit Filled Believers Handbook, Mwandishi Derek Prince, sura ya 48-52 kwa ajili ya mafundisho yaliyotimia juu ya somo la hukumu.¹²

1A. Hukumu ya waamini. Kiti cha Hukumu cha Kristo (kijacho).

2Wakorintho 5:10 inasema, "Kwa maana imetupasa sisi sote kudhihirishwa mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, ili kila mtu apokee ijara ya mambo aliyetenda kwa mwili, kadiri alivyotenda, kwamba ni mema au mabaya". Tambua hili halisemi chochote isipokuwa kizuri ama kibaya, hakuna katikati.

Hukumu hii si hukumu ya adhabu, bali ya thawabu. Naamini kuwa kama tungejua zaidi kuhusu hukumu hii, tungeishi maisha yetu tofauti. Je, umewahi kutazama mashindano ya olimpiki na ukaona "hukumu" pale mwishoni? Mkimbiaji wa kwanza kufika ndiye anayehukumiwa kwanza, na kupewa Medali ya Dhahabu; nafasi ya pili huhukumiwa na kupewa fedha, n.k.

Sidhani kuna mtu kati yetu anayejua yote kuhusu Mbingu, umilele, na maisha baada ya kifo. Lakini mimi, sitaki kupoteza maisha haya na kupoteza kitu ambacho kitaendelea milele!

Tunaambiwa kutakuwa na kujaribiwa kwa moto. 1Wakorintho 3:11-15 inasema, "Maana msingi mwingine, hakuna mtu awezaye kuuweka, isipokuwa ni ule uliokwisha kuwekwa, yaani, Yesu Kristo. Lakini kama mtu akijenga juu ya msingi huo, dhahabu au fedha au mawe ya thamani, au miti au majani au manyasi, kazi ya kila mtu itakuwa dhahiri. Maana siku ile itaidhihirisha, kwa kuwa yafunuliwa katika moto; na ule moto wenyewe utaijaribu kazi ya kila mtu, ni ya namna gani. Kazi ya mtu aliyojenga juu yake ikikaa, atapata thawabu. Kazi ya mtu ikiteketea, atapata hasara; ila yeye mwenyewe ataokolewa; lakini ni kama kwa moto."

Inaonyesha kama muda mwingi, zile thawabu zinaelezwa kama kupata mamlaka zaidi na kuwa karibu zaidi na Kristo.

¹². Spirit Filled Believers Handbook, Derek Prince, Creation House - Strang Communication Company, Lake, Mary, FL.1995.

1B. Kiti cha Hukumu cha Kristo (cha sasa).

Kunayo pia hukumu ya siku ya leo ya waamini.

Naamini kuwa sisi wote tumo katika hatua kama ifuatavyo:

a. Yesu hupanda mbegu ya Neno la Mungu katika maisha yetu kwa hitaji lolote analotaka kulitimiza.

b. Shetani hujaribu kuiiba ile mbegu, na/ ama kufanya ukuaji wake usiwe na matunda Marko sura 4.

c. Tunapitia kujaribiwa imani yetu wakati wa kipindi fulani.

d. Yesu huja kutuokoa na kuileta "hukumu" yetu.

Ajapo kutuletea kile alichohaidi, Je, atatukuta tukiwa waaminifu na tukisimama katika imani? Kama ni hivyo, tunashinda; la sivyo, tumeshindwa.

Imani yetu itajaribiwa kwa moto. 1Petro 1:7 inasema, "ili kwamba kujaribiwa kwa imani yenu, ambayo ina thamani kuu kuliko dhahabu ipoteayo, ijapokuwa hiyo hujaribiwa kwa moto, kuonekane kuwa kwenye sifa na utukufu na heshima, katika kufunuliwa kwake Yesu Kristo".

Je, unasimama kwa ajili ya uponyaji, hali ya kifedha, hali ya kifamilia, kama mwombezi wa mtu fulani, kwa utauwa zaidi, ama chochote? Yesu hurudi kwa ajili ya "hukumu", ya thawabu sasa ungali bado unaishi duniani. Zaburi 96:13 inasema "Mbele za BWANA, *kwa maana anakuja aihukumu nchi*. Atauhukumu ulimwengu kwa haki, na mataifa kwa uaminifu wake".

Yesu anawaambia wanafunzi wake kuhusu hukumu kuwa itafanyika hapa na sasa katika dunia hii. Mathayo 16:26-28 inasema, "Kwani atafaidiwa nini mtu akiupata ulimwengu wote, na kupata hasara ya nafsi yake? au mtu atatoa nini badala ya nafsi yake? Kwa sababu Mwana wa Adamu atakuja katika utukufu wa Baba yake pamoja na malaika zake; ndipo atakapompa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Amin, nawaambieni, Pana watu katika hawa wasimamao hapa, ambao hawataonja mauti kabisa hata watakaponwona Mwana wa Adamu akija katika ufalme wake".

Nawasilisha kuwa mtu angechukua maandiko mengi ya hukumu yanayohusika na waamini katika Agano Jipya, na kuyatumia kwenye hukumu tutakayopewa Mbinguni na kwa mazingira ya siku hizi leo. Iwapo hukubaliani nami, hilo ni sawa. Hayo ni maoni yangu tu, na kwa kweli,

yamekuwa uzoefu wangu. Lakini sitamani kukanyaga vidole vyako vya miguu vya theolojia katika swala hili.

2. Hukumu ya wasioamini.

Mwanzo wa kunukuu kutoka The Spirit Filled Believer Handbook, mwandishi Derek Prince, sura ya 513-515.¹³

¹³. Spirit Filled Believers Handbook, Derek Prince, Creation House - Strang Communication Company, Lake, Mary, FL.1995.

(Ufunuo 20:11-15). Kisha nikaona kiti cha enzi, kikubwa, cheupe, na yeye aketiye juu yake; ambaye nchi na mbingu zikakimbia uso wake, na mahali pao hapakuonekana. Nikawaona wafu, wakubwa kwa wadogo, wamesimama mbele ya hicho kiti cha enzi; na vitabu vikafunguliwa; na kitabu kingine kikafunguliwa, ambacho ni cha uzima; na hao wafu wakahukumiwa katika mambo hayo yaliyoandikwa katika vile vitabu, sawasawa na matendo yao. Bahari ikawatoa wafu waliokuwamo ndani yake; na mauti na Kuzimu zikawatoa wafu waliokuwamlo ndani yake. Wakahukumiwa kila mtu kwa kadiri ya matendo yake. Mauti na Kuzimu zikatupwa katika lile ziwa la moto. Hii ndiyo mauti ya pili, yaani, hilo ziwa la moto. Na iwapo mtu ye yote hakuonekana ameandikwa katika kitabu cha uzima, alitupwa katika lile ziwa la moto.

Huu ndio ukomo wa dhambi yote na uasi juu ya mamlaka na utakatifu wa Mungu Mwenyezi; kutupiwa milele katika ziwa la moto wa milele. Ni wale tu ambao majina yao yameandikwa kwenye kitabu cha uzima ndio watakwepa hukumu hii ya mwisho. Majina yaliyoandikwa katika kitabu hiki ni ya wale ambao wakati wa maisha yao duniani walijithamini, kupitia imani, kwa rehema na neema za Mungu. Haya yako katika makundi mbali mbali.

Wote ambao waliweka imani yao katika sadaka itasayo ya Kristo kwa ajili ya wanadamu, wote watakuwa tayari wameshafufuliwa mwanzoni mwa milenia. Watakuwa wamepita kwa njia ya hukumu yao stahili mbele ya kiti cha hukumu cha Kristo, si kwa hukumu ya mauti, bali kuikagua thawabu yao.

Inaonesha hakika kuwa wengi wa hao wanaoonekana mbele ya kiti cha enzi kikubwa, cheupe, watakuwa hawakutimiza masharti ya kupokea rehema ya Mungu na hivyo watahukumiwa kwenda katika ziwa la moto. Pamoja na hayo, kama ilivyoonyeshwa katika sura ya 46, hakika kutakuwa na makundi mawili ya watu mbele ya kiti cha enzi, kikubwa cheupe, ambao watakwepa hukumu ya mauti na kuingia uzima wa milele.

Kundi la kwanza linajumuisha watu kama Malkia wa Kusini na watu wa Ninawi, ambao walijithaminiwenyewe kwa

rehema za Mungu ambazo aliwapa katika ufunuo mfupi na wa kiuamuzi wake Yeye Mwenyewe. Maandiko hayaoneshi huenda ni wangapi katika historia ambao huenda walipewa nafasi inayofanana na hii.

Kundi la pili litahusisha wote ambao walikufa katika imani wakati wa milenia.

Twaweza kutazamia kuwa kutakuwa na wengine ambao Mungu atawatanulia rehema kutoka kwenye kiti chake cha enzi kikubwa, cheupe? Jibu kwa hili limefungiwa ndani ya Mungu anayefahamu yote. Kwetu, tukiwa na ufahamu wenye ukomo na mtazamo finyu, ni ujinga kuanza kuchangia mawazo.

Heri tuchukue msimamo ulioonyeshwa na Ibrahimu. (Mwanzo 18:25) "Hasha, usifanye hivyo, ukamwue mwenye haki pamoja na mwovu, mwenye haki awe kama mwovu. Hasha; Mhukumu ulimwengu wote asitende haki?"

Wale waliokwisha onja rehema zisizo na kipimo za Mungu wanahakikishiwa kuwa kamwe hatawazuilia rehema zake wale wanaozistahili.

(Warumi 11:33) "Jinsi zilivyo kuu utajiri na hekima na maarifa ya Mungu! hukumu zake hazichunguziki, wala njia zake hazitafutikani!"

Kuna kitu kimoja cha mwisho cha kukumbuka kuhusu hukumu ya wasioamini. Hasira ya Mungu iliwekwa juu ya Yesu katika hukumu ya mwisho ya dhambi. Uchaguzi hakika ni wako kuikubali ama kuikataa karama ya wokovu. Sehemu pekee iliyosalama ya kuwa, ni kuwa na uhakia kuwa umeshazaliwa mara ya pili. Hapo ndipo jina lako linaorodheshwa kwenye "kitabu cha uzima cha MwanaKondoo".

Jambo moja la mwisho la kukumbuka kuhusu hukumu ya waamini ni kuwa Mungu anatafuta njia za kukupa thawabu, sio za kukuhukum. Kusudia kuishi maisha yako duniani katika utii kwa sauti ya Bwana na katika kujiachilia kikamilifu kwake ili kwamba upokee thawabu zote zilizopo ziwekekanazo kwenye umilele.

Kuja Kwa Mara ya Pili.

Mwonekano mwingine wa hukumu ni kuja duniani kwa Yesu Kristo mara ya pili. Hatutatoa mafunzo kamili juu ya somo hili hapa, lakini Biblia iko wazi sana. Anakuja tena. Bwana kwa makusudi hatupatii undani wa lini anakuja tena. Tambua katika Matendo 1:7, Yesu kwa kweli anawaambia wanafunzi wake muda mfupi kabla hajapaa Mbinguni, "Si kazi yenu kujua lini nitarudi, kazeneni kuwa mashahidi wangu" [imefafanuliwa na mwandishi].

Alikuja mara ya kwanza kama mwokozi wetu anayeteseka, mbadala wetu, Kondoo wetu azichukuaye dhambi zetu. Mara ya pili atakapokuja kama Mfalme, kusimika Ufalme Wake.

Agano la Kale na Agano Jipya yamesheheni maandiko yanayohusu kuja mara ya pili kwa Yesu duniani. Haya hapa ni machache tu.

"Lakini, ndugu, hatutaki msijue habari zao waliolala mauti, msije mkahuzunika kama na wengine wasio na matumaini. Maana, ikiwa twaamini ya kwamba Yesu alikufa akafufuka, vivyo hivyo na hao waliolala katika Yesu, Mungu atawaleta pamoja naye. Kwa kuwa twawaambieni haya kwa neno la Bwana, kwamba sisi tulio hai, tutakaosalia hata wakati wa kuja kwake Bwana, hakika hatutawatangulia wao waliokwisha kulala mauti. Kwa sababu Bwana mwenyewe atashuka kutoka mbinguni pamoja na mwaliko, na sauti ya malaika mkuu, na parapanda ya Mungu; nao waliokufa katika Kristo watafufuliwa kwanza. Kisha sisi tulio hai, tuliosalia, tutanyakuliwa pamoja nao katika mawingu, ili tumlaki Bwana hewani; na hivyo tutakuwa pamoja na Bwana milele. Basi farijianeni kwa maneno hayo" (1Wathesalonike 4:13-18).

"kadhalika Kristo naye, akiisha kutolewa sadaka mara moja azichukue dhambi za watu wengi; atatokea mara ya pili, pasipo dhambi, kwa hao wamtazamiao kwa wokovu" (Waebrania 9:28).

"Na sasa, watoto wadogo, kaeni ndani yake, ili kusudi, atakapofunuliwa, tuwe na ujasiri, wala tusiaibike mbele zake katika kuja kwake" (1Yohana 2:28).

"Wapenzi, sasa tu wana wa Mungu, wala haijadhahirika bado tutakavyokuwa; lakini twajua ya kuwa atakapodhahirishwa, tutafanana naye; kwa maana tutamwona kama alivyo" (1Yohana 3:2).

"...wakasema, 'Enyi watu wa Galilaya, mbona mmesimama mkitazama mbinguni? Huyu Yesu aliyechukuliwa kutoka kwenu kwenda

juu mbinguni, atakuja jinsi iyo hiyo mlivyomwona akienda zake mbinguni” (Matendo 1:11).

" Msifadhaike mioyoni mwenu; mnamwamini Mungu, niaminini na mimi. Nyumbani mwa Baba yangu mna makao mengi; kama sivyo, ningaliwaambia; maana naenda kuwaandalia mahali. Basi mimi nikienda na kuwaandalia mahali, nitakuja tena niwakaribishe kwangu; ili nilipo mimi, nanyi mwepo. Nami niendako mwaijua njia" (Yohana 14:1-4).

"Mkijua kwanza neno hili ya kwamba katika siku za mwisho watakuja na dhihaka zao watu wanye kudhihaki, wafuatao tamaa zao wenyewe, na kusema, Iko wapi ahadi ile ya kuja kwake? kwa maana, tangu hapo babu zetu walipolala, vitu vyote vinakaa hali iyo hiyo, tangu mwanzo wa kuumbwa. Maana hufumba macho yao wasione neno hili ya kuwa zilikuwako mbingu tangu zamani, na nchi pia, imefanyizwa kutoka, katika maji, na ndani ya maji, kwa neno la Mungu; kwa hayo dunia ile ya wakati ule iligharikishwa na maji, ikaangamia. Lakini mbingu za sasa na nchi zimewekwa akiba kwa moto, kwa neno lilo hilo, zikilindwa hata siku ya hukumu, na ya kuangamia kwao wanadamu wasiomcha Mungu. Lakini, wapenzi, msilisahau neno hili, kwamba kwa Bwana siku moja ni kama miaka elfu, na miaka elfu ni kama siku moja. Bwana hakawii kuitimiza ahadi yake, kama wengine wanavyokudhani kukawia, bali huvumilia kwenu, maana hapendi mtu ye yote apotee, bali wote wafikilie toba. Lakini siku ya Bwana itakuja kama mwivi; katika siku hiyo mbingu zitatoweka kwa mshindo mkuu, na viumbe vya asili vitaunguzwa, na kufumuliwa, na nchi na kazi zilizomo, ndani yake zitateketea. Basi, kwa kuwa vitu hivi vyote vitafumuliwa hvyo, imewapasa ninyi kuwa watu wa tabia gani katika mwenendo mtakatifu na utauwa, mkitazamia hata ije siku ile ya Mungu, na kuihimiza; ambayo katika hiyo mbingu zitafumuliwa zikiungua, na viumbe vya asili vitateketea na kuyeyuka? Lakini, kama ilivyo ahadi yake, tunatazamia mbingu mpya na nchi mpya, ambayo haki yakaa ndani yake. Kwa hiyo, wapenzi, kwa kuwa mnatazamia mambo hayo, fanyeni bidii ili mwonekane katika amani kuwa hamna mawaa wala aibu mbele yake" (2Petro 3:3-14).

Vyovyote ama wakati wowote atakaporudi, ama kama utakutana naye mwili wako utakapofariki, yote hayo hayana tofauti kubwa. Theolojia yako kuhusu siku za mwisho hakika haijalishi, tarajia jambo moja.

Anakuja! Utakutana naye jicho kwa jicho; utakutana naye akiwa kama hakimu. Unapaswa kuwa tayari!

Tunahitaji kudumisha mtazamo wa Yesu ndani ya ufahamu..

Anasubiri kwa shauku kubwa kumpokea Bibi-Arusi, Kanisa. Katika destuli ya Kiyahudi mtoto wa kiume aliandaa nyumba ya arusi, katika shamba la baba yake, akifanya kazi pale mfululizo kwa matarajio ya siku ya arusi. Baba angekagua kila mara nyumba hiyo kuona kama imekuwa tayari. Pia, katika destuli za Kiyahudi hawakuwa wanapanga tarehe ya arusi. Bibi arusi alipaswa awe tayari muda wote. Mathayo 25:10 inasema, "Na hao walipokuwa wakienda kununua, bwana arusi akaja, nao waliokuwa tayari wakaingia pamoja naye arusini; mlango ukafungwa".

"Tazama, naja upesi, na ujira wangu u pamoja nami, kumlipa kila mtu kama kazi yake ilivyo. Mimi ni Alfa na Omega, mwanzo na mwisho, wa kwanza na wa mwisho. Heri wazifuao nguo zao, wawe na amri kuuendea huo mti wa uzima, na kuingia mjini kwa milango yake. Huko nje wako mbwa, na wachawi, na wazinzi, na wauaji, na hao waabuduo sanamu, na kila mtu apendaye uongo na kuufanya. Mimi Yesu nimemtuma malaika wangu kuwashuhudia ninyi mambo hayo katika makanisa. Mimi ndimi niliye Shina na Mzao wa Daudi; ile nyota yenye kung'aa ya asubuhi. Na Roho na Bibi-arusi wasema, Njoo! Naye asikiaye na aseme, Njoo! Naye mwenye kiu na aje; na yeye atakaye, na ayatwae maji ya uzima bure" (Ufunuo 22:12-17).

Hadithi yetu inianza na laana kutokana na uasi wa mwanadamu. "...ardhi imelaaniwa kwa ajili yako; kwa uchungu utakula mazao *yake* siku zote za maisha yako" (Mwanzo 3:17b).

Hadithi yetu inaishia na Mwana Kondoo akichukua laana zetu ili tuweze kubarikiwa. "Wala hapatakuwa na laana yo yote tena. Na kiti cha enzi cha Mungu na cha Mwana-Kondoo kitakuwamo ndani yake. Na watumwa wake watamtumikia" (Ufunuo 22:3). Amina!

Uwe halisi kwa Mungu.

Sasa sikiliza sauti Yake.

"Habari, Jina langu ni Yesu. Nakupenda".